**4 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Arobaini – Tarehe 4 Juni, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**MHE. LEAH J. KOMANYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 516

**Kituo cha Afya Mkulwe Kuanza Kazi Rasmi**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, lini Kituo cha Afya Mkulwe kitaanza kazi rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mkulwe kipo Kata ya Mkulwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali ilipeleka shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la maabara na wodi ya wazazi. Aidha, jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje *(OPD)* limekamilika na limeanza kutoa huduma mwezi Aprili, 2024.

Mheshimiwa Spika, serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la maabara na wodi ya mama na mtoto ili yaanze kutoa huduma ifikapo mwezi Julai, 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninataka kufahamu ni lini Zahanati ya Ndanga Mbuyuni, Wilaya ya Songwe pamoja na zahanati ambayo imejengwa katika Mtaa wa Boimanda katika Kata ya Chipaka Mji wa Tunduma zitaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, nilitaka kufahamu, je, Serikali imefanya tathimini ya kubaini vituo vya afya na zahanati ambazo zimejengwa na zimetumia matumizi ya fedha kuzidi kiwango ambacho kimepangwa na Serikali? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge alinipa taarifa kuhusiana na zahanati hizo lakini tunafanya mawasiliano kwa zahanati ambazo hazijakamilika ili tuweze kuona zinahitaji nini na lini zitaanza kufanya kazi.

Kwa hiyo, naomba kuhusiana na swali lake la kwanza tutafanya mawasiliano na tutampa mrejesho ziko hatua gani, zimekwama wapi na lini zitaanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, ni kwamba Serikali imekwishafanya tathimini ya vituo vyote, zahanati zote na hospitali zote za halmashauri zilizopelekewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali na ambayo haijakamilika. Zipo ambazo hazijakamilika kwa sababu ya matumizi ya fedha ambayo kwa kweli hayaridhishi, lakini zipo ambazo hazikukamilika kwa sababu fedha hazikutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa zile ambazo matumizi ya fedha hayakuwa sawa, watumishi wote waliothibitika kuhusika wamechukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria, lakini tunaendelea na ukamilishaji wa zahanati hizo na tutaendelea kufanya hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 517

**Ujenzi wa Zahanati Kijiji cha Masagalu – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Masagalu – Kilindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Masagalu ipo katika Kijiji cha Masagalu Kitongoji cha Masagalu Misheni ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilitoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la zahanati. Zahanati imekamilika kwenye baadhi ya vitengo ambapo huduma za wagonjwa wa nje zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi imetenga bajeti ya shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati hiyo katika mwaka wa fedha 2024/2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini Zahanati hii ya Masagalu ina majengo zaidi ya matatu au manne na kwa shilingi milioni 50 ni dhahiri kwamba haiwezi kukamilisha, lakini kwa sababu kuona ni kuamini, kwa nini usingepanga safari kwenda kuangalia zahanati hiyo ili uweze kutoa majibu sahihi kwa ajili ya masilahi mapana ya wananchi wa Masagalu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba tunayo Kata ya Negero ambayo wanapata huduma katika Kituo cha Afya Handeni kilometa 70, Bwagalu kilometa 80 na Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge kilometa 120. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya kwenye Kata hii ya Negelo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu Zahanati hii ya Masagalu ina majengo zaidi ya mawili/matatu na tunafahamu kwamba shilingi milioni 50 haitakamilisha majengo yote, lakini nimhakikishie kwamba ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali tunakwenda kwa awamu. Tulishaanza na shilingi milioni 100, tumejenga, wananchi wanapata huduma za *OPD*, tunakwenda na shilingi milioni 50 tutakamilisha jengo moja, lakini tutaendelea pia kutenga fedha kila mwaka wa fedha ili kuhakikisha yale majengo yamekamilika na yanatoa huduma zinazostahiki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kukagua zahanati hiyo na kuona namna nzuri ya kuikamilisha mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kituo cha afya katika Kata ya Negero ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge. Naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilindi kutuletea taarifa rasmi kama kata hiyo ni miongoni mwa kata za kimkakati ambazo zinakidhi vigezo kwa ajili ya kujenga kituo cha afya ili Serikali itafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kyebitembe wana zahanati ambayo ilianza kujengwa tangu

mwaka 2012. Je, Serikali haioni ni muda muafaka wa kuwasaidia kukamilisha hiyo zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa kila mwaka inapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati shilingi milioni 50 kila halmashauri kwa kila boma na maboma matatu kila halmashauri kila mwaka na hata mwaka huu wa fedha tayari Halmashauri ya Muleba imepata takribani shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu na miaka mitatu iliyopita ya fedha, fedha hizo zilikwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kusisitiza Menejimenti ya Halmashauri ya Muleba kama zahanati hiyo ni kipaumbele tangu mwaka 2012 ni wajibu wao kuhakikisha hizo fedha zinazopelekwa zinakwenda kukamilisha hiyo zahanati kwa sababu Mheshimiwa Rais amepeleka fedha kila mwaka shilingi milioni 150 kwa ajili ya maboma matatu Muleba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi kukamilisha aidha kutumia fedha za Serikali kuu au kutumia mapato ya ndani ili zahanati ianze kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 518

**Malipo ya *Arrears* na Kusafirisha Mizigo kwa Walimu Wastaafu – Kilwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, Serikali itawalipa lini walimu wastaafu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa malipo ya *arrears* na fedha za kusafirisha mizigo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madai ya watumishi wastaafu ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2024 jumla ya shilingi milioni 29.8 kati ya shilingi milioni 31.1 zililipwa ikiwa ni gharama ya kusafirisha mizigo ya walimu 53 kati ya walimu 55 waliokuwa wamestaafu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2024 Serikali imelipa shilingi milioni 125.3 kati ya shilingi milioni 129.1 ikiwa ni madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu 22 kati ya 25 waliostaafu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa kwa awamu madai mbalimbali ya wastaafu kote nchini ikiwemo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza kwamba wapo walimu ambao wamestaafu tangu mwaka 2018 ma wengime tangu mwaka 2020, ni miaka sita mpaka miaka minne bado hawajalipwa *arrears* wala fedha za kusafirisha mizigo. Mfano Mwalimu Khadija Hussein Teremsha amestaafu mwaka 2018 ni miaka sita sasa hajalipwa *arrears* wala fedha za kusafirisha mizigo. Mfano wa pili ni Mwalimu Salma Kaisi amestaafu mwaka 2020 anadai malimbikizo mpaka sasa ni miaka minne. Je, lini Serikali italipa fedha hizi kwa walimu hawa wastaafu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na changamoto kwa waajiri kutopeleka michango ya watumishi katika mifuko ya

hifadhi ikiwemo *PSSSF*. Walimu hawa ambao wamelipwa, baadhi yao waliambiwa wakachangie wenyewe kwenye mifuko hii badala ya mwajiri, mfano wa walimu hawa ni Mwalimu Khadija Bungurumo, amelipwa mafao yake baada ya kuambiwa akachangie mwenyewe. Je, huu ndiyo utaratibu? Ahsante.

**SPIKA:** Wale wa mafao wako wapi humu ndani? Wote hawapo.

Mheshimiwa Ally Kassinge, hili swali lako la pili nadhani linahitaji majibu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu swali la kwanza la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni haki ya watumishi wastaafu kulipwa mafao yao kwa wakati, lakini pia *salary arrears* kwa wakati, lakini pia kulipwa fedha za kusafirisha mizigo kwa wakati. Vilevile ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wastaafu hao wanalipwa. Pia Serikali hii sikivu imekuwa ikifanya hivyo na ndiyo maana katika jibu langu la msingi umeona namna ambavyo wastaafu wa Halmashauri ya Kilwa walivyolipwa kwa kiasi kikubwa na wachache ambao tunamalizia ni wale ambao tutawalipa katika mwaka huu wa fedha mwishoni.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao hawajalipwa ambao Mheshimiwa Mbunge amewataja, naomba baada ya kumaliza *session* hii ya maswali na majibu nikutane na Mheshimiwa Mbunge tuweze ku-*trace* taarifa zao ili tumwelekeze Mkurugenzi haraka iwezekanavyo wapate haki zao za kulipwa *salary arrears* pamoja na kusafirisha mizigo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama, wastaafu wanaambiwaje wachangie wenyewe?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, tumepokea hili jambo jipya ambalo

limeletwa na Mheshimiwa Mbunge, naomba kwa ridhaa ya kiti chako tulichukue jambo hili kusudi Wizara inayohusika ikiwezekana iweze kupata nafasi ya kulipokea hilo na kulitolea ufafanuzi wa kina kwa sababu mafao yote kwa wastaafu yanalipwa kwa kuzingatia sheria na utaratibu. Pia kwa mujibu wa sheria zilizopo hakuna mahali ambapo tumeandika kwamba mstaafu anapotaka kulipwa mafao yake anatakiwa yeye mwenyewe ndiyo alipie michango yake ili aweze kupata mafao.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunatakiwa tulichukue ili tulifanyie kazi ya kutosha na tutalitolea tu maelezo na maelekezo kwa wahusika wote nchini.

**SPIKA:** Sawa, sasa kwa sababu hii changamoto kwa kweli ni nzito kidogo, nadhani Mheshimiwa sijui hilo kama kuna Mbunge mwingine amepata changamoto kama hiyo, lakini kitendo cha mtumishi kuambiwa achangie ili yeye alipwe ni jambo zito kwa kweli. Mheshimiwa Mbunge, mkabidhi jina Mheshimiwa Waziri ili walifuatilie hilo kwanza kwa sababu ni wa muda mrefu. Ndiyo huyo umesema wa mwaka 2018?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, hawa ambao wamelipwa ni wa mwaka 2020 na waliambiwa wachangie wenyewe akiwemo Mwalimu Khadija Bungurumo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, wapo kadhaa, siyo mmoja tu?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, huu ni mfano tu, lakini wale wa 2018 hawajalipwa malimbikizo wala fedha za kusafirishia mizigo akiwemo Mwalimu Kaisi.

**SPIKA:** Hilo la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI amekwishajibu amesema mtaonana. Mimi nauliza huyu aliyeambiwa achangie ili alipwe mafao.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, wapo kadhaa.

**SPIKA:** Wapo kadhaa?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya mpelekee Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ili waweze kufuatilia jambo hilo kwa sababu kwa kweli ni kinyume na sheria, utaratibu na kinyume cha kila kitu. *(Makofi)*

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, wewe mpelekee hayo majina ili waweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, sasa aulize swali lake.

Na. 519

**Mradi wa *DMDP* – Mbagala**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, ni barabara zipi zimetengewa fedha katika Mradi wa *DMDP* awamu ya kwanza na barabara zipi zipo *DMDP* awamu ya pili katika Jimbo la Mbagala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika Mradi wa *DMDP* awamu ya kwanza zimejengwa barabara katika kata tatu za Kijichi, Mbagala na Mbagala Kuu. Katika Kata ya Kijichi zimejengwa kilometa 15.85 katika barabara za Sangara, Mariam, Serikali ya Mtaa, Mwanamtoti, Kijichi, Polisi, Tausi, Hosteli, Budodi, Diwani, Posta na Neruka.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mbagala Kuu zimejengwa kilometa 11.35 katika barabara za Mbagala Kuu, Mihande Jeshini, Sokoni, *Dispensary*, Giriki, Ponela, Balili, *KLPT*, Serenge, Ng'ombe na Miande Kijichi. Katika Kata ya Mbagala zimejengwa kilometa 6.87 katika barabara za Bughudadi, Kizinga, *Clinic,* Msikitini, Mangaya na Mwera.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *DMDP* awamu ya pili zimependekezwa kujengwa kilometa 31.82 kwa kiwango cha lami katika barabara za Ndunguru, Masaki, Masuliza, Maandazi, Kipati, Agape, Kilimahewa, Chasimba, Chamazi Magengeni, Saku na Tambani. Hadi sasa tayari barabara za urefu wa kilometa 18.48 zimesanifiwa na hatua za manunuzi zinaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Mradi huu wa *DMDP* utatekelezwa katika Kata ya Kiburugwa, Chamazi, Charambe, Mianzini, Mtaa wa Jeshi la Uokovu na Kichemchem?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuzielekeza halmashauri kutumia fedha za Mfuko wa Barabara na fedha za mapato ya ndani zinazotumika katika kujenga barabara kwenda kujenga barabara katika kata ambazo hazipitiwi na Mradi huu wa *DMDP?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli amekuwa akifuatilia sana maendeleo ya miundombinu ya barabara kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, katika Kata ya Kiburugwa, Mianzini, Chamazi, Charambe na katika Mitaa ya Jeshi la Uokovu na Kichemchem utekelezaji wa Mradi wa *DMDP*

awamu ya pili uko katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 31.82 za lami katika Kata za Kibondemaji, Tuangoma, Mbagala Kuu, Kilungule, Chamazi na Kiburugwa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huo pia usanifu unaendelea na usanifu unafanyika kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 61.03 za lami katika Kata za Kilungule, Mbagala Kuu, Kijichi, Kibondemaji, Tuangoma, Chamazi, Mianzini, Mbagala Kuu, Chalamba na Kibulugwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI ilishatoa maelekezo kwamba kuna baadhi ya Halmashauri za Manispaa, lakini Halmashauri za Majiji ziweze kutenga fedha ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa barabara na utekelezaji wa malekezo hayo ni dhahiri kwa sababu katika jimbo lako katika mwaka wa fedha 2022/2023 Manispaa ya Temeke ilitenga shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo, lakini katika mwaka wa fedha 2023/2024 Manispaa ya Temeke ilitenga shilingi bilioni 3.75, lakini katika mwaka wa fedha 2024/2025 Manispaa ya Temeke imetenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya barabara katika jimbo lako inaweza kujengwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 520

**Ujenzi wa *Fence* ya Umeme Hifadhi ya Mikumi**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga *fence* ya umeme katika Hifadhi ya Mikumi ili kuepusha usumbufu wanaoupata wananchi wanaopakana na hifadhi hiyo kutoka kwa wanyama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu hususani tembo pindi wanapoingia kwenye maeneo ya wananchi. Hatua hizo ni pamoja na kutumia helikopta, magari maalumu, ndege nyuki, matumizi ya mabomu baridi na doria za kawaida. Sambamba na hatua hizo, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna bora ya kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ina mpango wa kujenga uzio wa umeme wa majaribio katika eneo la kilometa 68 katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa maeneo yanayopakana na vijiji vya Wilaya ya Serengeti na Tarime. Kwa sasa Wizara ipo kwenye majadiliano na wadau wa maendeleo kwa lengo la kupata fedha. Aidha, endapo uzio huo utaonesha ufanisi, Serikali itaendelea na kujenga uzio kama huo katika maeneo mengine yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo Hifadhi ya Taifa Mikumi kulingana na upatikaji wa fedha.

**SPIKA**: Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, inaonekana kwamba Serikali mpaka sasa hivi haiko tayari kujenga ila bado iko kwenye majaribio, je, Serikali iko tayari kwenda kujifunza Kenya katika mbunga moja ya

Itsavo ambayo iko Mkoa wa Pwani wa Kenya ambao wenzetu wana mafanikio makubwa sana katika kuzuia kwa kutumia umeme?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kulikuwa na mpango wa kuchepusha barabara ambayo inapita katikati ya Mbuga ya Mikumi, barabara hiyo inaua sana wanyama walioko katika hiyo mbuga, je, huo mpango umefikia wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aleksia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa hivi tuko kwenye majadiliano kama nilivyosema ya kuweza kutumia teknolojia hii kuwadhibiti tembo. Watalaamu wetu wamekuwa wakijifunza kupitia mifumo mbalimbali, hapa nchini tunao mfumo huo ambao unamilikiwa na sekta binafsi, tayari wataalamu wetu wanajifunza kupitia mfumo huo. Wataalamu wetu wamekuwa wakijifunza kwa wenzetu wa nchi za Kenya na Afrika Kusini, tunachokiona ni kwamba tofauti ni kwamba kule Kenya maeneo haya ni maeneo madogo madogo ambayo umiliki wake ni wa watu binafsi, lakini kwetu sisi itahitaji kufanya kazi kubwa kwenye maeneo makubwa.

Kwa hiyo, wataalamu wetu wanajifunza nimhakikishie tupo *serious* kwenye jambo hili ili tuweze kukabiliana na wanyama hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mpango ule wa barabara Serikali inaendelea na mpango huu katika kuhakikisha kwamba tunachepusha barabara ile iweze kupitia Kilosa na kazi hizi zinaendelea, naomba tuendelee kuwa na subira wakati Serikali inakamilisha mradi huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kata za Tindiga, Kilangali, Mhenda na Mikumi zimekuwa na kadhia kubwa hii ya tembo ijapokuwa Serikali hii inasema kwamba inatafuta fedha, je, haioni wakati umefika sasa kuishirikisha sekta binafsi katika kuangalia jinsi ya ushiriki ya kudhibiti hawa tembo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye majibu yangu ya msingi nimesema kwamba tayari tunashirikiana na sekta binafsi kwa sababu kule iko *Ikorongo Game Reserve* sekta binafsi inashirikiana na wenzetu wa *TAWA* wamejenga mfumo wa uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 80 kwa kutumia umeme wa *solar,* lakini kama tulivyosema jana hapa wakati wa maelezo, tulisema ili kukabiliana na janga hili tunaangalia vilevile kushirikiana taasisi zetu za bima kuona ambavyo tunaweza kushirikiana. Kwa hiyo, sisi tumeanza na tutaendelea kushirikiana na wadau wengine ili kuhakikisha tunapambana na tatizo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 521

**Ujenzi wa Miundombinu ya Bandari ya Manda**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je , lini SerikaLi itajenga gati, ghala na jengo la abiria katika Bandari ya Manda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali *(feasibility study and preliminary design*) katika Bandari za Ziwa Nyasa ikiwemo Bandari za Itungi, Kiwira, Lupingu, Liuli, Matema, Mbamba Bay na Manda.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na matarajio ya ukuaji wa shehena na abiria ambapo ni moja kati ya vigezo vya ujenzi au maboresho ya bandari, imebainika kuongezeka kwa matumizi ya bandari zilizopo katika ziwa hilo. Ili kuwa na miundombinu inayoridhisha kuhudumia abiria na mizigo katika Bandari za Ziwa Nyasa, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia *TPA* imetenga shilingi 1,100,0000,000 kwa ajili ya maboresho ya Bandari za Ziwa Nyasa ikiwemo Bandari ya Manda ambayo imetengewa shilingi milioni 220 kwa kuanzia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaotegemea usafiri wa meli MV Mbeya kuna miezi miwili sasa wamekosa usafiri kwa sababu meli ile haifanyi safari zake na walishashauri Serikali kutokana na mafuriko itumie Bandari ya Matema.

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali kufuatilia hilo eneo ili wananchi waweze kuondokana na adha ya usafiri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa Nsele na Lifuma waliomba Serikali iende kukagua maeneo kwa ajili ya vituo vya meli, ni lini Serikali itatuma wataalamu wake ili kuwaondolea

adha wananchi ya kutembea mwendo mrefu baada ya kushuka kwenye kituo cha meli?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongezi za Mheshimiwa Mbunge Kamonga kwa Serikali kwa kufanya kazi kubwa hii ya miundombinu, lakini pili ni kweli meli yetu ya MV Mbeya iliyokuwa inafanya shughuli zake ilisimamisha safari zake kutokana na hali ya mvua, hivyo mara baada tutakapoona hali imetengamaa tutairudisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wake wa kutumia Bandari ya Matema tumeipokea na tunawaelekeza wenzetu wa *TPA* waanze kutazama miundombinu kama ushauri huu unaweza ukafanyiwa kazi tuweze kuwaza kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pili, tumepokea pia ombi la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na kutembelea maeneo ya Nsele ambayo yapo Kata ya Kilondo pamoja na Lifuma tuweze kuyatazama halafu tutajua namna ya kwenda nao baada ya kupata ushauri wa wataalamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake...

Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wawili kwa wakati mmoja, yule ambaye ana majibu ya Mheshimiwa Mbunge? Hakuna hata mmoja mwenye nayo? Basi nimtaje niliyemuona kwanza, Mheshimiwa nani amegonga meza? Eenh, mafunzo ya Kanuni inabidi tuendelee nayo mpaka tunamaliza Bunge hili.

Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

Na. 522

**Ongezeko la Nauli za Ndege Mara kwa Mara**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA K.n.y. MHE. MWANTUM DAU HAJI** aliuliza:-

Je, nini sababu ya ongezeko la nauli za usafiri wa ndege mara kwa mara nchini ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ongezeko la nauli za usafiri wa ndege hutegemea gharama za uendeshaji ambapo gharama kubwa ni mafuta ya ndege na vipuri. Vilevile gharama zote hizi zinategemea na fedha za kigeni. Hivyo kuongezeka kwa kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni kunaathiri gharama za uendeshaji ambazo zinasababisha mabadiliko ya gharama za tiketi.

**SPIKA :** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mabadiliko hayo anayoyasema yanasabishwa pengine na mabadiliko hayo ya pesa za kigeni, lakini nataka kujua, ili kupunguza gharama kwa wasafiri hasa wanaotoka Dodoma kwenda Mwanza, Dodoma – Arusha na Dodoma - Mbeya kwa nini wanazunguka Dar es salaam ndio waweze kwenda kuunganisha ? Huoni nayo ni gharama kubwa unawaongezea wasafiri?

**SPIKA :** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni sehemu ya ushauri, wakati yeye anazungumza hoja kwamba kwa nini

tunazunguka, tayari wenzetu wa Mtwara wameshaleta maombi yao mezani, wanaomba ndege itoke Dar es Salaam iende Mtwara, iende Songea hivyo bado kuzunguka kunategemea na unachukua abira kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ili usiwaache na pengine upunguze mizunguko ambayo ilikuwepo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 523

**Ujenzi wa *VETA* Majimboni**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *VETA* kutokana na wingi wa watu kwenye majimbo bila kujali ni wilaya au mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshemiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa vyuo vya ufundi stadi katika maeneo yote yenye mahitaji ili kutoa mafunzo kwa wananchi kwa lengo la kuwapatia ujuzi utakao wawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inaendelea kutekeleza azma ya kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila mkoa na wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo vya ufundi stadi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 64 ikiwemo na Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe. Ujenzi huo unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi, katika mwaka fedha 2024/2025 itaanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa shule za sekondari za ufundi mia moja. Shule hizo zitajengwa katika majimbo ambayo hayana Vyuo vya *VETA* pamoja na maeneo mengine yenye uhitaji wa vyuo vya ufundi stadi. Busanda ni miongoni mwa majimbo ambayo itajengewa shule ya ufundi ambayo itachukua nafasi ya Chuo cha *VETA,* nakushukuru sana.

**SPIKA :** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwenye swali hili nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa shule ya ufundi haiwezi kuchukua nafasi ya *VETA,* je, Serikali ina mpango au mkakati wa makusudi kurekebisha sera ili kujenga *VETA* kwenye maeneo yenye watu wengi ikiwemo Jimbo la Busanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Magessa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba mkakati wa Serikali umeanza utekelezaji wa ujenzi wa vyuo hivi vya *VETA* katika ngazi za mikoa na baadae tumekuja katika ngazi za wilaya ambayo ujenzi unaendelea kutekelezwa ili kuhakikisha kwamba wilaya zote zinakuwa na vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona kwamba kuna umuhimu wa kusogeza huduma hii karibu na tunafahamu kwamba kuna baadhi ya wilaya ni kubwa zina majimbo zaidi ya moja, Serikali ilikuja na mpango wa kuhakikisha kwamba

tunapeleka shule za ufundi katika majimbo ambayo hayajajengewa vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Magessa anazungumza suala la Busanda na umuhimu wa kujengewa chuo cha *VETA,* namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie tukamilishe kwanza mpango huu wa mikoa, wilaya pamoja na shule hizi za ufundi katika kila majimbo ambayo hayana Vyuo vya *VETA* baadae tufanye tathmini ili tuweze kuona umuhimu wa kupeleka maeneo yale mahususi ambayo yatahitaji ziada ya vyuo hivi katika maeneo hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwanza niishukuru Serikali kwa kututengea fedha shilingi 1,300,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi *VETA* Wilaya ya Nyang'hwale na mpaka sasa hivi tumeshapokea shilingi milioni 300 bado shilingi bilioni moja. Je Serikali iko tayari kuzitoa hizo shilingi bilioni moja ili ujenzi huo uendelee?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajenga vyuo hivi 64 kwa awamu na kumekuwa na utaratibu wa kupeleka fedha zile ambazo zinanunua *local materials* kwa maana ya mchanga, kokoto na mawe ndizo hizo Mheshimiwa Mbunge unazozungumza kwamba zimekuja zaidi ya shilingi milioni 300, lakini Serikali imefanya *bulk purchase* ya vifaa vingine kwa maana ya zile *LGS, light gauge steel, column* pamoja na *beam, cement,* nondo pamoja na mabati ambayo tunafanya *bulk purchase* na yataletwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kimsingi fedha iliyokuja ni zaidi ya hiyo kwa sababu vifaa hivyo ninavyovizungumza vyote viko

*site,* lakini Serikali tayari fedha hizi zipo kwa kadiri *consumption* itakavyokuwa inafanyika kule *site,* ndivyo pesa zitakavyokuwa zinakuja, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Chagula, swali la nyongeza, ama hukuwa...

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa *VETA* unasuasua pale Mbulu, je, lini unakuja kufanya ziara ili ujenzi ule uweze kuendelea kwa haraka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, nimwondoe hofu na wasiwasi kwa vile tuko hapa Bungeni na kutoka hapa kwenda Mbulu siyo mbali, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki cha maswali tuweze kukaa na kuangalia ratiba namna gani tunaweza kwenda hata wakati wa *weekend*, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, mlio upande wa Mawaziri nilitoa katazo hapa mbele si siku nyingi. Mpishe eneo la Mawaziri ili wasikilize maswali yanayowahusu na waweze kujibu, mtarejea huko kipindi cha maswali kikiisha.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sylvia Sigula.

Na. 524

**Udhibiti wa Wahamiaji Haramu Mipakani**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA K.n.y. MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kudhibiti wahamiaji haramu mipakani kabla hawajaingia nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimika mifumo ya kielektroniki wa mipaka *(e–border)* ambao unasaidia katika kudhibiti wageni wasio na sifa kabla hawajaingia nchini. Kwa kutumia mfumo huo Serikali imefanikiwa kuwazuia kuingia nchini kwa sababu mbalimbali jumla ya wageni 1,223 kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2022 hadi Mei, 2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya vikao vya kikanda, kimataifa na ujirani mwema kwa lengo la kupanga mipango ya pamoja ya kudhibiti uhamiaji haramu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini pamoja na mipango hiyo mizuri na majibu mazuri nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika wananchi wanaoishi mipakani hasa mikoa ya pembezoni ya Kigoma, Rukwa na Katavi wamekuwa wakipitia unyanyasaji sana kwa kesi hizi za uraia na wengine ni raia.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutoa mafunzo maalumu kwa maafisa uhamiaji ili wananchi hawa wa pembezoni wawe *treated* vizuri bila kuwa na unyanyasaji kwa sababu wengine wanapata kesi za uraia, lakini ukweli ni Watanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sylvia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wazo lake ni zuri, lakini hata hivyo tunao utaratibu wa kutoa mafunzo ama elimu kwa askari wa uhamiaji. Kwanza, wanapoajiriwa wanapata mafunzo, lakini hata wanapopandishwa vyeo na kuna *refreshers course* mbalimbali ambazo wanapata wakati wakiwa wanaendelea na majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hoja yake ya usumbufu wa baadhi ya wananchi mipakani tunalichukua kwa uzito mkubwa, lakini lazima atambue kwamba kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo katika maeneo ya mipaka ya nchi yetu kuna umuhimu wa askari wa uhamiaji, maafisa uhamiaji na maafisa wa Idara ya *NIDA* kujiridhisha juu ya watu ambao wanaweza kupata haki ya kuwa Watanzania ili haki hiyo iweze kutolewa kwa Mtanzania ambaye anastahiki badala ya kuwapatia watu ambao hawastahiki.

Kwa hiyo, tutaya-*balance* yote mawili kuhakikisha kwamba wale ambao ni Watanzania halali wanapata haki zao bila usumbufu, lakini vilevile tunasimamia kuhakikisha usalama wa nchi yetu unalindwa kwa kudhibiti wale ambao hawastahiki wasiweze kupata haki ambazo hawastahili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Felix, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na matukio ya wahamiaji wengi kukamatwa katikati ya nchi

katika mikoa ya Morogoro, Dodoma na Mbeya. Je, Serikali imekwishafanya uchunguzi kwamba hao wahamiaji wanapita wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wahamiaji hawa ambao wamekuwa wakikamatwa mara nyingi wanapita katika maeneno ambayo siyo rasmi. Tunatambua kwamba nchi yetu imepakana na nchi nyingi na maeneo ambayo mengine kwa kweli bado yana changamoto ya kuyadhibiti na ndiyo maana tunafanya jitihada mbalimbali ikiwemo kufunga mifumo hii ya kisasa ili kuweza kudhibiti, lakini kusaidia kuwezesha jeshi letu la uhamiaji kuweza kufanya doria za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiwawezesha kwa kuongeza idadi ya askari, ajira mpya zinatajiriwa katika mwaka huu wa fedha, vilevile tuliomba mwaka uliopita, lakini magari kwa ajili ya kufanya doria na vitendea kazi mbalimbali ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaendeleza msako wa wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi itakumbukwa wimbi kubwa la wahamiaji haramu hawa wanatoka katika nchi ya Ethiopia na hivi karibuni tumeamua kufanya mabadiliko ya utaratibu wa viza rejea kwa kuindoa nchi ya Ethiopia kutoka nchi ambazo zinatumia viza rejea.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo limesaidia sana kupunguza hili wimbi la wahamiaji haramu kama ambavyo nilieleza katika bajeti iliyopita kwamba kupitia maamuzi hayo tumeweza kuhakikisha kwamba tumepata Waethipia ambao wangepita katika njia haramu zaidi ya 3,500 ambao wamepita katika njia halali. Imetusaidia Serikali kukusanya fedha zaidi ya dola 170,000. Kwa hiyo, jambo hili pia limesaidia kupunguza. Kwa hiyo, mikakati

ni mingi ambayo tunaendelea nayo kama nchi kuweza kudhibiti hali hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wanatajwa kwa kuingia nchini bila vibali na unaitwa uharamu. Ukitaja nchi humu ndani, japokuwa kwako wewe unaendelea na hayo mambo ya uchunguzi huko isije ikaleta hoja ya kwamba pengine nchi fulani ilikuwa inatajwa kwamba ilikuwa inaleta watu ambao hawaingii nchini hapa kihalali.

Kwa hiyo, nadhani jibu lako likae kwa hiyo jumla ili tuiondoe hiyo nchi kwenye hayo majibu yako.

Mheshimiwa Kandege Josephat.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida kumekuwa na ruhusa kati ya wananchi ambao wamekuwa wakisafiri kati ya Tanzania na Kenya umbali fulani unaruhusiwa, lakini kwa upande wa Kalambo imekuwa tatizo kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, je, ni umbali gani ambao mwananchi kutoka nchi moja kwenda upande wa pili anaruhusiwa kusafiri bila shida? Kwa sababu wakati mwingine naenda kufanya shughuli labda naenda kwenye msiba, kumekuwa na shida kubwa katika mpaka wa Kalambo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampa pole Mheshimiwa Mbunge kwa wananchi wake kukutana na usumbufu ambao wanaupata, niwahakikishie kwamba nitakapotoka hapa nitakwenda kulifuatilia jambo hili ili usumbufu huo usijitokeze, kwa sababu hakuna tofauti kati ya watu wanaopakana *either*

wanapakana na Kenya, Rwanda, Burundi, *DRC* au kokote. Utaratibu wa sheria unatoa ruhusa kwa wananchi kuweza kuingia na kutoka kwa vibali maalumu katika maeneo ya mipakani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Martha Gwau.

Na. 525

**Kuwekeza kwenye Madini ya Chumvi na Magadi Manyoni**

**MHE. MARTHA N. GWAU K.n.y. MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwekeza kwenye madini ya chumvi na magadi katika Kata za Majiri na Sanza Wilaya ya Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* imefanya jitahada mbalimbali kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini ya chumvi katika Wilaya ya Manyoni, hususani katika kutoa mafunzo ya uchimbaji wa madini ya chumvi pamoja na uchakataji wake kwa kutumia nishati mbadala ya makaa ya mawe badala ya utumiaji wa kuni wanaoutumia kwa sasa. Takribani wachimbaji wadogo 60 wa kikundi cha wachimbaji wa chumvi katika Kijiji cha Kinangali, Wilayani Manyoni walipata elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali kupitia *STAMICO* inaendelea na mpango wa ujenzi wa kituo cha mfano cha

uchakataji chumvi mkoani Lindi na kiwanda hicho kitatumika kuchakata chumvi na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wazalishaji wa chumvi ili kuwajengea uwezo wa kuzalisha kwa tija na ubora stahiki wakiwemo wazalishaji wa chumvi wa kutoka Manyoni, Singida, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Gwau, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali ina mpango gani wa kutumia utafiti ambao tayari mmeshaufanya ili sasa kwa kutumia huo utafiti ili kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza katika chumvi hiyo inayopatikana Manyoni?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kuja na viwanda vidogo vya kimkakati ambavyo vitawezesha kuongeza thamani kwa chumvi hii ili kupatiwa soko la uhakika? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishafanya utafiti wa awali katika kuangalia ubora na uwepo wa chumvi safi katika eneo la Manyoni analoulizia Mbunge na huo utafiti wa awali sasa unakwenda kutafsiriwa kwenye utafiti wa kina ambao *STAMICO* kupitia mitambo ya uchorongaji ambayo tumeigiza itakwenda kufanya utafiti ili kupata taarifa sahihi za kiwango kinachovutia uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, viwanda hivi vidogo anavyoulizia Mbunge ni viwanda ambavyo tunavianzisha kwa kuanza na kiwanda kimoja cha mfano kule Lindi na baada ya ufanisi wa kile kituo cha uzalishaji chumvi kwa wachimbaji wadogo kufanikiwa teknolojia hiyo sasa itapelekwa katika sehemu mbalimbali kunakochimbwa na kuzalishwa chumvi nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU**: Mheshimiwa Spika, ahsante, Kata ya Kikio katika Jimbo la Singida Mashariki ni bonde lenye chumvi nyingi na kwa sababu haijhawahi kufanyiwa kazi kwa maana ya vikundi. Sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri tusaidie tuweze kuboresha viwanda na kuweza kuvutia wawekezaji katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hilo ni ombi la Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo, lipokee.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshimna na unyenyekevu nalipoke ombi lake na niielekeze taasisi yetu ya *GST* wakafanye utafiti wa awali ili tuweze kuendelea na taratibu za kutafiti zaidi kuhusu chumvi katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Ilindi ni moja ya kata maarufu kwa uzalishaji wa chumvi na kwa majibu ya Waziri inaonesha kama ni wanafanya baadhi ya maeneo.

Je, upi mkakati hasa katika eneo la kanda ya kati ili kuweka uzalishaji madhubuti na utafiti wa chumvi katika eneo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kulingana na Dira yetu ya *Vision 2030* tumedhamiria kufanya utafiti wa nchi nzima walau kwa 30% kufikia mwaka 2030 na kwa teknolojia ya kisasa tumeanza kurusha ndege isiyotumia rubadi *(drones)* katika maeneo mbalimbali nchini kung'amua maeneo hayo yenye

uwepo wa madini na haya madini ya chumvi ni sehemu ya madini ambayo tukishayatafiti tutaendelea na uhamasishaji wawekeze katika maeneo mbalimbali nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika ukanda wa Bahari ya Hindi ulipo Wilaya ya Mtwara kuna wawekezaji wakubwa wa chumvi, lakini wamekuwa wakipata changamoto kubwa ya masoko na viwanda.

Mheshimiwa Spika, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inawawekea mazingira wezeshi ili waweze kufanya shughuli zao kwa usahihi na kupata pesa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kwa sasa kwanza ni kuwapa elimu wachimbaji wa chumvi nchini ili waweze kuzalisha chumvi yenye ubora wa viwango vinavyohitajika kwa matumizi salama ya binadamu. Wawekezaji wakubwa tulionao sasa hivi kama Neelkanth changamoto yao kubwa ni ya miundombinu ya usafirishaji, lakini pia wa kukandamiza bei kwa sababu wanaona kama chumvi inayozalishwa kwa teknolojia inayotumika na wachimbaji wadogo haifikii ubora wanaouhitaji na ndiyo dhamira ya Serikali kupitia shirika lake la *STAMICO* kwenda sasa katika hatua ya kujenga vituo vya mfano ili chumvi yenye ubora na itakayokidhi mahitaji ya soko iweze kuzalishwa na kuuzwa kwa bei yenye tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 526

**Motisha kwa Wanawake Walioahidiwa Leseni za Uchimbaji Madini**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, Serikali imetoa motisha kiasi gani kwa wanawake 300 walioahidiwa kununuliwa leseni za uchimbaji madini na Mheshimiwa Rais?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikisha kupatikana kwa maeneo 15 ambayo yatatolewa leseni 15 kupitia Umoja wa Wanawake Wachimba Madini Mkoa wa Geita *(GEWOMA)* ambapo ni baada ya umoja huo kukamilisha usajili wa hivyo vikundi. Leseni hizo zitakapotolewa vitaundwa vikundi vya wanawake 20 katika kila eneo ambapo ni sawa na idadi ya wanawake 300 kwa leseni zote. Leseni hizo zitalipiwa ada zote muhimu na Serikali katika kipindi cha awali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaanzisha programu inayojulikana kama *Mining for a Brighter Tomorrow (MBT)* ya madini sasa ukiacha ya kilimo ambayo inalenga kuboresha sekta ya madini kwa kuweka mazingira bora zaidi ya kuwezesha uchimbaji kwa wanawake na vijana. Mpango huu unajumuisha mafunzo kwa wachimbaji, kuboresha teknolojia za uchimbaji na kuhakikisha uchimbaji unafanyika kwa njia endelevu na yenye tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa ni dhamira ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha wanawake wengi wanaingia katika uchimbaji wa madini na Mheshimiwa Rais aliahidi wanawake 300. Mpaka Serikali imetoa leseni moja kwa wanawake 47 kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, je, ni upi mpango wa haraka wa Serikali wa kuhakikisha hawa wanawake 253 waliobakia wanapata leseni haraka ili ahadi ya Mheshimiwa Rais iwe imetimia kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hivi karibuni kuna utafiti umefanyika Mkoa wa Rukwa na imegundulika kuna uwepo wa gesi ya *helium,* gesi ambayo kwa Tanzania nzima haipo, iko Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, Kata ya Milepa na Zimba.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kutoa elimu kwa vijana na wakina mama wa Mkoa wa Rukwa hasa maeneo hayo ili gesi hii adimu iweze kuwanufaisha vijana na kina mama wa mkoa huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge napenda kurejea majibu ya swali la msingi ambapo nimeeleza kwamba kuna leseni ambazo zimeshatengwa na ambazo zitagaiwa kwa vikundi vya watu 20/20 kwa hiyo wote 300 kama walivyoahidiwa na Mheshimiwa Rais wanakwenda kupata leseni kupitia vikundi. Kwa hiyo, hivyo vikundi vinakwenda kuwezeshwa na Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kulipiwa gharama za hizo leseni katika awamu ya kwanza au hatua za awali.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili la *helium,* utafiti wa hii gesi ya *helium* uko na unaendelea katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Rukwa. Hatua iliyofikiwa sasa hivi ya kuvumbua kwamba Rukwa ina-*deposit* kubwa ya gesi hiyo inapelekea sasa Serikali kwenda kutoa leseni kwa mwekezaji mkubwa ambaye baada ya kuingia makubaliano naye mchakato wa jinsi atakavyofuata sheria, kanuni na taratibu zetu ili wananchi wanaozunguka maeneo hayo waweze kufaidi kupitia huduma mbalimbali za mnyororo wa thamani unaopatikana uweze kuwafikia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba elimu itatolewa na wananchi wale watafaidi kwa njia mbalimbali ikiwemo kupitia mpango huu wa *local content* (ushirikishwaji wa Watanzania katika machimbo hayo), lakini pia kupitia *CSR* au mchango wa wale wawekezaji kwenye maendeleo ya jamii. Vikundi vyake vya wanawake na vya vijana vitafaidika na nampongeza sana kwa jinsi anavyowatetea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Geita una wanawake wengi wanufaika wa uchimbaji wa madini, je, wao pia watakuwa miongoni mwa wanufaika wa fursa hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania ni mnufaika wa madini ya aina yoyote yanapopatikana mahali popote nchini. Kwa hiyo, wana nafasi sawa ya kufaidika kama watakwenda kuwa katika maeneo hayo ama kwa kutoa huduma ama kujihusisha na madini ambayo uwezo wao wa kujihusisha nayo kwa kuchimba, kuchakata au kwa kufanya biashara unawezekana, watafaidika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali kwa kifupi. Nimemtaja Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kufahamu upi ni mpango wa Serikali kwa wale wachimbaji ambao wamepata leseni za uchimbaji na hawaendelezi yale maeneo kwa kufanya shughuli yoyote zaidi ya kuwa leseni ikiisha wana-*renew* tena, upi mpango wa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni zetu mchimbaji yeyote anapochukua leseni...

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, hamia pale kuna kiti.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mchimbaji yeyote anapopewa leseni ana muda wa miezi 18 aoneshe jitihada za kuiendeleza ile leseni yake. Baada ya hapo sasa hivi tuna mkakati wa kufuta leseni zote ambazo hazifanyiwi kazi, atapewa *notice* ya siku 30 ya kusema kwa nini haendelezi na hoja zake zinaporudi na kwamba hazioneshi dhamira ya kweli ya kuendeleza ile leseni yake tuko tayari kuifuta tuwape wale ambao wako *serious* na wako tayari kuwekeza ili nchi iendelee kunufaika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 527

**Ukarabati wa Bwawa la Mayuyu**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati Bwawa la Mayuyu ambalo ni muhimu kwa upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Kata za Kerenge, Magoma na Makumba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kufanya tathimini ya kitaalamu kuona endapo maji ya Bwawa la Mayuyu yanaweza kutumika kwa ajili ya matumizi ya maji ya kunywa kwa wananchi wa Kata za

Kerenge, Magoma na Makumba, Wilayani Korogwe, Mkoa wa Tanga. Awali bwawa hilo lilisanifiwa kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji na ufugaji wa samaki kabla ya kuathirika na mvua kubwa zilizonyesha Mkoani Tanga mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji kwenye kata hizo, Serikali imekamilisha Miradi ya Kwemazandu, Makangara na Mkwajuni - Sekioga inayohudumia vijiji vyote vitano vya Kata ya Magoma. Aidha, katika Kata ya Makumba vijiji viwili vya Makumba na Kitivo vinapata huduma ya maji safi kati ya vijiji vitatu wakati utekelezaji wa Mradi wa Kijiji cha Gombero unaendelea na umefikia 50% ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kufanya usanifu wa mradi utakaonufaisha vijiji vyote vitatu vya Kata ya Kerenge ambavyo ni Vingo, Kerenge-Makaburini na Kerenge-Kibaoni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Jambo hili ni la muda mrefu kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri, tangu mwaka 2019. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuwahakikishia watu wa Korogwe kwamba mwaka wa fedha ukianza jambo hili litafanyiwa kazi mapema iwezekanavyo kwa sababu tathmini ya awali ilishafanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama Mheshimiwa Naibu Waziri ametaja kwenye baadhi ya vijiji vile vya Kata ya Kerenge lakini kwenye kata hii tayari kuna mradi ambao unaendelea ambao unagusa na vijiji hivi. Lakini mkandarasi yuko pole pole na anaenda kwa kusuasua; kwenye mradi wa maji wa Kwetonge, Chekerei, Gombero na Mkumbara. Ni lini Serikali itatoa fedha ili wakandarasi wa miradi hii waweze kukamilisha kazi ambayo wameanza kwenye vijiji vilivyo ndani ya Jimbo la Korogwe vijijini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Mheshimiwa Mbunge anafuatilia kulingana na changamoto iliyotokea mwaka 2019. Kweli kabisa ni dhahiri kwamba wananchi wangepata uhakika wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirejea katika majibu yangu ya msingi, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kupeleka fedha na kuhakikisha kwamba tunafanya tathmini ya kitaalam na kujiridhisha kama yale maji ya Bwawa la Mayuyu yanafaa kutoa maji kwa ajili ya matumizi ya kunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namhakikishia na wananchi wake wote wa Jimbo lake la Korogwe Vijijini wawe na imani na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Ilani inatekelezwa na tutahakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kabisa katika Kata ya Kerenge kuna mradi ambao unaendelea na mpaka sasa umeshafikia asilimia 50. Tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ifikapo Disemba 2024 mradi huu utakuwa umeshakamilika na wananchi wataendelea kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa sasa aulize swali lake.

Na. 528

**Masoko ya Mazao ya Kimataifa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa masoko ya mazao ya kimataifa ambayo yametelekezwa miaka mingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 inaendelea na taratibu za kukamilisha ujenzi wa masoko matano (5) ya mazao ya kimkakati yaliyokuwa chini ya mradi wa *DASIP* katika Halmashauri za Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa kwa maana ya (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo zipo katika hatua ya upekuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa masoko haya katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya mchele na muhogo (Busoka); ndizi na maharage (Nkwenda); ndizi na parachichi (Kabanga); ndizi na viazi mviringo (Murongo); na mchele na mahindi (Sirari) katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Masoko haya ni ya muda mrefu na majibu yamekuwa ni kama yale yale, sasa, nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, unanihakikishia kwenye bajeti tuliyopitisha masoko haya yametengewa fedha ili yaweze kukamilishwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda Kyerwa kufanya mikutano kuwahakikishia wana-Kyerwa kuwa masoko haya yanaenda kujengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Spika, ahsante, cha kwanza nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kyerwa kwamba fedha zipo kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa masoko haya yote. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi hapa nimeainisha kwamba tupo katika hatua ya upekuzi, maana yake ni hatua ya mwisho, baada ya hapo ni kwenda kumkabidhi mkandarasi *site* aanze kazi. Kwa hiyo, nimuondoe shaka na niko tayari kwenda naye jimboni kuwaambia wananchi wa Kyerwa hiki ambacho nimekisema hapa na nina uhakika nacho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Stella Ikupa Allex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na 529

**Kukamilisha Uchakataji wa Idadi ya Watu Wenye Ulemavu Sensa 2022**

**MHE. STELA I. ALEX** aliuliza: -

Je, Serikali imekamilisha kuchakata na kufahamu idadi ya Watu wenye Ulemavu kwa kila halmashauri kwa mujibu wa Sensa 2022?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekamilisha uchakataji wa taarifa za Sensa za Hali ya Ulemavu katika ngazi zote za utawala. Kwa ufupi matokeo yanaonesha kuwa, kiwango cha watu wenye ulemavu wa aina yoyote ile nchini kimeongezeka hadi 11.2% mwaka 2022 kutoka 9.3% iliyokuwa mwaka 2012. Aidha, kuna kiwango kikubwa

zaidi cha wanawake wenye ulemavu (11.6%) ikilinganishwa na wanaume (10.9%). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Sensa ya mwaka 2022 yamechambuliwa hadi ngazi zote za utawala. Kwa sasa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na ile ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, wanakamilisha kutengeneza kanzidata ya watu wenye ulemavu hadi ngazi ya kitongoji ambayo imelenga kuwatambua walemavu wote kwa majina, mahali wanapoishi, na namba zao za simu za mikononi kama zilivyokusanywa Agosti, 2022 na taarifa nyingine za kijamii, kiuchumi na mazingira ya kundi hili. Kanzidata itazinduliwa ndani ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Allex, swali la nyongeza.

**MHE. STELA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na hatua nzuri ambazo zimefikiwa; je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba taarifa hizi zinapatikana katika mifumo iliyo rafiki kulingana na aina za ulemavu? Mfano, maandishi ya nukta nundu pamoja na maandishi yaliyokuzwa na mifumo ya sauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imejipangaje kutoa elimu ya umuhimu wa matumizi ya taarifa hizi ili kundi hili liweze kuhudumiwa ipasavyo kulingana na aina za ulemavu na idadi? Kwa sababu kuna maeneo mengi unakuta kwamba huduma haitolewi ipasavyo kutokana na kwamba taarifa hizi hazipo ama hazijafika na yamkini hawana uelewa wa uwepo wa taarifa hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA**: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Ikupa kwa juhudi zake za ufuatiliaji wa mambo mbalimbali kwa watu ama ndugu zetu wenye ulemavu. Mafunzo ya njia ya maandishi kwa nukta nundu, Serikali imeshirikiana na vyama vyao na tayari wameshaanza kutafsiri kwa lugha zao ambazo zinahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kanzidata itazinduliwa tarehe 08, Mwezi wa Sita mwaka huu, niwaombe ama niwakaribishe wale wadau wote kuhudhuria katika tukio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili; Serikali inaendelea kutoa elimu katika ngazi na makundi mbalimbali wakiwemo ndugu zetu wenye ulemavu. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba watakuwa wanapata huduma kulingana na idadi yao kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Nina tangazo la wageni walioko Bungeni asubuhi hii na tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha; yupo Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ambaye ni Spika Mstaafu na Kamishna wa Sensa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bi. Jenifa Omolo - Naibu Katibu Mkuu, Huduma za Hazina, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Bwana Elijah Mwandumbya - Naibu Katibu Mkuu, Usimamizi wa Uchumi; Bi. Amina Shaaban - Naibu Katibu Mkuu, Usimamizi wa Fedha za Umma; Bwana Emmanuel Tutuba - Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; Bwana Alphayo Kidata - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Bi. Wendy Massoy - Naibu Mkaguzi Mkuu, Ukaguzi wa Serikali Kuu kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG);* Dkt. Albina Chuwa - Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Bwana Arafat Haji - Mtendaji Mkuu wa Benki ya Watu wa Zanzibar; Bwana Ernest Maduhu Mchanga - Katibu wa Tume ya Pamoja ya Fedha; Bi. Fatma Simba - Kamishna Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Dkt. Baghayo Saqware - Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima; Bi. Khadija Said - Naibu Kamishna Mamlaka ya Usimamizi wa Bima; Bi. Lilian Mbassy - Mtendaji Mkuu Benki ya *TIB*; Bwana Frank Nyabudenge ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Bwana Adam Charse Mihayo - Mkurugenzi Mkuu Benki ya Biashara Tanzania. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Bwana Kaimu Abdi Mkeyenge - Mkurugenzi Mkuu Shirika la Bima la Taifa; Ndugu Eliakim Maswi - Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; Profesa Geraldine Rasheli - Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini; Ndugu James Mahanga Sando - Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Rufaa za Zabuni; Bwana Geofrey Malekano - Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania; Bwana James Mbalwe - Mkuu wa Taasisi ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania na Mheshimiwa Bahati Ndeserua - Katibu Bodi ya Rufani za Kodi. *(Makofi)*

Wengine ni *CPA*. Nicodemus Mkama - Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana; Dkt. Leonada Mwagike - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; Bi. Dorothy Mwanyika - Mwenyeliti wa Bodi ya Wakala wa Ununuzi na Ugavi Serikalini; Bwana Godfred Mbanyi - Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi na Bwana Erastus Vicent Mtui - Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi. *(Makofi)*

Pia yupo Bi. Mariam Juma Hamad, mke wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamad Chande, karibu sana. (*Makofi)*

Yupo pia Bi. Rahma Jamal Sharif, mdogo wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni watumishi kutoka *Heart Team Africa Foundation*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge, tusikilizane kidogo, bado nimesimama.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni watumishi kutoka *Heart Team Africa Foundation* inayofanya shughuli zake kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na hawa ni Dkt. George Longopa, Daktari Bingwa, Mkuu wa Idara ya Tiba *JKCI*, Ndugu Linda Gideon, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu - *Heart Team Africa Foundation*, Ndugu Abdulrahman Muya - Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu *JKCI* na Ndugu Irene Mbonde, Kaimu Mkuu wa Mawasiliano, *Heart Team Africa Foundation*. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 16 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni wahitimu wenzake wa Shahada ya Sheria mwaka 1986 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa wameshashika nyadhifa mbalimbali Serikali na baadhi yao wameshastaafu na hii haina uhusiano na Mheshimiwa Rweikiza kustaafu Bunge. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kati yao yupo Ndugu Esaka Mugasa ambaye ni Kamishna wa Polisi Mstaafu, yuko pia Mheshimiwa Sirilius Matupa - Jaji Mstaafu, yuko pia Mheshimiwa Julius Mallaba - Jaji Mstaafu. Wengine hawa wanaendelea na kazi zao kama mawakili, hawa ni mawakili wa kujitegemea, yuko Ndugu Sabasaba Mashiku, Ndugu Christian Rwegoshora, Ndugu Agricola Magoho, Ndugu Christina Kimale, Ndugu Protase Ishengoma, Ndugu John Kalinjuna na Ndugu Francis Nkoka. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine, wageni 13 wa Mheshimiwa Hamad Chande ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na hawa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Jimbo la Kojani - Wete kutoka Kaskazini Pemba Zanzibar,

wakiongozwa na Ndugu Said Shaame ambaye ni Katibu wa Mbunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Selemani Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na huyu ni Afisa Udahili Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambao ni marafiki zake kutoka Kahama na Muleba. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Munira Khatib, rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Ramadhan Ighondo, mtoto wake kutoka Singida. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Rose Busiga ambaye ni mchungaji kutoka Kanisa la *EAGT* Vwawa, Mbozi Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Dorothy Kilave ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni mwimbaji wa nyimbo za injili kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni wafanyakazi kutoka *MUCOBA Bank*. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Asia Halamga ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na hawa ni watumishi kutoka Taasisi ya *Foundations for Ambassador Gender Development Initiative*. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambao ni walimu na wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Oysterbay, Kawe Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 92 na walimu nane kutoka Shule ya ya Awali na Msingi *Zabikha Islamic* ya Kinyerezi, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 92 na walimu 14 kutoka *Camaldolese Nuns of Mafinga,* Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanafunzi 59 na walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi Bahari kutoka Kunduchi Mtongani, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao, tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 76 kwa jambo ambalo limetokea leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikitoa majibu kwa swali namba 518, ambalo lilihusu wastaafu kutakiwa kujilipia malimbikizo ya madeni ambayo muajiri unakuta hajapeleka, ili waweze ku-*qualify* kupewa mafao yao. Sasa Serikali imesema kwamba, ni suala jipya na wakaomba walichukue.

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia suala hili limekuwa likizungumzwa sana hapa kwenye michango mbalimbali wakati wa bajeti kwa miaka mitatu mfululizo na mpaka limeweza kushikiwa shilingi na Wabunge mbalimbali wakachangia, lakini

pia, hata maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa, tumeshtushwa sana, siyo tu kwa kada ya walimu kama alivyouliza Mbunge mwenzetu hapa, bali ni wafanyakazi mbalimbali wamekuwa wakilazimika kujilipia, ili waweze ku-*qualify* kwa ajili ya kupewa mafao yao. Tuna *evidence* kwa kada mbalimbali kama maaskari, wauguzi na wengine wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimesimama kuomba Mwongozo wako, kama tutakuwa tunawasilisha mambo mbalimbali ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi na Serikali na Serikali inakuwa inaahidi kwenye Bunge lako Tukufu hapa kupitia *Hansard*, lakini leo wanakuja wanasema kwamba, ni jambo jipya. Kwa kweli, inatia walakini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka uweze kutoa Mwongozo wako kwa jambo kama hili ambapo Serikali inasema ni suala jipya wakati limeshazungumzwa mara kadhaa. Ni nini kinaweza kufanyika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Serikali. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge, namheshimu sana. Ninadhani angefuatilia vizuri maelezo ambayo tulikuwa tunayatoa wakati wa kujibu lile swali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza la kimsingi ni swali lile la nyongeza lilikuwa ni swali ambalo halihusiani na swali la msingi ambalo lilikuwa limewekwa na kujibiwa na ndiyo maana ulilihamisha swali hilo kutoka kwenye Wizara iliyokuwa inajibu na kulileta Ofisi ya Waziri Mkuu, eneo ambalo linashughulika na masuala ya pensheni. Tukamwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza tulikiri siyo utaratibu, lakini tukaomba Mheshimiwa Mbunge atupe ushirikiano, ili Wizara ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, inayoshughulika na masuala ya pensheni ipate nafasi ya kulishughulikia suala hilo kwa umakini na kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umetupa maelekezo na tumeyapokea. Kwa hiyo, kama tatizo hili bado lipo linaendelea kujitokeza Serikali iko tayari kulifanyia kazi, lakini kipindi hiki chote ambacho tunaendelea na utendaji kazi siyo kwamba, matatizo haya Serikali imekuwa haiyashughulikii, imekuwa ikiendelea kuyashughulikia. Tuko tayari kuendelea kuyashughulikia kila yanapojitokeza na ikiwezekana kuendelea kutoa maonyo kwa Watumishi wa Serikali wanaowalazimisha Watumishi wa Umma kulipa hiyo fedha wakati ni kinyume cha utaratibu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali iko makini kwenye jambo hili na imeendelea kuchukua hatua. Mara kadhaa mmewasikia Waheshimiwa Mawaziri wakikemea jambo hili na hata leo tumelisema Bungeni. Tutaendelea kuchukua hatua na kutoa taarifa kama Bunge lako litaona kwamba, inatupasa tufanye hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Esther Matiko hapa akiomba Mwongozo juu ya jambo ambalo limetokea hapa Bungeni kuhusu majibu yaliyotolewa baada ya Mheshimiwa Ally Kassinge, ambaye alikuwa na Swali la Msingi Namba 518, kuuliza Maswali ya Nyongeza. Aliuliza maswali ya nyongeza mawili na swali mojawapo nikasema liko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na linapaswa kushughulikiwa na Mheshimiwa Waziri, ambaye chini yake ndiyo kuna ile mifuko.

Sasa kwa namna Mheshimiwa Kassinge alivyouliza swali lake, liliashiria kuna watumishi, kwanza mwanzoni nilielewa kama kuna mtumishi ambaye alilazimika kuulipa mfuko madeni ambayo mwajiri hakupeleka, ili yeye aweze kulipwa mafao yake. Baadaye nilipomuuliza zaidi, akasema huyo aliyemtaja ni wa mfano, lakini ni wengi. Kwa hiyo, nikamwambia awapelekee Serikali kwa kutambua kwamba, Mheshimiwa Waziri anayehusika na hilo eneo hakuwepo kwa sababu, la sivyo, ningemuuliza yeye mwenyewe hapa ndani. *(Makofi)*

Sasa kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, hili jambo limewahi kujitokeza huko nyuma na kwamba, baadhi ya Wabunge wamewahi kupata nafasi ya kuchangia

kwamba, mifuko kwa namna moja au nyingine inawadai waajiriwa walipe mchango wa mwajiri, ili walipwe mafao yao. Sasa jambo hilo haliruhusiwi. *(Makofi)*

Mtakumbuka kuna wakati hapa nilisema, Serikali iangalie namna ya huyu mstaafu ambaye anacheleweshewa malipo, kama ambavyo michango ikicheleweshwa kupelekwa kwenye mifuko, Sheria inasema italipwa kwa riba. Vilevile huyu anayecheleweshewa na yeye alipwe kwa riba kwa sababu, inachelewa sana. Sasa Sheria hiyo bado hatujaletewa, naamini Serikali inaendelea kulifanyia kazi hilo. *(Makofi)*

Sasa jambo hili Mheshimiwa Jenista alieleza awali nilipomsimamisha akasema, wamelichukua, apelekewe majina na nimemwona Mheshimiwa Mbunge akiwa amepeleka majina pale kuashiria kwamba, yamepokelewa, lakini kama ni tatizo ambalo lipo kwa ukubwa ambao umeelezewa na Mheshimiwa Esther Matiko maana yake linajitokeza hapa na pale la mifuko kuwadai wastaafu malipo. Kwanza wakati huo anakuwa hafanyi kazi, anasubiri malipo, wewe unamwambia alete yale ambayo anadaiwa mwajiri. Sasa yeye anakuwa amejiajiri mwenyewe.

Jambo hili Waheshimiwa Wabunge si rahisi kulitolea Mwongozo kwa sababu, siko na takwimu hapa, lakini nalipeleka hili jambo kwa Kamati yetu ambayo ofisi hii inaripoti kwake, ili waweze kulifuatilia kwa ukamilifu kwa maana ya Serikali kule itapata nafasi ya kupeleka taarifa. Pia, kama iko sababu, waitwe Wakurugenzi hawa wa hii Mifuko yote hapa nchini, ili wakaeleze kule kwenye Kamati ni mazingira gani. Hapa sasa siyo wa Serikali pekee pengine na wa binafsi kwa sababu, mifuko yote iko chini ya ofisi hii, basi waende kule wakaeleze ni mazingira gani wanamdai mwajiriwa fedha. *(Makofi)*

Pia, nadhani tutapata majibu halisi ya hata huu ucheleweshaji wa malipo kwa wastaafu. Kamati yetu itakapolileta hapa ndani, tutajua wanatushauri, Bunge, tufanye maamuzi gani. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, jambo hili linaenda kwenye Kamati yetu na hiyo Kamati itatuletea taarifa wakati ambao

huwa tunasikiliza taarifa za kazi za Kamati. Kwa hiyo Serikali itapeleka majibu kwenye Kamati, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, Jambo la Dharura.

**SPIKA:** Eeh! Mheshimiwa Mulugo. *(Kicheko)*

**JAMBO LA DHARURA**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 54 na 55, lakini kwa sababu ya muda naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, huko Jimboni kwangu kuna taharuki kidogo, kwanza naishukuru Serikali kwa kuboresha Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa kutumia Mfumo wa *TMX*. Nasi tumeukubali na tunaendelea vizuri, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna baadhi ya wanunuzi ambao *last week* tarehe 27, tumefanya mnada vizuri kwa kutumia Mfumo wa *TMX,* lakini mpaka hivi ninavyosema wananchi hawajalipwa fedha takribani shilingi 600,000,000 na huyo mnunuzi hapatikani, ingawa jana Serikali ya Wilaya ya Songwe ilifanya juu chini mpaka wakamkamata, lakini watu wa *TMX* wameamua kutangaza mnada upya ambao ilikuwa ufanyike jana, lakini tukazuia na leo tumezuia kwa sababu, hata bei ikishuka, hatujajua fedha za wananchi itakuwaje? Kwa maana *last week* waliuza kilo moja kwa shilingi 3,811. Shida iliyopo ni kwamba, kuna taharuki kwa wananchi, hawajui, wanasubiri fedha na yule mtu hajalipa fedha. Naomba Serikali inisaidie.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Mulugo hapa akitumia Kanuni ya 54 kuwa, ana jambo la dharura. Anaeleza udharura huo kwamba, huko jimboni kwake kuna mnunuzi ambaye kwa utaratibu ule uliopo sasa, amefuata huo utaratibu, amechukua mazao ya wananchi, lakini hajawalipa bado. Sasa, anaeleza kwamba, hawana uhakika, sasa si

wameshauza na hili jambo ni la kibiashara jamani, sasa hawana hakika na nini? Kwa sababu, mimi sijui taarifa za ziada kuhusu jambo hili, yaani ni kwa nini unataka Bunge lifanye maamuzi kuhusu jambo hili?

Nadhani kuna ule utaratibu wa kawaida na kwa maelezo uliyoyasema, umefuatwa. Kama ule utaratibu umefuatwa, hela zidaiwe kwa ule utaratibu ambao huwa unafuatwa. La ziada ambalo unataka Bunge lifanye sijalisikia. Yaani ni kwa nini lije hapa Bungeni kama Hoja ya Dharura?

Yaani jambo gani ambalo limefanyika tofauti na kawaida, ambalo ungetaka Bunge hili sasa lifanye maamuzi ambayo ni ya udharura? Nakuruhusu usimame.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, kawaida ya minada, unatangaza bei, wiki iliyopita kilo ilikuwa ni shilingi 3,811 kwa Mfumo wa *TMX*. Sasa baada ya fedha kutokupatikana na huyo mnunuzi kama vile amekuwa tapeli, amewatapeli wananchi na amekamatwa na hana uwezo wa kulipa fedha. Sasa *TMX* wametangaza mnada mwingine kwa mazao yaleyale. Sasa, je, bei ikishuka na mwananchi hajui chochote na anadai fedha, itakuwaje? Naomba Bunge lijadili mnisaidie jambo hili.

**SPIKA:** Sawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mulugo, kwa sababu hata wewe katika maelezo yako hapo hauashirii kama vile unajua bei ambayo itauzwa, pengine itafika shilingi 5,000 ama itafika shilingi 2,000, je, tutarudi hapa tena kujadili kwamba, bei imepanda au imeshuka? Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge jambo hili halitimizi masharti yaliyoko kwenye Kanuni ya 55. Kwa hiyo, liendelee kwa utaratibu wake wa kawaida, pale ambapo litatimiza masharti ya Kanuni yetu ya 55, basi tutaweza kulijadili hapa ndani. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namuita sasa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ili aje awasilishe Hoja ya Wizara yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kabla sijasema, naanza kwa kuipongeza sana Timu ya Yanga kwa kupata makombe yote ikiwa imeongeza kombe lingine Jumapili. Yanga wamejua kutupa raha mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya mafungu nane ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu, kwa kunijalia uzima na afya njema na kuniwezesha kusimama hapa kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge, punguzeni sauti kidogo, tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa

Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, kumsaidia kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba, hususan katika usimamizi wa fedha za umma pamoja na uchumi jumla. Tunapenda kumhakikishia kuwa, jukumu la usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla lipo salama.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kulisimamia kikamilifu ikiwemo ukusanyaji, utafutaji na ugawaji wa rasilimali fedha kwenye miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na huduma za jamii, ili kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa Watanzania. Tunamwombea afya njema, hekima na busara katika kubadilisha fikra, mifumo na mwelekeo wa Taifa letu kwa kuendelea kuleta maendeleo endelevu na jumuishi kwa watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa hekima, busara na weledi wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa weledi, umahiri na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama – Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika – Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini katika kutekeleza majukumu yao ya kukusaidia wewe na Mheshimiwa Naibu Spika katika kuliongoza Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata heshima ya kuteuliwa kushika nafasi mbalimbali katika kipindi cha Juni, 2023 hadi Mei, 2024. Waheshimiwa Wabunge hao ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya

Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Oran Manase Njeza – Mbunge wa Mbeya Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe – Mbunge wa Kibiti kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo. Aidha, nawashukuru pia, wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kupokea, kuchambua, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2024/25.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wao umekuwa na tija katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Kwa niaba ya Wizara ya Fedha na taasisi zake, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, tutaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa Pamoja, ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi waliotupatia dhamana ya kusimamia masuala ya kisera katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa yangu yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. Vilevile, naomba kukumbusha kuwa, hii ni Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, Bajeti Kuu ya Serikali itakuja tarehe 13, kama ulivyoiweka kwenye ratiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nijielekeze kwenye hoja iliyo mbele yetu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu matatu ambayo ni, Muhtasari wa Majukumu ya Wizara, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2023/24 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25, ikijumuisha vipaumbele vya Wizara na Taasisi zake pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muhtasari wa Majukumu ya Wizara pamoja na eneo la kwanza la Kitabu cha Hotuba baada ya Utangulizi, vinapatikana katika Ukurasa wa 7. Ninaomba hotuba yangu yote, kama nilivyosema, iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2023/24, mafungu nane ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 15.87, kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 15.31 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 556.38 ni matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo ikiwa ni shilingi trilioni 13.62 ikiwemo huduma ya deni la Serikali ambayo ni shilingi trilioni 10.48 na matumizi ya mishahara ikiwa ni shilingi trilioni 1.69. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani ikiwa ni shilingi bilioni 482.55 na fedha za nje ikiwa ni shilingi bilioni 73.82.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 97.13 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ikiwa ni shilingi bilioni 87.72 na matumizi ya maendeleo ikiwa ni shilingi bilioni 9.4. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi bilioni 70.83 na mishahara ikiwa ni shilingi bilioni 16.89. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 8.83 na fedha za nje shilingi bilioni 583.88.

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizopokelewa kwa mafungu nane ya Wizara ya Fedha hadi Aprili, 2024, ni shilingi trilioni 11.90 sawa na 75% ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, matumizi halisi yalifikia shilingi trilioni 11.27 sawa na 95% ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo kwa idara, vitengo na taasisi ilikuwa shilingi trilioni 2.07, huduma ya deni la Serikali ilikuwa ni shilingi trilioni 8.48, mishahara ilikuwa ni shilingi bilioni 334.48 na kwa upande wa maendeleo ilikuwa ni shilingi bilioni 383.68. Vilevile hadi Aprili, 2024 Fungu 45 limepokea jumla

ya shilingi bilioni 81.45 sawa na 84% ya makasio ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 39.79, kati ya makadirio yote ya Serikali ya kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44.39 kwa mwaka 2023/2024. Kati ya kiasi hicho Fungu 21 lilitarajiwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 39.74 ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 26.73, Idara ya Fedha za Nje shilingi trilioni 5.47 na Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali shilingi trilioni 7.54.

Mheshimiwa Spika, Fungu 23 ilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 60 na Fungu 50 shilingi milioni 300. Hadi Aprili, 2024 Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 32.49 sawa na ufanisi wa 82% ya leo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya shilingi trilioni 21.31, Idara ya Fedha za Nje shilingi trilioni 4.92, Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali trilioni 6.18 na maduhuli kupitia Fungu 23 shilingi bilioni 79.23 na Fungu 50 shilingi milioni 950.

Mheshimiwa Spika, kupitia Fungu 001, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 10.48 kwa ajili ya kuhudumia deni ya Serikali pindi linapoiva, hadi Aprili, 2024 Wizara imelipa kwa *notice* za madai deni lililoiva jumla ya shilingi trilioni 8.48 sawa na ufanisi wa asilimia 81 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.63 ikijumuisha riba ya shilingi trilioni 1.98 na mtaji shilingi trilioni 2.65 na deni la nje ni shilingi trilioni 3.83 ikijumuisha riba ya shilingi trilioni 1.34 na mtaji shilingi trilioni 2.49.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024 Wizara ilipanga kufanya tafiti nne kwenye maeneo ya maendeleo ya Sekta ya Fedha na Uchumi jumla, ili kuwezesha maamuzi ya kisera. Aidha, Wizara ilitarajiwa kufanya tathmini ya huduma za Wizara kwa wadau na mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024. Hadi Aprili 2024 Wizara imefanikiwa kukamilisha tafiti mbili ikiwa ni sawa na 50% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imekamilisha tathmini ya huduma za Wizara kwa wadau, Mapitio ya Utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango Pamoja na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024 Wizara ilipanga kuboresha Mfumo wa Uhasibu Serikali *(MUSE),* kuboresha mfumo wa usimamizi wa bajeti *(CBMS),* kuunganisha mfumo wa *MUSE* pamoja na mifumo mingine ya usimamizi wa fedha za umma, kuboresha mfumo wa usimamizi wa mali za Serikali *(RE-GAMIS),* kuunganisha Balozi kumi za Tanzania katika mfumo wa *MUSE,* kuunganisha taasisi mpya na mfumo wa *MUSE* na kuzijengea uwezo taasisi katika kutumia mifumo ya usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara imefanikiwa kuboresha Mfumo wa *CBMS* ili kuongeza ufanisi katika kudhibiti mipango na bajeti ya Serikali, kuunganisha mfumo wa *MUSE* katika Balozi zetu saba za Tanzania katika nchi ya Ufaransa, Australia, Ujerumani, Uturuki, Uingereza, China pamoja na Uswiss na kuboresha moduli tano za mfumo wa *GAMIS*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imetoa mfumo wa matumizi kwa Taasisi za umma 269, kazi nyingine zinazoendelea ni kuwezesha Taasisi za umma 477 kuandaa taarifa za hesabu za fedha kwa kutumia mfumo *(MUSE)* na kuwajengea uwezo watumiaji wa Mfumo wa *MUSE* katika Balozi zetu 17.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kupokea maoni na mapendekezo mbalimbali kwa wadau kuhusu umuhimu wa elimu ya huduma za fedha kwa umma katika kukuza shughuli za kiuchumi na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara imeanza utekelezaji wa mkakati wa utoaji wa elimu ya fedha vijijini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya elimu ya fedha kwa umma ya mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, makundi yaliyopewa kipaumbele katika zoezi letu linaloendelea la elimu ya fedha kwa umma ni wajasiriamali wadogo, wanawake, vijana, watu wenye mahitaji maalum na waajiriwa kwa kuwa ni makundi yaliyoathirika zaidi katika mikopo iliyojulikana kama Mikopo ya Kausha Damu. Maeneo yaliyofikiwa hadi sasa ni Halmashauri za Mikoa ikiwemo Mikoa ya Manyara, Singida pamoja na Kagera.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa elimu ya fedha kwa wananchi wetu ni zoezi endelevu. Hivyo, elimu itaendelea kutolewa na kuboreshwa kulingana na mazingira, mahitaji pamoja na maoni ya wadau wetu. Aidha, kwa sisi Wabunge, tukiwa kama sehemu ya jamii, tunaweza kuendelea kutembelea mtandao wetu wa elimu ya fedha kwa umma kupitia *website* kama ambavyo imeoneshwa kwenye hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliendelea kufanya mapitio ya kuboresha miundo ya kitaasisi ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Aprili, 2024 Wizara ilifanikiwa kuanzisha kituo cha ubia kati ya sekta ya umma pamoja na sekta binafsi, ofisi ya akaunti ya changamoto za milenia pamoja na kuzindua na kuwezesha taasisi za suluhisho la malalamiko pamoja na taarifa za kodi kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha taasisi hizo ni kuimarisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya Serikali pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara hapa nchini hususan kuondoa au kupunguza vikwazo vya kibiashara na malalamiko kwa walipakodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kuchagua eneo la ushirikiano na Shirika la Changamoto za Milenia ya Marekani *(MCC)* ambapo pamoja na mambo mengine, msaada utatolewa na Shirika hilo utakaotumika kutekeleza programu za maendeleo zinazolenga kupunguza ama kuondoa vikwazo vya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalumu, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA ikiwemo pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya ofisi na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi mikoani.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024 ofisi imefanya kaguzi 1,450 ikijumuisha kaguzi za Serikali Kuu 537, Mamlaka za Serikali za Mitaa kaguzi 625, Mashirika ya Umma kaguzi 215, ukaguzi wa ufanisi 14, kiufundi 10, kiuchunguzi saba, maalumu 12 na mifumo ya TEHAMA kaguzi 30. Aidha, ofisi imekamilisha kuandaa ripoti jumuishi sita za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinazowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Machi 28, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024, Wizara ilikabiliana na changamoto zifuatazo: Moja, ilikuwa ni huduma hafifu ya matengenezo ya mashine za *EFD,* kukosekana kwa mtandao na mwamko mdogo wa wananchi kudai na kutoa risiti za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ilikuwa ni kuongezeka kwa mahitaji ya ziada ya rasilimali fedha kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo masuala ya mafuriko na tatu ilikuwa ni baadhi ya walipa kodi kuficha taarifa za miamala ya kibiashara na kuendelea kuwepo kwa biashara za magendo, hususan mipakani na mwambao wa bahari.

Mheshimiwa Spika, njia ya kukabiliana na changamoto hizo imekuwa ni kuimarisha matumizi ya mfumo wa *Virtual Fiscal Devices,* kutoa risiti kama mbadala wa mashine za *EFD,* kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudai na kutoa risiti kwenye biashara wakati wa matumizi ya kielektroniki, kuimarisha soko la ndani la fedha na kufanya mapitio ya mpango na bajeti kugharamia mahitaji ya ziada na kurejesha miundombinu iliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapendekezo ya mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara na Fungu 45, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/2024 sasa napenda kuwasilisha mapendekezo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vipaumbele itakuwa ni kutafuta na kukusanya fedha, mapato ya shilingi trilioni 44.19 kati ya maoteo yote ya Serikali ya kukusanya jumla ya shilingi trilioni 49. Kipaumbele kingine ni kuimarisha na kusimamia mifumo ya mapato na matumizi pamoja na mali za Serikali ikiwemo *IDRAS, TANCIS, MUSE, NeST, CBMS* pamoja na *GAMIS*.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhudumia deni la Serikali kwa wakati na kuboresha kanzidata ya kutunza taarifa za deni; nne, ni kutoa elimu ya huduma za fedha kwa wananchi kwa lengo la kukuza huduma ujumuishi fedha hapa nchini; na tano, ni kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani, Kamati za Ukaguzi pamoja na Waratibu wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2024 vipaumbele ni kama ifuatavyo: Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2023/2024; kufanya ukaguzi wa kiufundi, ufanisi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA; kufanya kaguzi maalumu na kiuchunguzi kulingana na mahitaji; kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga na kukarabati ofisi za mikoa; na kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi na za Kisekta ili kuwa na uelewa wa pamoja wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato, kati ya shilingi trilioni 49.35 zinazokadiriwa kukusanywa na Serikali kwa mwaka 2024/2025, Wizara ya Fedha imekadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44.19. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 29.42, misaada na mikopo nafuu shilingi trilioni 5.13, mikopo ya

kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje shilingi trilioni 9.60 na maduhuli shilingi bilioni 45.01.

Mheshimiwa Spika, aidha, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inakadiriwa kukusanya shilingi milioni 850 ikiwa ni mapato ya kodi ya pango kutokana na upangishaji wa majengo ya Ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi kwa mwaka 2024/2025, Wizara ya Fedha inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 18.17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu nane ya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 17.63 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha huduma ya deni la Serikali ambalo ni shilingi trilioni 13.13, mishahara shilingi bilioni 946.45, matumizi mengineyo shilingi bilioni 937.30 kwa mafungu ya Wizara na Taasisi zake, Huduma za Mfuko Mkuu shilingi trilioni 2.61 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 544.05.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iidhinishiwe jumla ya shilingi bilioni 112.73 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 101.26 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11.47 ni matumizi ya maendeleo. Mchanganuo huo wa matumizi kwa mafungu nane ya kibajeti ya Wizara ya Fedha na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi unapatikana ukurasa wa 69 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuhitimisha hoja yangu, na kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chande ni *two in one,* ametosheleza Wizara na anafanya majukumu yangu yawe mepesi katika utekelezaji wake. Aidha, nawashukuru sana

Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi zake wakiongozwa na Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Naibu Katibu Mkuu, Bi. Amina Shaaban; Bi. Jenifa Omolo na Bw. Elijah Mwandumbya kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Wakuu wa Idara, vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na taasisi zake, kwa ushirikiano na utekelezaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku. Ahsanteni sana na kazi iendelee.

Mhehimiwa Spika, kwa wale wapigakura wa Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri wasihangaike kutafuta mgombea mwingine, Naibu Waziri anatosha na analisaidia Taifa katika mujukumu yake anayopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu pamoja na Waheshimiwa Wabunge pamoja na umma wa Watanzania kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Fedha ambayo ni *www.mof.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB,), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango na

Bajeti ya mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25.

**2. *Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana hapa kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25.

**3. *Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuamini mimi na Naibu Waziri Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb,), kumsaidia kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, hususan katika usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla. Tunapenda kumhakikishia kuwa, jukumu la usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla lipo salama na tutaendelea kusimamia kikamilifu ukusanyaji, utafutaji na ugawaji wa rasilimali fedha kwenye miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na huduma za jamii ili kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Tunamwombea afya njema, hekima na busara katika kubadilisha fikra, mifumo na mwelekeo wa Taifa letu kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya watanzania.

**4. *Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb,), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb,), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa hekima, busara na weledi wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kikatiba.

**5. *Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa weledi, umahiri na uadilifu. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama – Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip

Mwanyika – Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Ninawaahidi ushirikiano thabiti katika utekelezaji wa majukumu yao ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuongoza vikao vya Bunge.

**6. *Mheshimiwa Spika,*** pia, nawapongeza waheshimiwa wabunge waliopata heshima ya kuteuliwa kushika nafasi mbalimbali serikalini kati ya Juni 2023 na Mei 2024. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb,), Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb,), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi (Mb,), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba (Mb,), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb,), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**7. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Oran Manase Njeza – Mbunge wa Mbeya Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe – Mbunge wa Kibiti kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, ninawashukuru pamoja na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kupokea, kuchambua, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2024/25. Maoni na ushauri wao umekuwa na tija katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru waheshimiwa wabunge kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika utekelezaji wa majukumu ya wizara na Serikali kwa ujumla. Kwa niaba ya wizara na taasisi zake, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, tutaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi waliotupa dhamana ya kusimamia masuala ya kisera katika Taifa letu.

**8. *Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge na watanzania wote kwa ujumla, kufuatia

vifo vya viongozi wetu wastaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina. Aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Vilevile, nitoe pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na watanzania wote walioondokewa na wapendwa wao pamoja na uharibifu mkubwa wa mali kutokana na majanga mbalimbali ikiwemo maporomoko ya udongo yaliyotokea Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara na mkoani Mbeya; mafuriko yaliyotokea katika wilaya za Kibiti na Rufiji mkoani Pwani; wilaya ya Malinyi, Ulanga, Mlimba na Halmashauri ya Mji Ifakara mkoani Morogoro; jijini Arusha pamoja na maeneo mengine katika mikoa mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nijielekeze kwenye hoja iliyo mbele yetu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni: Muhtasari wa Majukumu ya Wizara; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24; na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25 ikijumuisha vipaumbele vya Wizara na Taasisi zake pamoja na makadirio ya mapato na matumizi.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 619A la tarehe 30 Agosti 2023, Wizara ya Fedha imekasimiwa majukumu ya kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi; kusimamia miongozo ya usimamizi wa fedha na mali za Serikali; kuratibu upatikanaji wa fedha na kuimarisha uhusiano wa masuala ya fedha kwa taasisi za kikanda na kimataifa; kuandaa na kusimamia miongozo na utekelezaji wa bajeti ya Serikali; kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu

wanaolipwa na Hazina; kuendeleza sekta jumuishi ya fedha; kufuatilia na kutathmini programu za kuondoa umaskini; kudhibiti utakasishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi; kusimamia masuala ya pamoja ya fedha kati ya SMT na SMZ; kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi; kusimamia michezo ya kubahatisha; na kutoa mafunzo ya masuala ya fedha, ununuzi, takwimu na mipango.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

### 3.1 Mwenendo wa Matumizi hadi Aprili 2024

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 15.87 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 15.31 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 556.38 matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi trilioni 13.62, ikiwemo huduma ya deni la Serikali shilingi trilioni 10.48 na matumizi ya mishahara shilingi trilioni 1.69. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 482.55 na fedha za nje shilingi bilioni 73.82.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi liliidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 97.13 kwa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida shilingi bilioni 87.72 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 9.41. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo shilingi bilioni 70.83 na mishahara shilingi bilioni 16.89. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 8.83 fedha za nje shilingi milioni 583.88.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya fedha zilizopokelewa kwa mafungu nane (8) ya wizara hadi Aprili 2024 ni shilingi trilioni 11.90, sawa na asilimia 75 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, matumizi halisi yalifikia shilingi trilioni 11.27, sawa na asilimia 95 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo kwa idara, vitengo na taasisi yalikuwa shilingi trilioni 2.07, huduma ya deni la

Serikali shilingi trilioni 8.48, mishahara shilingi bilioni 334.48 na maendeleo shilingi bilioni 383.68. Vilevile, hadi Aprili 2024, Fungu 045 limepokea jumla ya shilingi bilioni 81.45, sawa na asilimia 84 ya makisio ya mwaka 2023/24. Matumizi halisi yalifikia shilingi bilioni 77.52, sawa na asilimia 95 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yalikuwa shilingi bilioni 57.54, mishahara shilingi bilioni 15.55 na shilingi bilioni 4.43 zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilipokelewa na kutumika kwa kila fungu ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na.1 – 3.

### 3.2 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

#### 3.2.1 Kukusanya na Kutafuta Mapato ya Jumla ya Shilingi Trilioni 39.79

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 39.79, kati ya makadirio yote ya Serikali ya kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44. 39 kwa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, Fungu 21 lilitarajiwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 39.74 ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 26.73, Idara ya Fedha za Nje shilingi trilioni 5.47 na Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali shilingi trilioni 7.54; Fungu 23 lilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 60; na Fungu 50 shilingi milioni 300. Hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 32.49, sawa na ufanisi wa asilimia 82 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya shilingi trilioni 21.31, Idara ya Fedha za Nje shilingi trilioni 4.92, Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali shilingi trilioni 6.18 na maduhuli kupitia Fungu 23 shilingi bilioni 79.23 na Fungu 50 shilingi milioni 950.

#### 3.2.2 Kuhudumia Deni la Serikali

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Fungu 001, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 10.48 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali pindi linapoiva. Hadi Aprili 2024, wizara imelipa kwa wakati notisi za madai ya deni lililoiva jumla ya shilingi trilioni 8.48, sawa na ufanisi wa asilimia 81 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi

hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.63, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.98 na mtaji shilingi trilioni 2.65, na deni la nje ni shilingi trilioni 3.83, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.34 na mtaji shilingi trilioni 2.49.

### 3.2.3 Kufanya Tafiti, Tathmini na Mapitio ya Kitaalamu Kuhusu Mifumo ya Usimamizi wa Uchumi, Mipango na Bajeti ya Serikali

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kufanya tafiti nne (4) kwenye maeneo ya maendeleo ya sekta ya fedha na uchumi jumla ili kuwezesha maamuzi ya kisera. Aidha, wizara ilitarajia kufanya tathmini ya huduma za wizara kwa wadau na mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24. Hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kukamilisha tafiti mbili (2), sawa na asilimia 50 ya lengo la mwaka. Aidha, wizara imekamilisha tathmini ya huduma za wizara kwa wadau, mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24 pamoja na kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

### 3.2.4 Kuboresha na Kuunganisha Mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kuboresho Mfumo wa Uhasibu Serikalini - MUSE; kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti - CBMS; kuunganisha mfumo wa MUSE na mifumo mingine ya usimamizi wa fedha za umma; kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali - GAMIS; kuunganisha Balozi 10 za Tanzania katika mfumo wa MUSE; kuunganisha taasisi mpya na mfumo wa MUSE; na kuzijengea uwezo taasisi katika matumizi ya mifumo ya usimamizi wa fedha za umma.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuboresha mfumo wa CBMS ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa mipango na bajeti ya Serikali, kuunganisha mfumo wa MUSE

katika balozi saba (7) za Tanzania katika nchi ya Ufaransa, Austria, Ujerumani, Uturuki, Uingereza, China na Uswisi na kuboresha moduli tano (5) za mfumo wa GAMIS. Aidha, wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa GAMIS kwa taasisi za umma 269. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kuwezesha taasisi za umma 477 kuandaa taarifa za hesabu za fedha kwa kutumia mfumo wa MUSE, kuwajengea uwezo watumiaji wa mfumo wa MUSE katika balozi 17 za Tanzania na kuunganisha mfumo wa MUSE kwenye taasisi za umma 15.

### 3.2.5 Kujenga Uwezo wa Watumishi katika Usimamizi wa Masuala ya Fedha

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani katika sekta ya umma ili kuendana na viwango vya kitaaluma vya kimataifa - Certified Internal Auditor (CIA) na Certified Information System Auditor (CISA); kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani katika taasisi za umma kuhusu matumizi ya mfumo wa ukaguzi - Government Internal Audit Management Information System (GIA MIS); kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani katika maeneo ya ukaguzi wa taarifa za fedha na mchakato wa ukaguzi unaozingatia vihatarishi; kujenga uwezo wa maafisa masuuli na wenyeviti wa kamati za ukaguzi kuhusu mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani katika taasisi za umma; na kuwajengea uwezo waratibu wa usimamizi wa vihatarishi kuhusu mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani 64 kuhusu viwango vya kitaaluma vya kimataifa vya ukaguzi wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma; kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani 80 kuhusu matumizi ya mfumo wa GIA-MIS; kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani 724 katika ukaguzi wa taarifa za fedha; na kufanya tathmini ya ubora wa ukaguzi kwa taasisi 140. Aidha, katika kipindi hicho, wizara imefanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika halmashauri 22 za mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Manyara. Vilevile, wizara imetoa mafunzo kwa kamati za ukaguzi

katika taasisi za umma 17 pamoja na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi 51.

**21.** ***Mheshimwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kufanya kaguzi maalumu sita (6) ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Maeneo yaliyohusika na kaguzi hizo ni: Mfumo wa usimamizi wa mapato ya VIZA; malimbikizo ya pensheni kwa wastaafu; madai ya mifuko ya hifadhi ya jamii na Shirika la Taifa la Bima – NIC; ruzuku kwa Shirika la Reli la Tanzania na Zambia – TAZARA; na akaunti za mirathi katika mahakama. Kaguzi nyingine za kimkakati zilizofanyika ni Mradi wa Barabara ya Mabasi Yaendayokasi Awamu ya 4 na 5 katika mkoa wa Dar es Salaam na ufanisi wa miradi nane (8) ya kimkakati katika halmashauri sita (6) Tanzania Bara.

### 3.2.6 Kuboresha Miundombinu ya Ofisi za Wizara na Taasisi zake pamoja na Miundombinu ya Kufundishia na Kujifunzia

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa jengo la wizara katika Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma, ofisi za wizara mkoani Geita, ofisi za Soko la Bidhaa Tanzania na kuwezesha uboreshaji wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia Chuo cha Uhasibu Arusha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika. Hadi Aprili 2024, ujenzi wa jengo la wizara katika mji wa Serikali Mtumba umefikia asilimia 65, jengo la ofisi za wizara mkoani Geita asilimia 64 na usanifu wa jengo la ofisi za Soko la Bidhaa Tanzania umekamilika na mkandarasi wa ujenzi amepatikana. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 12.36 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kujifunzia na kufundishia inayotekelezwa na Chuo cha Uhasibu Arusha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika.

## 3.3 Utekelezaji wa Afua Nyingine

### 3.3.1 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa wa Masuala ya Kikodi

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2023/24, wizara imehitimisha majadiliano ya mikataba minne (4) ya utozaji kodi mara mbili kati ya Tanzania na nchi washirika. Nchi hizo ni Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Kisultani ya Oman, Jamhuri ya Iran na mkataba wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo hatua za kusainiwa kwa mikataba hiyo zinaendelea. Aidha, mkataba wa utozaji kodi mara mbili kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu umesainiwa na utekelezaji wake utaanza Januari 2025. Manufaa ya kuhitimishwa na kusainiwa kwa mikataba hiyo ni kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi husika, kuvutia mitaji kutoka nje, kuongezeka kwa fursa za ajira, kupanua wigo wa fursa za kibiashara na soko la malighafi, bidhaa na huduma zinazozalishwa na wawekezaji wa ndani. Vilevile, hatua iliyofikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 aya ya 46 (b - d).

### 3.3.2 Elimu ya Huduma za Fedha

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara inaendelea kupokea maoni na mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wadau kuhusu umuhimu wa elimu ya huduma za fedha kwa umma katika kukuza shughuli za kiuchumi na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2023/24, wizara imeanza kutekeleza Mkakati wa Utoaji wa Elimu ya Fedha Vijijini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Fedha kwa Umma ya Mwaka 2021/22-2025/26. Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais –TAMISEMI, na taasisi za usimamizi ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Dhamana pamoja na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeunda timu maalumu ya wataalamu kutoa elimu kwa umma, hususan vijijini kwa utaratibu wa semina, warsha, makongamano, filamu, runinga, redio, mitandao ya kijamii na mafunzo kwa waratibu waliopo katika halmashauri zetu.

**25. *Mheshimiwa Spika,*** makundi yaliyopewa kipaumbele katika zoezi letu linaloendelea la elimu ya fedha kwa umma ni wajasiriamali wadogo, wanawake, vijana, watu wenye mahitaji maalumu na waajiriwa kwa kuwa ni makundi yaliyoathirika zaidi na mikopo ijulikanayo kama kausha damu. Maeneo yaliyofikiwa hadi sasa ni halmashauri za mikoa ya Singida, Manyara na Kagera. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, elimu ya fedha kwa wananchi wetu ni zoezi endelevu; hivyo, elimu itaendelea kutolewa na kuboreshwa kulingana na mazingira, mahitaji na maoni ya wadau. Aidha, kwa kuwa sisi wabunge ni sehemu ya jamii, tunaweza kutembelea mtandao wetu wa elimu ya fedha kwa umma kupitia https://www.youtube.com/@MofURT au HAZINA TV kupata elimu ya fedha, na muhimu zaidi kuwa mabalozi wetu wa elimu ya fedha kwa umma.

### 3.3.3 Uhakiki na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

**26. *Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Fedha ni ufuatiliaji na uhakiki wa mahitaji na matumizi ya fedha za umma. Hadi Aprili 2024, wizara imefanya uhakiki wa mapendekezo ya fidia ya jumla ya shilingi bilioni 37.79 kwa wananchi walioridhia kuachia maeneo yao kupisha miradi ya maendeleo. Aidha, wizara imefanya uhakiki wa madai ya fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yaliyotwaliwa na Serikali kwa ajili ya upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Kigoma, Ofisi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na maeneo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika mikoa ya Pwani na Arusha. Vilevile, katika kipindi cha rejea, wizara imetoa nyaraka mbili za udhibiti wa bajeti za mafungu ya kisekta ili kukabiliana na msukumo wa mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan mafuriko. Kadhalika, wizara imeandaa kitabu cha bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 Toleo la Wananchi, na kuandaa taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Serikali kila robo mwaka na kuweka kwenye tovuti ya wizara ili kuongeza uwazi.

### 3.3.4 Uendelezaji wa Soko la Ndani la Fedha

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya fedha, wizara imeendelea kuandaa na kutekeleza miongozo mbalimbali ili kuendeleza soko la ndani la fedha. Kwa mwaka 2023/24, wizara imefanikiwa kuratibu na kuweka sokoni hatifungani ya kijani ya shilingi bilioni 53.12, ikiwa ni hatifungani ya kijani ya kwanza kutolewa na taasisi za umma hapa nchini. Hatua hiyo imefikiwa, ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa njia mbadala. Napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwarobaini wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika taasisi, mashirika na mamlaka za serikali za mitaa umepatikana. Aidha, Wizara ya Fedha iko tayari kushirikiana na taasisi na mashirika ya umma, manispaa pamoja na halmashauri zetu kuandaa nyaraka za matarajio kutafuta fedha kupitia dirisha hili kutekeleza miradi ya kipaumbele bila kutegemea bajeti kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

### 3.3.5 Maboresho ya Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Kitaasisi

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, wizara iliendelea kufanya mapitio na kuboresha miundo ya kitaasisi ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuanzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Ofisi ya Akaunti ya Changamoto za Milenia pamoja na kuzindua na kuwezesha Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi kuanza kutoa huduma. Lengo la kuanzisha taasisi hizo ni kuimarisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mipango ya Serikali pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, hususan kuondoa au kupunguza vikwazo vya kibiashara na malalamiko ya walipakodi. Aidha, wizara imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kuchagua eneo la ushirikiano na Shirika la Changamoto za Milenia la Marekani - MCC ambapo pamoja na mambo mengine, msaada utakaotolewa na shirika hilo utatumika kutekeleza programu za maendeleo zinazolenga kupunguza au kuondoa vikwazo vya kibiashara.

### 3.3.6 Uandaaji wa Miongozo ya iser ana Kisheria

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kuandaa miongozo mbalimbali ya kisera, kisheria na kitaalamu ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; kuhuisha Mpango Mkakati wa Wizara kuendana na mabadiliko ya muundo na mgawanyo wa majukumu ya Serikali; kutunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja na kanuni zake; kuhuisha Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani; na kuandaa Mkakati wa Muda wa Kati wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani (2024/2025 – 2026/2027).

### 3.3.7 Usimamizi wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imetoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia. Ushauri na mafunzo ya kitaalamu yametolewa kwa Wakala wa Barabara Tanzania katika kuandaa nyaraka za mradi wa barabara ya haraka kutoka Kibaha hadi Morogoro (kilomita 205) ambapo hatua za ununuzi wa mbia zinaendelea kwa sehemu ya Kibaha - Mlandizi - Chalinze (kilomita 78.9) na Wakala wa Mabasi Yaendayokasi kuhusu ununuzi wa mbia wa uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayokasi jijini Dar es Salaam. Aidha, mashauriano yanaendelea kuhusu upanuzi na ujenzi wa barabara ya haraka kati ya Morogoro na Dodoma kwa utaratibu wa ubia.

### 3.3.8 Usimamizi wa Mali za Umma

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, jumla ya taasisi za umma 334 zimewezeshwa kuandaa, kuhuisha na kuweka kumbukumbu ya mali zenye thamani ya shilingi trilioni 13.66 katika mfumo wa GAMIS. Aidha, katika kipindi hicho, wizara imetoa vibali 123 vya kuondosha mali chakavu na kuwezesha minada 100 katika taasisi za umma ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.6 zilikusanywa katika minada hiyo. Vilevile, wizara imefanya uhakiki wa mali katika vituo 388 vya Serikali ambapo taarifa zimeandaliwa na mapendekezo kuwasilishwa kwa maafisa masuuli kwa hatua stahiki.

### 3.3.9 Huduma za Mafao ya Kustaafu, Pensheni na Mirathi

**32. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kusimika Mfumo wa Malipo ya Pensheni - TPPS kwenye taasisi tatu (3) na kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo kwa watumiaji 100. Aidha, wizara imeendelea kulipa kwa wakati mafao ya wastaafu wanaolipwa na Hazina kila mwezi na kuwasilisha stahiki ya michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Vilevile, timu ya wataalamu iko mbioni kukamilisha tathmini kuhusu mfumo endelevu wa usimamizi na uboreshaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina.

### 3.3.10 Udhibiti wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi

**33. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imefanikiwa kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu; Kanuni za Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu za mwaka 2023; Amri ya Uteuzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Utakasishaji Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi; na kuanzisha Mfumo wa Taifa wa Takwimu za Udhibiti Utakasishaji Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi.

### 3.3.11 Usimamizi wa Masuala ya Pamoja ya Fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar

**34. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, wizara imekamilisha stadi kuhusu kodi ya zuio katika kampuni na mashirika ya mawasiliano ya simu, benki za biashara na bima zilizosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya biashara katika pande mbili za Muungano. Aidha, uchambuzi wa takwimu kuhusu mwenendo wa mapato na matumizi ya Muungano kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi 2023/24 umekamilika.

### 3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Taasisi

**35. *Mheshimiwa Spika,*** wizara inatekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia taasisi ikijumuisha taasisi za elimu; bodi za kitaalamu

na kitaaluma; taasisi za benki na fedha; taasisi za usimamizi wa kodi, ununuzi na ugavi na michezo ya kubahatisha; uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; na takwimu.

**3.4.1 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, taasisi tano (5) za mafunzo na elimu ya juu zilitarajia kudahili jumla ya wanafunzi 76,272, ikijumuisha ngazi ya astashahada 13,100, stashahada 17,607, shahada 42,337 na shahada ya uzamili 3,228; kuendeleza wahadhiri 210 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili (57) na uzamivu (153); kufanya tafiti 79; na kutoa huduma elekezi 786. Hadi Aprili 2024, taasisi hizo zilidahili jumla ya wanafunzi 75,712, sawa na asilimia 99.3 ya lengo ikijumuisha ngazi ya astashahada 13,778, stashahada 14,654, shahada 42,030 na shahada ya uzamili 5,250. Aidha, jumla ya wahadhiri 180 wamewezeshwa kujiendelezakitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili (44) na uzamivu (136). Vilevile, taasisi zilifanya jumla ya tafiti 48, sawa na asilimia 60.8 ya lengo na kutoa huduma elekezi 142, sawa na asilimia 18.1 ya lengo la mwaka.

**3.4.2 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilipanga kusajili wahasibu na wakaguzi 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kufanya mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa wahasibu na wakaguzi 12,000; kutoa ushauri wa kiufundi kwa taasisi na kampuni 10 kuhusu matumizi ya viwango vya kitaifa na kimataifa katika uandaaji wa hesabu na ukaguzi; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65 za ukaguzi; kufanya mapitio ya mtaala wa uhasibu nchini na kufanya mapitio ya vitabu vya rejea kwa wanafunzi kwa masomo 12; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 12,500; na kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 150.

**38. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Bodi imesajili wanachama 2,237, sawa na asilimia 745 ya lengo la mwaka katika ngazi mbalimbali za uhasibu na ukaguzi; imetoa mafunzo kuhusu uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi kwa wahasibu na wakaguzi 11,184, sawa na asilimia 93 ya lengo; imetoa ushauri wa kiufundi kwa taasisi na kampuni tisa (9) kuhusu matumizi ya viwango mbalimbali katika uandaaji wa hesabu na ukaguzi, sawa na asilimia 90 ya lengo; imefanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa hesabu kwa taasisi na kampuni 68, sawa na asilimia 91 ya lengo; na imefanya ukaguzi wa ubora kwa kampuni 52 za ukaguzi, sawa na asilimia 80 ya lengo. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kufanya mapitio ya mtaala wa uhasibu nchini na vitabu vya rejea kwa masomo 12, sawa na asilimia 100 ya lengo; na kusajili watahiniwa 7,238 ambapo 6,711 walifanya mitihani Novemba 2023. Aidha, Bodi iliendesha mitihani kwa watahiniwa 1,451 wenye taaluma za kimataifa. Vilevile, watahiniwa 137 walisajiliwa katika kozi ya diploma ya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma.

**39. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilipanga kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000. Hadi Aprili 2024, Bodi imesajili watalaamu 1,697 wa ununuzi na ugavi, sawa na ufanisi wa asilimia 48; na kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa watalaamu 2,749, sawa na asilimia 42. Aidha, Bodi imeendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 976, sawa na asilimia 24. Sababu za kutofikia malengo ni hofu ya mabadiliko ya mitaala ya wataalamu wa ununuzi na ugavi yaliyofanywa na Bodi mwaka 2023; na baadhi ya waajiri kutotenga fedha za mafunzo endelevu ya kitaaluma katika bajeti zao kwa wataalamu wa ununuzi na ugavi.

### 3.4.3 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

**40. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 26.7; kuendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato;

kuendelea kutoa elimu ya kodi; na kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato. Aidha, Bodi ya Rufani za Kodi, Baraza la Rufani za Kodi na Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi zilitarajia kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri, malalamiko na taarifa za kodi kutoka kwa walipakodi na wadau wa kodi pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma za usuluhishi wa masuala ya kodi.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya shilingi trilioni 21.3, sawa na ufanisi wa asilimia 96.9 ya lengo la Julai 2023 hadi Aprili 2024 na asilimia 79.8 ya lengo la mwaka. Aidha, katika kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, Mamlaka imeanza ujenzi wa mfumo wa usimamizi wa kodi za ndani - IDRAS ambao ni mahsusi kwa usajili, ukadiriaji, ukusanyaji wa kodi na ufuatiliaji wa walipakodi.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine yaliyopatikana ni kutekeleza mradi wa kuunganisha mifumo ya ndani na taasisi nyingine za serikali ikiwemo mfumo wa kuzalisha vitambulisho vya Taifa - NIDA na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA na kuboresha moduli ya lango la huduma kwa mlipakodi na moduli ya uwasilishaji wa ritani za kieletroniki kwa mapato ya ndani. Hatua zilizochukuliwa kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato ni pamoja na: kuanzisha divisheni mpya ya walipakodi wa kati na wadogo chini ya Idara ya Kodi za Ndani; kuimarisha mifumo ya kubadilishana taarifa na wadau wa ndani na nje ya nchi; kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya vitendo vinavyoashiria ukwepaji kodi; na kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu masuala ya kodi, hususan umuhimu wa kudai na kutoa risiti za kielektroniki - EFD na matumizi na uhakiki wa stempu za kielektroniki - ETS. Aidha, Mamlaka imetoa elimu ya kodi kwa walipakodi kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, vipindi vya redio na televisheni, matangazo ya kodi, mikutano ya wadau wa kodi, kampeni, mitandao ya kijamii na vipeperushi.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Bodi ya Rufani za Kodi imepokea mashauri ya kodi 437 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 3,456.5 na imesikiliza na kutolea uamuzi mashauri 388 ya

kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 2,780.1 na dola za Marekani 439,281. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi limesajili jumla ya mashauri 112 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 2,790 ambapo mashauri 64 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 137.9 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri 56 ya kodi bishaniwa ya shilingi bilioni 2,510 yako katika hatua mbalimbali za usikilizaji na kutolewa maamuzi. Vilevile, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi imepokea malalamiko 40, imesuluhisha malalamiko 22 na malalamiko 18 yapo katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Kadhalika, Taasisi imeanzisha mfumo wa kupokea malalamiko kwa njia ya simu (call center) ambapo mlalamikaji au mtoa taarifa anaweza kuwasilisha malalamiko kwa kupiga simu ya bure namba 0800111022. Jitihada hizo zimewezesha ongezeko la mwamko wa wananchi na walipakodi kuwasilisha malalamiko yao kwa uhuru na uwazi.

**44. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha walipakodi wanakuwa na uelewa na kunufaika na huduma zinazotolewa, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi imeendelea kujitangaza kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na kufanya vikao na wahariri wa vyombo vya habari na vikundi vya wafanyabiashara katika Mkoa wa Dar es Salaam kuhusu uwepo wa ofisi, majukumu yake na namna ya kuwasilisha malalamiko. Aidha, taasisi imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya umoja wa wafanyabiashara katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Lindi na Dar es Salaam kwa lengo la kutoa elimu ya usuluhishi wa masuala ya kodi.

### 3.4.4 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

**45. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilipanga kutoa leseni 11,880 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 2,273 ni leseni mpya na leseni 9,607 ni za kuhuisha, kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 101 na kusimamia mchakato wa uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa. Hadi Aprili 2024, Bodi imetoa jumla ya leseni 9,805, sawa na ufanisi wa asilimia 82 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, leseni 6,261 zimehuishwa na 3,544 ni leseni mpya. Aidha, Bodi imekagua jumla ya waendeshaji 87 wa

michezo ya kubahatisha, sawa na asilimia 86 ya lengo la mwaka. Vilevile, Bodi imeteua kampuni ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa na tayari imesaini mkataba wa uendeshaji kwa mujibu wa sheria ya michezo ya kubahatisha.

**3.4.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa**

**46. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kuanzisha bidhaa mpya za masoko ya mitaji; kufanya mapitio ya kanuni na miongozo ya utoaji wa bidhaa katika masoko ya mitaji; na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji na bidhaa. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania lilipanga kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa soko wa kielektroniki ili kuongeza idadi ya bidhaa zinazouzwa na kununuliwa kupitia mfumo huo.

**47. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imewezesha uanzishaji wa bidhaa mpya na bunifu kwenye masoko ya mitaji ikiwemo hatifungani ya kijani na hatifungani yenye mguso na matokeo chanya kwa jamii; hatifungani yenye mguso wa jinsia; na hatifungani zinazokidhi misingi ya Shariah (Sukuk Bonds). Aidha, Mamlaka imewezesha kutolewa kwa hatifungani ya kwanza Afrika yenye ubunifu unaojumuisha vipengele vinavyogusa taasisi za umma, maboresho ya miundombinu ya maji, utunzaji wa mazingira na miradi yenye uwezo wa kujiendesha kibiashara - Subnational Water Infrastructure Green Revenue Bond iliyotolewa na Mamlaka ya Maji, Tanga. Vilevile, Mamlaka imeandaa Mwongozo wa Kuendesha na Kusimamia Bidhaa za Mitajihalaiki pamoja na Mwongozo ya Utoaji wa Hatifungani Zinazokidhi Misingi ya Shariah. Miongozo hiyo imeidhinishwa na imechapishwa kwenye Gazeti la Serikali kwa matumizi ya umma.

**48. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Soko la Bidhaa Tanzania limeendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa soko wa kielektroniki ili kuongeza idadi ya bidhaa zinazouzwa na kununuliwa kupitia mfumo huo. Uhamasishaji umefanyika sambamba na kufanya mauzo ya bidhaa mbalimbali ikiwemo

ufuta, kahawa, choroko, mbaazi, chai na kakao. Aidha, mnada wa kwanza wa zao la chai ulifanyika Novemba 2023.

### 3.4.6 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

**49. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi - M3 kwa kiwango kisichopungua asilimia 10 ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi; kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi; kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Aidha, kutokana na mabadiliko ya mifumo ya usimamizi wa uchumi, Benki Kuu ya Tanzania ilianza kutumia mfumo mpya unaotumia riba ya benki kuu ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sera ya fedha, usimamizi wa sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Aidha, utaratibu wa kutumia riba ya benki kuu katika utekelezaji wa sera ya fedha, sekta ya fedha na uchumi jumla unaenda sambamba na mabadiliko ya mfumo wa utoaji taarifa kwa umma.

**50. *Mheshimiwa Spika,*** licha ya kukabiliwa na changamoto ya mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia, ukwasi katika uchumi ulitosheleza mahitaji ya shughuli za uzalishaji ambapo ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi - M3 ulikua kwa wastani wa asilimia 15.5 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.1. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 19.2 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 ikilinganishwa na malengo ya ukuaji wa asilimia 16.4. Vilevile, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.5 Desemba 2023 ikilinganishwa na dola bilioni 5.4 Juni 2023, kiwango kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.5, ikiwa ndani ya lengo la nchi la wastani wa miezi 4.

**51. *Mheshimiwa Spika,*** sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, na vihatarishi kupungua kutokana na matarajio ya uchumi wa dunia kuendelea kuimarika. Sekta ya kibenki ambayo ni sehemu

kubwa ya sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, yenye kutengeneza faida, ukwasi na mtaji wa kutosha. Ubora wa rasilimali uliendelea kuongezeka, ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 4.3 Desemba 2023 kutoka asilimia 5.5 Juni 2023. Hali hiyo inaashiria kuendelea kupungua kwa vihatarishi katika utoaji wa mikopo kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi pamoja na hatua za kisera na kiusimamizi zinazoendelea kuchukuliwa na benki kuu ili kupunguza mikopo chechefu.

**52. *Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa sera ya fedha katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 umewezesha riba ya mikopo ya siku saba (7) katika soko la jumla la fedha baina ya benki kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3.5 hadi 7.5. Wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 17 ambapo sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa kwenye shughuli za kilimo, uchimbaji wa madini, usafirishaji na uzalishaji viwandani. Sekta ndogo ya benki imeendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha, huku ikiendelea kutengeneza faida na uwiano wa mikopo chechefu kuendelea kuwa chini ya asilimia 5 ya mikopo yote.

**53. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 45.10, kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.50, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 120, thamani ya mali za Benki kufikia shilingi bilioni 562.70 na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wateja shilingi bilioni 62. Hadi Desemba 2023, Benki ilikusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 41.56, sawa na asilimia 92.15 ya lengo na kutengeneza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.79, sawa na asilimia 107.9 ya lengo. Aidha, Benki ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 161.60, sawa na asilimia 134.67 ya lengo na thamani ya mali ilifikia shilingi bilioni 606.94, sawa na asilimia 107.86 ya lengo. Vilevile, Benki ilifuatilia urejeshaji wa mikopo ya shilingi bilioni 92.0, sawa na ufanisi wa asilimia 148.4 ya lengo.

**54. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023, Benki ya Maendeleo TIB ilipanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.62 kwa miradi ya maendeleo kwenye sekta ya maji, nishati na

uongezaji thamani mazao ya kilimo; kukusanya shilingi bilioni 41.69 kama marejesho ya mikopo kutoka kwa wateja; na kukusanya shilingi bilioni 7.39 ikiwa ni marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa kwenye mizania ya benki. Hadi Desemba 2023, benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 9.74, sawa na asilimia 83.82 ya lengo. Aidha, Benki ilipokea marejesho ya mikopo ya shilingi bilioni 42.63, sawa na asilimia 102.30 ya lengo. Vilevile, benki ilikusanya shilingi bilioni 6.51 kutoka kwa wateja kama marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa kwenye mizania ya benki, sawa na ufanisi wa asilimia 88.09 ya lengo.

**55. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023, Benki ya Biashara Tanzania ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 184.2; kukuza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 12.4; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 904; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,121; kukuza mali za benki kufikia shilingi bilioni 1,446; kukuza mtaji kufikia shilingi bilioni 123.8; na kuunda mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo. Hadi Desemba 2023, mapato ya benki yalifikia shilingi bilioni 192.1, sawa na asilimia 104.3 ya lengo; mikopo iliyotolewa ilifikia shilingi bilioni 911.2, sawa na asilimia 100.8; amana zilifikia shilingi bilioni 1,120.7, sawa na asilimia 99.9 ya lengo; mtaji wa benki ulifikia shilingi bilioni 118.9, sawa na asilimia 96 ya lengo; na benki ilikuza mali kufikia shilingi bilioni 1,389.3, sawa na asilimia 96.1 ya lengo. Aidha, benki ilipata hasara ya shilingi bilioni 44.4 kabla ya kodi kutokana na kufutwa kwa mali chechefu iliyorithiwa ya shilingi bilioni 54.4 kutokana na kuunganishwa na benki nyingine tatu (3). Vilevile, mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo unaendelea kusimikwa na kufungamanishwa na mifumo mingine ya benki.

**56. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF ulipanga kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 44.8 kwa wajasiriamali 38,000; urejeshaji wa mikopo usipungue asilimia 95; na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa au wanufaika 5,500. Hadi Desemba 2023, Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 49.78, sawa na ufanisi wa asilimia 111 ya lengo kwa wajasiriamali wadogo 37,024, sawa na ufanisi wa asilimia 97 ya lengo la mwaka. Aidha, kiwango

cha urejeshaji wa mikopo kilifikia asilimia 95.87 dhidi ya lengo la asilimia 95 kwa mwaka 2023. Vilevile, Mfuko umetoa elimu kwa wadau 2,705, sawa na asilimia 49.1 ya lengo la mwaka. Sababu ya kutofikia lengo la elimu ni kutokana na Mfuko kusitisha utoaji wa mikopo ya vikundi ili kufanya mapitio ya mfumo wa usimamizi wa mikopo kwa vikundi.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5; na kuhamasisha taasisi za Serikali, mifuko ya hifadhi za jamii, mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Hadi Aprili 2024, rasilimali za mifuko ziliongezeka hadi shilingi bilioni 2,012.8 kutoka shilingi bilioni 1,535.8 Juni 30, 2023, sawa na ongezeko la asilimia 31.1; na idadi ya wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa asilimia 19.2. Sababu za kuvuka malengo ya 2023/24 ni kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu faida ya uwekezaji wa pamoja; matumizi ya teknolojia katika utoaji huduma na ongezeko la mawakala waliosajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilipanga kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 32; kufanya ukaguzi wa kampuni za bima; kuandaa mwongozo wa bima za kilimo; kuhamasisha wadau wa bima kuandaa bidhaa za sekta ya kilimo; na kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja wa bima kwa wakati. Aidha, Shirika la Bima la Taifa lilipanga kukamilisha taratibu za kupata ithibati ya cheti cha ubora cha utoaji huduma kwa wateja (ISO 9001:2015); kuongeza wateja wapya 116 wa bidhaa za taasisi; na kubuni bidhaa tatu (3) mpya zitakazokidhi mahitaji ya soko.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imekamilisha uchambuzi wa mikataba 344 ya bima mtawanyo kwa kampuni 29, sawa na asilimia 90.6 ya lengo; imefanya ukaguzi kwa wadau wa bima 259; kuandaa Mwongozo wa Bima za Kilimo; na kampuni 14 za bima zimeanzisha Konsotia

ya Kilimo - Tanzania Agriculture Insurance Consortium (TAIC) iliyozinduliwa Julai 01, 2023. Aidha, Mamlaka imepokea na kushughulikia malalamiko 288 ya wateja wa bima. Vilevile, Shirika la Bima la Taifa limefanikiwa kupata ithibati ya cheti cha ubora cha ISO 9001 :2015 pamoja na cheti cha ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania; na kuandikisha wateja wapya 222, sawa na ufanisi wa asilimia 191.4.

### 3.4.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**60. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kusambaza matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022; kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za sensa; kuendelea kuandaa taarifa za sensa za kisekta kulingana na ratiba; na kufanya tafiti za kitaalamu kuhusu watu wenye uwezo wa kufanya kazi, mapato na matumizi ya kaya binafsi, ajira, mapato na ustawi wa watoto katika jamii.

**61. *Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili 2024, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kusambaza matokeo ya Sensa kwa kutumia teknolojia ikiwemo tovuti, kanzidata na programu tumizi kupitia simu za kiganjani kwa lengo la kuwafikia wadau wengi iwezekanavyo. Aidha, uchambuzi wa kina, kuandaa kanzidata ya viashiria vya watu wenye ulemavu, utoaji wa elimu na mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 umeendelea kufanyika. Uchambuzi unaoendelea kwa sasa ni takwimu za ndoa na uzazi, elimu, hali ya umaskini kwa kutumia viashiria visivyotumia fedha - non-monetary ítems na makadirio ya idadi ya watu kuanzia mwaka 2023 hadi mwaka 2063. Vilevile, kazi ya uchambuzi wa viashiria vilivyoainishwa katika dodoso la sensa imekamilika kwa asilimia 80 kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Uchambuzi wa Matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022 na ule wa Umoja wa Mataifa. Kadhalika, utoaji wa mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 umefanyika kwa asasi za kiraia kupitia vyama vinavyowaunganisha, viongozi wa kimila na mabalozi wa Tanzania nje ya Nchi. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka - TDHS/MIS (2022) ambao ulikamilika na matokeo

kuzinduliwa Oktoba 28, 2023, Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2024 na Utafiti wa Ajira na Mapato wa Mwaka 2023 katika Sekta Rasmi Nchini.

### 3.4.8 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**62. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilipanga kuendelea na ujenzi wa mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao awamu ya pili; kutoa mafunzo kwa watumishi 2,000 kutoka katika taasisi nunuzi 1,000 na wazabuni 5,000 kuhusu mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma; kufanya kaguzi ya thamani ya fedha katika taasisi nunuzi 85 na kaguzi ya ukidhi wa sheria kwa taasisi nunuzi 300; na kufanya mapitio ya nyaraka sanifu za zabuni. Aidha, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma ilipanga kutoa mafunzo kwa wajumbe, wafanyakazi wa mamlaka, wazabuni na taasisi nunuzi kuhusu utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kusimamia rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma. Vilevile, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ulipanga kuanza ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Kigoma, na ofisi na vituo vya mafuta katika mikoa ya Njombe na Arusha pamoja na Wilaya ya Kahama, Korogwe na Masasi; kuboresha mfumo wa GIMIS ili kuwezesha matumizi ya kadi katika huduma za ununuzi wa mafuta; na kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini uwezekano na mahitaji ya kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu pamoja na tanki za mafuta.

**63. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma - NeST awamu ya kwanza na umeanza kutumika rasmi Oktoba 2023; watumishi 12,812 kutoka taasisi 813, wazabuni 2,259 na makundi maalumu 248 wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa NeST; ukaguzi wa ukidhi wa sheria umefanyika kwa taasisi nunuzi 239, sawa na asilimia 79.7 ya lengo; na Mamlaka imefanya ukaguzi wa thamani ya fedha kwa taasisi nunuzi 89, sawa na asilimia 104.7 ya lengo. Aidha, mafunzo kuhusu utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kushughulikia rufaa za ununuzi wa umma yametolewa kwa wajumbe na wafanyakazi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma; na

jumla ya mashauri 41 yamepokelewa, kusikilizwa na kutolewa uamuzi.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini umetekeleza miradi ya ujenzi katika mikoa ya Arusha (asilimia 15), Njombe (asilimia 7), Kigoma (asilimia 13) na Wilaya ya Kahama mradi upo katika hatua za awali - mobilization. Mradi wa Kigoma unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Novemba 2024, miradi ya Arusha na Njombe inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Aprili 2025 na mradi wa Korogwe upo katika hatua za ufuatiliaji wa hati ya kiwanja. Aidha, Wakala umetangaza zabuni ya uboreshaji wa mfumo wa GIMIS ili kuwezesha matumizi ya kadi katika huduma za ununuzi wa mafuta. Vilevile, katika kipindi hicho, Wakala umekamilisha andiko na hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata mshauri elekezi kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini mahitaji ya kuunganisha mfumo wa GIMIS na miundombinu ya mafuta, yaani pampu na matenki kwa lengo la kuongeza tija na udhibiti wa huduma ya mafuta.

### 3.4.9 Michango ya Taasisi za Wizara katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, taasisi za Wizara ya Fedha zilitarajia kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 239.05, ikijumuisha gawio shilingi bilioni 231.20 na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 7.85. Hadi Aprili 2024, taasisi za wizara zimechangia jumla ya shilingi bilioni 108.37, sawa na asilimia 45.33 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 100.80 zimetokana na gawio, ikiwa ni ufanisi wa asilimia 44 na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 7.57, sawa na ufanisi wa asilimia 96.

### 3.4.10 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 taasisi zilizo chini ya wizara zilitarajia kutekeleza jumla ya miradi 11 ikijumuisha ujenzi wa madarasa, maktaba, kumbi za mihadhara, migahawa, maabara za kompyuta, nyumba za watumishi na majengo ya ofisi. Hadi Aprili 2024, miradi mitatu (3) imekamilika na kuanza

kutoa huduma na miradi nane (8) ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi iliyokamilika ni jengo la ofisi za makao makuu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, jijini Dodoma; na ukumbi wa mihadhara awamu ya pili na hosteli ya wanafunzi awamu ya kwanza katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Kampasi ya Dodoma na Mwanza mtawalia.

**67. *Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na: ujenzi wa jengo la utawala na uzio katika Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (asilimia 98); ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 97) na utawala na taaluma (asilimia 35) katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania Kampasi ya Mwanza na Kigoma mtawalia; ujenzi wa hosteli ya wanafunzi awamu ya tatu (asilimia 80) na hosteli ya wanafunzi awamu ya pili (asilimia 5) katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa Kampasi ya Miyuji na Mwanza mtawalia; na ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 93) na hosteli mbili (2) za wanafunzi (asilimia 49) katika Chuo cha Uhasibu Arusha Kampasi ya Babati.

### 3.5 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbelevya Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**68. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma; kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalumu, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA; kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya ofisi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi mikoani.

**69. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Ofisi imefanya kaguzi 1,450 ikijumuisha ukaguzi wa Serikali Kuu (537), Mamlaka za Serikali za Mitaa (625), Mashirika ya Umma (215), Ukaguzi wa Ufanisi (14), Kiufundi (10), Kiuchunguzi (7), Maalumu (12) na Mifumo ya TEHAMA (30). Aidha, Ofisi imekamilishaji kuandaa Ripoti jumuishi sita (6) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Machi 28, 2024.

## 3.6 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Mikakati ya Kukabiliana nazo

### 3.6.1 Changamoto

**70. *Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2023/24, wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:

i. Huduma hafifu ya matengenezo ya mashine za EFD, kukosekana kwa mtandao na mwamko mdogo wa wananchi kudai na kutoa risiti za kielektroniki za EFD;

ii. Kuongezeka kwa mahitaji ya ziada ya rasilimali fedha kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na

iii. Baadhi ya walipakodi kuficha taarifa za miamala ya kibiashara na kuendelea kuwepo kwa biashara za magendo, hususan mipakani na mwambao wa bahari.

### 3.6.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

**71. *Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, wizara imechukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Kuhamasisha matumizi ya mfumo wa Virtual Fiscal Devices (VFD) kutoa risiti kama mbadala wa mashine za EFD;

ii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudai na kutoa risiti za kielektroniki;

iii. Kuimarisha soko la ndani la fedha ili kuwezesha utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa kutumia vyanzo mbadala vya mapato;

iv. Kufanya mapitio ya mipango na bajeti ili kugharamia mahitaji ya ziada ya kurejesha miundombinu iliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi;

v. Kuboresha mifumo ya usimamizi wa mapato ikiwemo doria mipakani na mwambao wa bahari ili kudhibiti biashara za magendo na udanganyifu; na

vi. Kufungamanisha mifumo ya mipango na bajeti za kisekta na mifumo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## 4.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

**72. *Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya wizara pamoja na taasisi kwa mwaka 2023/24, sasa napenda kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/25.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka 2024/25 umeandaliwa kwa kuzingatia sera, mikakati, sheria, mipango na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; mikakati na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne; Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 uliofanyiwa mapitio ya muda wa kati; na masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabianchi na UKIMWI.

### 4.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara

**74. *Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya mafungu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

i. Kutafuta na kukusanya mapato ya shilingi trilioni 44.19 kati ya maoteo ya shilingi trilioni 49. 35 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali;

ii. Kuimarisha na kusimamia mifumo ya mapato, matumizi na mali za Serikali ikiwemo IDRAS, TANCIS, MUSE, NeST, CBMS na GAMIS;

iii. Kuhudumia deni la Serikali kwa wakati na kuboresha kanzidata ya kutunza taarifa za deni;

iv. Kutoa elimu ya huduma za fedha kwa wananchi kwa lengo la kukuza huduma jumuishi za fedha nchini; na

v. Kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi pamoja na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma.

**4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**75. *Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na:

i. Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma kama yalivyoidhinishwa na Bunge mwaka 2023/24;

ii. Kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA;

iii. Kufanya kaguzi maalumu na kiuchunguzi kulingana na mahitaji;

iv. Kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga na kukarabati ofisi za mikoa; na

v. Kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi na za Kisekta ili kuzielewa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### 4.3 Vipaumbele vya Taasisi za Wizara kwa Mwaka 2024/25

**76. *Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, baadhi ya majukumu ya wizara yanatekelezwa kupitia taasisi za elimu, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi wa masuala ya fedha, kodi, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji pamoja na takwimu. Vipaumbele vya taasisi hizo kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

#### 4.3.1 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu

**77. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, taasisi tano (5) za elimu zilizo chini ya wizara zinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 86,098, ikijumuisha ngazi ya astashahada 12,450, stashahada 18,848, shahada 49,549 na uzamili 5,251. Kati ya idadi hiyo, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatarajia kudahili wanafunzi 17,775, Taasisi ya Uhasibu Tanzania wanafunzi 30,972, Chuo chaUhasibu Arusha wanafunzi 19,136, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini wanafunzi 16,652 na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika wanafunzi 1,563. Aidha, taasisi hizo zinatarajia kuendeleza watumishi 152 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili (26) na uzamivu (126). Vilevile, taasisi hizo zinatarajia kufanya tafiti 85 na kutoa huduma elekezi 818.

**78. *Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka 2024/25, taasisi za elimu zinatarajia kupokea shilingi bilioni 8.94 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitano (5) inayolenga kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

#### 4.3.2 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

**79. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 29.42. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 28.87 ni mapato ya kodi na shilingi bilioni 541.10 ni mapato yasiyo ya kodi. Aidha, Mamlaka itaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti biashara za magendo ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Vilevile, Mamlaka inatarajia

kupokea jumla ya shilingi bilioni 25.97 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo kuimarisha na kuboresha mifumo ya usimamizi wa mapato ya Serikali, kununua vitendea kazi na kuboresha mazingira mahali pa kazi, hususan majengo ya ofisi.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi ya Rufani za Kodi inatarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi yanayotokana na maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; kuandaa Juzuu ya Taarifa za Sheria za Kodi Tanzania; na kuhuisha Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 408 pamoja na kanuni zake. Vilevile, Baraza la Rufani za Kodi linatarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi yanayotokana na maamuzi ya Bodi ya Rufani za Kodi. Kadhalika, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi inatarajia kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya taasisi; kupokea na kutatua malalamiko ya walipakodi; kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kupokea na kuchakata malalamiko; kuratibu kutungwa kwa sheria mpya ya taasisi; na kujenga uwezo kwa watumishi katika maeneo ya uendeshaji na usuluhishi wa malalamiko.

#### 4.3.3 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu inatarajia kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kutoa mafunzo ya uandaaji na ukaguzi wa taarifa za fedha kwa wahasibu na wakaguzi 12,500; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65 za ukaguzi; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa awamu mbili kwa watahiniwa 14,540; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji kwa awamu mbili kwa watahiniwa 1,451; na kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 150. Aidha, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kufanya ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Bodi kwa taasisi za umma na binafsi na kuhuisha kanzidata ya wataalamu

wa ununuzi na ugavi. Vilevile, Bodi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi; kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa watahiniwa 6,500; na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000.

### 4.3.4 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imepanga kutoa leseni 12,456 ikijumuisha leseni mpya 1,126 na kuhuishwa leseni11,330; kufanya kaguzi 12 kwa kuzingatia vihatarishi katika michezo mbalimbali ya kubahatisha; kutekeleza operesheni nne (4) za kutokomeza michezo haramu ya kubahatisha; kukusanya mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha ya jumla ya shilingi bilioni 24.89; kuendelea kuelimisha jamii juu ya athari hasi za michezo ya kubahatisha; na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

### 4.3.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mitaji ubia (venture capital); kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida za masoko ya mitaji; kuidhinisha bidhaa mpya mbili (2) kuwezesha taasisi na kampuni katika sekta ya umma na binafsi kupata fedha za kugharamia biashara na miradi ya maendeleo; na kuboresha mifumo ya usimamizi wa shughuli za masoko ya mitaji. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania linatarajia kuanza ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu Dar es Salaam lenye thamani ya shilingi bilioni 8.35 ikiwa ni ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

### 4.3.6 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo mpya unaotumia riba ya benki kuu. Kulingana na mwenendo wa uchumi wa dunia, utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 unatarajiwa kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kuwa ndani ya lengo la asilimia 5; kudhibiti kiwango cha

riba za mikopo ya siku saba (7) baina ya benki; kudhibiti mwenendo wa sera ya fedha ili kunaendana na malengo ya utekelezaji wa programu ya Extended Credit Facility (ECF); kufuatilia taasisi za fedha kupanga riba na viwango vya kubadilisha fedha kwa kuzingatia nguvu ya soko; na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya benki ili kudhibiti akiba ya fedha za kigeni.

**85. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 56.54; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 20.83 kutoka shilingi bilioni 18.79 ya mwaka 2023; kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 197 ikilinganishwa na shilingi bilioni 161.6 zilizotolewa mwaka 2023; kuongeza thamani ya mali za Benki kufikia shilingi bilioni 866.23 kutoka shilingi bilioni 606.94 mwaka 2023; na kufuatilia marejesho ya mikopo shilingi bilioni 70 kutoka kwa wateja.

**86. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Benki ya Maendeleo TIB imepanga kuongeza mtaji wa benki hadi shilingi bilioni 204.61 kutoka shilingi bilioni 86.61 mwaka 2023; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 89.02 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.74 mwaka 2023; kuongeza mali za benki hadi shilingi bilioni 545.48 kutoka shilingi bilioni 425.15 mwaka 2023; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya benki shilingi bilioni 17.44 na mkopo iliyoko katika mizania ya benki shilingi bilioni 30.38; na kusimika mifumo mitatu (3) ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

**87. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Benki ya Biashara Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 225; kukuza faida ya benki kabla ya kodi shilingi bilioni 37.3; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,173; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,340; kukuza mali za benki hadi shilingi bilioni 1,701 kutoka shilingi bilioni 1,389.3 mwaka 2023; kukuza mtaji wa benki hadi shilingi bilioni 147 kutoka shilingi bilioni 118.9 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja hadi 881,122 kutoka wateja 831,122 mwaka 2023; na kukamilisha uundaji na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF unatarajia kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 48 kwa wajasiriamali 48,000; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 3.28 kutoka shilingi bilioni 1.89 mwaka 2023; kukuza mtaji hadi shilingi bilioni 65.48 kutoka shilingi bilioni 61.14 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja hadi 48,000 kutoka wateja 37,024 mwaka 2023; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya mfuko shilingi bilioni 2 na mikopo iliyo katika mizania shilingi bilioni 48.53; na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 11.03.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS inatarajia kuongeza rasilimali za mifuko hadi shilingi bilioni 2,642.7 kutoka shilingi bilioni 2,012.8 mwaka 2023/24; kuongeza idadi ya wawekezaji hadi 367,500 kutoka 310,806 mwaka 2023/24; na kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 28.03 kutoka shilingi bilioni 18.82 mwaka 2023/24.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inatarajia kujenga mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya tozo za ada ya bima; kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi jijini Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 3.80; kufanya ukaguzi kwa wadau wa bima 259 (kampuni 25 na matawi 30, madalali 66, mawakala 150, benkiwakala10 na matawi 20 na wauza bima kidijiti nane (8)); kuchambua mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 36; kutoa elimu ya bima kwa umma; kuidhinisha bidhaa mpya tano (5) zinazokidhi mahitaji ya watu wenye kipato cha chini; na kuongeza wasajili wapya wa bima 105.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Shirika la Bima la Taifa linatarajia kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu bidhaa na huduma za shirika; kuboresha utoaji huduma kwa wateja kupitia uandikishaji wa Cheti cha Ubora (ISO 9001:2015) katika ofisi 11 za kanda; kupunguza muda wa malipo ya madai kutoka siku 16 hadi saba (7); kuongeza wateja wapya 324 wa bidhaa za taasisi kutoka wateja 222 mwaka 2023/24; kubuni bidhaa mpya mbili (2) na kuboresha bidhaa tatu (3) kuendana na mahitaji ya

soko; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 85.57 kutoka shilingi bilioni 51.42; na kuongeza mapato ya taasisi kutoka shilingi bilioni 244.34 hadi shilingi bilioni 314.78.

#### 4.3.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**92. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatarajia kuendelea na jukumu lake la msingi la kutoa takwimu rasmi za kijamii, kiuchumi na mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Takwimu, SURA 351. Aidha, shabaha nyingine ni kuchambua, kusambaza na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika ngazi ya halmashauri, majimbo, kata, shehia, mtaa, kijiji hadi kitongoji; kuendelea na Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2024; Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na Ufuatiliaji wa Kaya wa Mwaka 2024/25; Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2023/24; na kufanya Sensa ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar inatarajia kujenga majengo ya ofisi katika mikoa ya Pemba, Lindi na Simiyu kwa gharama ya shilingi bilioni 3.4 kila moja kwa ajili ya kuhudumia mkoa wa Pemba, Kanda ya Kusini na Kanda ya Ziwa. Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatarajia kujenga kituo cha kisasa cha kuchakata takwimu Jijini Dodoma.

#### 4.3.8 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**93. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inatarajia kukamilisha ujenzi wa moduli tatu (3) za mfumo wa NeST; kufanya tafiti tatu (3) kuhusu matumizi ya fomula ya mabadiliko ya bei katika miradi ya ujenzi, ununuzi endelevu na matumizi ya force account, na ununuzi kwa njia ya mzabuni mmoja ikilinganishwa na ushindani; kuandaa na kupitia nyaraka sanifu 42 na miongozo tisa (9) ya ununuzi wa umma kwa matumizi ya taasisi nunuzi; kutoa elimu kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa watumishi 8,160 kutoka katika wizara, taasisi za serikali, sekretarieti za mikoa na halmashauri, wazabuni 4,000, asasi za kiraia 100, makundi

maalumu 110 na wanafunzi 4,000 wa vyuo vikuu; na kufanya ukaguzi wa ununuzi kwa taasisi nunuzi 500.

**94. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma imepanga kusajili na kusikiliza rufaa 55; kutoa mafunzo kwa wazabuni 800 kuhusu moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa; na kutoa mafunzo kwa wakuu wa idara/vitengo 300 vya ununuzi na sheria kuhusu usimamizi wa malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki. Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini unatarajia kununua magari manne (4) ya kusafirishia mafuta; kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu na matenki ya mafuta; na kuanzisha utoaji wa huduma za mafuta kwa kutumia kadi kupitia mfumo wa GIMIS. Aidha, Wakala unatarajia kujenga ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika Wilaya ya Mbarali (Mbeya), Masasi (Mtwara), Korogwe (Tanga) na Jiji la Arusha; na ujenzi wa ofisi ya Mkoa Dar es Salaam.

### 4.3.9 Michango ya Taasisi za Wizara katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

**95. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, taasisi za Wizara ya Fedha zinatarajia kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 233.99. Kati ya kiasi hicho, gawio ni shilingi bilioni 224.15 na mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 9.84.

## 4.4 Mapendekezo ya Bajeti ya Mafungu ya Wizara na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2024/25

### 4.4.1 Mapato

**96. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya shilingi trilioni 49.35 zinazokadiriwa kukusanywa na Serikali kwa mwaka 2024/25, Wizara ya Fedha imekadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44.19. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 29.42, misaada na mikopo nafuu shilingi trilioni 5.13, mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje shilingi trilioni 9.60 na maduhuli shilingi bilioni 45.01. Aidha, Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inakadiria kukusanya shilingi

milioni 850 ikiwa ni mapato ya kodi ya pango kutokana na upangishaji wa majengo ya Ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali nchini.

### 4.4.2 Matumizi

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Wizara ya Fedha inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 18.17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu nane (8) ya kibajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 17.63 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha huduma ya deni la Serikali shilingi trilioni 13.13, mishahara shilingi bilioni 946.45, matumizi mengineyo shilingi bilioni 937.30 kwa mafungu ya wizara na taasisi zake, Huduma za Mfuko Mkuu shilingi trilioni 2.61 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 544.05. Aidha, ninaomba Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iidhinishiwe jumla ya shilingi bilioni 112.73 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 101.26 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11.47 matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi kwa mafungu nane (8) ya kibajeti ya Wizara ya Fedha na Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi umeoneshwa katika **Jedwali Na.1** na mchanganuo wa kina katika **Kiambatisho Na.4**

**Jedwali Na.1: Mchanganuo wa Matumizi ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MATUMIZI YA MAENDELEO | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Deni la Serikali | 13,131,838,005,000 | 0 | 13,131,838,005,000 |
| **6** | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 13,046,426,000 | 1,229,451,000 | 14,275,877,000 |
| **10** | Tume ya Pamoja ya Fedha | 4,408,314,000 | 1,598,249,000 | 6,006,563,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **13** | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | 3,768,237,000 | 0 | 3,768,237,000 |
| **21** | Hazina | 1,635,427,521,000 | 495,063,000,000 | 2,130,490,521,000 |
| **22** | Huduma za Mfuko Mkuu | 2,629,932,850,000 | 0 | 2,629,932,850,000 |
| **23** | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 62,362,459,000 | 7,292,385,000 | 69,654,844,000 |
| **50** | Wizara ya Fedha | 149,621,451,000 | 38,864,752,000 | 188,486,203,000 |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA** | | **17,630,405,263,000** | **544,047,837,000** | **18,174,453,100,000** |
| **45** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 101,260,832,000 | 11,468,000,000 | 112,728,832,000 |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE** | | **17,731,666,095,000** | **555,515,837,000** | **18,287,181,932,000** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha***

## 5.0 HITIMISHO

**98. *Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb,), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, nawashukuru watendaji wakuu wa wizara na taasisi zake wakiongozwa na Dkt. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu

Bi. Amina Kh. Shaaban, Bi. Jenifa C. Omolo na Bw. Elijah G. Mwandumbya kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya wizara na taasisi. Vilevile, nawashukuru wakuu wa idara, vitengo na wafanyakazi wote wa wizara na taasisi zake, kwa ushirikiano na utekelezaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku. Asanteni sana na Kazi Iendelee.

**99. *Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu pamoja na waheshimiwa wabunge na umma wa watanzania kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya wizara ambayo ni www.mof.go.tz.

**100. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri ahsante sana na namwona Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe aje awasilishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu Nane ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya Nane cha Kanuni za Kudumu za Bunge kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kuisimamia Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zilizopo chini yake. Vilevile, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti imechambua Mafungu Nane ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na kujiridhisha kwamba mapendekezo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja, yanafaa kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 001 – Deni la Serikali;

(ii) Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali;

(iii) Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha;

(iv) Fungu 013 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu;

(v) Fungu 021 – Hazina;

(vi) Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu;

(vii) Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali;

(viii) Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; na

(ix) Fungu 050 – Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Wizara ya Fedha ina jumla ya Mafungu Nane pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Fungu 45. Jedwali Na.1 linaonyesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti wa

Mafungu yote yaliyo chini ya Wizara ya Fedha hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Spika, ilifanya uchambuzi wa Mafungu yote Nane na masuala yafuatayo yalibainika: -

(i) Mheshimiwa Spika, Fungu 01 – Deni la Serikali; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa shilingi trilioni 10.48 kwa ajili ya kulipa Deni la Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 6.0 kwa ajili ya kulipa deni la ndani lililoiva na shilingi trilioni 4.40 ni kwa ajili ya kulipa deni la nje lililoiva. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 18.33 ni kwa ajili ya kusimamia Deni la Serikali na shilingi bilioni 170 ni kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2024, shilingi trilioni 8.485 zimetolewa sawa na 84.48% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 3.92 zimetumika kulipa deni la nje na shilingi trilioni 4.92 zimetumika kulipa deni la ndani. Shilingi bilioni12.5 zimetumika kusimamia deni na shilingi milioni 93.54 zimetumika kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

(ii) Mheshimiwa Spika, Fungu 06 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Fungu hili limekuwa likikabiliwa na changamoto ya upungufu wa Wakaguzi wa Ndani 916, pamoja na bajeti ndogo ikilinganishwa na majukumu yake ambayo ni kukagua matumizi na mapato ya Serikali na kusimamia Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani wa Serikali. Endapo kitengo hiki kingetengewa bajeti ya kutosha kingesaidia kupunguza hoja za ukaguzi ambazo huwa zinaibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Idara hii kwa kuitengea fedha za kutosha zitakazowezesha kuajiri watumishi na kuongeza vitendea kazi.

(iii) Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina; fungu hili ndilo linasimamia bajeti ya Serikali. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439

kinaweka masharti ya uhamisho wa fedha ndani ya Fungu na baina ya Mafungu. Vile vile, Kanuni za Sheria ya Bajeti zimeweka ukomo usiozidi 7% kwa Afisa Masuuli kuhamisha fedha ndani ya fungu na ukomo usiozidi 5% ya bajeti ya Serikali kwa uhamisho wa fedha kati ya mafungu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini changamoto kwenye Kanuni hiyo ambayo haijaweka ukomo wa kiasi cha uhamisho ndani ya fungu unaozidi asilimia saba ambao Afisa Masuuli anapaswa kuomba idhini kwa Waziri wa Fedha. Kutokuwepo kwa ukomo unaozidi uhamisho wa asiliami saba kumefanya Maafisa Masuuli kufanya uhamisho unaohitaji kibali cha Waziri unaoathiri utekelezaji wa baadhi ya shughuli ndani ya Fungu. Aidha, kanuni zinazoweka ukomo, zimeweka ukomo wa fedha zinapohamishwa bila kuweka ukomo wa fedha zinapopelekwa. *(Makofi)*

(iv) Mheshimiwa Spika, Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa na Bunge kiasi cha shilingi trilioni 2.31. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 13.07 ni kwa ajili ya mishahara ya Maafisa wa Umma wanaolipwa kupitia Fungu 22 na shilingi trilioni 2.3 ni kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya shilingi trilioni1.61 zimepokelewa sawa na 69.57% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 8.9 ni mishahara na shilingi trilioni1.6 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia utekelezaji na utendaji kazi wa Fungu hili na inaitaka Serikali kushughulikia masuala yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kurahisisha utaratibu wa pensheni zinazolipwa kwa wastaafu kupitia Hazina pamoja na kuhuisha viwango vyake;

(b) Kamati imebaini kwamba, wastaafu nchini wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo viwango vya mafao ambavyo haviakisi hali ya sasa ya Maisha;

(c) Kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kufuatilia mafao yao; pamoja na

(d) kuhakiki nyaraka za taarifa za wastaafu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) Serikali kuhuisha viwango vya mafao kwa wastaafu ili kuendana na hali halisi ya maisha; *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie; Serikali kuhuisha viwango vya mafao kwa wastaafu, ili kuendana na hali halisi ya maisha; *(Makofi)*

(ii) Kuweka vituo vya kufuatilia pensheni katika ngazi za wilaya ili kusaidia wastaafu kutosafiri umbali mrefu kufuatilia stahiki zao; na

(iii) Kutunza nyaraka zenye taarifa za watumishi na wastaafu kidijitali ili kuondoa usumbufu kwa watumishi waliostaafu na watakaostaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ina jukumu la kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali. Aidha, majukumu mengine ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali yamebainishwa katika Ibara ya 143(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo yamerejewa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa Fungu 45; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilitengewa Jumla ya shilingi bilioni 97.13; kati ya Fedha

hizo shilingi 70.83 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9.41zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Fungu hili lilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi milioni 900. Hadi Aprili, 2024, Fungu 45 limepokea jumla ya shilingi bilioni 81.45 sawa na 83.9% ya Bajeti yote. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Na.2.

Mheshimiwa Spika, masuala ya Msingi yaliyobainika katika utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika majadiliano baina ya Kamati na Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali masuala yafuatayo yalibainika:-

(i) Ofisi ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina changamoto ya uhaba wa watumishi wenye ujuzi na taaluma unahitajika;

(ii) Maslahi yasiyoridhisha ya watumishi wa Ofisi ya *CAG,* hivyo kuathiri utendaji kazi wake;

(iii) Mawanda ya ukaguzi yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, ongezeko la bajeti haliendani na ongezeko hilo. Mfano, Kwa mujibu wa Kanzidata ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, Serikali ina jumla ya mifumo 460 ya TEHAMA. Hadi kufikia tarehe 19 Machi, 2024, Ofisi ya *CAG* ilifanya kaguzi za mifumo 49 tu kwenye Taasisi 24 za Serikali;

(iv) Utolewaji wa Fedha kwa Miradi ya Maendeleo wa ndani si wa kuridhisha ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2024 kiasi kilichotolewa ni 24.4% ya bajeti iliyoidhinishwa ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Hatua hii imekwamisha juhudi za kuwaondoa wakaguzi wa *CAG* kutoka kwenye majengo ya kukaguliwa na ukarabati wa Ofisi ya Kitengo cha Usaidizi wa Kiufundi katika Ukaguzi *(TSSU)* Jengo la Makao Makuu Dodoma. *(Makofi)*

(v) Hati za madai zenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 3.1 zilizowasilishwa Wizara ya Fedha na *CAG* kwa ajili ya malipo hazijalipwa na Serikali hadi Aprili.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, Kamati ilishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Serikali ifanye marekebisho ya maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuwianisha na nchi nyingine. Taarifa ya marekebisho hayo yawasilishwe mbele ya Kamati mwezi Januari, 2025 ili kuhakikisha kwamba watumishi wa ofisi wanalipwa malipo stahiki. Aidha, Kamati iliagiza Ofisi ya *NAOT* ipitie upya muundo wake ili kuona endapo unaenda sanjari na mahitaji ya kiukaguzi ya sasa; *(Makofi)*

(ii) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilisha Hati za Madai ya Wakandarasi zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 5.02. Hadi Aprili, 2024 Ofisi hiyo imepokea jumla ya shilingi bilioni 1.91 sawa na 38% ya hati zilizowasilishwa Wizara ya Fedha. Kamati inaitaka Serikali kufanya malipo ya hati za madai zilizobakia zenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 3.1 zilizowasilishwa Wizara ya Fedha;

(iii) Kamati iliagiza Serikali kuipatia *NAOT* kibali cha kuajiri na kuongeza Bajeti ya Mishahara ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kuajiri ajira 81 ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi. Hatua hii itawezesha Ofisi ya *CAG* kupanua mawanda ya ukaguzi katika maeneo ya kaguzi wa Mifumo ya TEHAMA, Ukaguzi wa Kiufundi, Ukaguzi wa Sekta ya Madini na Uziduaji pamoja na Ukaguzi wa Miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi; na

(iv) Kamati iliagiza Wizara ya Fedha kuhakikisha ifikapo tarehe 30 Juni, 2024 inatoa fedha zote za maendeleo zilizosalia kwa fungu hili ili liweze kutekeleza miradi yake ya maendeleo hususan ujenzi wa ofisi mikoani ili kuwaondoa wakaguzi kwenye Ofisi za wakaguliwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Nane ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2024/2025. Jedwali Na.3 kwenye Taarifa ya Kamati linaonesha mchanganuo wa maombi ya fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa baadhi ya Mafungu; baada ya uchambuzi wa Mafungu yote Nane, Kamati ilibaini na kupendekeza masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; Idara hii ina jukumu la kusimamia wakaguzi wote wa ndani nchini pamoja na kuwajengea uwezo ili waendane na viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Idara hii imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani. Kukosekana kwa mafunzo kunasababisha hesabu kutoandaliwa kwa kuzingatia misingi ya ukaguzi. Hali hii inasababisha wingi wa hoja za ukaguzi pamoja na kuachwa nyuma na mabadiliko ya mifumo. Ofisi hii imetengewa kiasi cha shilingi 629,770,000 kwa ajili ya mafunzo. Hata hivyo, kiwango hiki hakikidhi mahitaji ikizingatiwa kwamba, Idara hii ina jumla ya wakaguzi wa ndani 1,553 wanaojumuisha wakaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliielekeza Serikali kuongeza jumla ya shilingi 2,255,000,000 kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani pamoja na kununua vitendea kazi kama vile magari na tarakilishi mpakato kutokana na kuwepo na uhaba wa vitendea kazi hivyo. Serikali ilikubali pendekezo hilo na kutoa kiasi hicho cha fedha ambacho kitasaidia kuongeza ufanisi katika kusimamia mapato na matumizi ya Serikali na utendaji wa Taarifa za kiuhasibu.

Mheshimiwa Spika, hii ndio kazi ya Kamati ya Bajeti inayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepanga kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) uliorejewa mwaka 2022/2023 ambao unajielekeza kwenye kuimarisha shughuli za ukaguzi wa nje wa Sekta ya Umma hapa nchini. Kimsingi, ofisi imelenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali kama vinavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza vipaumbele vyake imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 113.629 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi milioni 900 fedha za maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi bilioni 111.83 fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa ni shilingi bilioni 99.46 ambazo zinajumuisha shilingi bilioni 20.64 fedha za mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 78.82 fedha za matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo kiasi kinachoombwa ni shilingi bilioni 11.47 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8.83 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2.64 ni fedha za nje. Jedwali Na.4 lililo kwenye Taarifa ya Kamati linaonesha mchanganuo wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Maombi ya Fedha kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilionyesha kuna ongezeka kwa 14.2% ikilinganishwa na bajeti ya ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili halikuzingatia mabadiliko ya viwango vya kubadilishia fedha, gharama za mafuta pamoja na ongezeko la maeneo ya kiukaguzi yaliyotokana na maagizo ya Kamati. Baada ya mashauriano, Kamati ilishauri kwamba, bajeti ya ofisi hii iongezwe shilingi bilioni 1.8 na hivyo kufanya jumla ya bajeti nzima kwa kifungu hili kuwa shilingi bilioni 113.629. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; jumla ya Fedha zote zinazoombwa na Mafungu Nane ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2024/2025 ni Shilingi trilioni18.32. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 3.51 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 14.17 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 632.57 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Jedwali Na.5 lililopo kwenye Taarifa ya Kamati linaonesha maombi ya fedha kwa Wizara ya Fedha na mafungu yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Uteuzi wa Wajumbe katika Bodi ya Rufani za Kodi *(TRAB);*

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara, *TRAB* ina wajumbe katika Mikoa 14. Aidha, Kamati ilibaini kuwa mikoa 12 ambayo ni Manyara, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Lindi, Mara, Mbeya, Njombe, Rukwa, Songwe na Tabora haina wajumbe. Kukosekana kwa Wajumbe katika Bodi kunasababisha mashauri ya kodi kuchukua muda mrefu kusikilizwa na kuwa na mrundikano wa mashauri ambayo hayajasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 imeainisha mashauri 967 ya kodi kwenye Bodi ya Rufani za Kodi zenye thamani ya shilingi trilioni 10.48 ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 5.65. sawa na 117% ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.83 za Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuchelewa kwa uteuzi wa wajumbe muhimu wa kusikiliza kesi. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa taratibu za uteuzi wa wajumbe katika mikoa hiyo zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha taratibu za uteuzi katika mikoa 12 iliyobaki, ili kuharakisha usikilizwaji wa kesi za kodi katika maeneo hayo. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaowezesha Mjumbe kutoka katika mkoa mmoja kusikiliza kesi katika mkoa mwingine, ili kupunguza mrundikano wa kesi.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili kuweka ukomo wa muda kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuwasilisha Taarifa ya Malalamiko ya Kodi kwa Ofisi ya Msuluhishi. Malalamiko yanayoshughulikiwa na ofisi hii ni yale yanayohusu utaratibu wa usimamizi wa sheria za kodi, masuala ya huduma yasiyoridhisha na ya kiutawala ambayo yalitumiwa au yalidaiwa kutumiwa isivyo haki katika usimamizi wa sheria za kodi na ukiukwaji wa ahadi binafsi zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato katika mkataba wa mlipakodi wakati wa kutoa huduma kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa sheria iliyoanzisha ofisi hii haibainishi ukomo wa muda wa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kuwasilisha taarifa za malalamiko kwa Ofisi ya Msuluhishi. Changamoto hii imepelekea kuchelewa kwa upatikanaji wa taarifa na hivyo Ofisi ya Msuluhishi kushindwa kuchakata malalamiko ndani ya muda wa siku 30.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi na kuweka muda kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kutoa majibu kuhusu malalamiko ya walipakodi ili kuwezesha malalamiko kusikilizwa ndani ya siku 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kuzitaka Taasisi zote za Fedha kutoa Taarifa za Miamala Shuku kwa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu *(FIU)*. Katika uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya kitengo hiki, Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

(i) Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 inataka mtoa taarifa kuwasilisha taarifa ya miamala anayotilia shaka au shughuli anazofahamu kuwa zinahusika na mapato ya uhalifu, watoa taarifa wengi wamekuwa hawatekelezi takwa hilo la kisheria;

(ii) Kumekuwa na ushirikiano hafifu baina ya Taasisi zinazoshughulikia taarifa fiche katika kutoa mrejesho wa hatua zilizochukuliwa ili kurahisisha na kuboresha utendaji kazi wa Kitengo hiki. Mfano, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, *FIU* iliwasilisha taarifa fiche 333 kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali na kati ya hizo, taarifa 46 tu ndio zilijibiwa. Changamoto hii inasababisha Kitengo hiki kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi; na

Mheshimiwa Spika, namba tatu; taasisi za kuchambua zinashughulikia zaidi makosa tangulizi bila kuangalia mazalia au mapato haramu na kusababisha matumizi madogo ya taarifa fiche za fedha. Hali hii inasababisha hatua kutochokuliwa za kukamata, kutaifisha au kunyang'anya mapato ya uhalifu na hivyo kuikosesha nchi ushawishi wa takwimu za namna ambavyo mfumo wetu wa kudhibiti fedha haramu ulivyo thabiti.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba watoa taarifa wote wanawasilisha taarifa kwa mujibu wa sheria na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya waliothibitika kutenda makosa chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa dhahabu zinazonunuliwa na Benki Kuu ya Tanzania; Mwaka wa Fedha 2023/2024, Benki Kuu ya Tanzania iliweka lengo la kuhifadhi tani sita za dhahabu (fedha) ambazo hadi kufikia mwezi Mei 2024, kiasi kilichonunuliwa ni kilogramu 418 sawa na 14.35% ya lengo la mwaka. Kushindwa kufikia lengo kumesababishwa na sababu zifuatazo: -

(i) Malipo ya mrabaha wa asilimia sita inayotozwa kwa wauzaji kwenye viwanda vya kuchenjulia dhahabu nchini;

(ii) Serikali kupakia moja ya tatu ($^1/_3$) ya malipo ya mrabaha kwa njia ya fedha badala ya kupokea mrabaha kama dhahabu;

(iii) Serikali kupokea gawio kwa kampuni za madini ambazo ni mwanahisa kwa njia ya fedha badala ya dhahabu;

(iv) Benki Kuu kununua dhahabu kutoka kwenye kampuni za dhahabu, kiwango cha dhahabu chenye thamani sawasawa na kile kinacholipwa Serikani kama mrabaha kwa asilimia sita na

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye dhahabu inayonunuliwa na Benki Kuu, badala ya kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa asilimia sifuri. Hali hii inasababbisha wauzaji kupendelea kuuza nje ili waombe marejesho ya *VAT (VAT Import)* badala ya kuiuzia Benki Kuu kwa sababu kwa kufanya hivyo kutasababisha kushindwa kuomba marejesho ya kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

(i) Serikali kupunguza mrabaha kwa wauzaji wa dhahabu Benki kuu kutoka asilimia sita hadi asilimia nne inayotozwa;

(ii) Serikali kupokea moja ya tatu ($^1/_3$) ya malipo ya mrabaha kwa njia ya dhahabu;

(iii) Serikali kupokea gawio kwa kampuni za madini ambazo ni mwanahisa kwa njia ya dhahabu;

(iv) Serikali kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Kodi kwa ongezeko la thamani na kuanza utaratibu wa Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kutoza kiwango cha asilimia sifuri kwa dhahabu inayouzwa Benki Kuu; na

(v) Serikali kusamehe mrabaha wa asilimia sita kwa kampuni za dhahabu zinazouza dhahabu kwa benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yataleta matokeo chanya kwa kuimarisha akiba ya fedha za kigeni itakayokidhi mahitaji ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kuhimiza kupunguza matumizi ya fedha taslimu *(cashless)*; Kamati ilibaini kuwa moja ya changamoto katika ukusanyaji wa kodi ni matumizi ya fedha taslimu. Aidha, Serikali imekuwa ikishindwa kufuatilia miamala ya biashara kwa sababu ya malipo kufanyika kwa fedha taslimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko ya Sheria ya Mfumo wa Malipo Sura Na. 437 na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura Na. 438 na kuanzisha sharti la kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa. Aidha, mabadiliko haya yanaweza kuweka mazingira mahsusi yatakayowezesha matumizi ya fedha taslimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi na kuhimiza watoa huduma za kifedha kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kufungua akaunti na kuweka fedha zao kwenye benki na kuwahamasisha kuacha kutumia fedha taslimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupunguza gharama za miamala katika mfumo wa malipo madogo ya papo kwa hapo *(TIPS)*; mwaka 2021 Serikali ilianzisha Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa hapo *(Tanzania Instant Payment System - TIPS)*. Mfumo huu umewezesha kuunganisha watoa huduma wote wanaotumia mfumo wa malipo ya rejareja *(retail payment)* kupitia simu za mikononi, benki au msimbo wa *QR*.

Mheshemiwa Spika, mfumo huu umeongeza ufanisi katika utumiaji wa miamala midogo midogo kutoka kwa mtoa huduma

mmoja kwenda mwingine kwa uharaka na uhakika zaidi. Hadi kufikia Mwezi Machi 2024, jumla ya watoa huduma 45 walikuwa wamesajiliwa katika mfumo huo na jumla ya miamala milioni 344.85 yenye thamani ya shilingi trilioni 20.540 ilifanyika kupitia mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo imepunguza gharama za kutumia fedha kutoka benki moja kwenda benki nyingine kwa mujibu wa tangazo la Benki Kuu tarehe 22 Aprili, 2024. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa bado viwango vya tozo vya miamala vimebaki kuwa juu katika kuhamisha fedha kutoka mtandao mmoja wa simu kwenda mtandao mwingine au kutoka katika mtandao wa simu kwenda benki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya gharama za miamala kutoka mtandao mmoja wa simu kwenda mtandao mwingine au kwenda benki na kutoka benki moja na kwenda benki nyingine. Lengo la mapitio hayo ni kuhakikisha gharama hizo zinaakisi punguzo la gharama linalotokana na Mfumo wa *TIPS*. Hatua hii inasaidia kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwa na kufanya malipo kwa kupitia mifumo ya benki na mitandao ya simu na Serikali itakusanya mapato zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa sekta ya huduma ndogo ya fedha nchini; sekta ndogo ya fedha ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Sura Na. 342. Sekta hii ni muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi wa kipato cha chini wakiwemo vijana, wanawake, wajasiriamali, kaya na makundi maalumu. Hadi kufikia Desemba 2023, Benki Kuu imetoa leseni 1569 kwa watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili (II) ambao ni watoa huduma ndogo za fedha wasiopokea amana *(Non - Deposit Take Microfinance Service Providers)*. Aidha, sekta hii imekuwa na changamoto ya ongezeko la vikundi vidogo vya kukopesha fedha visivyo rasmi na visivyozingatia sheria na kanuni za sekta hii ambavyo vimekuwa vikitoza asilimia kubwa ya riba isiyo rafiki kwa mkopaji. Changamoto hii imekuwa ikiwaathiri wakopaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 52 cha Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha kinaweka masharti ya kumlinda mteja. Kifungu icho kina masharti yafuatayo, ninanukuu;

"Kifungu Na. 50:

*(1) A microfinance service providers shall comply with the principles of consumer protection as provided for in the applicable laws and in the regulations made under this Act;*

*(2) Subject to sub section (1), the principles of consumer protection prescribed in the regulations shall include:*

*(a) Terms and conditions of credit or related service that are transparent, fair, legible and protect the rights and interests of microfinance consumers or members;*

*(b) Complaints handling and dispute resolution mechanism; full disclosure of relevant information on the products and services provided;*

*(d) Requirement for the vetting of the standard credit contracts or agreements and financial education to the consumers.*

*(f) Transparency on interest rates, fees or penalties; and*

*(g) Any other principle for the purpose of ensuring fair treatment of consumers.*

*(4) Not withstanding the provisions of sub sections (2) and (3), any term or condition stipulated in a contract or any relevant document purporting to grant to a microfinance service provider authority to unilaterally introduce or modify interest rate or any other loan condition shall be null and void; and*

*(5) Where a microfinance service provider without reasonable cause, fails to comply with the provisions of this*

*section, the Bank or Delegated Authority shall take such measures as may be appropriate to ensure compliance.*"

Mheshimiwa Spika, masharti niliyoyasoma katika Kifungu hiki ni tiba ya mikopo kausha damu. Ni wazi kwamba Wizara ya Fedha wana wajibu wa kuhakikisha masharti ya Kifungu hiki yanafuatwa kikamilifu na wakopeshaji. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wakopeshaji wote nchini wanafuata masharti ya Kifungu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ninapenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Aidha, ninapenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wa kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nimshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El Maamri Mwamba, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao katika kujadili, kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninapenda kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles Kichere kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kamati ya Bajeti itahakikisha katika kipindi chote kwamba, Ofisi yake inapata rasilimali fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Majina ya Wajumbe kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi *(ndc)*, kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninaliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu nane ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Fedha yenye thamani ya shilingi 18,318,540,654,799 ambazo shilingi 3,513,424,470,850 ni mishahara na shilingi 14,171,648,516,000 ni matumizi mengineyo na shilingi 632,567,667,949 ni matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa, ninaomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA PAMOJA NA MAFUNGU YALIYO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2023/24 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

mafungu 8 ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya Nane cha Kanuni za Kudumu za Bunge kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kuisimamia Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zilizopo chini yake. Vilevile, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge ya Bajeti imechambua Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, na kujiridhisha kwamba mapendekezo ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja, yanafaa kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Mafungu hayo ni kama ifuatavyo: -

i. **Fungu 001** – Deni la Serikali
ii. **Fungu 006 –** Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali
iii. **Fungu 010 –** Tume ya Pamoja ya Fedha
iv. **Fungu 013 –** Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu
v. Fungu 021 – Hazina
vi. **Fungu 022 –** Huduma za Mfuko Mkuu
vii. **Fungu 023 –** Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
viii. **Fungu 045** – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
ix. **Fungu 050 –** Wizara ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** hivyo, Taarifa hii inayowasilisha leo imejielekeza katika maeneo makuu matatu ambayo ni: -

i. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/24;

ii. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25; na

iii. Maoni na Mapendekezo ya Ujumla ya Kamati.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha ina jumla ya Mafungu 8 pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi fungu 45. **Jedwali namba 1** linaonyesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti za mafungu yote yaliyo chini ya Wizara ya Fedha hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024

**Jedwali Na. 1. Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha Mafungu 8 kwa mwaka 2023/24**

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2023/24 | Fedha zilizotolewa hadi Aprili, 2024 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| **001. Deni la Serikali** | | | |
| Matumizi mengineyo | **10,480,130,968,000** | **8,853,939,090,000** | **84.48** |
| **006. Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali** | | | |
| Mishahara | 1,948,234,000.00 | 1,468,447,400.00 | 75.37 |
| Matumizi mengineyo | 9,724,229,733.33 | 6,215,343,914.12 | 63.92 |
| Maendeleo Ndani | 875,750,000.00 | 360,000,000.00 | 41.12 |
| Maendeleo Nje | - | - | |
| **Jumla Ndogo** | **12,548,213,733.00** | **8,043,791,314.12** | **64.10** |
| **010. Tume ya Pamoja ya Fedha** | | | |
| Mishahara | 813,300,000 | 581,201,460.00 | 71.46 |
| Matumizi mengineyo | 2,650,549,000 | 2,010,405,357.20 | 75.85 |
| **Jumla Ndogo** | **3,463,849,000** | **2,591,606,817.20** | **74.82** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **013. Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu** | | | |
| Matumizi mengineyo | 3,861,365,000 | 3,090,748,912.07 | 80.04 |
| Maendeleo Ndani | - | | |
| Maendeleo Nje | 455,000,000 | 0.00 | 0.00 |
| **Jumla Ndogo** | **4,316,365,000** | **3,090,748,912.07** | **71.61** |
| **021. Hazina** | | | |
| Mishahara | 1,609,987,716,000 | 276,201,368,590.52 | 17.16 |
| Matumizi mengineyo | 724,516,334,000 | 1,106,818,202,793.41 | 152.77 |
| Maendeleo Ndani | 457,553,092,000 | 361,942,787,399.55 | 79.10 |
| Maendeleo Nje | 33,294,058,000 | 6,828,661,345.85 | 20.51 |
| **Jumla Ndogo** | **2,825,351,200,000** | **1,751,791,020,129.33** | **62.00** |
| **022. Huduma ya Mfuko Mkuu** | | | |
| Mishahara | 13,065,211,000 | 8,913,119,318.70 | 68.22 |
| Matumizi mengineyo | 2,296,006,721,075 | 1,597,458,524,375.00 | 69.58 |
| **Jumla Ndogo** | **2,309,071,932,075** | **1,606,371,643,693.70** | **69.57** |
| **023. Idara ya Mhasibu Mkuu** | | | |
| Mishahara | 7,157,764,000.00 | 5,675,952,301 | 79.29 |
| Matumizi mengineyo | 57,796,726,925.44 | 44,921,195,236.85 | 77.72 |
| Maendeleo Ndani | 1,880,000,000.00 | 1,214,160,000 | 64.58 |
| Maendeleo Nje | - | - | |
| **Jumla ndogo** | **66,834,490,925.44** | **51,811,307,538** | **77.52** |

| 50. Wizara ya Fedha | | | |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 58,240,283,129 | 42,508,114,810 | 72.98 |
| Matumizi mengineyo | 67,565,953,217 | 52,542,709,833 | 77.77 |
| Maendeleo Ndani | 27,969,087,000 | 16,969,872,092 | 60.67 |
| Maendeleo Nje | 33,041,720,251 | - | 0 |
| **Jumla Ndogo** | **186,817,043,597** | **112,020,696,735** | **59.96** |
| **Jumla Kuu** | **15,888,534,062,330.80** | **12,389,659,905,139.40** | **77.98** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali*

## 2.1. Uchambuzi wa Mafungu

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 mafungu 8 ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya **shilingi 15,888,534,062,330.80**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024 jumla ya **shilingi 12,389,659,905,139.40** zilipokelewa sawa na **asilimia 77.98** ya bajeti iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo, **shilingi 8,853,939,090,000** ni kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali, **shilingi 335,348,203,880.22** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 2,813,057,130,421.65** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha kwa upande wa fedha za maendeleo **shilingi 387,315,480,837.40** zilitolewa, kati ya fedha hizo **shilingi 380,486,819,491.55** ni fedha za ndani na **shilingi 6,828,661,345.85** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Mafungu yote 8 na masuala yafuatayo yalibainika:-

### 2.1.1. Fungu 01 – Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Fungu hili liliidhinishiwa **shilingi 10,480,130,968,000** kwa ajili ya kulipa deni la Serikali. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 6,059,835,157,000** ni kwa ajili ya kulipa deni la ndani lililoiva, **shilingi 4,401,797,890,000** ni kwa ajili ya kulipa deni la nje lililoiva. Aidha, kiasi cha **shilingi 18,327,921,000** ni kwa ajili ya

kusimamia deni la Serikali na **shilingi 170,000,000** ni kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili 2024, **shilingi 8,853,939,090,000** zimetolewa sawa na **asilimia 84.48** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho **shilingi 3,919,281,144,000** zimetumika kulipa deni la nje, **shilingi 4,922,052,257,000** zimetumika kulipa deni la ndani, **shilingi 12,512,145,000** zimetumika kusimamia deni na **shilingi 93,544,000** zimetumika kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

**2.1.2. Fungu 06 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Fungu hili kabla ya uhamisho liliidhinishiwa kutumia jumla ya **shilingi 10,948,899,733.33**. Fungu hili liliongezewa fedha na kufanya bajeti yake baada ya uhamisho kuwa **shilingi 12,548,213,733.00** na kati ya fedha hizo, **shilingi 1,948,234,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 9,724,229,733.33** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 875,750,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **shilingi 8,043,791,314.12** zimetolewa sawa na **asilimia 64.10** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,468,447,400** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 6,215,343,914.12** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 360,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Fungu hili limekuwa likikabiliwa na changamoto ya upungufu wa wakaguzi wa ndani 916, pamoja na bajeti ndogo ikilinganishwa na majukumu yake ambayo ni kukagua matumizi na mapato ya Serikali na kusimamia vitengo vya ukaguzi wa ndani wa Serikali. Endapo kitengo hiki kingetengewa bajeti ya kutosha kingesaidia kupunguza hoja za ukaguzi ambazo huwa zinaibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Idara hii kwa kuitengea

fedha za kutosha zitakazowezesha kuajiri watumishi na kuongeza vitendea kazi.

### 2.1.3. Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Pamoja ya Fedha iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **shilingi 3,463,849,000** kati ya fedha hizo, **shilingi 2,650,549,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **shilingi 813,300,000** ni kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **shilingi 2,591,606,817.20** sawa na **asilimia 74.82** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotolewa, **shilingi 581,201,460.00** ni mishahara na **shilingi 2,010,405,357.20** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ibara ya 134 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Pamoja ya Fedha inatakiwa kuwa na makamishna wasiozidi saba ambao watateuliwa na Rais, na watakuwa na kazi ya kusimamia Tume kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka mitano. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba mpaka sasa Tume haina makamishna walioteuliwa. Hatua hii imekuwa ikiathiri utekelezaji wa majukumu yake. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kumshauri Mhe. Rais kuteua Makamishna wa Tume ili ifanye kazi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.1.4. Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU)

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Fungu 13 liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 4,316,365,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,861,365,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 455,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **shilingi 3,090,748,912.07** zilipokelewa sawa na **asilimia 71.61** ambazo ni fedha za matumizi mengineyo. Mpaka sasa Serikali bado haijatoa fedha za maendeleo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ilitakiwa kuwekwa chini ya uangalizi wa Kikosi Kazi cha Kusimamia mwenendo wa kudhibiti Utakatishaji

wa Fedha haramu (Financial Action Task Force -FATF) jambo hili lingekuwa na madhara hasi kwa Taifa. Hatua hii inatokana na kasoro zilizobainishwa na Kikosi Kazi hicho kwamba Tanzania ni eneo oevu la kutakatisha fedha. Hivyo, Kitengo hiki kilitengeneza mipango mikakati 21 kwa ajili ya kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Kikosi Kazi hicho. Hata hivyo, ni mikakati 5 kati ya mipango 21 ndio imefanyiwa kazi. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inafanyia kazi mikakati iliyobaki ili nchi isiwekwe chini ya uangalizi wa chombo hicho.

**a) Serikali Kurasimisha Sekta isiyo Rasmi**

**Mheshimiwa Spika,** sekta isiyo rasmi nchini ni eneo linaloweza kutumika katika ufadhili wa ugaidi na utakasishaji wa fedha haramu. Hivi sasa miamala shuku mingi inatokana na biashara ya kubadilisha fedha za kigeni katika maeneo yasiyo rasmi na hivyo inakuwa vigumu kuweza kufuatilia taarifa zake. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kurasimisha Sekta isiyo rasmi ambayo inakadiriwa kuwa **asilimia 60** ya uchumi. Hatua hii itasaidia kufuatilia taarifa za miamala shuku kwa ukaribu zaidi na hivyo kudhibiti vitendo vya utakasishaji wa fedha haramu.

**2.1.5. Fungu 21 – Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Fungu 21 liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 2,825,351,200,000.** Kati ya fedha hizo **shilingi 2,334,504,050,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 490,847,150,000** ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, Fungu 21 limepokea jumla ya **shilingi 1,751,791,020,129.33** sawa na **asilimia 62**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,383,019,571,383.93** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 368,771,448,745.40** ni fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** fungu hili ndilo linasimamia bajeti ya Serikali. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaweka masharti ya uhamisho wa fedha ndani ya Fungu na baina ya Mafungu. Vilevile, Kanuni za Sheria ya Bajeti zimeweka ukomo usiozidi **asilimia 7** kwa Afisa Masuuli kuhamisha fedha ndani ya fungu na ukomo usiozidi **asilimia 5** ya bajeti ya Serikali kwa uhamisho wa

fedha kati ya mafungu. Aidha, Kamati imebaini changamoto kwenye Kanuni hiyo ambayo haijaweka ukomo wa kiasi cha uhamisho ndani ya fungu unaozidi **asilimia 7** ambao Afisa Masuuli anapaswa kuomba idhini kwa Waziri wa Fedha. Kutokuwepo kwa ukomo unaozidi uhamisho wa **asilimia 7** kumefanya Maafisa Masuuli kufanya uhamisho unaohitaji kibali cha Waziri. Jambo hili lina athiri  utekelezaji wa baadhi ya shughuli ndani ya Fungu. Aidha, kanuni zinazoweka ukomo zimeweka ukomo wa fedha kuhamishwa bila kuweka ukomo wa fedha kupokelewa.

**2.1.6. Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu w**a Serikali

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Fungu hili liliidhinishiwa na Bunge kiasi cha **shilingi 2,314,839,338,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 13,065,211,000** ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 022, na **shilingi 2,296,006,721,075** ni kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **shilingi 1,606,371,643,693.70** zimepokelewa sawa na **asilimia 69.57** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,913,119,318.70** ni mishahara na **shilingi 1,597,458,524,375** ni matumizi mengineyo. **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia utekelezaji na utendaji kazi wa Fungu hili na inaitaka Serikali kushughulikia masuala yafuatayo: -

**a) Serikali kurahisisha utaratibu wa Pensheni zinazolipwa kwa Wastaafu kupitia Hazina pamoja na Kuhuisha viwango vyake.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba wastaafu nchini wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo viwango vya mafao ambavyo haviakisi hali ya sasa ya maisha na kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kufuatilia mafao yao ili kuhakiki nyaraka za taarifa za wastaafu licha ya kuwepo kwa mifumo ya TEHAMA. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

i. Serikali kuhuisha viwango vya mafao kwa wastaafu ili kuendana na hali halisi ya maisha;

ii. Kuweka vituo vya kufuatilia pensheni katika ngazi za Wilaya ili kusaidia wastaafu kutosafiri umbali mrefu kufuatilia stahiki zao; na

iii. Kutunza nyaraka zenye taarifa za Watumishi na wastaafu kidijitali ili kuondoa usumbufu kwa watumishi waliostaafu na watakaostaafu.

**b) Serikali kufanya tathmini ya mishahara ya Watumishi wa Umma ili iendane na hali ya uchumi.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba watumishi wengi wa Serikali wanalipwa mishahara midogo isiyoendana na kupanda kwa gharama za maisha. Kwa kutambua suala hili Serikali imekuwa ikiwalipa watumishi posho ili kupunguza ugumu wa maisha. Jambo hili humsaidia mtumishi kwa muda anaokuwa kazini lakini halimsaidii baada ya kustaafu kwa sababu posho hazitumiki katika kukokotoa pensheni. Posho hizo zinaweza kuongezwa ama kupunguzwa wakati wowote. Hivyo, hiki sio chanzo cha uhakika cha mapato kwa mtumishi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo Kamati inaishauri Serikali kuongeza viwango vya mishahara kwa Watumishi ili kuongeza kiwango cha pensheni watakachopokea pindi wanapostaafu. Aidha, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kujumuisha kiwango cha posho katika mishahara ya watumishi ili kuongeza kiasi cha pensheni pindi watumishi hao watakapostaafu.

**2.1.7. Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 66,834,490,925.44.** Kati ya fedha hizo **shilingi 57,796,726,925.44,** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 7,157,764,000** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 1,880,000,000** fedha za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya **shilingi 51,811,307,538** zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na **asilimia 77.52.** Kati ya kiasi hicho, **shilingi 5,675,952,301** ni kwa

ajili ya mishahara, **shilingi 44,921,195,236.85** ni matumizi mengineyo na **shilingi 1,214,160,000** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu linalotekelezwa na Fungu hili ni kusimamia mifumo ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba ukusanyaji wa mapato kwenye Serikali za mitaa umekuwa ukisua sua kutokana na matumizi hafifu ya mifumo na hivyo kusababisha upotevu wa mapato. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuimarisha Mfumo wa Tausi ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

### 2.1.8. Fungu 50: Wizara ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 186,817,043,597**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 125,806,236,346** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 61,010,807,251** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Bajeti ya Fungu hili iliongezeka kwa **shilingi 17,159,149,597** kutokana na uhamisho wa fedha nje ya bajeti ya fungu. Uhamisho huu ulifanyika kwa ajili ya kuwezesha usikilizaji wa mashauri ya kodi, ujenzi wa mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma, utekelezaji wa programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma, marekebisho ya mishahara na kugharamia malipo ya madai ya fidia.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya **shilingi 112,020,696,734** zimetolewa sawa **asilimia 60**. Kati ya fedha hizo **shilingi 42,508,114,810** ni mishahara, **shilingi 52,542,709,833** ni matumizi mengineyo na **shilingi 16,969,872,092** ni fedha za ndani za maendeleo. Aidha, fedha za nje za maendeleo hazikutolewa.

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele (c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ina jukumu la kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali. Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na majukumu juu ya mambo yafuatayo;-

i. Kuhakikisha kwamba fedha zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali matumizi yake yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 136 ya Katiba hii, na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

ii. Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Bunge, na ambazo zimetumika, zimetumiwa kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

iii. Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

### 3.1. Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Fungu 45

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ilitengewa Jumla ya **shilingi 97,134,274,000** kati ya

Fedha hizo **shilingi 70,830,676,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida **shilingi 9,411,878,000** zilikuwa ni kwa ajili utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, fungu hili lilipangiwa kukusanya maduhuli ya **shilingi 900,000,000**. Hadi mwezi Aprili 2024 Fungu 45 limepokea jumla ya **shilingi 81,449,340,687** sawa na **asilimia 83.9** ya Bajeti yote. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyo onekana kwenye jedwali Namba 2 hapo chini.

**Jedwali Na. 2. Mchanganuo wa Fedha za Matumizi zilizotolewa hadi Aprili, 2024**

| Aina ya Matumizi | Bajeti iliyoidhinishwa 2023/24 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 16,891,720,000 | 15,553,632,760 | 92.1 |
| Matumizi Mengineyo | 70,830,676,000 | 61,469,495,574 | 86.7 |
| Maendeleo Ndani | 8,828,000,000 | 4,426,212,353 | 50.1 |
| Maendeleo Nje | 583,878,000 | - | 0.0 |
| JUMLA | **97,134,274,000** | **81,449,340,687** | **83.9** |

***Chanzo**: Randama Fungu 45, 2024*

**3.2. Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Katika majadiliano baina ya Kamati na Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali masuala yafuatayo yalibainika: -

i. Ofisi ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina changamoto ya uhaba wa Watumishi wenye ujuzi na taaluma unahitajika;

ii. Maslahi yasiyoridhisha ya watumishi wa Ofisi ya CAG yanayoathiri utendaji kazi wa watumishi;

iii. Ongezeko la mawanda ya ukaguzi ambayo hayaendani na ongezeko la Bajeti. Mfano Kwa mujibu wa Kanzidata ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Serikali ina jumla ya mifumo 460 ya TEHAMA. Hadi kufikia tarehe 19 Machi, 2024 Ofisi ya CAG ilifanya kaguzi za mifumo 49 tu kwenye Taasisi 24 za Serikali;

iv. Utolewaji wa Fedha kwa Miradi ya Maendeleo si wa kuridhisha ambapo hadi mwezi Aprili 30 kiasi kilichotolewa ni **asilimia 24.4** ya Bajeti iliyoidhinishwa ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/24. Hatua hii imekwamisha juhudi za kuwaondoa wakaguzi wa CAG kutoka kwenye majengo ya wakaguliwa na ukarabati wa Ofisi ya Kitengo cha Usaidizi wa Kiufundi katika Ukaguzi (TSSU) jengo la Makao Makuu Dodoma.

v. Hati za madai zenye thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 3.1** zilizowasilishwa na CAG Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo hazijalipwa na Serikali hadi mwezi Aprili.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, Kamati imetoa ushauri kwa Serikali kwa masuala yafuatayo;

i. Serikali ifanye marekebisho ya maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuyahuisha na nchi nyingine. Taarifa ya marekebisho hayo iwasilishwe mbele ya Kamati mwezi Januari, 2025 ili kuhakikisha kwamba Watumishi wa Ofisi wanalipwa malipo stahiki. Aidha, Kamati iliagiza Ofisi ya NAOT ipitie upya muundo wake ili kuendana na mahitaji ya kiukaguzi ya sasa;

ii. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilisha Hati za Madai ya Wakandarasi zenye jumla ya thamani ya **shilingi bilioni 5.02.** Hadi mwezi Aprili, 2024 Ofisi hiyo imepokea jumla ya **shilingi bilioni 1.91** sawa na **asilimia 38** ya hati zilizowasilishwa Wizara ya Fedha. Kamati inaitaka Serikali kufanya malipo ya hati za madai zilizobakia zenye thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 3.1** zilizowasilishwa Wizara ya Fedha;

iii. Kamati iliagiza Serikali kuipatia NAOT kibali cha kuajiri na kuongeza Bajeti ya Mishahara ya mwaka 2024/25 kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kuajiri watumishi 81 ili kukabiliana na upungufu uliopo. Hatua hii itawezesha Ofisi ya CAG kupanua mawanda ya ukaguzi katika maeneo ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA, Ukaguzi wa Kiufundi, Ukaguzi wa Sekta ya Madini na Uziduaji pamoja na Ukaguzi wa Miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi; na

iv. Kamati iliagiza Wizara ya Fedha kuhakikisha ifikapo tarehe 30 Juni, 2024 inatoa fedha zote za maendeleo zilizosalia kwa fungu hili ili liweze kutekeleza miradi yake ya maendeleo hususan ujenzi wa ofisi mikoani ili kuwaondoa wakaguzi kwenye Ofisi za wakaguliwa.

**4.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

**4.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu nane ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Fedha pamoja na mafungu yaliyo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 18,204,911,822,799**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 17,583,812,154,850** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 621,099,667,949** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Jedwali namba 3 ni mchanganuo wa maombi ya fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa Fedha 2024/25.

**Jedwali Na.3. Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2024/25**

| Fungu | Matumizi Mengineyo | Mishahara | Miradi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 01 | 13,131,838,005,000 | - | - | 13,131,838,005,000 |
| 06 | 11,151,638,000 | 1,894,788,000 | 1,229,451,000 | 14,275,877,000 |
| 10 | 833,157,000 | 3,575,157,000 | 1,598,249,000 | 6,006,563,000 |
| 13 | 3,768,237,000 | - | - | 3,768,237,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21 | 847,578,588,000 | 754,543,566,850 | 572,114,830,949 | 2,174,236,985,799 |
| 22 | 15,119,603,000 | 2,614,813,247,000 | | 2,629,932,850,000 |
| 23 | 7,083,142,000 | 55,279,317,000 | 7,292,385,000 | 69,654,844,000 |
| 50 | 73,653,878,000 | 62,679,831,000 | 38,864,752,000 | 175,198,461,000 |
| **Jumla** | **14,091,026,248,000** | **3,492,785,906,850** | **621,099,667,949** | **18,204,911,822,799** |

***Chanzo:*** *Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha*

**4.1.1. Uchambuzi wa Baadhi ya Mafungu**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa mafungu yote 8, Kamati ilibaini na kupendekeza masuala yafuatayo:-

**a) Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina jukumu la kusimamia Wakaguzi wote wa ndani nchini pamoja na kuwajengea uwezo ili waendane na viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Idara hii imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani. Kukosekana kwa mafunzo kunasababisha hesabu kutoandaliwa kwa kuzingatia misingi ya ukaguzi. Hali hii inasababisha wingi wa hoja za ukaguzi pamoja na kuachwa nyuma na mabadiliko ya mifumo. Ofisi hii imetengewa kiasi cha **shilingi 629,770,000** kwa ajili ya mafunzo. Hata hivyo, kiwango hiki hakikidhi mahitaji ikizingatiwa kwamba Idara hii ina jumla ya wakaguzi wa ndani 1,553 wanaojumuisha wakaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliilekeza Serikali kuongeza jumla ya **shilingi 2,255,000,000** kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani pamoja na kununua vitendea kazi kama vile magari na tarakilishi mpakato kutokana na kuwepo na uhaba wa vetendea kazi hivyo. Serikali ilikubali pendekezo hili na kutoa kiasi hicho cha fedha ambacho kitasaidia kuongeza ufanisi katika kusimamia mapato na matumizi ya Serikali na uandaaji wa Taarifa za kiuhasibu.

**b) Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha kwa kipindi chote haijawahi kuwa na Ofisi za kudumu na badala yake imekuwa ikipanga katika majengo mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, kwakuwa Taasisi nyingi za Umma zimehamia Dodoma na hivyo kuacha majengo yake Dar es salaam, ni vyema wakaomba moja ya jengo ili watumie kama ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Tume imepatiwa jengo lililokuwa la Baraza la uwezeshaji jijini Dar es salaam, ambapo zimetengwa jumla **shilingi 1,598,249,000** katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya ukarabati. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatolewa kabla ya tarehe 30 Machi, 2025 ili kukamilisha ukarabati wa Ofisi kuliko kuendelea kulipa kodi ya pango. Aidha, upatikanaji wa Ofisi kwa upande wa Zanzibar, Kamati ilijulishwa kuwa mchakato bado unaendelea ili Tume iweze kupata Ofisi katika moja ya Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar.

**c) Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Umma, kutoa miongozo ya kihasibu, mapato na matumizi ya mali za umma na kusimamia uendeshaji wa mifumo ya fedha. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Idara hii inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Wahasibu. Hata hivyo, bajeti ya mafunzo ya Idara hii imepungua kutoka **shilingi 3,512,069,500** mwaka 2023/24 hadi **shilingi 2,389,900,000** mwaka 2024/25 ikiwa ni pungufu ya **shilingi 1,122,169,500**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa mahitaji ya fedha kwa ajili ya mafunzo ya wahasibu, ilibaini kiasi kinachohitajika ni **shilingi 2,122,169,500**. Hivyo, Kamati iliilekeza Wizara kuongeza kiasi hicho cha fedha kwa Idara hii kwa ajili ya kufanya mafunzo. Serikali ilikubaliana na Kamati na

kuongeza bajeti ya Fungu hili kutoka **shilingi 67,532,675,000** hadi **shilingi 69,654,844,000.**

**d) Fungu 021 – Hazina - Taasisi ya Msuluhishi wa Migogoro na Taarifa za Kodi (Tax Ombudsman)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Taasisi hii ilitengewa jumla ya **shilingi 3,500,000,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba fedha hizi hazitoshi kulingana na mahitaji ya kutatua malalamiko ya kodi, kutoa elimu kwa Umma kuhusu uwepo wa Ofisi na kufanya mafunzo kwa Watumishi kuhusu uendeshaji na usuluhishi wa malalamiko. Hivyo, Kamati ililekeza Wizara kuiongezea Taasisi hii kiasi cha **shilingi 1,050,000,000** kwa ajili ya kugharamia mahitaji hayo. Serikali ilikubaliana na Kamati na kuongeza bajeti ya Taasisi hiyo kutoka **shilingi 5,162,821,000** hadi **shilingi 6,212,821,000.**

**4.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka wa fedha 2024/25 imepanga kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka mitano (2021/22 – 2025/26) uliorejewa mwaka 2022/23 ambao unajielekeza kwenye kuimarisha shughuli za Ukaguzi wa Nje wa Sekta ya Umma hapa nchini. Kimsingi, Ofisi imelenga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

a) Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma kama yalivyoidhinishwa na Bunge Mwaka 2023/24 chini ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma na kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla au ifikapo tarehe 31 Machi, 2025;

b) Kufanya kaguzi za Kiufundi, Ufanisi, Miradi ya Maendeleo na Mifumo ya TEHAMA;

c) Kufanya kaguzi maalum na wa kiuchunguzi kulingana na mahitaji ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na maombi ya kaguzi hizo kutoka vyombo mbalimbali vya Serikali ikiwemo TAKUKURU na wadau wengine;

d) Kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi na za Kisekta ili kuzielewa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge;

e) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya Ofisi;

f) Kuanza ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa ya Ruvuma na Mwanza awamu ya kwanza pamoja na kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Ukaguzi katika Mikoa ya Songwe na Katavi. Aidha, Ofisi imepanga kufanya ukarabati wa majengo ya Ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali nchini;

g) Kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za uendeshaji wa Ofisi, ulipaji wa stahili mbalimbali za Watumishi kwa wakati na upatikanaji wa vitendea kazi ikiwemo tarakilishi, samani na magari;

h) Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu shughuli za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi;

i) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwenye maeneo mapya yanayohitaji kukaguliwa ikiwemo Sekta ya Uziduaji, Miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi, Ukaguzi wa Kiufundi, Mifumo ya TEHAMA na ukaguzi wa wakati (Real Time Audit); na

j) Kuimarisha Viwango vya utendaji kazi wa Ofisi na kutoa elimu kwa watumishi kuhusu namna bora ya kutekeleza

mikakati yenye kuhuisha ubora wa viwango vya Kimataifa (ISO9001: 2015 Certified).

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza vipaumbele vyake imepanga kutumia jumla ya **shilingi 113,628,832,000** katika mwaka wa fedha 2024/25. Kiasi hicho kinajumuisha **shilingi 900,000,000** fedha za Maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na **shilingi 111,828,832,000** fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa ni **shilingi 99,460,832,000** ambazo zinajumuisha **shilingi 20,638,564,000** fedha za Mishahara ya Watumishi na **shilingi 78,822,268,000** fedha za Matumizi Mengineyo.

Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi kinachoombwa ni **shilingi 11,468,000,000** kati ya fedha hizo **shilingi 8,828,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 2,640,000,000** ni fedha za nje. Jedwali namba 4 linaonyesha Mchanganuo wa Fedha hizo.

**Jedwali Na. 4. Makadirio ya Bajeti ya Fungu 45 kwa mwaka 2024/25**

| Maelezo | Bajeti iliyoidhinishwa 2023/24 (A) | Mkadirio Mwaka 2024/25 (B) | Tofauti (B-A) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Maduhuli** | 900,000,000 | 900,000,000 | 0 | 0 |
| **Matumizi ya Kawaida** | | | | |
| Mishahara | 16,891,720,000 | 20,638,564,000 | 3,746,844,000 | 22.18 |
| Matumizi Mengineyo | 70,830,676,000 | 78,822,268,000 | 7,991,592,000 | 11.28 |
| Jumla ya Matumizi ya Kawaida | **87,722,396,000** | **99,460,832,000** | 11,738,436,000 | **13.38** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | | | | |
| Fedha za ndani | 8,828,000,000 | 8,828,000,000 | 0 | |
| Fedha za nje | 583,878,000 | 2,640,000,000 | 2,056,122,000 | 352.15 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Jumla Matumizi ya Maendeleo** | **9,411,878,000** | **11,468,000,000** | **2,056,122,000** | 21.85 |
| **Jumla Fungu 45** | **98,034,274,000** | **111,828,832,000** | **13,794,558,000** | **14.07** |
| **Ongezeko kutokana na Agizo la Kamati** | **-** | **1,800,000,000** | **1,800,000,000** | **-** |
| **JUMLA KUU** | **98,034,274,000** | **113,628,832,000** | **15,594,558,000** | **15.91** |

***Chanzo**: Randama ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 2024*

### 4.2.1. Uchambuzi wa Maombi ya Fedha kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 iliyowasilishwa mbele ya kamati ilionyesha kuna ongezeka kwa **asilimia 14.2** ikilinganishwa na bajeti ya ofisi hiyo kwa mwaka 2023/24. Ongezeko hili halikuzingatia mabadiliko ya viwango vya kubadilishia fedha, gharama za mafuta pamoja na ongezeko la maeneo ya ukaguzi yaliyotokana na maagizo ya Kamati. Baada ya mashauriano Kamati ilishauri kwamba bajeti ya Ofisi hii iongezwe **shilingi bilioni 1.8** na hivyo kufanya jumla ya bajeti nzima kwa fungu hili kuwa **shilingi bilioni 113.629.**

### 4.2.2. Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya Fedha zote zinazoombwa na Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2024/25 ni **Shilingi 18,318,540,654,799**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,513,424,470,850** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 14,171,648,516,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 632,567,667,949** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Jedwali Na. 5. Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyochini yake kwa mwaka 2024/25**

| Fungu | Matumizi Mengineyo | Mishahara | Miradi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 01 | 13,131,838,005,000 | - | - | 13,131,838,005,000 |
| 06 | 11,151,638,000 | 1,894,788,000 | 1,229,451,000 | 14,275,877,000 |
| 10 | 833,157,000 | 3,575,157,000 | 1,598,249,000 | 6,006,563,000 |
| 13 | 3,768,237,000 | - | - | 3,768,237,000 |
| 21 | 847,578,588,000 | 754,543,566,850 | 572,114,830,949 | 2,174,236,985,799 |
| 22 | 15,119,603,000 | 2,614,813,247,000 | | 2,629,932,850,000 |
| 23 | 7,083,142,000 | 55,279,317,000 | 7,292,385,000 | 69,654,844,000 |
| 50 | 73,653,878,000 | 62,679,831,000 | 38,864,752,000 | 175,198,461,000 |
| **Jumla Ndogo** | **14,091,026,248,000** | **3,492,785,906,850** | **621,099,667,949** | **18,204,911,822,799** |
| 45 | 80,622,268,000 | 20,638,564,000 | 11,468,000,000 | 113,628,832,000 |
| **JUMLA KUU** | **14,171,648,516,000** | **3,513,424,470,850** | **632,567,667,949** | **18,318,540,654,799** |

***Chanzo:*** *Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya CAG,2024*

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25, Kamati inatoa maoni na Mapendekezo yafuatayo: -

### 5.1. Uteuzi wa Wajumbe katika Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB)

**Mheshimiwa Spika,** katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara, TRAB ina wajumbe katika Mikoa 14. Aidha, Kamati ilibaini kuwa mikoa 12 ambayo ni Manyara, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Lindi, Mara, Mbeya, Njombe, Rukwa, Songwe, na Tabora haina wajumbe. Kukosekana kwa Wajumbe katika Bodi kunasababisha mashauri ya kodi kuchukua muda mrefu kusikilizwa na kuwa na mlundikano wa mashauri ambayo hayajasikilizwa. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2022/23 imeainisha mashauri **967** ya kodi kwenye Bodi ya Rufani za Kodi zenye thamani ya **shilingi trilioni 10.48** ikiwa ni ongezeko la

**shilingi trilioni 5.65** sawa na **asilimia 117** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 4.83** za mwaka wa fedha 2021/22. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuchelewa kwa uteuzi wa Wajumbe muhimu wa kusikiliza kesi. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa taratibu za uteuzi wa wajumbe katika Mikoa hiyo zinaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha taratibu za uteuzi katika mikoa 12 iliyobaki ili kuharakisha usikilizwaji wa kesi za kodi katika maeneo hayo. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaowezesha Mjumbe kutoka katika Mkoa mmoja kusikiliza kesi katika Mkoa mwingine ili kupunguza mlundikano wa kesi.

**5.2. Kuboresha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili kuweka ukomo wa muda kwa Kamishina wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuwasilisha Taarifa za Malalamiko ya kodi kwa Ofisi ya Msuluhishi**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi ilizinduliwa rasmi Januari 23, 2024 na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu Sheria ya Fedha namba 8 ya mwaka 2019 ambayo ilirekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi *(Tax Administration Act)* Sura 438 kwa kuongeza sehemu III A – ‘‘Establishment of Tax Ombudsman’’ na marekebisho yake yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha namba 3 ya mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii ina inapokea, inasajili na kusuluhisha malalamiko yatokanayo na usimamizi wa Sheria za Kodi na kutoa mapendekezo ya maboresho ya mfumo wa ukusanyaji kodi nchini kwa lengo la kurahisisha na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji kodi na kuongeza uwajibikaji wa walipa kodi kulipa kodi kwa hiari. Malalamiko yanayoshughulikiwa na Ofisi hii ni yale yanayohusu utaratibu wa usimamizi wa sheria za kodi, masuala ya huduma isiyoridhisha na ya kiutawala ambayo yalitumiwa au yanadaiwa kutumika isivyo haki katika usimamizi wa sheria za kodi na ukiukwaji wa ahadi binafsi zilizotolewa na Mamlaka ya Mapato katika Mkataba wa Mlipakodi wakati wa kutoa huduma kwa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Sheria iliyoanzisha Ofisi hii haibainishi ukomo wa muda kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuwasilisha taarifa za malalamiko kwa ofisi ya Msuluhishi. Changamoto hii imepelekea kuchelewa kwa upatikanaji wa Taarifa na hivyo, Ofisi ya Msuluhishi kushindwa kuchakata malalamiko ndani ya muda wa siku 30. Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi na kuweke muda kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kutoa majibu kuhusu malalamiko ya walipakodi ili kuwezesha malalamiko yasikilizwe ndani ya siku 30.

### 5.3. Serikali kuzitaka Taasisi zote za Fedha kutoa Taarifa za Miamala Shuku kwa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU)

**Mheshimiwa Spika,** Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kina jukumu la kushughulikia taarifa za miamala shuku, taarifa za miamala ya fedha taslimu, taarifa za miamala ya fedha kielektroniki, taarifa za matamko ya usafirishaji wa fedha taslimu na nyaraka za kifedha mipakani. Kitengo hiki huchambua taarifa hizo na kuandaa taarifa fiche (intelligence reports) na kuzisambaza kwa taasisi za uchunguzi kwa ajili ya kuthibitisha uhalali wa miamala hiyo au vinginevyo. Katika uchambuzi wa Bajeti ya kitengo hiki, Kamati imebaini changamoto zifuatazo;-

i Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha Haramu Sura ya 423 inataka mtoa taarifa kuwasilisha taarifa ya miamala anayotilia shaka au shughuli anazofahamu kuwa zinahusika na mapato ya uhalifu, watoa taarifa wengi wamekuwa hawatekelezi takwa hilo la Sheria;

ii Kumekuwa na ushirikiano hafifu baina ya Taasisi zinazoshughulikia taarifa fiche katika kutoa mrejesho wa hatua zilizochukuliwa ili kurahisisha na kuboresha utendaji kazi wa Kitengo hiki. Mfano, katika mwaka wa fedha 2022/23 FIU iliwasilisha taarifa fiche 333 kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali na kati ya hizo, taarifa 46 tu ndio zilijibiwa. Changamoto hii inasababisha Kitengo hiki kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi; na

iii Taasisi za uchunguzi zinashughulikia makosa tangulizi zaidi bila ya kuangalia mazalia au mapato haramu na kusababisha matumizi madogo ya taarifa fiche za fedha. Hali hii inasababisha hatua kutochukuliwa za kukamata, kutaifisha au kunyang'anya mapato ya uhalifu na hivyo kuikosesha nchi ushawishi wa takwimu za namna ambavyo mfumo wetu wa kudhibiti fedha haramu ulivyo thabiti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba watoa taarifa wote wanawasilisha taarifa kwa mujibu wa Sheria na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya waliothibitika kutenda makosa chini ya Sheria hiyo.

**5.4. Kutoza Kodi ya Ongezeka la Thamani kwa kiwango cha Asilimia 0 kwa Dhahabu zinazonunuliwa na Benki Kuu ya Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Septemba, 2022 Bodi ya Benki Kuu ya Tanzania iliidhinisha Mpango wa Ununuzi wa Dhahabu kwa lengo la kuimarisha akiba ya fedha za kigeni. Katika mwaka wa fedha 2023/24 Benki Kuu ya Tanzania iliweka lengo la kununua na kuhifadhi tani 6 za dhahabu fedha, ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2024 kiasi kilichonunuliwa ni kilogramu 418 sawa na **asilimia 14.35** ya lengo la mwaka. Kushindwa kufikia lengo kumesababishwa na sababu zifuatazo;-

i Malipo ya mrabaha ya asilimia 6 inayotozwa kwa wauzaji kwenye viwanda vya kuchenjulia dhahabu nchini;

ii Serikali kupokea 1/3 ya malipo mrabaha kwa njia ya fedha badala ya kupokea mrabaha kama dhahabu;

iii Serikali kupokea gawio kwa makampuni ya madini ambayo ni mwanahisa kwa njia ya fedha badala ya dhahabu;

iv Benki Kuu kununua dhahabu kutoka kwenye makampuni ya dhahabu kiwango cha dhahabu chenye thamani sawa sawa na kile kinacholipwa Serikalini kama mrabaha wa **asilimia 6**;

v Kusamehe Kodi ya Ongezeko la thamani kwenye dhahabu inayonunuliwa na Benki Kuu badala ya kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa **asilimia 0**. Hali hii inasababisha wauzaji kupendelea kuuza nje ili waombe marejesho ya VAT (VAT input) badala ya kuuzia Benki Kuu kwa sababu kwa kufanya hivyo kutasababisha kushindwa kuomba mrejesho wa Kodi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo;

i Serikali kupunguza mrabaha kwa wauzaji wa dhahabu Benki Kuu kutoka **asilimia 6** hadi **asilimia 4** inayotozwa;

ii Serikali kupokea 1/3 ya malipo mrabaha kwa njia ya dhahabu;

iii Serikali kupokea gawio kwa makampuni ya madini ambayo ni mwanahisa kwa njia ya dhahabu;

iv Serikali kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya Ongezeko la Thamani kwa dhahabu inayouzwa Benki Kuu; na

v Serikali kusamehe mrahaba wa **asilimia 6** kwa makampuni ya dhahabu yanayouza dhahabu kwa Benki Kuu.

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yataleta matokea chanya kwa kuimarisha akiba ya fedha za kigeni itakayokidhi mahitaji ya Taifa.

### 5.5. Serikali kuhimiza kupunguza matumizi ya Fedha Taslimu (Cashless)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ulibaini kuwa moja ya changamoto katika ukusanyaji wa kodi ni matumizi ya fedha taslimu. Aidha, Serikali imekuwa ikishindwa kufuatilia miamala ya biashara kwa sababu ya malipo kufanyika kwa fedha taslimu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Mifumo ya Malipo Sura ya 437 na Sheria ya

Usimamizi wa Kodi Sura 438 na kuanzisha sharti la kufanya malipo kwa njia ya kieletroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa. Aidha, mabadiliko hayo yanaweza kuweka mazingira mahususi yatakayo wezesha atomize ya fedha taslimu. Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi na kuhimiza watoa huduma za kifedha kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kufungua akaunti na kuweka fedha zao kwenye mabenki na kuwahamasisha kuacha kutumia fedha taslimu.

**5.6. Benki Kuu kuharakisha Mfumo wa Kufuatilia Mapato yanayotokana na Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchini pamoja na Malipo yanayotokana na mauzo hayo.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba takwimu za mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi zimekuwa zikitofautiana kati ya zile zinazotolewa na mabenki, zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na zinazotolewa na Wizara husika. Kukosekana kwa taarifa hizi kunasababisha nchi kutokuwa na takwimu sahihi ya mauzo nje ya nchi. Vilevile, Utofauti wa takwimu unasababisha iwe vigumu kuthibitisha endapo mapato yote ya mauzo nje yamerudishwa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hiyo, Kamati inaitaka Benki Kuu kuharakisha mchakato wa kuunda Mfumo wa Kufuatilia Mapato yanayotokana na Mauzo na Malipo ya Uagizaji wa Bidhaa Nje ya Nchi (System for Tracking Export Proceeds and Import Payments). Mfumo huu utawezesha Benki Kuu kupata takwimu sahihi za fedha za kigeni zinazoingia nchini kutokana na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

**5.7. Serikali Kupunguza Gharama za Miamala katika Mfumo wa Malipo Madogo na ya Papo kwa Papo (TIPS)**

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2021, Serikali ilianzisha Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa Papo (*Tanzania Instant Payment System* - TIPS). Mfumo huu umeweza kuwaunganisha watoa huduma wote wanaotumia mifumo ya malipo ya rejareja (retail payments) kupitia simu za mikononi, benki au Msimbo wa QR. Mfumo huu umeongeza ufanisi katika utumaji wa miamala

midogo kutoka kwa mtoa huduma mmoja kwenda mwingine kwa haraka na uhakika zaidi. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, jumla ya watoa huduma **45** walikuwa wamesajiliwa katika mfumo huu na jumla ya miamala **millioni 344.84** yenye thamani ya **shillingi trilioni 20.540** ilifanyika kupitia mfumo huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo imepunguza gharama za kutuma fedha kutoka benki moja kwenda benki nyingine kwa mujibu wa tangazo la Benki Kuu la tarehe 22 Aprili, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado viwango vya tozo za miamala vimebaki kuwa juu katika kuhamisha fedha kutoka mtandao wa simu mmoja kwenda mtandao mwingine, au kutoka katika mtandao wa simu kwenda benki. Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya gharama za miamala kutoka mtandao mmoja wa simu kwenda mtandao au kwenda benki na kutoka benki moja kwenda benki nyingine. Lengo la mapitio hayo ni kuhakikisha gharama hizo zinaakisi punguzo la gharama linalotokana na matumizi ya mfumo wa TIPS. Hatua hii itasaidia kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kufanya malipo kwa kupitia mifumo ya benki na mitandao ya simu na Serikali itakusanya mapato zaidi.

### 5.8. Mapendekezo kuhusu Mawanda ya ukaguzi kwa Ofisi ya CAG.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba katika mwaka wa fedha 2024/25 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ipanue mawanda ya ukaguzi na kufanya ukaguzi katika miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa kupitia mkopo kutoka IMF Extended Credit Facility (ECF), mifumo inayotumika Serikalini kama vile mifumo ya usimamizi wa mapato na matumizi ya umma pamoja na utendaji kazi wa watumishi wa Umma.

### 5.9. Usimamizi wa Sekta ya huduma ndogo za Fedha nchini

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ndogo ya fedha ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Sura 342. Sekta hii ni muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi wa kipato cha chini wakiwemo vijana, wanawake,

wajasiriamali, kaya na makundi maalum. Hadi kufikia Desemba, 2023, Benki Kuu imetoa leseni 1,569 kwa watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili ambao ni watoa huduma ndogo za fedha wasiopokea Amana (Non-deposit Taking Microfinance Service Providers). Aidha, Sekta hii imekuwa na changamoto ya ongezeko la vikundi vidogo vya kukopesha fedha visivyo rasmi na visivyozingatia Sheria na Kanuni za Sekta hii, ambavyo vimekuwa vikitoza asilimia kubwa ya riba isiyo rafiki kwa mkopaji. Changamoto hii imekuwa ikiwaathiri wakopaji wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 52 cha Sheria ya Sekta ndogo ya Fedha kinaweka masharti ya Kumlinda mteja. Kifungu hicho kina masharti yafuatayo nanukuu:-

***50.-(1) A microfinance service providers shall comply with the principles of consumer protection as provided for in the applicable laws and in the regulations made under this Act.***

***(2) Subject to sub section (1), the principles of consumer protection prescribed in the regulations shall include-***

***(a) terms and conditions of credit or related service that are transparent, fair, legible and protect the rights and interests of microfinance consumers or members; (b) complaints handling and dispute resolution mechanism; full disclosure of relevant information on the products and services provided;***

***(d)requirement for the vetting of the standard credit contracts or agreements; and***

***(e) financial education to the consumers;***

***(f)transparency on interest rates, fees or penalties; and***

***(g)any other principle for the purpose of ensuring fair treatment of consumers.***

***(4) Notwithstanding the provisions of sub sections (2) and (3), any term or condition stipulated in a contract or any relevant***

***document purporting to grant to a microfinance service provider authority to unilaterally introduce or modify interest rate or any other loan condition shall be null and void.***

***(5) Where a microfinance service provider without reasonable cause, fails to comply with the provisions of this section, the Bank or Delegated Authority shall take such measures as may be appropriate to ensure compliance.***

**Mheshimiwa Spika,** Masharti niliyoyasoma katika kifungu hiki ni tiba ya mikopo kausha damu. Ni wazi kwamba Wizara ya Fedha wana wajibu wa kuhakikisha masharti ya kifungi hiki yanafuatwa kikamilifu na wakopeshaji. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wakopeshaji wote nchini wanafuata masharti ya kifungu hicho.

**6.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Akson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) pamoja na Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge. Aidha, napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mhe. Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati wa kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023/24 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25. Vilevile, nimshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El Maamri Mwamba, Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao katika kujadili, kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Charles Kichere kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2023/24 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa

fedha 2024/25. Kamati ya Bajeti itahakikisha katika kipindi chote kwamba, Ofisi yake inapata rasilimali fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 10 Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 11 Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12 Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 13 Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 14 Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 15 Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 16 Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 17 Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 18 Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb | Mjumbe |
| 19 Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 20 Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Fedha yenye jumla ya **shilingi 18,318,540,654,799** ambapo **shilingi 3,513,424,470,850 n**i mishahara, **shilingi 14,171,648,516,000** ni matumizi mengineyo na **shilingi 632,567,667,949** ni matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
04 Juni, 2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmekuwa na vikao vingi sana humu Bungeni. Kanuni ya 73(3); Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala atatakiwa:

(a) Kuingia na kutoka au kutoka kwenye Ukumbi wa Bunge kwa staha na atainamisha kichwa kuelekea kwa Spika au atafanya mkunjo wa goti kwa heshima, kila mara Mbuge huyo atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake; *(Makofi)*

(b) Kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye Ukumbi wa Mikutano bila sababu; *(Makofi)*

(c) Kutopita kati ya Kiti cha Spika na Mbunge anayesema;

(d) Kutosoma kitabu chochote, gazeti au barua isipokuwa kama vitu hivyo vinahusu shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo; na

(e) Kuondoa mlio wa simu na kutozungumza na simu. ‘(e) Kuondoa mlio wa simu na kutozungumza na simu.’

Waheshimiwa Wabunge, tumesikiliza maoni ya Kamati yetu ambayo yanahusu hoja ya Wizara ya Fedha na baada ya kuyasikiliza hayo, ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao mmeomba kuchangia hoja hii na tutaanza kuwataja na tutaendelea na huo utaratibu.

Ninawakumbusha tena Waheshimiwa Wabunge, orodha inavyokuwa inaletwa hapa mbele haimaanishi wewe utakuwa wa namba hiyo kuchangia kwa sababu hapa mbele kuna maombi mengi yanakuja, wengine wanawahi kwenye Kamati, wengine wanakuwa na dharura.

Tutaanza na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Fedha na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, ninapenda nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa uhai na anavyotuwezesha.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais; kwanza kwa jinsi anavyohangaika kutafuta fedha kwa ajili ya wananchi wake lakini nieleze masikitiko yangu kuhusu Wizara hii ya Fedha. Mheshimiwa Rais ametupatia ruzuku ya mbegu sisi wakulima wa nchi nzima. Mheshimiwa Rais ametupatia ruzuku ya mbolea sisi wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa sababu ametambua kwamba asilimia kubwa ya wakulima ni maskini, asilimia kubwa ya wakulima bado wanahitaji kuwezeshwa lakini Wizara hii ya Fedha kupitia *TRA*, mimi ninasema wana uvivu wa kufikiri kwa sababu badala ya kuhangaika kutafuta vyanzo vingine vya mapato, wao wanakwenda kumkaba mkulima.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *TRA* inasema wakulima wote nchini lazima watumie mashine za *EFD*. Sasa, unapomwambia mkulima kupitia hivi Vyama vya Msingi vya *AMCOS* vitumie

mashine ya *EFD,* unamfanya kwanza yule siyo mkulima unam-*treat* kama mfanyabiashara. Kwa sababu mkulima hana leseni ya biashara, mkulima halipi kodi, mkulima analipa ushuru.

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali hapa Bungeni kwa Mheshimiwa Waziri na nilisikitika majibu yake kwa sababu yeye anaamini kwamba hivi Vyama vya Msingi vya Ushirika vinafanya biashara lakini wale ni wakulima wadogo wadogo. Mwingine mwenye gunia tano, mwingine mwenye gunia 10, mwingine mwenye gunia 20, wameungana wanakwenda kupeleka mazao yao mnadani na *transaction* yao wanafanya *once a year* (mara moja kwa mwaka).

Mheshimiwa Spika, sasa, unapomwambia huyu atumie mashine ya *EFD*, maana yake kwamba mwisho wa mwaka ...

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenisongole kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri wana nafasi ya kujibu huko mwishoni.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hiyo ya kwamba tutajibu mwishoni lakini ninataka nimpe taarifa muongeaji kwamba, *TRA* siyo wavivu wa kufikiri. *TRA* wanatekeleza sheria zilizotungwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TRA* hawatungi sheria hata moja; wanatekeleza sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu na nilipojibu swali nilisema, Waheshimiwa Wabunge, kama kuna sheria tunaiona ni mbovu, wiki ijayo tunajadili sheria hizo. Kwa hiyo, sheria zote tunazoziona ni mbovu tuzitoe halafu na zile tutakazotunga ndizo *TRA* watakazotekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeona nimpe taarifa kwamba *TRA* hawatungi sheria, hawatungi sheria hizo wanatekeleza sheria tulizotunga sisi. Kwa hiyo, mahali pazuri pa kufikiri na kuacha uvivu wa kufikiri ni hapa tunapotunga. Wale wanatekeleza sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hii sheria ya wakulima kutumia *EFD* ni sisi tumetunga hapa ndani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, sheria inavyosomeka sasa hivi, sheria inavyosomeka sasa hivi ndivyo tulivyopitisha. Tulipitisha kwamba, mtu yeyote anayefanya shughuli inayozidi shilingi milioni 11 kwa mwezi anatakiwa atumie mashine ya *EFD*.

Mheshimiwa Spika, tumeongea na Waziri wa Kilimo tumekubaliana kwamba kwenye sheria hizi tunazozileta, jana tulikuwa na kikao kizuri sana. Tumekubaliana turekebishe maeneo yale na tutafute eneo zuri ambalo litatoza Sekta ya Kilimo bila kumuhusisha mkulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ...

**SPIKA:** Sawa Mheshimiwa umeshaeleweka, maana nilikuwa nimekuuliza swali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kanuni zetu zinatuzuia kutumia maneno yanayoudhi. Hawa wenzetu hawa tumewapa tu fursa ya kukusanya kodi lakini wanatekeleza sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kama ni maneno yanaudhi ungetumia kanuni nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, umesikia kwamba sisi tumetunga sheria ya namna hiyo. Mtakapotuletea maoni yenu tafadhali ondoeni jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, hii taarifa mimi siipokei kwa sababu Bunge la mwaka juzi la mwezi Septemba tulikataa na kufuta *withholding tax*. Sasa *TRA* wanairudisha kwa mlango wa nyuma na Waziri wa Kilimo hapa ni shahidi alituletea tukaikataa.

Mheshimiwa Spika, sasa wameshindwa kukusanya ushuru bandarini, wameshindwa ku-*create* vyanzo vingine vya mapato, wanataka kuwaonea wakulima maskini, hii siyo sawa, hii siyo sawa na kinachosikitisha ukienda kwenye ukurasa wa *Instagram* wa Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa *Instagram* wa Mheshimiwa Waziri anasema mwenyewe, naomba uniruhusu nii-*play*. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. George R. Mwenisongole alicheza video yenye sauti ya Waziri wa Fedha kutoka mtandao wa Instagram)*

"*.....tax the rich and give services to the poor, yaah! Sisi tunawapa ahueni matajiri halafu tunawatoza maskini, tunawafanya maskini waendelee kuwa maskini. Sasa tunakuwaje na tozo, tunakuwaje na ushuru wa mazao, mkulima anakutana na mageti, mageti, and then we have a lot of money, hatukumbuki hata kama tumeshaikusanya au hatujaikusanya, that is to make watu wetu waliopo vijijini waendelee kuwa maskini and to make the rich to enjoy like they are in heaven wakati bado wapo wamezungukwa na maskini. Hatuwezi kuwa tunatoza ushuru wa samaki kwenye kikapu halafu tunaacha watu wengine with a lot of money....*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuache kupiga makofi tumsikilize, tusikilize kwa sababu mimi sisikii kinachosemwa, atakaponiletea hoja hapa Mheshimiwa Mbunge nitashindwa kujua naifanyeje, kwa hiyo nipeni muda nimsikilize Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa hebu rudia, rudia sijasikia kwa hiyo sitajua unachokisema ni nini.

*(Hapa Mhe. George R. Mwenisongole alicheza video yenye sauti ya Waziri wa Fedha kutoka mtandao wa Instagram)*

*"....tax the rich and then we give services to the poor. Yaah! Tukiwapa ahueni matajiri halafu tunawatoza maskini tutawafanya maskini waendelee kuwa maskini. Sasa tunaachaje, tunakuwaje na tozo, ushuru wa mazao, mkulima tu anakutana na mageti, mageti and then we have a lot of money hatukumbuki hata kama tumeshawahi kukusanya au hatujaikusanya, that is to make watu wetu waliopo kijijini waendelee kuwa maskini and then to make the rich enjoy like they are in heaven wakati bado wapo wamezungukwa na maskini, hatuwezi tukawa tunatoza ushuru wa Samaki kwenye kikapu halafu tukaacha watu with all this amount of money, watu hatujui hata kama tumeshaikusanya ama hatujaikusanya, we can't live like that. Kamishna wewe unajisikia furaha kukusanya ushuru kwenye matembele halafu...and you don't know kama umeshakusanya trilioni 19, you don't have the record kwamba umeshaikusanya ama lah! And then uende kukusanya kwenye kiosk? Uende kukusanya kwa bodaboda? Why it should be like that? Unachukua ile fedha halafu?"(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amemaliza kwa kumuuliza Kamishina wa *TRA* "*why should be like that*" sasa mimi nimuulize *why should be like that* kwa hawa maskini wakulima unaong'ang'ania kuwatoza kodi, wakati kwenye ukurasa wako wa *Instagram* umeongea kitu tofauti, ulikuwa sahihi kwenye ukurasa wa *Instagram* lakini *practical* unafanya tofauti! Sasa Mheshimiwa Waziri sisi tukueleweje? Kwanza mimi ningekushauri kwanza uondoe hiyo kwenye *Instagram* kwa sababu siyo ambayo inaku-*represent*.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili jambo siyo sahihi, mwisho wa siku tunapoenda mtawalazimisha hata mfugaji ambaye ana ng'ombe zake anaamua kwenda mnadani kupeleka ng'ombe zake mtamtaka naye awe na *EFD* mashine. Mwisho wa siku hata mtu anayelima bustani nyumbani, amelima mbogamboga zimezidi anaamua kidogo aende akauze mtamtaka awe na *EFD* mashine, hauwezi ukaenda hivyo kwa kum-*treat* kila mtu ni mfanyabiashara! Hii mnamchonganisha Mheshimiwa Rais na wakulima. Tangu lini Mkulima akapewa mashine ya *EFD*? Hii haiwezekani Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo tukiendelea Wizara ya Fedha ndiyo kila kitu, Mawaziri wote wanalazimika kwenda kumpigia magoti Mheshimiwa Waziri ili afanye malipo yao. Mimi kwangu Mbozi tuna Kambi ya Jeshi ya Itaka ya JKT, pale wananchi wameondolewa, ikafanyika tathmini, wanadai shilingi bilioni tatu na milioni 500, nimemsumbua sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, nimeuliza swali hapa Wizara ya Ulinzi, kila nikiuliza anasema bwana ni Hazina! kila akiuliza ni Hazina! kila kitu kimekwamia Hazina!

Mheshimiwa Spika, tukiacha hilo, Mheshimiwa Rais ametupa Mbozi Chuo cha Uvuvi na Kilimo, nimemsumbua sana Mheshimiwa Waziri Ulega kwa nini ujenzi hauanzi, kila mara, mwisho wa siku akanambia bwana mimi hapa nilichofanya nimejitahidi nimekatakata kwenye bajeti yangu nimepata shilingi milioni 50 ndiyo nimepeleka lakini mambo yote ni Hazina.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nashindwa kuelewa Mheshimiwa Waziri, unashida gani na Mbozi? Kila kitu Mbozi kinakwama kwa sababu ya Hazina. Hivi Mfuko wa Jimbo kwenye Jimbo langu mimi bado sisi haujaingia, Mkurugenzi wangu nikimuuliza ananiambia Hazina hawajaachia hela. Sasa leo nataka Mheshimiwa Waziri utuambie nani mkweli kati yako wewe au Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, sasa haya mambo yataendelea mpaka lini? Kwa hiyo, mimi kwa kweli nina uchungu sana, kwa sababu sasa naona kama Wizara ya Fedha inakuwa ni kwazo kwa wananchi wangu wa Mbozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kusema hayo mimi nitaunga mkono hoja pale nitakapopata maelezo kamili kuhusu haya niliyoyaongea, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa na mimi ya kuchangia Wizara hii ya Fedha. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimpongeze kwa kazi kubwa anayofanya ya kutafuta fedha yeye binafsi lakini ya kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha ambazo tunazitumia katika miradi hii ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba kwa dhati nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Kaka yangu Dkt. Mwigulu Lameck Madelu Nchemba, Mbunge wa Jimbo la Iramba na kama alivyosema kwa Mheshimiwa Chande wasihangaike kutafuta mgombea mwingine na mimi nimhakikishie kwamba Jimboni kwake hawatahangaika kutafuta mgombea mwingine, kwa sababu anatosha na anafanya kazi kubwa na tunaiyona.

Mheshimiwa Spika, pili nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri alisema ni *two in one* naye wasitafute mgombea mwingine kwa sababu anatosha na anafaa. Nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara na kwa sababu ni mwanamke sikushangaa kwamba mambo ni mazuri na yanaenda, ya kurekebisha yapo lakini yanaenda vizuri. Nipongeze Watendaji wa Taasisi zote za Wizara hii *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepongeza kwa sababu kadhaa, kwanza ni mapato kuongezeka lakini miradi inaenda, tunaona zahanati zinajengwa, shule zinajengwa, mishahara inalipwa, ajira zinatolewa kila mara. Kwa hiyo lazima tupongeze kwa juhudi hata kama bado hatujafikia lengo lakini tunaona kazi kubwa inafanyika. Mimi nitakuwa na jambo moja tu kwa leo na jambo lenyewe niliongelee suala zima la mikopo au ukopeshaji ambao Wizara ndiyo inajukumu la ku-*regulate* na kuhakikisha kwamba shughuli nzima ya ukopeshaji au ukopaji na kila kitu inaratibu vizuri na Wizara ndiyo inatakiwa itengeneze *formal* na i-*shape* hii *financial market system*. Sasa nataka nitoe jambo moja la kwamba Wizara inatakiwa ku-*invest* kwenye *system* ambayo inaweza ika-*control* wakopaji na wakopeshaji.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 29/03/2023 wakati anapokea ripoti ya *CAG,* Mheshimiwa Rais alisema kuhusiana na mikopo

chechefu na akahoji kwa nini mikopo chechefu inatokea katika taasisi zetu za Serikali, akasema alishangaa kuona kuna mtu mmoja mfanyabiashara mmoja alikopa mabilioni katika benki sita na akaondoka nchini, lakini kingine baada ya kufanya hivyo wakataka kufanya *restructuring* ya hiyo mikopo lakini alishangaa hata dhamana alizoweka ni *fake* hazikuwa dhamana sahihi. Mheshimiwa Rais alisema tunapo chechemea na mikopo chechefu na nchi nayo ina chechemea lakini akamalizia kusema anaomba tujirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kum-*quote* Mheshimiwa Rais na mimi niliuliza Bungeni hapa tarehe 27 Mei mwaka huu. Niliuliza je, kuna kampuni ngapi nchini za kuchakata taarifa za wakopaji ambao ni hizi *credit reporting* au *credit reference*. Hizo *credit reference* zitaangalia hali ya mkopaji na zitaangalia uwezo wa kifedha wa mkopaji na kutoa *point* kwamba huyu ni mkopaji mzuri, huyu wa kati na huyu ni mbaya, lakini nilipouliza maswali niliambiwa zipo mbili na zikatajwa na nikauliza je, *microfinance* ndogo ambayo wakiwemo na hawa tunaowaita wanatoa mikopo kausha damu nao si wanaleseni? Hawa wadogo wadogo maana tusije tukazibana benki kubwa na hawa wadogo nao wana ripoti *BOT*? Nikaambiwa ndiyo lakini nikauliza je, *BOT* wana-*update* kwa muda gani, yaani wanakaa miezi sita baada ya hizo *financial institution* kuwaletea ripoti za wakopaji, wanakaa muda gani ku-*update* sasa, nikajibiwa pia kwa sababu unapo-*update* unamsaidia anayetoa wa pili kufanya maamuzi sahihi ya kuangalia *underwriting* ya mkopo.

Mheshimiwa Spika, nikajibiwa kwamba wana-*update* mara kwa mara. Sasa baada ya kutoa mfano wa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake na baada ya swali langu la msingi niseme hivi, Wizara ndiyo inajukumu kubwa la ku-*regulate* na kuhakikisha kwamba sekta ya ukopaji inaenda vizuri kwa kuangalia riba, Wizara pia ina mamlaka ya ku-*protect* wanaokopesha. Kwa sababu tusiangalie tu kuwaminya riba punguza, punguza lakini lazima pia tuwajengee mazingira ya wao kuwa *safe* wanapotoa ile mikopo, kwa sababu hakuna mtu anataka ku-*invest* asiingize faida. Kwa hiyo, *to play both sides,* katika Serikali iwe na mchango

wake, wakopaji sisi tuwe na mchango wetu lakini na hizo *lending* ziwe na mchango wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashauri mambo matatu Mheshimiwa Waziri Kaka yangu, jambo la kwanza hizi *credit bureau* kama zipo, ni zipo nilijibiwa sasa *BOT* wao wana-*update* muda gani? Kwa sababu wakati Mheshimiwa Rais anasema mkopaji mmoja kakopa mabilioni ndani ya mwezi mmoja kwa benki sita, hii ina maana gani? Ina maana kwamba hakukuwa na *reference check* ndiyo maana benki *A* wakatoa, benki *B* wakatoa, benki *C* wakatoa ikaenda mpaka ya sita.

Mheshimiwa Spika, hizi *credit bureau* ndiyo mkombozi mkubwa wa *lending* na Serikali ndiyo itasaidia kuweka mazingira *safe* kwa wakopeshaji. Kwa sababu tunapowaambia washushe riba lazima tuangalie mazingira tuliyowatengenezea sisi kama Serikali ya wao kuhakikisha hela zao hazipotei, ndiyo maana utaona hata wafanyakazi ambao mikopo yao tunawaita wale *safe borrowers* bado wanapewa riba kubwa kwa sababu labda zile *financial institution* zinataka ku-*compensate* na wale ambao ni mikopo chechefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwanza *BOT* wana- *update* kwa muda gani na *BOT* wanasheria gani kali ambayo wale wanaokopesha, zile *financial institution* wanatakiwa kuripoti wateja wao *daily*?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mawazo kwamba unapokuwa umemu-*approve* mtu mkopo awe *updated* kwanza kwenye *system* kabla hajakuwa *disburse* hizo hela, kwa sababu uki-*update* benki *A*, benki *B* kesho wakiangalia anapoomba mkopo watajua kumbe huyu alichukua mkopo benki *A* anakuja na kwetu leo kuchukua. Kwa hiyo, hilo suala la kukopa mwezi mmoja benki sita hayatakuwepo, kwa sababu hatuna *formal system* ya ku-*control* wakopaji na wakopeshaji wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara kwa sababu hili lipo chini yenu mratibu ipasavyo, kwa sababu sekta ya mikopo ni sekta kubwa na inagusa kila mwananchi na ndiyo maana tunalia

kila siku. Kila mtu anakopa Mheshimiwa Waziri, siku hizi imekuwa kama *basic needs*, ukienda kwenye nguo na nini unaweka ya mikopo mwisho, kwa sababu kila mtu anakopa umeona! Kwa hiyo, sasa kama kila mtu anakopa na kama ni sekta *sensitive* Wizara lazima ije na mkakati *sensitive* pia.

Mheshimiwa Spika, mkakati siyo wa nguvu ni wa *system*, kwa sababu ukishaweka *system in place* halafu unaweka sasa sheria za anayevunja hiyo *system,* sheria zinakuwaje? Ikibainika *financial institution A* imemkopesha mtu hajaweza ku-*update* na *financial institution B* imekuja kumkopesha ina maa anakuwa *punished*. Kwa hiyo, Serikali na Wizara ndiyo inatakiwa ifanye hayo yote kwa ajili ya kuwasaidia wote wakopaji na wakopeshwaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, jambo lingine siku hizi *technology* ni kila kitu, hakuna haja ya kwamba eti *financial institutions* zitoke zianze kupeleka vitu *BOT*, *BOT* wakae waanze kusubiri tuna-*update* kesho au kesho kutwa, Hapana! lakini pale pale wale zile *credit bureau* mlizowapa leseni mbili wanaweza wakawapa *access* kila *financial institution* waweze kuingiza wale kopaji watakachofanya wao *BOT* ni kuwa-*approve*, kwa hiyo wakisha *approve* inakuwa *updated* kwa watu wote, siyo lazima wao wapeleke *BOT* waanze kuingiza wanaweza wakaingiza wao na *BOT* kazi yake ikawa ni ku-*approve*.

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sasa la mwisho baada ya kengele kugonga tena? Ahante sana. *(Kicheko)*

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Jonas William Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi kupeleka kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii. Pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Hamad Chande, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na viongozi wote na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa jinsi wanavyoisimamia Wizara hii na kuandaa taarifa hii kuileta hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitaanza na upande wa mapato nikiangalia sana kwenye upande wa *TRA* - Mamlaka ya Mapato. Kwanza niwapongeze kwa kazi nzuri ya kuendelea kukusanya mapato ya Serikali kama tunavyoona yanaongezeka, pamoja na makusanyo hayo bado tunachangamoto na tunatakiwa tuendelee kuongeza nguvu ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha Pato la Taifa ukilinganisha na kiasi kinachokusanywa *ratio* yake ni ndogo sana. Nimechukua mfano wa nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ukilinganisha na Pato la Taifa, *ratio* inayokusanywa kwenye upande wa kodi ni asilimia 11.8, nchi ya Uganda asilimia 13.1, nchi ya Rwanda asilimia 16.6, Kenya asilimia 18.1 na Burundi asilimia 13.6. Kwa hiyo, unaona kabisa sisi tupo chini kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki ukiangalia *ratio* ya kodi pamoja na Pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaona kabisa bado kuna umuhimu wa wenzetu wa *TRA* na Wizara hii kuhakikisha kwamba inasimamia ili tuweze kuendelea kukusanya mapato na

tukilinganisha Pato letu la Taifa na kodi tunazokusanya tuone kabisa kwamba kuna kazi nzuri inafanyika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo nilikuwa naomba nitoe mchango wa mawazo kwenye suala hili kwamba, ili tuweze kukusanya mapato ya kutosha kitu cha kwanza inatakiwa tuendelee kuimarisha mifumo yetu ya TEHAMA. Mifumo yetu ya ukusanyaji wa kodi inatakiwa iimarishwe na tuhakikishe kwamba mifumo hiyo inasomana ili kama kuna changamoto yoyote inaweza ikajitokeza kwenye mfumo ambayo itatufanya tusipate mapato ya kutosha iweze kugundulika mapema.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tunatakiwa tulifanye ni kurasimisha sekta isiyo rasmi, sisi tunazingatia sana kukusanya mapato na kusimamia sekta ambazo ziko rasmi lakini sekta ambayo haiko rasmi inafikia asilimia 60. Kwa hiyo, kama Serikali itaamua kupeleka nguvu kwenye sekta isiyo rasmi na kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa tutakuwa na uhakiki mkubwa sana wa kupata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine sasa hivi wanatumia *cashless economy* kwamba, hakuna malipo ya fedha taslimu na kama yanafanyika ni kule kijijini kwa kiwango kidogo sana. Kwa hiyo, kama Serikali itajiingiza kwenye mfumo wa kuhakikisha kwamba, tunakwenda kwenye mfumo wa malipo pamoja na kutoa huduma kwa kutumia mifumo itasaidia sana kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata ule mchango alioutoa ndugu yangu Mheshimiwa Mwenisongole kwamba, watu wadogo wanadaiwa kodi; tukiweka *cashless economy* kila mmoja atalipa kodi na hakuna atakayelalamika. Sana sana tutaendelea kujadiliana kupunguza viwango vya kodi, lakini kila mmoja atalipa kodi na tutakuwa na wigo mpana wa kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara iendelee kuangalia sera zetu za kodi pamoja na kupunguza misamaha ya kodi. Suala lingine ambako Serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa sana ni

kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali. Serikali imewekeza fedha nyingi na sasa hivi tunaendelea kuwekeza kwenye *SGR* na miradi mingine mikubwa mikubwa.

Mheshimiwa Spika, Masajili wa Hazina anatakiwa aweke mifumo ya uhakika kwanza ili kusimamia haya Mashirika yafanye kazi kwa tija. Pili, kuweka mifumo ya uhakika ya ukusanyaji wa kodi katika haya Mashirika yetu ili yaweze kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuna Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Mhasibu Mkuu wa Serikali, anasimamia mifumo yote ya malipo na ya ukusanyaji wa mapato. Mimi binafsi ningekuwa ninaomba Mhasibu Mkuu, aweke nguvu kubwa kwenye kusimamia mfumo wa TAUSI kwa ajili ya kuhakikisha kwamba makusanyo yetu ya mapato kupitia kodi za Serikali za Mitaa na maeneo mengine ambayo yanahusiana na Serikali za Mitaa yaweze kukusanywa ili tuendelee kupata fedha nyingi za kutosha kwa ajili kutekeleza miradi yetu ya maendeleo na kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la matumizi, mimi nitaongelea sehemu moja kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali wanafanya kazi nzuri sana na ndio jicho la Bunge kuhakikisha kwamba kuangalia shughuli zote za Serikali zinakwenda vizuri na mapato na matumizi yanasimamiwa vizuri kwa upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii inafanya kazi vizuri sana na inatoa ripoti ambazo zinatusaidia sisi kuangalia ni wapi tunaelekea lakini kuna changamoto katika utendaji wa hii Ofisi. Ukiangalia Serikali ina jumla ya mifumo 460 ambayo imewekwa kwenye Wizara mbalimbali na taasisi mbalimbali, lakini uwezo wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kukagua mifumo yote inakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwanza, yeye mwenyewe Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, bado hana mifumo ya kutosha. Kwa hiyo, niiombe Serikali iendelee kuongeza nguvu kwenye Ofisi ya

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili kuhakikisha kwamba, anaimarishiwa mifumo ya TEHAMA na aweze kufanya kazi ya ufasaha ili sisi tuweze kupata taarifa na kufuatilia mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Mimi nianze kwa kusema kwamba tunashukuru sana kwamba Mheshimiwa Rais, anashughulika sana kuhakikisha kwamba, tunapata misaada na mikopo ya masharti nafuu. Nimeona juzi kuna mkataba umesainiwa huko Korea wa dola bilioni 2.5 kama shilingi trilioni 6. Ni fedha nzuri na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza kuhamasisha hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumshukuru na tumpongeze Mheshimiwa Waziri, wetu wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, pamoja na Naibu wake na Uongozi wa Wizara nzima kwa mambo mazuri ambayo wanaendelea kuleta. Hali ya Dunia ni ngumu sana sasa hivi. Hali ya uchumi Duniani ni ngumu na kila nchi inapitia kwenye matatizo *budget deficits* zimeongezeka karibu kila mahali, lakini tunaona kwamba, bado tunaweza tukatekeleza bajeti yetu. Tuwashukuru sana na tunawapongeza.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwanza, kwa kimoja, kimoja kinachohusu kwenye Jimbo langu nimekuwa nimemuomba Mheshimiwa Waziri, kwa muda mrefu toka niingie hapa Bungeni. Kuna wananchi wangu wa eneo la Ngona pale Njia Panda na eneo la Mabungo pale Uchira ambao toka mwaka 2013 walichukuliwa maeneo yao kwa nia ya kujenga Kituo cha *One Border Stop Centre*.

Mheshimiwa Spika, madai yalikuwa kwenye pale *Border* ilikuwa kama shilingi 5,000,000,000 na kule Mabungo kama shilingi 3,000,000,000 lakini kwa sababu muda ulipita sana naona Mheshimiwa Waziri, aliweza kutuma watu wakafanya tathmni mwaka uliopita, ili watathmini upya. Sijui gharama zinazojitokeza sasa ni ngapi? Ni muda mrefu na naomba kwamba anifikirie kama anataka mimi nirudi hapa Bungeni basi alipe hizo fedha na hayo madai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo niseme hivi uwiano huu tunaoona kati ya kodi za ndani za Serikali yetu kwa Pato la Taifa, umekuwa mdogo ni 11.8 kama mwenzangu Mheshimiwa Mbunda alivyosema lakini ninajiuliza; je, kwenye nchi nyingine wana-*treat* namna gani tozo? Kwa sababu kuna tozo nyingi ambazo si kodi, tozo kwenye kule *OSHA* ukizijumlisha *TBS* na tozo kwenye Mamlaka zetu zote zinakusanywa *separate* lakini ni kodi. Ni kodi zinatakiwa ziingizwe kwenye kodi halafu hizi Mamlaka ziweze kupata mgao wa fedha zao za bajeti zao kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naamini pengine ukizijumuisha zote hizo ili huo uwiano wetu unaweza ukawa ni tofauti kidogo. Pengine inaweza ikawa ni njia moja wapo kwanza ya kutatua kero ya kuwepo na mamlaka nyingi, leseni nyingi za biashara na usumbufu wa wawekezaji kutoka Kituo kimoja kwenda Kituo kingine cha Mamlaka kupata leseni au kulipia hizi leseni na mambo mengine yanayoendelea**.** Kwa hiyo, mimi ninafikiri Mheshimiwa Waziri aangalie na ikiwezekana ifanyike mapema iwezekanavyo ili tuweze kuji-*assess* sisi tupo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada hapo pia niseme hivi, *concept* ya ukomo wa bajeti *(budget constraint)* isipotekelezwa sawa sawa utabakia tunaenda pabaya sana. *What is happening?* Kwamba, wewe unatengeneza *budget constraint*, lakini ule ukomo unaweka miradi mipya kabla ya kujua kwamba, kuna *back log,* kuna madai ya wazawa wenzetu ma-*contractors*, wazabuni wa Serikali ya miaka mingi ambayo haijalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilitakiwa hapa wanapoweka ukomo, basi kwanza ondoa yale madeni ambayo unatakiwa ulipe, kwa

sababu ni *contracts* ambazo zimeshafanyika miaka ya nyuma. Tusipofanya vile tunaenda pabaya, kwa sababu hayo madeni bahati mbaya haya madeni madai ya wakandarasi pamoja na wazabuni hususan wazawa unakuta kwamba, haya madeni hayana *first charge*. Sisi tuliokopesha Serikali kupitia dhamana za Serikali ndio tuna *first charge*. Wale hawana *first charge* wamekopa mikopo ili kutekeleza miradi ile.

Mheshimiwa Spika, ile miradi sasa wanajua kwamba wao watalipwa wakalipe benki. Badala yake mzawa, mdai wa Serikali anakaa miaka mitano hajalipwa fedha zake. Kwa hiyo, sasa ile mikopo inaji-*multiply* mara mbili, inajiongeza mara mbili kwa riba ya *16 percent* mkopo wa milioni 20 baada ya miaka mitano inakuwa *compound rate* ni milioni 40.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema tuangalie tuwape na hawa kipaumbele cha kulipwa haya madeni ambayo ni makubwa. Tunajua sitaki sehemu kusemwa, kwa sababu hizo *figure* hazijulikani sawa sawa lakini, tunazijua kule kwenye Kamati ya Bajeti, tunajua ni *figures* kubwa kidogo. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri aangalie hivyo ili mwaka unaokuja tuangalie ule ukomo u-*adjust for the pipelined debts* ambayo ni haya madeni ambayo hayana *first charge* kule kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kuna matatizo ya bajeti nzima ya malipo ya madeni. Nasema madeni yale ambayo ni *properly booked* ya dhamana yale ya nje na ya ndani. Nimeangalia utaona kwamba, ongezeko la *debt service* kwenye riba za ndani; ongezeko la mwaka 2023/2024 kwenda 2024/2025 ni *30 percent, ok*? Ukienda kwenye mtaji wa ndani inaongezeka *service* yake ni *14.3 percent.*

Mheshimiwa Spika, sasa angalia la nje, kwa sababu la nje ndio lililo tete; mtaji wa nje ongezeko ni *30 percent* na riba ya nje inaongezeka kwa *76 percent almost.* Yaani huwezi ku-*imagine 76 percent* na inaendelea, kwa sababu hali ya riba zimekuwa zipo juu bado na ni kwamba, madeni yote ya nje yana vipengele vya *adjustment* wanasema *repricing as the market changes. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna uwezekano kwamba, hata mwaka huu tulivyopanga kwamba, itaongezeka kwa *76 percent*, pengine itaongezeka zaidi, kwa sababu ile mikopo ya biashara imeanza kuiva na inalipiwa hizi riba ambazo ni *very high*. Kwa hiyo, mimi ninafikiri Waziri aangalie kama kweli hataomba tuongeze hiyo bajeti yake ya ku-*service* mikopo *all the same*.

Mheshimiwa Spika, ili tusije kuingia kwenye matatizo ya kutokulipa halafu tukaanza kuonekana kama ni nchi ambayo haipo *credit wealth.* Baada ya kusema hivyo, yamkini niseme hivi pia. Katika hii *issue* ya madeni mimi nafikiri inahitajika kuwa na *long term financing plan* tuweze kuwa na kutengeneza kabisa kwamba, tuta-*finance* namna gani. Natumaini kile kitengo chetu cha kusimamia madeni kina uwezo wa kufanya jambo kama hilo likatusaidia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote tunayozungumza kuhusiana na mapato nimezungumza kidogo mwanzoni pale, lakini mimi nashauri kwamba, Serikali lazima iandae ikamilishe sasa sera ya kodi. Sera hii ya kodi iweze kuingiza masuala yale tuliyokuwa tunazungumza kikamilifu ya kuwa na *tax calendar* ambayo itahusu zaidi upande wa ushuru wa forodha pamoja na ushuru wa kawaida pamoja na tozo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba hiyo ikifanyika itaweza pia kuainisha kwamba, namna gani tuta-*treat* mapato ya Mamlaka ambayo yanakusanywa yenyewe na yanaweza ku-*adjust* yenyewe inavyotaka bila kusimamiwa vizuri na inakuwa sasa ni kero kwa upande wa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningetaka nizungumzie ni *issue* ya *coordination* kati ya Wizara hii ya Fedha ambayo ilikuwa imehodhi pia masuala mazima ya mipango. Sasa hawa wana *coordinate* namna gani mambo yao na hii Wizara mpya ya Mipango na Uwekezaji pamoja na Tume ya Mipango. Hata hizi bajeti zao sijaona.

Mheshimiwa Spika, nimeona hiyo *mic* yako imewaka. Basi naomba niunge hoja mkono na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mimi mchango wangu nitaanzia kwenye hoja ya Kamati ya Bunge, ambayo imezungumzia uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Rufani za Kikodi. Kwamba, katika Mikoa 26 Tanzania Bara, Mikoa 12 haina Wajumbe na wao wamerejea Taarifa ya *CAG,* lakini wamezungumzia tu Wajumbe wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hii ni kwamba, uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Mikoa haujafanyika. Vilevile, hakuna Wenyeviti na hakuna Makamu Wenyekiti na kuna uhaba wa bajeti za Mahakama za Kirufaa za Kikodi.

Mheshimiwa Spika, sasa hali hii kama ambavyo amesema na kama ambavyo Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amekuwa akizungumza mara kwa mara imesababisha rufani za kodi zenye thamani ya trilioni 10.48 na ni ongezeko la trilioni 5.65 toka mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, mimi nina bango kitita hapa ambalo ni la Bunge hili. Unafahamu na tutaenda hivi karibuni baada ya kumaliza hii bajeti ya Wizara ya Fedha, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ili tuweze kujadiliana mambo gani yalizua mjadala ili hatimaye kama Bunge tuweze kutoa *directives* ili sasa baadaye Serikali ije na mkakati wa kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni ya tarehe 8 Juni, 2022 ambapo tulikuwa tunajadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 na kwa makadirio vilevile ya mwaka 2022/2023. Sasa hoja ya tatu, inasema hivi, ya mwaka 2022 inasema, hadi tarehe 31 Disemba, 2021, kesi zenye thamani ya shilingi trilioni 5.18 zilikuwa kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa ya Mamlaka ya Mapato".

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni miaka miwili iliyopita leo tunaambiwa imeongezeka mpaka shilingi trilioni 10. Sasa Kamati

ilipendekeza nini kipindi kile? Tuliitaka Wizara ya Fedha, kuitaka Serikali kuanzisha mkakati maalum wa kumaliza mashtaka ya Bodi ya Mahakama za Rufaa za Kodi ili Serikali ipate mapato yake stahiki na wafanyabiashara warejeshewe fedha zao endapo wanastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo lina sura mbili; kwa nini? Sheria ya Usimamizi wa Kodi *(Tax Administration Act) Cap 2, Cap* 438, Kifungu 51(5) kinasema hivi, "Kabla ya rufaa yoyote ya kodi kusikilizwa lazima mlipa kodi ama alipe 1/3 ya kodi yote aliyofanyiwa makadirio au alipe kodi isiyobishaniwa". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa lugha hii tunasema nini? Kwa hiyo, katika hizo shilingi trilioni 10 zilizokuwepo huko kuna mfanyabiashara analalamika lakini ametakiwa afanye *deposit* kama ambavyo nimezungumza hapa. Kesi haziamuliwi mfanyabiashara anaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sura ya pili, Serikali na yenyewe vilevile *TRA* tumesoma hapa wanaweza kukusanya trilioni 21. Nyingine tutakopa kopa huko. Mzee wa benki hapa amezungumza madhara ya riba ambazo tunapata kama Taifa, halafu tuna shilingi trilioni 10 tumezikalia. Zimeongezeka kutoka shilingi trilioni tano mpaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge limeelekeza Serikali imepuuza mwaka wa pili. Sasa vitu kama hivi vinaweza kuonesha viashiria kwamba, sisi kama Bunge hatuna meno. Ndio maana Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti, inakaa inaelekeza nendeni mkateue hawa watu maamuzi yafanyike. Hawafanyi tunarudi miaka miwili baadaye pesa zimeongezeka mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Bajeti, inazungumza hoja zile zile. Kwa hiyo, mambo kama hayo ni dharau kwa Bunge, ni dharau kubwa sana. Naomba utulie Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; kwa mujibu wa Tangazo la Serikali, Wizara ya Fedha, ina wajibu wa kuratibu upatikanaji wa

fedha na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Mimi shida ambayo ninayo kubwa ni linapokuja suala la utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Haina maana kupitisha pesa halafu ikija utekelezaji tunatekeleza kwa uduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina taarifa za miaka mitano za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anapokwenda kufunga mahesabu pale Hazina alikuta kuna shilingi ngapi? 2018/2019, 30 Juni, wakati mnalialia hapa mnaenda kuanza mwaka mwingine wa fedha mnapigwa *sound*, Hazina kulikuwa kuna shilingi trilioni mbili. Mahesabu yalivyofungwa pesa zipo pale. 2019/2020, 30 Juni, Hazina kulikuwa kuna shilingi trilioni 1.156 zipo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021/2022 Hazina kulikuwa kuna trilioni 2.5 mpaka 30 June zimelala pale na wakati huo bajeti ya maendeleo hapa nazungumza bajeti za maendeleo *my friend,* sizungumzii pesa nyingine, nazungumza kale kamgao ambako wananchi wamekusanya kadi, wamelipishwa kodi ili huduma zirudi ambazo sisi hapa Bungeni tunaambiwa pesa inakuja, pesa inakuja na watu wanapiga makofi, uchaguzi ukikaribia unashtuka hee mbona kule mambo siyo? 2.5 trilioni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii taarifa ya juzi tunaambiwa katika fedha za miradi 6.5 trilioni zilizotolewa, 2.31 mpaka 30 Juni*,* 2023, 2.31 trilioni iko Hazina taarifa ya juzi ya *CAG*. Sasa unajiuliza, tuna wataalam wa nini wa kusaidia nchi iende? Tunajiuliza tunapanga bajeti ya mwaka mmoja ya nini kama mwaka mmoja unapita kati ya trilioni 6, trilioni 2.5 watu wamekalia uchumi pale Hazina, hivi tutaona mabadiliko kwa wananchi ambao tunawaongoza? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimepitia taarifa ya Kamati hapa jedwali la Kamati *page* namba 7 ya Taarifa ya Kamat fungu 01 linasema Hazina matumizi mengineyo *(OC)* Bajeti ambayo Bunge hili lilipitisha mwaka 2023/2024 ya *OC* watu wa Hazina hao sizungumzii hayo mafungu mengine nane sijui saba nazungumzia Hazina. Walipewa bilioni 724 ndiyo Bunge tulipitisha hapa, mpaka *April* 2024 kwa mujibu wa Jedwali la Taarifa ya Kamati

wametumia trilioni 1.106 matumizi mengineyo sawa na nyongeza ama sawa na 152% ya bajeti tuliyowapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza unajiuliza tunapitisha bajeti *this amount,* kila mtu anajua matumizi maengineyo kazi yake ni nini. Kwa Hazina peke yake mmeongeza mpaka 1.106 trilioni *from* bilioni 724 kwa kipi mnachikifanya? Ndiyo maana unafika hapa yaani kama Kimei anaanza kumwambia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu naomba unipatie hela, yaani unambembeleza, hela sio za Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, hela ni za Watanzania. Ifike sehemu tuwe na nidhamu, watu wanakusanya kodi kwa maumivu makubwa zikifika kwenye kapu rudisheni kwa nidhamu sio mpigiwe magoti kama pesa ni za kwenu… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya kengele ya pili imeshagongwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Hassan Omar King atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa Hamahnilo ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Naipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia inavyojitahidi kukusanya fedha na kupeleka maendeleo ingawaje kwamba kila asubuhi unapoamka unatakiwa unawe uso ili ujisafishe uweze kuona vizuri. Kwa hiyo na mimi nitachangia kwa mintarathi hiyo kwamba zinakuwepo kasoro ndogondogo ni lazima tunawe uso tusonge mbele ili tuwe tunaona vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma katika Hotuba ya Kamati katika *paragraph* ya 2.1.6 ambayo ipo katika ukurasa wa 14. Kamati imeishauri Serikali kuhuwisha viwango vya mafao kwa wastaafu ili kuendana na hali halisi ya maisha. Hii ni ushauri na

mimi pia nimeupokea katika hali nzuri kabisa lakini nina ziada hapa, hata hao wazee ambao walitakiwa kiwango cha chini cha mafao yao basi wapo wazee ambao hawapewi kwa mujibu wa sheria kile kiwango cha chini, mbali hapa tunapotaka kuhuwisha lakini wapo hao.

Mheshimiwa Spika, pia wapo ambao wamepunjwa viinua mgongo vyao na hao wapo. Natoa ushahidi hapa wa mifano, mfano mmoja kuna Mbunge hapa ananiangalia mzee wangu ananiangalia, tunaangaliana hapa akikubali nilitaje jina lake anyooshe mkono nitalitaja. Alikuwa anapewa kiwango cha chini kidogo kuliko kiwango cha chini kilichokuwa kinahitajika aliposema kwa kuwa ni Mbunge alisema alisikilizwa na analipwa, baba upo? Sasa je, mwananchi wa kawaida alikuwepo mama wa Mbunge mmoja na alinituma mimi nikaenda nikasema baada ya wiki akarekebishiwa kiwango cha chini chake akapewa na malimbikizo akalipwa lakini wakaja wazee wastaafu jumuiya, ulituletea mwaka jana katika Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walikuja wazee wana kilio kile kile wale wazee hawajasikilizwa lakini na mimi nikaja na wazee wangu wa Jangombe leo nilikuwa niwalete wawepo pale, nilikuwa nimepata mwaliko na Naibu Waziri wa Fedha nije nao lakini kwa bahati muda haujatosha hawakuja. Wazee wangu wa Jangombe wana malalamiko hayo hayo lakini hawajafanyiwa chochote, kuna kitengo cha pensheni Mheshimiwa Waziri, tumezungumza na watu mmoja mmoja, tumezungumza mpaka katika *level* hiyo ya Mawaziri, kama hapatoshi twende juu tunaweza kwenda juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kuna hadithi moja ya mguu wa punda, kuna mtu alimuona mtu ana mguu wa punda alifikiria ni binadamu akamuonesha alivyofungua nguo akamwona ana mguu wa punda akashtuka akaona akimbilie kwa mtu anayefuata akamwambia bwana eeh, yule pale bwana ana mguu wa punda na yule naye akamuonesha kama huu? Akakimbia pale akaona amfuate mwingine labda atanusurika, kufika kule akamwambia bwana wale pale wawili wana miguu ya

punda. Akamwambia kama huu? Kwa hiyo, ndiyo hii Wizara tulishapita kila hatua, watu wote tunapokwenda mfano ndiyo ule ule hakuna kesi hata moja ambayo imekuwa-*solved.* Kwa hiyo, na mimi nikasema nikitoe hiki kisa cha mguu wa punda, unaanza kwa maafisa wadogo unapanda mpaka unafika ngazi ya juu, tuende wapi? Kwa hiyo, mimi nimeisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wana madai yao katika pensheni hii lakini hii inatokana na sababu ambazo wamezishauri Kamati. Kamati wamesema kuweka vituo vya kufuatilia pensheni katika ngazi ya wilaya ili kusaidia wastaafu kutosafiri umbali mrefu kufuatilia stahili zao, kesi hii sisi tunawatoa watu Zanzibar. Nasikitika sana tena sana kwa nini hili halisikilizwi? Tunalizungumza kila Wizara, tunalizungumza Wizara ya Muungano tunasema hebu pale Zanzibar tuwe na ofisi ya Hazina na huduma, nyinyi mmeweka kijiofisi na meza watu hawafanyi chochote. Mimi ninatoa kesi hapa, ukipeleka *PSSF* kuna mstaafu mmoja nikaambiwa huyu anahusiana na *PSSF*, tulipopeleka cheque namba tukaambiwa kesi yenu nendeni Zanzibar. Walipoingiza kwenye kompyuta zao yule mzee tatizo lake ndani ya siku mbili lilikuwa-*solved,* hiyo *PSSF* ya juzi, wakati Hazina ipo karne na dahari na dahari huko nyuma wanashindwa na huyu mtoto waliyemzaa wa *PSSF* ambaye kazaliwa 1999, Hazina ipo tokea miaka ya sitini huko. Kwa hiyo, tunaliomba hili jambo lifanyiwe kazi, ingelikuwa kuna watu wanafanyiwa vitu vizuri wangeliendelea.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kutunza nyaraka zenye taarifa za watumishi, mimi kila nikija na watu ambao ni wastaafu wa *East Afrika* na nimewaleta pale kuna mtu hapa nitamtaja jina yupo nyuma hapa naweza hata nikamtaja jina. Kila siku tunapigiana simu mwisho juzi ananiambia sipo ofisini, mwezi uliopita ananiambia yupo likizo. Hii miguu ya punda itamalizia wapi kila tunapokwenda tunaambiwa kwamba mtu ndiyo hali ile ile. Haya mambo yanaendeje? Hii ni nchi ni yetu, tuhudumieni. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hutaki nirudi? Mimi nimefanya kikao na wazee wastaafu wamenipa malalamiko yao leo nikienda wananihoji nifanye nini napatia wapi ufumbuzi wa suala hili ikiwa kila unayemfuata hali ndiyo ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia jambo jingine, jambo linahusiana hapa na uratibu wa masuala ya mikopo ambayo inasimamiwa; tunajua kwamba *regulator* ni *BOT*, Kamati katika *paragraph* 5.9 imesema usimamizi wa sekta ya huduma ndogo ya fedha nchini ambayo ni *micro- finance*. *BOT* wametoa leseni wanasema kwamba 1,569 kwa hawa wanaotoa lakini kuna changamoto kwenye sehemu hii, mbali ya riba watu wanavunjiwa heshima sana na hizi taasisi zinazotoa mikopo midogo midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Maryprisca Mahundi Mheshimiwa Naibu Waziri nilimpelekea kesi nashukuru yule Waziri yupo shapu sana. Ameshughulikia suala amenipa watu mpaka mimi nimeungwa kwenye *group* ya watu wenye madeni kwa sababu yule mtu aliyekopa labda wanayemuhisi pengine katika *contact* zake kuna namba ya Mheshimiwa Mbunge kwa hiyo, na mimi naungwa kwenye madeni tuwalipie kule. Kwa hiyo, wanafedhehesha watu, wanarusha vitambulisho kwa hiyo watu wanadhalilishwa. *BOT* tunayo sera ya mikopo midogo, tuna sheria, tuna *regulations*, tufuatilie hivi vitu ili wananchi wasidhalilishwe hawa ndiyo wateja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, sikamati shilingi lakini kwa kuwa nimeona miguu ya punda yote kwa hiyo, inabidi kwamba nitafute ambaye hana mguu wa punda anisaidie. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege atafutiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipatia nafasi niwe miongoni mwa wachangiaji. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya kuweza kusimama katika Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu ambao wamempongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa nzuri ambayo anafanya ili kuhakikisha kwamba maendeleo yanamfikia

kila Mtanzania. Nitakuwa mwizi wa fadhila nisipomshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa sana katika Kamati yetu na mengi ambayo tumekuwa tukiwashauri wamekuwa wasikivu hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utakuwa katika maeneo matatu; eneo la kwanza tumesema katika Taarifa yetu ya Kamati juu ya kuiaondoa Tanzania kutoka katika matumizi ya fedha kwa maana ya noti na sarafu kwenda kwenye *cashless economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hiyo itasaidia sana Taifa kwani manufaa ya kwenda kwenye *cashless economy* yapo wazi. Kwa uchache pamoja na yale ambayo yametajwa kwenye taarifa yetu naomba nisisitize yafuatayo. Kwanza katika kautafiti kadogo nilikofanya inaonesha kwamba kwenda kwenye *cashless* economy kwanza ni *convenient* kwa maana ya kwamba ukitaka kutuma pesa au kupokea pesa au kufanya malipo ni rahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa shuhuda, Watanzania wengi wangependa walipe malipo yao ya kodi za viwanja lakini ukitaka kupata *control number* mpaka sijui uende manispaa, uende wapi unafika unaambiwa kuwa ofisa ambaye anahusika hayupo lakini tukishakuwa kwenye cashless economy ni kwamba taarifa zitakujia kwenye simu yako kiganjani, utalipa kwa wakati na Serikali itapata malipo yake ambayo ni stahili. Pia *cashless economy* katika hali ya kawaida ina-*encourage inclusion* kwa maana ya kwamba kila mwananchi atakuwa ameshiriki kwenye sekta ya fedha na utafiti ambao umefanywa na Benki ya Dunia inaonesha kwamba *cashless economy* inaondoa *gap* kwa maana ya *gender gap* inateremka kwa asilimia 4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafsiri yao ni nini? Hata hawa wakina mama ambao wamekuwa hawahusishwi kwenye uchumi huu wa kutumia pesa kwa maana ya noti watakuwa kwa vyovyote vile na wao wanashiriki katika uchumi wao, ni wakati muafaka sisi kama taifa tuhakikishe kwamba tunakwenda huko.

Mheshimiwa Spika, tulipata nafasi ya kwenda nchi moja jirani, unafika wakati unataka kulipa kwa *taxi driver* anasema naomba nikupe *PIN number* ili uweze kulipa. Hii pia inasaidia hata hii habari ya kuwa na ujambazi unapungua kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu hakuna pahali ambapo unakutana na pesa. Pia inapunguza rushwa, rushwa ni rahisi sana pale ambapo watu wanakubaliana niletee kiasi fulani lakini kwa kutumia *system* pesa zitaenda kule ambako zinatakiwa ziende.

Mheshimiwa Spika, hata suala zima la *tax evasions* kwa kutumia *cashless* hakuna mtu ambaye atatumia fursa kirahisi kuweza kukwepa kodi na hapa tumesikia zinakuja tafsiri kwamba baadhi ya watu wanabaguliwa wanaambiwa walipe kodi lakini nini ambacho kinasababisha mtu alipe kodi? Ni kipato chake na sio kazi anayofanya ndiyo ambayo inamsababisha alipe kodi. Kwa hiyo, inakuwa ni rahisi kuhakikisha kwamba yeyote ambaye anastahili kulipa kodi analipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana mwanzo ukawa mgumu tukasema vijijini kwetu itakuwaje? Naamini Mheshimiwa Waziri anakuja kwenye bajeti kuu atasema kutakuwa na kiwango ambacho kitaruhusiwa kutumia noti za kawaida lakini hizo noti nyingine kwa mfano kuanzia shilingi 50,000 isikubaliwe pahala popote ikatumika *cash* twende kwenye *system* ya kutumia simu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika kama kuna maeneo ambayo tumefanya vizuri kama Taifa huwezi kuamini kwamba kwenye *mobile transaction* sisi tumefanya vizuri lakini kuna watu ambao wamekuja nyuma yetu wanafanya vizuri zaidi ni wakati muafaka sisi turudi katika mambo ambayo tulianzisha kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo naomba nichangie ni kuhusiana na *BOT* kuendelea kununua dhahabu, ni uamuzi ambao ulifanywa na Bunge lako Tukufu, ni uamuzi wa busara. Dhahabu ambayo tulijaliwa na Mwenyezi Mungu sikuzote inapanda thamani ukilinganisha na *hard currency* kwa maana ya dola, euro ukienda zinzshuka thamani yake. Kuna mambo machache ambayo ni lazima tufanye kama Taifa, Benki kuu

inaponunua dhahabu kuweka kama reserve wananunua kwa niaba ya Watanzania wote. Haiwezekani sheria ambazo zinatumika anaponunua mfanyabiashara wa kawaida na inaponunua *BOT* kwa niaba yetu sisi sote sheria zikafanana si sahihi, lazima kuwe na *preferential treatment* kwa *BOT*, vikwazo vyote ambavyo vinasababisha *BOT* wasinunue dhahabu kwa wingi viondolewe na tuwe na wivu kabisa kwamba hawa wananunua kwa niaba ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Mheshimiwa Waziri ni vizuri ule mrabaha ambao unapata *in terms of cash* busara itumike tusipokee *cash* tupokee dhahabu maana hicho ndiyo cha kwetu na tukakiweka hicho kitatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hata sheria ya *VAT* sasa hivi inavutia kwa mfanyabiashara binafsi kununua dhahabu ku-*export* kuliko *BOT* kununua. Lakini pia tunapata faida gani kama Benki Kuu itanunua dhahabu kwa bei kubwa kuliko mwingine yeyote *so long* wanatumia pesa ya Kitanzania ambayo tuna uhakika dhahabu hii inaendelea kupanda thamani. Itakuwa ni kivutio kikubwa sana na hasa kwa wachimbaji wadogo watakuwa na uhakika wa soko na fedha hizo zitatumika maana watawekeza ndani ya Taifa hili. Hakuna mchimbaji mdogo ambaye anaenda kuwekeza Dubai wote watawekeza Tanzania. Kwa hiyo, iwe ni namna ya kuwasaida wachimbaji wadogo tuwape bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna hili jambo limekuwa likitia mashaka, kuna dhahabu ambayo inatoka nje ya Tanzania lakini kwa masharti tuliyokuwa nayo jinsi ambavyo ni magumu wanalazimika kwenda kuuza kwa nchi jirani na hizo nchi jirani zinaonekana kwamba zinauza dhahabu nje ya nchi nyingi wakati hawana hata shimo moja la mgodi la kuchimba dhahabu, itatuchukuwa muda gani kujifunza kwamba kwenye uchumi ni suala la kufa na kupona? Tuna shida gani pale ambapo dhahabu tukaipokea kutoka kwa majirani zetu kama sisi hatusababishi wakaenda kupigana vita? Wakija hapa kwetu wanaona fahari ya kuuza dhahabu, kwanza tunaelewana kwa lugha lakini eti tunaweka sheria ambazo tunataka mpaka tu-*trace* sijui ili itoke wapi? Inatuhusu nini mtu ameleta dhahabu tununue isaidie

maendeleo ya Watanzania tukidhani bado tunafanya shughuli za ukombozi, ukombozi tulishamaliza alimaliza Baba wa Taifa sasa hivi tuna kazi ya kujenga uchumi. Fursa yoyote ya kuleta uchumi kwa Watanzania tuna kila sababu ya kuchangamkia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo naomba kuchangia ni kuhusiana na kuimarisha ofisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu kama muda utaruhusu Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya na tutamalizia naye.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nipate kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti kwamba hakuna kipindi katika historia ya nchi yetu ambacho fedha za maendeleo zimekwenda kwenye miradi kama kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita na hili sihitaji kulijengea hoja sana kwa sababu kila Mbunge anakotoka analo la kusema kutokana na miradi ambayo Serikali imefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaposimama hapa kuongea ni vile tumeona Mheshimiwa Rais ametuonesha uelekeo wa kwamba, mambo yanawezekana kwa hiyo, na sisi tunakuwa tunasimama kuendelea kushauri katika kipindi hiki ambacho tumeona mambo yakifanyika, Mheshimiwa Rais akiyafanya, ili kama nchi tupige hatua za kimaendeleo kwa pamoja. Sasa yapo mapungufu

katika maeneo ya makusanyo ya mapato ambayo kimsingi ni lazima tuyafanyie kazi kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kwenye mfumo wa utumishi wa nchi yetu hizi nafasi za Maafisa Masuuli tukae chini upya tuone namna ya kuwapata. Haiwezekani uwe na Afisa Masuuli mwenye dhamana ya Wizara au Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Serikali anajua tu kutumia, lakini hajui kukusanya. Ni lazima hawa watu tuwe tunawapata kwa viwango fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua kwa sasa Maafisa Masuuli wengi mamlaka zao za uteuzi zipo kwa Mheshimiwa Rais, lakini bado sisi, kama Bunge, tunayo nafasi ya kuja kutunga Sheria upya kuweka viwango vya namna ya kuwapa Maafisa Masuuli wa Wizara, Maafisa Masuuli wa Wakala wa Serikali, Maafisa Masuuli wa Idara mbalimbali za Serikali na Maafisa Masuuli wa Halmashauri zetu, ili tuhakikishe kwamba, tunapopitisha mapato na matumizi hapa wakatusaidie namna ya kukusanya kama ambavyo wanafanya vizuri kwenye kutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa mifano ya mapungufu machache katika usimamizi wa Mapato ya Serikali Kuu. Sitaongea sana, nitataja maeneo machache au taasisi chache; ambayo yanatokana na ukaguzi wa hesabu za vitabu vya Taasisi za Serikali, Idara, Wizara au Wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pungufu la kwanza ni kutokukusanya mapato ya kikodi na yasiyo ya kikodi. Zipo taasisi zetu hazikusanyi vizuri. Nitatolea mfano Mwaka 2022/2023 na, *off course,* mchango wangu wote takwimu zake zinajikita katika Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilishindwa kukusanya takribani shilingi bilioni 32 katika Mradi wa Kupima, Kupanga na Kurasimisha Ardhi. Mradi umefanyika kwa zaidi ya asilimia 90, hati zimetolewa, lakini mapato hayajakusanywa, shilingi bilioni 32. Mimi naamini kaka yangu Mheshimiwa Jerry, Waziri wa sasa wa Ardhi, hili atalifanyia kazi kwa sababu, tuna imani nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara, Taasisi, Wakala na Idara za Serikali kutokukusanya mapato yasiyo ya kikodi, jumla ya shilingi bilioni 61. Hiki siyo kitu kizuri. Ndiyo maana nasema hawa Maafisa Masuuli ni lazima tuangalie namna nzuri ya kuwapata. Wametoa huduma, lakini makusanyo ya maduhuli hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa zimeshindwa kukusanya shilingi bilioni 8.9 kwa sababu ya kukataliwa kwa madai yao na Mfuko wa Bima ya Afya. Kwa nini yamekataliwa?

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu, wamejaza tu fomu vibaya. Hebu fikiria unakuwa na Afisa Masuuli mahali, kwa kushindwa tu kujaza fomu, ameshindwa kuzijaza fomu vizuri halafu tunakosa shilingi bilioni 8.9 ambazo zilikuwa zirudi zinunue dawa na kuhudumia watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali za Rufaa za Mikoa nazo pia kuna wakati ambapo Bima ya Afya imeshindwa kuzirejeshea gharama ambazo zimetibu watu, kiasi cha shilingi bilioni 12.5. Kwa hiyo, ndugu zangu haya mambo ni limlolongo lirefu hivi ambalo ni lazima tuangalie *entirely* kwenye mfumo wa Serikali, watendaji wakuu kwenye maeneo mbalimbali tunawapataje? Nasisitiza kuwa, hatuwezi kuwa na aina ya watu ambao wanajua kutumia, lakini hawajui kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* wamekopesha pembejeo za shilingi bilioni 25 na mwaka huo wa takwimu hizo ambazo nazitaja walikuwa wameshakiri kwamba, shilingi bilioni 20 hazitaweza kurudi. Hizi ni fedha ambazo zinatakiwa zirudi zikawasaidie wengine na haya ndiyo mapato ya Serikali ambayo tunayapigania hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *REA* wanapata mgao kutoka *TANESCO* kwenye mauzo ya umeme, kiasi cha asilimia tatu ya mauzo wanapewa *REA,* kwa ajili ya kuendeleza miradi yetu ya umeme vijijini. Mwaka huo nilioutaja hawakurejeshewa shilingi bilioni tisa na *TANESCO* kwa maana *TANESCO* walikusanya shilingi trilioni 3.25

na asilimia tatu ya hiyo ilitakiwa iwe shilingi bilioni tisa, haikurudi kule; *obvious* miradi ya umeme haitatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa na Maafisa Masuuli ambao wanajua kutumia, lakini hawajui kukusanya. Wizara, Taasisi na Idara za Serikali makusanyo ni pungufu ukilinganisha na bajeti. Hapa natolea mfano wa idara tisa ambazo zilikuja hapa tukazipitishia bajeti ambazo kwa ujumla wake ilikuwa ni shilingi bilioni 381. Wao wamekwenda kukusanya shilingi bilioni 172 halafu wapo tu. Pia, kuna Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo, Mfuko wa Pembejeo, Mfuko wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Mfuko wa Taifa wa Maji, Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rukwa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, hizi taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jingine Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ardhi. Mimi nashukuru kaka yangu mchapakazi, Mheshimiwa Mchengerwa yupo, ataenda kutusaidia, mtusaidie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ardhi tuliwapitishia hapa, Mwaka huo wa 2022/2023, wakatoe hati ambazo zingetuwezesha kupata shilingi bilioni 147.5 lakini kazi hiyo haikwenda kufanyika. Sasa ukiangalia haya mambo ndiyo yanafanya mwisho wa siku tunakuja kulaumiana hapa kwamba, kuna jambo halikufanyika kwa sababu, fedha haikupatikana. Ni lazima tukaangaze Serikali yote kwa ujumla, hasa watendaji wakuu, Maafisa Masuuli wa maeneo hayo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo hili ambalo limetajwa la *TRA* na habari ya kodi zilizoshikiliwa kwenye Mahamaka za Rufaa za Kikodi, shilingi trilioni 10. Ndugu zangu kwenye hili nafikiri yapo mambo ambayo sisi tunatakiwa kufanya hapa Bungeni, ili kulirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni tupitie upya Sheria zetu za Kikodi. Sheria zetu za Kikodi zinaleta mazingira ambayo yanasababisha mlundikano wa hizi fedha kwenye Mahakama zetu za Rufaa za Kikodi. Kwa mfano, mtu asipotoa *EFD* anatozwa

*penalty* au asilimia 20 ya *amount* ambayo hajatolea risiti. Fikiria, mtu ambaye haja-*declare* shilingi milioni 200, asilimia 20 ya shilingi milioni 200 ni shilingi milioni 40. Hakuna mtu ataweza kulipa hiyo. Ataenda ku-*pack* kwenye Mahakama ya Kodi, atatulia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii Sheria siyo tu kwamba, haituwezeshi kupata tulichokusudia, lakini inafanya wafanyabiashara wengi wakajifiche kwenye Mahakama za Kikodi. Vilevile, Sheria hizi wakae chini wazungumze nje ya mfumo, hata wakija kuelewana, Mheshimiwa Waziri fedha hii hautaipata. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, kengele yangu ya mwisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa, ya pili hiyo. Ahsante sana.

**MHE KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kuna Sheria ambayo tumesema...

**SPIKA:** Mheshimiwa ni ya pili. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ooh, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu. Tutamalizia na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia Bajeti ya Wizara hii ya Fedha mchana wa leo. Kwanza naanza kwa kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuamka salama na kuwa ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, la pili ni, kwa kuwa, Wizara hii inaratibu upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali,

nachukua fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha nchi yetu kupitia bajeti tunazozipitisha hapa Bungeni tunapata fedha za kutosha na fedha zinazopatikana zinaenda kwenye miradi iliyokusudiwa. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu, Dkt. Natu na watendaji wote. Kiukweli wamekuwa wasikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati yako ya Bajeti Mheshimiwa Waziri Mwigulu na viongozi wenzie wamekuwa wasikivu. Mambo mengi tuliyowashauri mara kwa mara wamekuwa wakiyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi, kwa kuwa, kama nilivyosema, kazi kubwa ni kuratibu upatikanaji wa fedha, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha kupatikana wa mkopo wa shilingi trilioni sita. Nataka niseme kwa kweli, kwa masharti ya riba ya asilimia 00.1 ambayo yamefafanuliwa kulipa ndani ya miaka 40 na kwa *grace period* ya miaka 25, hakuna nchi yoyote ambayo inaweza kukataa fursa hii na ukizingatia nchi hiyo inatekeleza miradi mingi ya kimkakati kwa wakati mmoja. Nchi hiyo imepanua shughuli nyingi za jamii; sekta ya afya, sekta ya elimu, sekta ya kilimo na sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, imeendelea kuajiri watumishi wengi kwa hiyo, ni wazi kuwa kazi nzuri inayofanyika ya kukusanya mapato ya ndani. Hapa naipongeza sana *TRA* ambayo imeendelea kufanya vizuri na tunaona ukubwa wa majukumu. Kwa hiyo, unapopata fursa ya nafuu ya namna hiyo kwa kiwango kidogo cha riba kwa kweli, ni lazima tumshukuru Mheshimiwa Rais na tumpongeze sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Mwigulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pamoja na pongezi hizo mimi nirejee alipomalizia Mheshimiwa Reuben. Licha ya kuwa tunafanya vizuri, na hapa nikiwa kama balozi wa kodi, nawapongeza sana *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwenye hili suala la mashauri ya kodi nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu, kwenye hizi shilingi trilioni 10 ambazo mashauri haya yapo kwenye *TRAB* na *TRAT,* kuna jambo dogo tu ambalo na sisi kamati tumeshauri. Ninaipongeza taarifa yetu, kama Mjumbe, muwasilishaji Makamu Mwenyekiti amewasilisha vizuri. Suala la kuteua wajumbe kwa mikoa 14, kwa hii mikoa 12 iliyobaki hili jambo liko ndani ya uwezo wako Mheshimiwa Waziri. Ni suala la kutangaza tu hizi nafasi, mikoani wapo, kuweka mkakati wa kulimaliza ndani ya mwezi mmoja na kumaliza teuzi mbalimbali, ili haya mashauri yasikilizwe, lakini hizi shilingi trilioni 10 ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi sambamba na hilo la kutangaza hizo nafasi, pia muwezeshe hizo *TRAB* na *TRAT* na Mahahakama ya Rufaa kwa fedha, vitendea kazi na maslahi ya watumishi wa maeneo, ili wafanye kazi usiku na mchana tupate hii kodi. Kwa hiyo, hili naliona liko ndani ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake ni namna gani ambavyo bado kuna muamko mdogo wa kudai risiti, kutoa risiti na kampeni mbalimbali. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa, sensa tuliyoifanya 2022 imeainisha na pia, kulikuwa na madodoso ya kutuuliza ni shughuli gani tunazofanya, nakuomba, ili kutatua changamoto na kuongeza wigo wa walipakodi, Serikali mtumie takwimu za sensa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walipakodi ni wachache kwa hiyo, unakuta wengi hawalipi. Kwa mfano, Watumishi wa Serikali ndiyo wanaolipa kodi ya inayopatikana kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri na Serikali walau muwatizame hawa Watumishi wa Serikali. Badala ya kuwalipa zile posho, ili kuwasaidia kukabiliana na masuala mbalimbali ya kuichumi, naomba sehemu ya posho ziingie kwenye mishahara yao, Serikali inaweza kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na watumishi wa Serikali, niwaongelee wastaafu. Mheshimiwa Hassan amesema vizuri kwamba, wastaafu sasa hivi muhuishe vile viwango wanavyolipwa kwa mwezi kwa sababu, maisha yamepanda. Wamefanya kazi nzuri na hili linawezekana pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nataka niseme kuhusu hizi pesa mnazopeleka kwenye miradi ya maendeleo. Kwa kweli, mimi nimefurahi mwaka huu nimeona miradi mingi ya maendeleo, zaidi ya miradi 90 ya zaidi ya shilingi bilioni 96. Nataka niseme kweli, hela zimefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi *UWT* tumeona miradi 869 na mabilioni ya fedha, lakini kuna changamoto. Kwa mfano, mwaka huu wa fedha unaoendelea, kuna hili jambo la pesa kushikiliwa, pesa zinasoma kwenye mfumo, lakini Maafisa Masuuli wanashindwa kuzitumia kwa sababu, zinashikiriwa. Nakuomba Mheshimiwa Mwigulu utoe kauli mahususi, ili tuondoe mkanganyiko kwenye Halmashauri zetu. Tujue zinashikiliwa kwa utaratibu gani, kama ni mifumo yetu hii ya fedha ufafanuzi utolewe, ili tusiwape lawama watendaji wetu kuonekana pengine hawajawajibika, kuonekana pengine ni wazembe, lakini kwa hili mtoe ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mfumo wa manunuzi, Serikali mmefanya vizuri sana kuunda mfumo wa manunuzi na ninampongeza Mr. Maswi kwa kazi nzuri, lakini ninachoomba tu ni tusikilize maoni baada ya kuanza kutekelezwa. Kwa sababu, pia, ipo changamoto wadau waliokuja kwenye kamati walikuwa wanasema kwamba, kidogo kuna mkwamo katika kuhakikisha manunuzi yanayotangazwa, yanafanyika kwa haraka. Kwa hiyo, pamoja na nia nzuri, mmetumia wataalam wa ndani na mmefanya mapinduzi makubwa, lakini nawaomba kushughulikia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni, nakushukuru wewe kwa kutupa fursa Kamati yetu ya Bajeti na kuwawezesha wadau kuja kwenye Kamati yetu. Tunayoyasikia kwenye kamati ambayo tunaamini Serikali mmekaa na kupitia kongamano la kodi na kongamano la uwekezaji tulilofanya mwaka jana, kuna

maendeleo makubwa ambayo mmekuwa mkiyafanya kwa kuwasikiliza wadau. Naomba hili suala la tozo nyingi, hasa kwenye utekelezaji wa *blueprint,* nalo Serikali mlisimamie ili wale wadau, hasa wenye viwanda na wafanyabiashara, ufike wakati mfumo wa kodi na hii mifumo ambayo kupitia hata *TRA*, mara wanasema uko chini basi muwe mmefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya mimi naendelea kuishukuru Serikali. Kuona ni kuamini, kazi inafanyika. Ukija *site* miradi inaonekana, lakini msiwasahau wanaodai, hasa wa ndani. Nimeona hapa tuliwapitishia shilingi trilioni 10, mpaka sasa hivi mmeshalipa deni la Serikali shilingi trilioni nane na zaidi mmelipa deni la ndani. Pia, tuwatazame hawa wakandarasi, hasa wakandarasi wanawake. Mmetaka kuwawezesha na kuwapa uwezo basi zinapoletwa zile hati za malipo naomba muwalipe.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba mtoe ufafanuzi kwa sababu, inavyoonekana kwenye ziara zetu, viongozi wa kisiasa, tunapopokea malalamiko ya wafanyabiashara kama kuna jambo ambalo pengine linakwamisha halmashauri naomba mtoe ufafanuzi, ili mipango yenu ieleweke kwamba, watalipwa lini na kwa kiwango gani. Baada ya kusema maneno haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na hongereni Wizara ya Fedha. Kazi iendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa maoni yangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ameniwezesha kuiona siku hii.

Mheshimiwa Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutafuta fedha na kuidhinisha, ili ziweze kupelekwa katika maeneo yetu. Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Naibu Waziri Chande, Katibu Mkuu na

watumishi wote waliopo idara na Wizara ya Fedha kwa utendaji kazi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najielekeza katika utekelezaji wa majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kumekuwa na ongezeko la mawanda ya ukaguzi mwaka hadi mwaka, lakini hayaakisi au hayaendani na bajeti inayotengwa katika ofisi hii ya mkaguzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Serikali Mtandao tuna mitandao 460, lakini ukaguzi ulifanyika kwa mifumo 49 tu ambayo ni katika taasisi 24 za Serikali, baadhi ya Taasisi za Serikali haziko katika mfumo. Ukiangalia pia, mifumo hii haisomani yenyewe kwa yenyewe kwa hiyo, inampa kazi ya ziada Mkaguzi wetu Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mawanda kumesababisha Ofisi ya *CAG* kufanya kazi ya ukaguzi kwa wakati *(real time auditing),* ambayo inasababisha kuokoa fedha katika miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo *SGR*, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na miradi mingine. Ukaguzi huu unahitaji fedha nyingi, wataalam wenye ujuzi na taaluma kubwa. Kwa hiyo, ni ukweli usiopingika ofisi hii, kulingana na upanuzi wa mawanda, inahitaji kuongezewa fedha kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa ufanisi, lakini sisi tulitamani iende zaidi ikafanye ukaguzi wa *real time audit* katika manunuzi makubwa ya Serikali kwa sababu, zaidi ya asilimia 70 ya bajeti yetu imejielekeza katika manunuzi. Kwa kufanya hivyo, tutaokoa fedha zaidi ama tutasababisha miradi isitekelezwe chini ya kiwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kuungana na Kamati ya Bajeti nikiwa nio Mjumbe, kwanza nashukuru na kupongeza Maoni ya Kamati yaliyosomwa na Makamu Mwenyekiti. Kamati imehimiza kupunguza matumizi ya fedha taslimu ambayo yamekuwa ni changamoto katika ukusanyaji wa kodi. Hii inaipa ugumu *TRA*

kufuatilia miamala mingi ya kibiashara ambayo imefanywa kwa fedha taslimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana na Ushauri wa Kamati wa kufanya mabadiliko katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438, kwa kuweka sharti la kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki kwa wakati kwa kufanya manunuzi ya huduma na fedha taslimu. Mimi napendekeza Mheshimiwa Waziri katika kanuni zake labda aweke kiwango cha kuanzia. Kwamba, ni kiwango gani tufanye kwa matumizi ya kielektroniki, lakini Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kwa matumizi ya kielektroniki na pia, watoe elimu, kwa ajili ya kufungua akaunti benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isimamie kwa kupunguza gharama ya kufanya miamala hii. Watu wengi wanakwepa kutumia miamala ya kibenki ama ya simu kutokana na makato kuwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilimtumia mwananchi mmoja fedha ya ununuzi wa saruji kwenye akaunti, akaniambia niweke na fedha ya kutolea. Maana yake ni ukweli usiopingika kwamba, hata fedha zinazoletewa pale dukani kwake haweki benki, anazibeba kama zilivyo anapeleka labda kwa wakala mkuu wa *cement* au wa bidhaa yoyote kwa sababu, anakwepa makato makubwa. Kwa kufanya hivyo, ni *risk* kwa mfanyabiashara, hivyo, Serikali iendelee kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali ione namna ya kutoa motisha kwa wafanyabiashara, mathalan kuna mtu unaenda kununua bidhaa za shilingi milioni 10, vifaa vya mabomba, unamwambia utoe fedha kwa benki, anakwambia nenda pale pembeni ukatoe kwa wakala halafu uniletee fedha taslimu. Kwa hiyo, Serikali haina budi kuangalia kuna changamoto gani ya kwa nini wafanyabiashara wanafanya hivyo. Huenda kuna gharama kubwa ama ni utaratibu wa kuweza kukwepa ulipaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Maoni ya Kamati ya kupunguza gharama ya miamala katika mfumo wa malipo

madogo madogo, *TIPS,* kama nilivyosema. Wengi wanaofanya ni wananchi wale wa kiwango kidogo kwa sababu, gharama za kutuma fedha kwenye miamala ya simu zimekuwa kubwa. Pamoja na hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kupunguza gharama za kutuma fedha kutoka benki moja kwenda nyingine kwa mujibu wa Tangazo la Benki Kuu la Tarehe 22, lakini kwa upande wa miamala ya simu gharama hizo bado ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninashukuru kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu kwa leo. Nitawatangaza Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao kwenye mchango wa mchana ama jioni tutakaporejea.

Tutaanza na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Mhandisi Chiwelesa, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na tutaendelea kuwataja wengine kwa kadiri muda utakavyokwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao wameingia hapa Bungeni tukiwa tumeshatangaza wageni waliokuwa wamepata nafasi ya kuingia asubuhi. Sasa niwatangaze hawa wageni tulionao hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba - Waziri wa Fedha na hawa ni viongozi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo wa taasisi zilizo chini ya Wizara, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo wawakilishi wa Benki ya *PBZ*, *TAGB* na *CRDB,* karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wengine ni Wajumbe wa Bodi ya Taasisi ya Ukaguzi wa Ndani na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini *(GPSA)*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ambaye ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hawa ni Viongozi wa Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambao ni ndugu zake kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni mchungaji kutoka Runzewe, Kanisa la Efatha – Geita, viongozi, manabii, mitume, wainjilisti na walimu wa neno la Mungu kutoka Makanisa ya Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Haya wageni nane wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni walimu kutoka Shule ya Sekondari Ihande, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 80 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni waalimu wastaafu kutoka Manispaa ya Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Wageni 30 wa Mheshimiwa Joseph Kamonga. Hawa ni wapiga kura wake kutoka Jimboni Ludewa, Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Na pia wapo wageni 101 wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni wanafunzi 90 na walimu 11 kutoka Shule ya Msingi Nalopa ya Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hii Wizara ya Fedha. Kwanza naishukuru sana na ninaipongeza Serikali ya Mama yetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya katika kuleta maendeleo katika nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya. Kama tunavyofahamu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mojawapo ya kazi yake kubwa anayoifanya pamoja na timu yake kwanza ni kutafuta fedha ambazo ni za makusanyo ya ndani, hali kadhalika na kutafuta fedha nyingine za mikopo na misaada kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu za maendeleo katika nchi yetu. Kazi hiyo ni nzuri,

pamoja na changmoto ndogo ndogo za hapa na pale ambazo zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, kwamba pamoja na makusanyo ambayo tunakusanya, kulingana na mahitaji tuliyonayo, bado yale makusanyo tunayopata hayatoshi. Kwa kuwa hayatoshi, ndiyo maana utaona fedha zetu nyingi za makusanyo zinalipa madeni, zikilipa na mshahara, tayari tunabaki na fedha ambazo haziwezi kufanya shughuli zozote za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukubaliane tu kwamba Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa kidogo ya kuhakikisha kwamba anajitahidi kuendelea kupata fedha zaidi ambazo zitatusaidia sisi wenyewe tukaweza kujiendesha. Maana leo hii unakuta karibu fedha nyingi ambazo zinatusaidia tufanye maendeleo, ni zile tunazokopa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama makusanyo yote tunamalizia kwenye mkopo pamoja na kulipa mishahara, sasa ni lini tutafika mahali ili tuweze kusimama tuweze kujiendesha kama nchi? Kwa hiyo, nadhani hiyo ni chanagmoto kidogo tuliyonayo. Ndiyo maana hata baadhi ya nchi zile ambazo zinatupatia mikopo, zikitikisika zenyewe na sisi nao tumeendelea kuumia zaidi huku.

Mheshimiwa Spika, nadhani hiyo ni changamoto kubwa ambayo lazima kama Serikali Mheshimiwa Waziri aiangalie kwamba ni namna gani atatusaidia kutatua taizo hilo. Leo kama hivi tunavyoongea, wakati mwingine ninavyoona katika mtazamo wangu, ni kwamba tukipata, yaani inakuwa ni kama *boom* ya chuo. Yaani *boom* ikipatikana, basi walau nchi inachangamka, lakini ikifikia mahali mikopo ikiisha tunarudi kwenye zile zile tabu zetu.

Mheshimiwa Spika, leo hivi tunavyoongea, hali ya uchumi kwa wastani ni ngumu, yaani hata kwenye mzunguko fedha hazipo. Hata leo hivi tunavyozungumza, ukizunguka tu hapa Mjini Dodoma, zile shughuli zote zilizokuwa zinafanyika kama shughuli za ujenzi, utaona tu makreni yamening'inia, lakini hakuna ujenzi

unafanyika. Hiyo inaonesha kwamba ni kwa sababu sasa hatuna fedha.

Mheshimiwa Spika, hata katika maeneo mengine, ukiangalia miradi mingi sasa katika kipindi hiki, hiyo miradi ya barabara zile kambi unakuta zimesimama. Mradi umeanzishwa, umefanyika kidogo, lakini wamesimama kwa sababu hawana fedha. Mfano, hata ukifika pale kwangu Musoma, kuna mradi wa uwanja wa ndege tuliuanza pale nadhani toka mwaka 2017 na tulitegemea kama ule mradi ungekuwa umekamilika, lakini mpaka leo upo kwenye wastani wa 53%. Mradi unafikia mahali unasimama na ukiwafuata wale Wachina wanakwambia hatuna fedha, tunaidai Serikali yenu fedha nyingi, kwa hiyo, tumesimama. Kwa hiyo, inakuwa ni changamoto kidogo.

Mheshimiwa Spika, hata wale watu wengine wa kawaida nao wanaendelea kudai, unakuta mbali na mkandarasi, hata wale watu waliopaswa kupewa fidia pale uwanja wa ndege ambao wao *process* zote zilishakamilika, lakini tumefika mahali hapo ukienda kumwuliza Waziri husika anakwambia kila kitu kipo kule Wizarani na sasa hakuna fedha.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Mheshimiwa Waziri aangalie kwamba ni namna gani ataendelea kufidia haya, na kuona namna ambavyo tutaendelea kuwasaidia hawa watu wetu. Kibaya zaidi, siyo hilo tu suala la fidia, lakini hata kwenye ile miradi, mfano makandarasi wetu wa ndani, ndiyo hawalipwi kabisa; wale wazabuni, hawalipwi kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inaashiria nini? Tafsiri yake ni kwamba unamkuta mtu amekopa halafu aka-*supply* na baada kuwa ame-*supply* kinachofuatia ni kwamba ameshindwa kulipa ule mkopo wake na matokeo yake ile dhamana yake kwa maana ya nyumba inaenda kukamatwa na kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tafsiri yake ni kwamba kumbe hii Serikali sasa nayo inaendelea kuchangia kuwasili watu wetu na hili nadhani ni jambo halikubaliki. Tuna kila aina ya sababu ya kuona kwamba ni namna gani Mheshimiwa Waziri ataweza

kutukomboa katika adha hii, kwa maana ya haya madeni yaliyopo yaweze kulipika na maisha yaendelee.

Mheshimiwa Spika, leo unaweza kufika mahali wakati mwingine hata halmashauri inakaa wiki mbili hakuna *transaction* ya malipo yoyote inayofanyika. Ukiuliza wanakwambia kwamba ni mfumo. Mfano mimi nakumbuka hata fedha zangu za Mfuko wa Jimbo zilipoingia, zikaonekana zimeingia. Tunaenda ku-*draw* tunaambiwa fedha hazitoki. Sasa fedha hazitoki kwamba imekuwaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii yote ni hali ambayo inaendelea kuonyesha kwamba changamoto bado ni kubwa na kuna kila aina ya sababu ya kuhakikisha kwamba tunapambana na hatimaye tuweze kutoka kwenye hali hii tuliyonayo ili maisha ya Watanzania yaendelee kuwa mazuri. Pamoja na hayo, nashauri tu mambo matatu kwa haraka kwa ajili ya muda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, kengele imegonga?

**SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. VEDASUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Fedha. Jambo la kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Anafanya kazi nzuri sana kwa sababu sisi Wabunge ambao tuko kwenye majimbo huko

tunaona *flow* ya fedha kwenye majimbo yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kama siyo msimamo mzuri wa Serikali kwenye ukusanyaji wa mapato, na pia kama siyo kuwa na utashi wa kisiasa kwamba nini kinatakiwa kwenye nchi, tusingefika hapa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais, na watendaji wote wa Wizara ya Fedha. Hongera sana na tunawaunga mkono kwa yale ambayo wanayafanya.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni moja tu, nina hoja kuhusu *cashless economy* ambayo Kamati imeshauri kupitia maoni yao waliyotoa kwenye maoni namba tano pale, wamesema, "*Serikali kuhimiza kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwa maana cashless*." Pia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa Na. 213 nao wamelizungumza hilo jambo suala la *cashless economy*.

Mheshimiwa Spika, nizungumze jambo moja. Kama nchi ni lazima tuchague upande wa kuelekea. Nilizungumza hilo wakati wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuhusu hili jambo la *cashless economy*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapa kuna wataalamu wa Wizara ya Fedha, lakini kuna wakubwa wa *TRA* wapo hapa, tunaomba kusema kwamba, *cashless economy* ndiyo uwelekeo wa dunia kwa sasa. Kwa nini tunazungumzia *cashless economy?* Ni kwa sababu cha kwanza inaongeza *taxbase* kwenye nchi. Moja kati ya hoja kubwa ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba *taxbase* ya walipaji kodi kwenye nchi ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, kati ya watu milioni 60 tuna watu milioni tatu au milioni mbili na *point* ndiyo wanalipa kodi. Kwa hiyo, tukifanya *cashless,* hatuna mdhamana. Tuki-*facilitate* watu kutumia zaidi *mobile money, credits card, internet, cheque* tutaweza kukusanya mapato kwa ukubwa sana. Kwa nini tunahitaji hii *cashless economy?* Tunapambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, mtego mkubwa wa rushwa upo hapa. Tutaweza kufuatilia fedha zinatoka wapi, zinaenda wapi na zinafanya nini kupitia mfumo huu ambao tukiamua kuutumia na kuipeleka hii nchi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kuongeza mapato na ukusanyaji wa mapato. Naipongeza *TRA* kwa sababu ukusanyaji wa mapato, licha ya njia ambazo zinatumika zinagombanisha sana wafanyabiashara na ninyi, lakini mmekuwa mkijitahidi kukusanya mapato. Watumishi wa *TRA* ninawapongeza sana kwa sababu ukusanyaji wa fedha ndiyo unaosababisha sisi Wabunge hapa ndani tukae, tujinasibu, tujisifie kwamba Serikali inapeleka miradi kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze wazi kwamba nchi yoyote, chakula cha Taifa lolote, ni kodi. Nchi yoyote ili iendelee, lazima tulipe kodi. Katika ulipaji kodi, lazima tuangalie namna nzuri ambazo zinaweza kusababisha tukakusanya kodi bila changamoto kubwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba kipaumbele kikubwa ni kusimamia mifumo ya kuhakikisha kwamba wanakusanya kodi. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, Kamati imeshauri, leteni mabadiliko ya Sheria tuhimize Watanzania kutumia mifumo ya *cashless economy* kwa ajili ya kukusanya mapato katika kupata bidhaa na kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa nini napenda hili suala lifanyike? Kwanza litafanikiwa kwa sababu Watanzania wengi wana *access* ya *internet* kwa sasa. Kwa ripoti ya Waziri wa Habari aliyepita nusu ya Watanzania wana *access* ya simu, wana *access* ya *internet*. Tukitumia hii *cashless economy,* tunaweza kufanikiwa mambo mengi sana. Moja ni kudhibiti masuala ya rushwa, lakini kubwa ni *taxbase* kama nilivyoizungumza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hili jambo litafanikiwa tu endapo mambo kadhaa yatafanyika. La kwanza, nimezungumza mabadiliko ya sheria. La pili, watu wa *TRA* ni vyema wakatoa *incentives* kwa watu ambao wanatumia *cashless economy* kwa kuweka *incentives* ambazo zinamfanya mtu aende huko akalipe fedha.

Mheshimiwa Spika, mathalan, unaweza ukapunguza *VAT*. Ukitoa *VAT at least* mtu anayelipa kwa kutumia mfumo kwa 16%, 15% na yule anayelipa kwa *cash* akalipa kwa 18% *obviously* lazima wananchi watakimbilia kwenye hii. Hii itatusaidia kama *TRA* kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, kubwa lingine ni kuzungumza na mabenki, mabenki watafurahia sana hii njia kwa sababu *survival* ya mabenki au kuishi kwa mabenki yoyote duniani ni *deposit* za wananchi. *Deposits* zitapatikana kwa kupitia *cashless economy*. Lazima tuwaondoe watu kwenye *mindset* ya kukaa na fedha.

Mheshimiwa Spika, katika hili Taifa mtu anajiona yuko *proud* sana akiwa na fedha, mabulungutu ameyashika mfukoni, anatembea nayo barabarani au ameyaweka nyumbani kwake, wakati katika hali ya kawaida ana-*risk* maisha yake na ana-*risk* uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri waongee na mabenki, kumekuwa na malalamiko kwamba kutoa fedha benki kwenda kwenye simu, makato yamekuwa juu sana. Mkishusha haya, yatasaidia Watanzania kutoka huko kwenye matumizi ya fedha taslimu na wakaenda kwenye *cashless economy*.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi hii itafanikiwa endapo mtawahakikishia Watanzania jambo moja. La kwanza, usalama wa fedha zao. Usalama wa fedha zao ndiyo msingi wa hili jambo Mheshimiwa Waziri. Kama hatutawahakikishia usalama wananchi, wataogopa kuweka fedha kwenye mabenki na kwenye mitandao ya simu kwa maana hizo *M-PESA, TIGOPESA* na shughuli nyingine za *mobile transaction*. Lazima tu-*support* usalama wa fedha za wananchi kwanza ili nao pia waweze kuwa na nia ya kuweka fedha huko.

Mheshimiwa Spika, pia kuwa na uhakika wa *network*. Kukusanya fedha kupitia kwenye mtandao kumekuwa na *records* nzuri sana. Naweza kutoa mfano mmoja wa Hospitali ya Tumbi Dar es Salaam. Hospitali hii kabla hatujafunga mfumo, kwa

maana ya ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo, walikuwa wanakusanya kama shilingi milioni tatu hivi kwa mwezi, au milioni sita.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufunga mfumo pale kupitia *GOTHOMIS,* wale watu wanakusanya zaidi ya shilingi milioni 30, shilingi milioni 40 kwa mwezi. Maana yake nini? Kuna *loopholes* nyingi sana za kutokukusanya kodi. Mapato ya fedha na ya Serikali yanapotea kwa sababu hatuna mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hili liwe ni moja kati ya mkakati wake. Lazima tufanye *reforms*, lazima tufanye *revolution* katika Taifa hili ambalo kwa asilimia kubwa tunatajwa kama ni namba mbili kwa usalama na upatikanaji wa mtandao barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hilo walifanye kwa kasi kubwa kuhakikisha kwamba nchi yetu inaenda kwenye matumizi ya fedha kupitia mifumo ya *cashless*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kumekuwa na changamoto kwamba, sisi kama Taifa tuna *geographical position* nzuri sana ya ku-*control* soko la kiuchumi kwenye Afrika Mashariki na Kati. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, upatikanaji wa dola kwenye Taifa letu uimarishwe kwa sababu sisi tuna *potential hub* ya kibiashara. Nchi nyingi zinazotuzunguka zinatuangalia Tanzania kama kitovu cha kiuchumi ku-*support* nchi ambazo zinatuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi kama *Mauritius* amefanikiwa kulifanya hili jambo, sisi Tanzania kwa nini tunakwama? Ni lazima Taifa letu likaendelea kusimamia mifumo yetu, *physical policy* zetu, upatikanaji wa dola uka-*support* biashara na wafanyabiashara wa nchi yetu na hata wale wa kigeni waone kama Tanzania ndiyo kimbilio la upatikanaji wa fedha za kigeni na baadaye tuweze kukimbiza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa ni ya kwangu, lakini kubwa ni kufanya *revolution* kwa ku-*support cashless economy* kwenye Taifa letu. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri namtakia kila la heri, na pia tunapongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Sisi wananchi wa Makete tunamwahidi kwamba tutaendelea kumuunga mkono, na pia tunawaunga mkono ninyi na tunawaunga mkono watu wa *TRA* kwa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuwezi kupata vituo vya afya, hatuwezi kupata barabara, hatuwezi kupata umeme wala hatuwezi kupata huduma nyingine zozote kama fedha hazikusanywi. Kusanyeni fedha ili Taifa lisonge mbele. Wanaopinga ukusanyaji wa fedha kwenye nchi yetu, ni watu ambao wanalisaliti na wanahujumu uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mataifa ya nje, utakuta mtu anajisikia aibu; au kosa kubwa zaidi kwenye mataifa hayo mengine ambayo tunayasifia yameendelea, *the shameless mistake* unayoweza ukaifanya ni kukwepa kodi kwenye nchi yako. Sisi lazima tusisitize watu walipe kodi, lakini lazima tupunguze mianya ya upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa. Kwa sababu ya muda nitajikita kwenye mambo kama matatu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni madeni ya wakandarasi, wazabuni na wahandisi washauri. Ni dhahiri bajeti hii inayopita na miradi mingi ambayo inafanywa na Serikali tunaifanya kwa kushirikiana na wenzetu ambao wengine watatu-*supply* baadhi ya vitu, wengine wanajenga na wengine wanatoa ushauri kwenye ujenzi ule. Watu hawa wamebeba mzigo mkubwa sana wa kusaidia bajeti zetu na kusaidia maeneo yetu kwa muda mrefu sana, na walio wengi wamekopa, wamefilisiwa na hawajalipwa pesa zao kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nilisemee hili kwa sababu mhusika ni Mheshimiwa Waziri wa Fedha, na ndiyo *custodian* wa fedha zote za nchi hii na ndiyo ambaye anawa-*feed* hawa wenzake kwenye Wizara za Kisekta. Nilitaka hiki kilio cha Wakandarasi akisikie na aone jinsi ya kukifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati nikichangia bajeti ya Wizara hii nilisema jambo moja, kwamba huwezi kuwa wewe unatoa pesa halafu kesho tarehe 30 Juni tukitoka hapa, miradi inatangazwa *almost* ya 5,000,000,000,000 au 7,000,000,000,000 kwa mwezi huo huo wakati bajeti yake ni ya kukusanya ndiyo aweze kulipa wale watu, hatutaenda.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake Watanzania wanaumizwa kwa sehemu kubwa na ushauri wangu wakati ule, nilishauri kwamba ni lazima Waziri na Wizara za Kisekta wa-*interlink* ili pale inapoonekana mtu anatangaza awe anajua. Akiona yaliyotangazwa ni mengi anaweza kutoa ushauri, akawaaambia subirini kwanza kwa sababu bajeti ni miezi 12 na lazima tuelewe kwamba Waziri ndiye anayepanga na bahati nzuri yuko kwenye Tume ya Mipango na juzi nimeona anaapishwa pale na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nina uhakika akikaa vizuri na wenzake wakaweka mipango mizuri, haya madeni ya wakandarasi yatalipwa kwa wakati vile vile wataweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tarehe 21 Novemba, 2023 niliona Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aliitisha mkutano wa wakandarasi, wahandisi washauri, wale ambao ni wazawa na Mheshimiwa Waziri alikuwepo pale. Kilio cha watu wengi na hasa

ambao tumekuwa kwenye hii sekta kwa muda mrefu tumekuwa tunalia na pesa yetu ambayo ni ya walipa kodi Watanzania kuwa inapelekwa nje na Watanzania wakibaki kama watwana hapa. Nishukuru Mungu mwenyewe alikubali na akatoa ahadi ya kupandisha kiwango ambacho kitakuwa kinafanywa na wakandarasi wazawa kutoka bilioni kumi mpaka bilioni 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nategemea tupate majibu kipindi anamaliza hapa tujue ile kanuni ameifikisha wapi ili miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara na ujenzi wa baadhi ya shughuli za Serikali, kodi inayokusanywa ikibaki ina-*rotate* humu ndani, uchumi wa Tanzania utakua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Mheshimiwa Waziri iko shida ambayo nimekuwa naiona na hii shida ni ya muda mrefu. Mikopo wanayopewa wakandarasi bado riba yake ni kubwa mno. Wengi wanacheza kwenye asilimia ishirini na, lakini kitu ambacho najiuliza, Serikali ndio mwajiri wa wakandarasi na pesa ipo na Waziri amekuwa anatuhakikishia pesa ipo na makusanyo tunayaona. Sasa anashindwa vipi kukaa na mabenki, pesa ambayo iko *assured* ni pesa ya Serikali, leo wakandarasi wanakopeshwa kwa riba kubwa namna ile.

Mheshimiwa Spika, walio wengi wanaumia, wanaumia kwa sababu umemkopesha mtu kwa riba ya zaidi ya 20%, halafu pesa yake umeichelewesha kwa zaidi ya miezi sita, matokeo yake hata faida aliyokuwa anaipata yote anaishia kulipia deni la riba benki. Haya nayasema kwa Mheshimiwa Waziri ili ayasikie kwa sababu kuna baadhi ya benki zimefikia *stage* wamesema hawatafadhili hata miradi ya maji kwa sababu miradi ya maji madeni yake yanachelewa. Mimi niko huku na wakandarasi najua, hili jambo namwambia kabisa, kwa sababu inafikia *stage* siyo kusema Watanzania wote wana dhamana za kuweka benki, kwa sababu miradi hii ni ya Serikali, mabenki yamekuwa yanaiamini mikataba inayosainiwa kati ya wakandarasi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mtu labda anapeleka mradi wa bilioni kumi anapewa *fifty percent* akafanye kazi, *fifty percent* atakatwa

kule, lakini unapochelewesha pesa ya yule mtu, benki wanakata ile ya kwao, wanakata mpaka anayopata kupitia riba, unakuta benki inabaki inamdai yule mkandarasi, yaani inachukua kila kitu mpaka inabaki inamdai hata hela hana.

Mheshimiwa Spika, sasa tuliombe hili awaangalie Watanzania hawa alioapa kuwasaidia kwa kuongezea hiyo wapunguziwe riba, lakini awalinde kwa kuhakikisha malipo yao yanatoka mapema, kwa sababu hakuna mkandarasi Mtanzania ambaye ana-*raise invoice* za kuidai Serikali riba. Sasa wasaidie hata wao tabu wanayoipata benki, naamini Waziri anaweza akaimaliza kama Waziri wa Fedha ili hawa watu wafanye kazi kwa amani na wampe ushirikiano mzuri ambao anauhitaji.

Mheshimiwa Spika, wiki mbili zilizopita niliona alikuwa anaongelea habari ya watu kulipa kodi. Hakuna mtu anayepinga kulipa kodi, maana hatutaweza kujenga uchumi wa nchi hii na miundombinu hii ambayo tunaisema bila kulipa kodi, lakini nataka nirejee Waraka Na.4 wa Hazina wa mwaka 2019, unaoelekeza Maafisa Masuuli wote wa Nchi hii kukusanya madeni ya wakandarasi wanaodaiwa kodi kupitia madeni yao wanayodai Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa huu waraka unasema unakusanya madeni ya kodi kwa watu wanaoidai Serikali. Sasa hapa naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri, yaani mimi nimei-*supply* Serikali na bahati mbaya sana maelekezo yao yalivyo ni kwamba kila anaye-*supply* ili aweze kulipwa ni lazima atoe *invoice* ya *EFD,* sasa unakuta saa nyingine nimeshatoa *invoice* ya *EFD,* naanza kudaiwa *VAT* au kodi nyingine pale, halafu unanilipa baada ya mwaka mmoja au miaka miwili. Nilikopa pesa benki, siku natakiwa nilipwe na benki hela yote wanaenda wanaichukua kupitia maelekezo waliyowapa Maafisa Masuuli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, lazima ajue wakandarasi wengi wanafanya kazi hizi kupitia mikopo. Sasa inapotokea mimi naidai Serikali, wamechelewesha malipo yangu kwa zaidi ya mwaka mmoja. Siku ananilipa tena anamwelekeza Afisa Masuuli anikate mimi pesa ambayo

imekuwepo kule, ananidai kodi, wakati mimi sijamdai *interest* wala sijadai chochote kile na pesa inakatwa juu kwa juu, kiasi kwamba mtu hawezi kulipa benki tena kwa sababu hata ile pesa Waziri ameshaichukua.

Mheshimiwa Spika, mtu yule anadaiwa mishahara na wafanyakazi wake, pesa Serikali imeizuilia kule imeichukua. Naomba hili jambo nililisema wakati nahutubia hapa kwa mara ya kwanza nikiwa nimeingia Bungeni mwaka 2021, wakati ule tunachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie, najua ni waraka na bahati nzuri juzi alisema kwamba, anatekeleza maelekezo ya Serikali. Kwa hiyo, kama kuna *any means* ya kuleta hizi sheria au nyaraka hizi ambazo zimekuwepo na taratibu hizi, azilete tuzibadilishe, zinawaumiza watu. Tunataka watu walipe kodi, lakini walipe kodi huku Serikali ikiwajibika.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama leo kuna mkandarasi na yeye akijua kwamba anadai Wizara fulani na yeye je, aende Mahakamani akaweke *Court injunction* Benki kwamba hela iliyoko benki naye aichukue. Ninachopenda watu walipe, lakini kwa kuelewana, kama unamdai mtu hela ya kodi uelewe deni lake, *invoice* alileta lini na bahati nzuri madai yanakwenda kwake, aangalie na watu wa Hazina, wajue huyu mtu alileta lini wampe *soft terms* za kuwalipa huku na yeye aki-*service* deni analodaiwa benki. Kwa hiyo, wakandarasi wengi wamefilisika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, aweze kutusaidia hilo.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji waliopita wameongelea habari ya dola. Hili ni Taifa ambalo bado linaendelea. Vitu vingi tuna-*import* kutoka nje ya nchi. Nimwambie Waziri ukweli kabisa usiofiochika, wafanyabiashara na Watanzania wengi wanao-*import* vitu kutoka nje wanaumia sana, maana *rate* ambazo unaziona leo kwenye mabenki ile 2,650 haiko mtaani na wala huwezi kuipata na benki hata kupata dola elfu tano kwa siku kwa mfanyabiashara ni *issue*.

Mheshimiwa Spika, leo ukienda benki watakwambia wanakupa dola mia, sasa mtu ana kazi ya dola laki mbili, dola laki

tatu, dola mia utaikusanya kwa miezi mingapi na faida yenyewe itatoka wapi. Kwa hiyo, tumwombe Waziri kama kuna *anything that he can do* kuliepusha hili Taifa na hizi zahama ambazo tunazipata kutoka kwenye dola, hebu basi aingie atusaidie kwa maana *custodian* wa hilo jambo ni yeye, hatuna pengine pa kukimbilia. Tunamwomba atusaidie, alione, najua ni tatizo la dunia lakini wenzetu Wakenya wamelipunguza kwa asilimia kubwa. Tuone hata Waziri *the way* ambavyo anaweza akafanya ili tatizo la dola lipungue.

Mheshimiwa Spika, *black market* leo inafanya biashara kubwa zaidi kuliko pesa ambayo iko kwenye mzunguko. Pesa ya dola hairudi benki kwa sababu mtu aliye na dola mtaani akirudisha benki ataenda kulipwa kwa hela ndogo. Kwa hiyo, dola zinauzwa mtaani zaidi kuliko huku. Sasa tunaenda kuangusha uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, tumwombe, najua Mheshimiwa Mwigulu amekuwa mzalendo, *he can do this in a better way* akawasaidia wafanyabiashara, akamsaidia Mheshimiwa Rais ili hatimaye uchumi huu ambao amewakabidhi waweze kuusimamia uweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la dola namwomba Waziri, naamini ataliweza. Tumwombe kupitia Bunge hili, kama Bunge tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone jinsi atakavyookoa uchumi wa nchi hii kupitia *scarcity* ya dola ambayo inaendelea mtaani. Haiwezekani wanasema benki dola inauzwa 2,650, mtaani sasa hivi dola inaenda 2,850, 2,900 na wengi ndio wanafuata hizo dola huko. Kwa hiyo, Waziri atusaidie ili aweze ku-*stabilize* uchumi wa nchi kuliko dola kubaki mtaani, watu wana-*trade* wakati hairudi benki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Mohamed Said Issa ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu. Naomba nizungumzie mambo matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, mara nyingi tunapozungumzia masuala ya kukusanya kodi baadhi ya watu wamekuwa wakisema wigo wa kodi wa nchi yetu ni mdogo sana na hauwezi kutusaidia kukusanya kiasi cha fedha cha kutosha kwa ajili ya kugharamia maendeleo ya nchi yetu. Mimi nina mawazo tofauti kidogo na jambo hilo. Kwangu mimi tatizo letu la msingi ni usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa kodi pamoja na udhibiti wa mapato ya Serikali na katika hilo, kuna kasoro tatu, nitazifafanua.

Mheshimiwa Spika, kasoro ya kwanza, tunatumia zaidi ya 70% ya fedha za Serikali kwa ajili ya manunuzi Serikalini. Mwaka mwaka jana tulifanya marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Manunuzi Serikalini na tulifikiri kwamba tutapata mwarobaini wa tatizo hilo la kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali, kwa bahati mbaya mamlaka hii inakabiliwa na matatizo mawili makubwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kwanza, kila ukitaka kufanya mawasiliano unaambiwa mtandao uko chini kwa zaidi ya siku tatu; lakini la pili taasisi nyingi za Serikali hazijajiunga na mfumo huu. Sasa najiuliza hili linatokea kwa kudra za Mwenyezi Mungu au kuna mkono wa binadamu. Mheshimiwa Waziri atakuwa analijua vizuri zaidi jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kasoro ya pili, ukizungumza na wafanyabiashara na wawekezaji wanasema mfumo wetu wa kodi Tanzania hauna tofauti na nchi nyingine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tatizo letu kubwa ni utitiri wa kodi. Mamlaka mbalimbali zinashindana kwa kutoza kodi na wakati mwingine mamlaka mbili zinatoza kodi ya aina moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, pale Bandarini *CAMARTEC* anaangalia ubora wa vifaa vya kilimo, *TBS* anaifanya kazi hiyo hiyo, matokeo yake gharama za uzalishaji, gharama za utoaji huduma Tanzania zinapanda sana. Nitatoa mfano katika Sekta ya Utalii, ambayo ni sekta moja inayoathiriwa na utitiri wa kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, Mwezi Machi tulifanya ziara Nchini Kenya, ziara ya kikazi. Tulikaa kwenye Hoteli moja ya Kitalii ya hadhi ya juu sana kwa usiku mmoja tulilipa dola 55, hoteli hiyo hiyo Tanzania unalipa zaidi ya dola 120.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ukizungumza na wataalam wa kodi ya mapato Tanzania wanasema sekta isiyo rasmi ina uwezo mkubwa sana wa kuchangia zaidi ya 30% ya mapato ya Serikali, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hatujailea na kuirasimisha sekta hiyo. Miaka mitano iliyopita Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilikuja na pendekezo zuri tu hapa, Serikali ilileta utaratibu wa kuwatoza wafanyabiashara wadogowadogo elfu ishirini kwa mwaka mzima. Jambo hili liliwapunguzia machinga tatizo kubwa la kulipa gharama mbalimbali, kwa bahati mbaya jambo hili sijui limemalizikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili, nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa sana la Dola ya Kimarekani kwa sasa, badala ya kutumia fedha za kigeni chache tulizonazo tunazitumia kwa ajili ya kuagiza sukari, kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula, kwa ajili ya kuagiza mbolea, kwa ajili ya kuagiza *furniture,* wakati nchi hii inaweza kutengeneza vitu hivi hapa hapa nchini, badala ya kutumia pesa kwa ajili ya kuagiza mitambo, vifaa vya tiba ambavyo hatuwezi kuvitengeneza hapa nchini tunatumia fedha hizo kwa mambo haya. Nafikiri jambo hili halikubaliki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu walio makini, Wamarekani, watu wa Ulaya, watu Wachina wanawalinda wafanyabiashara wao, wawekezaji wao, wakulima wao. Sisi badala ya kuwalinda wakulima wa Tanzania, badala ya kuwalinda wawekezaji, kweli

tunafanya utaratibu huu, tunaagiza kila kitu, tunafungua mlango kila kitu kiingie, wenzetu hawafanyi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya tatu, mwaka juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuja kwenye Bunge lako Tukufu akasema, Serikali itafanya utafiti na uchambuzi wa kina kushughulikia gharama ya matumizi ya magari na mafuta Serikalini. Sisi Wajumbe wa Bunge lako Tukufu tulilifurahia sana jambo hilo, lakini mpaka sasa Waziri amekaa kimya hajasema jambo lolote kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili, Waziri alituahidi hapa kwamba Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba shughuli zote za Serikali zitafanywa kwa mtandao. Jambo hilo Waziri baada ya hapo, haelezi lolote. Sasa tumewasikia hapa Waheshimiwa Wajumbe wanasema mifumo ya kukusanya mapato Serikalini haizungumzi. Sasa nadhani, Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mtandao Serikalini ina kazi ya kufanya katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha na taasisi zake. Halikadhalika nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri, kwa uwasilishaji mzuri, halikadhalika maoni ya Kamati na mimi kule ni mjumbe iwapo yatafanyiwa kazi yatakwenda kuwa nyenzo muhimu sana kwenye Wizara hii ya Fedha na taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani maendeleo tunayaona kule Ludewa maana yake fedha zinapatikana kwa wingi. Kila kata wananchi wanapata miradi mikubwa, wanaiona

kwa macho. Kwa hiyo, tuendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na tumhakikishie kwamba wananchi wa Ludewa wako tayari kuendelea kumuunga mkono na kuiunga mkono Serikali kwa sababu hata bajeti ya mwaka jana tulipata fedha kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na uchangiaji wangu. Nitaanza na eneo ambalo Kamati yetu imelisemea, eneo la mafao ya wastaafu. Wastaafu wamelitumikia Taifa hili kwa muda mrefu na wengi ambao sasa wako kwenye Mawizara au huko kwenye Mifuko ya Hifadhi nao wakumbuke kwamba ni wastaafu watarajiwa. Kwa hiyo, unachomtendea mwingine leo aliyestaafu kabla yako ukumbuke na wewe utakuja kustaafu, utamtafuta Mbunge wako aje akusemee hapa Bungeni. Kwa hiyo, naomba wazingatie sana eneo hili la mafao ya wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuwe na mfumo mzuri wa kutunza kumbukumbu za wastaafu kwa kutumia mifumo na hata inapotokea uhitaji wa kuwahakiki hao wastaafu ni vema Serikali ikawafuata kwenye wilaya zao. Tusiwaite kwenye maeneo ya mbali kama mikoani, unakuta mstaafu mwingine kama Mwalimu wangu Laurent Mkinga amenifundisha shule ya msingi, amestaafu muda mrefu sana, umri umekwenda au wastaafu wengine. Unavyomwita Mkoani kwanza unamuongezea gharama, nauli kutoka pale na wengine unakuta mpaka wasindikizwe na wasindikizaji wawili, watatu, hatari za kugongwa na pikipiki au magari. Kwa hiyo, ni muhimu kuwaepushia hizi gharama za nauli, malazi na chakula Serikali iwafuate maeneo ya jirani. Hili naomba sana lizingatiwe. Hata vile viwango vyao ambavyo wanalipwa, nimeona hata baadhi ya Wabunge wamesema viangaliwe upya kwa sababu gharama za maisha zimepanda sana ili nao waweze kujikimu kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya mishahara, Kamati yetu imesemea jambo hili na mimi siyo vibaya nikasisitiza kidogo. Serikali iendelee kufanya utafiti wa ongezeko la gharama za maisha, gharama za maisha zimeongezeka sana. Kwa hiyo,

iangalie uwezekano pia wa kuongeza fedha, bajeti na mishahara ili iweze kuwapunguzia watumishi maumivu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unakuta kundi la watumishi ndio watu ambao wanaishi kwenye nyumba za kupanga kwa muda mwingi na wanashindwa kujenga za kwao kwa sababu ya majukumu. Kwa hiyo, tukiangalia eneo hili tutaongeza ya watumishi kuweza kufanya kazi na tutaongeza tija katika Taifa letu. Kwa kuwa Kamati yetu imeeleza kwa kina naomba niseme kwa ufupi kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo la madeni ya wakandarasi. Nilikuwa nimepata takwimu chache, kuna Mfuko wa Taifa wa Maji karibia shilingi bilioni 471.5 zinadaiwa; Mfuko wa Barabara shilingi bilioni 571.8; na Mfuko wa Nishati vijijini shilingi bilioni 128.7. Fedha hizi kwa jinsi ninavyomjua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na msaidizi wake fedha hizi siyo nyingi na wanaweza wakakutana na hawa wafanyabiashara. Pia, nimemsikia Mheshimiwa Engineer Ezra amesema na ametoa takwimu jinsi *TRA* wanavyowadai bila kujali wamelipwa au bado, wanavyofilisiwa kwa ajili mikopo ameeleza kwa kina sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba sana Wizara hii iangalie sana haya madeni hata kama siyo yote ila ukikaa nao hawa wakandarasi mnaweza mkatengeneza namna nzuri ya kuweza kuwalipa ili na wao waweze ku-*service* vizuri mikopo yao benki.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa mkandarasi mmoja alipewa Mradi wa Maji pale Ludewa Mawengi. Sasa huyu tukampigania akasaidiwa akalipwa *advance payments* lakini sasa madeni ya maeneo mengine, ni madeni ya muda. Sasa hii hela anayopewa ndiyo inabidi a-*service* mikopo, apunguze mishahara kwa watumishi wake na vitu vingine. Kwa hiyo, naomba eneo hili Serikali ilichukulie kwa uzito wa pekee na kuweza kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine la Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani. Ofisi hii iweze kufanyiwa maboresho makubwa ili

kuweze kuwa na watumishi wa kutosha, vitendea kazi, wajengewe uwezo na mafunzo ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi mkubwa zaidi. Pia, uhuru katika utendaji wao wa majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, ninatoa mfano mmoja, *CAG* alifanya ukaguzi wa muda halisi (*realtime audit)* katika Mradi wa *SGR* na Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (uzalishaji wa umeme). Yako mambo mengi ambayo waliweza kuyaona mapema na kwa wakati na wakashauri ambayo yakaiepushia Serikali hasara. Kuliko yale ya kusubiri mpaka Mradi utekelezwe ndiyo *CAG* anakuja baadaye, tayari hasara inakuwa imeshatokea. Hata hivyo, tukiboresha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa kuwapa fedha za kutosha, vitendea kazi na kuwajengea uwezo watasaidia sana kupunguza hizi hoja za *CAG* kwa sababu watakuwa wanakwenda kwa wakati katika miradi yote yenye fedha nyingi. Watakuwa wanakwenda mara kwa mara kufanya ukaguzi na kuwashauri maafisa masuuli. Kwa hiyo, tutalinda sana na kuokoa fedha nyingi ambazo ni kodi za Watanzania kwa kuboresha tu Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niipongeze tu Ofisi ya *CAG* kwa kazi nzuri hiyo niliyoitolea mfano, ukaguzi huo wa muda halisi wa *SGR* na Bwawa la Mwalimu Nyerere waliweza kuokoa fedha nyingi sana. Hii waendelee kufanya kwenye miradi mingine mikubwa ili kuokoa kodi za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni la muhimu sana kwa sababu matumizi ya Serikali ni 70% ya fedha zote za Serikali. kwa hiyo, ile miradi yote tungeweka mwongozo au sheria kwamba mradi wowote unaovuka kiasi fulani cha fedha ambazo ni fedha nyingi ni lazima ufanyiwe ukaguzi wa mara kwa mara kabla haujaisha ili tuweze kuepusha hasara kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika niweze kupongeza watu wa *TRA* wanafanya kazi nzuri sana ya kukusanya kodi. Nimeona kwenye taarifa yako ukurasa wa 52 umeainisha changamoto ambazo zinaathiri utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali.

kuna eneo umetaja changamoto ya zile mashine za *EFD* na kwamba Serikali inatafuta njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Wizara kwa maamuzi haya na ninajua kuna vijana wengi wa *IT* ambao wanaweza wakatengeneza mifumo ambayo ikaunganishwa hata na simu za mkononi na zikatoa risiti kwa njia ya meseji, siyo lazima risiti ya karatasi kwanza ni gharama. Wizara imeanza jitihada ya kuifanya mifumo yetu iweze kusomana, hata risiti ya meseji nayo ni risiti halali. Vilevile, waangalie lile eneo la wafanyabiashara, mfanyabiashara anavyokwenda halmashauri kuchukua leseni ya biashara, wanamwambia nenda *TRA*. Kijana anayetaka kufanza biashara akifika *TRA* wanampigia mahesabu ya kodi wakati bado hajaanza kufanya biashara. Hili nalo liangaliwe ili waweze kupewa *grace period. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona muda umekwisha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imekwishagonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng’anzi Ulenge, ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kuweza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu ili kuweza kutoa mawazo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu leo utajikita kwenye mambo yanayohusu Zanzibar, lakini pia yanayohusu Tanzania nzima. Kwa hiyo, wale wachambuzi wakichambua wajue kwamba mchango huu ulielekea wapi, wasi *-collect* tu

wakasema haya yote ni ya kwetu, mengine siyo ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la *TRA* namna wanavyokusanya kodi. *TRA* ni chombo chetu kinachokusanya kodi lakini kuna maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais alitoa kwao kwamba, *TRA* wawe rafiki kwa wafanyabiashara. Jambo hili Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo mazuri sana na Watanzania walilifurahia sana. Sasa kuna mambo ambayo mpaka leo bado *TRA* wamejifanya kwamba wao ni polisi wa kuwakwida hawa wafanyabiashara. Sasa kuna jambo moja ambalo mimi bado ninaliona kwamba siyo jambo zuri kwa sababu wafanyabiashara hawa hivi karibuni zilitoka takwimu huko kwenye mitandao kwamba, Watanzania wengi fedha zao hazipitii benki. Hazipitii benki kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wengi wanahofu kwamba, unapoweka fedha benki *TRA* kwao inakuwa ni *tax base* yao. Sasa tujiulize, wakati mwingine umefungua akaunti, ndugu zako wameuza nyumba na hawana pakuziweka hizo fedha, siyo wafanyabiashara wanaamua kwamba tuwekee fedha zetu. Pia, kuna mwingine yuko mbali hana akaunti anaomba kwamba naomba akaunti yako niingize fedha zangu ili nikija huko nizichukue. Sasa, kwa nini *TRA* wanafanya *account* mpaka leo? Hili jambo wafanyabiashara wengi hawalipendi na wanashindwa kuweka fedha benki kwa ajili ya kuona kwamba akaunti za benki ni *tax based*. Mheshimiwa Waziri, mimi napenda sana utakapokuja ku-*wind up* utuelekeze namna ya kuondoa jambo hili. Mtafute mbinu mbadala ambazo ni rafiki kwa wafanyabiashara na hazitakuwa kikwazo. Huo ni mchango wangu wa kwanza *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nigusie kidogo hii sehemu ya dola. Bunge lililopita nilichangia hapa nikakuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, je tunataka kufahamu ni nani dalali kati ya *BOT* na Benki? Kwa sababu mnasema ninyi mnatoa fedha lakini benki hakuna na biashara zinafanyika, kontena zinaingia kila uchao, kwa nini sasa hatujui wapi zinapitia? Tunaona kwamba, wale wajanja ndiyo wanaweza kufanya hili jambo, wengine ndiyo

kama alivyosema Mheshimiwa Mhandisi Ezra kwamba huko mtaani inafikia 2,800 mpaka 2,900.

Mheshimiwa Spika, sasa hatujui tatizo ni nini au mtuambie kwamba, sisi *BOT* hatutoi hizo zinapitia katika sehemu nyingine. Ukija ku-*windup* hapa utueleze nini kinatokea? Nini kinafanyika? Biashara inafanyika dola hazionekani. Utupatie njia mbadala ambayo wengine wataifahamu ili Watanzania watumie njia hiyo kufanya biashara na biashara iwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, lingin linahusu Zanzibar. *TRA* ni moja katika nchi yetu na ni Taasisi ya Muungano, lakini inapofanya kazi yake inafanya kazi *generally* lakini kule Zanzibar uchumi wake ni tofauti na huku Tanzania Bara. Kwa kuangalia suala hilo, pale Zanzibar ukienda kuhesabu viwanda ambavyo viko rasmi haviwezi kufika hata vitano. Pengine ni viwanda vile vya cherehani, sijui vya nini, ni viwanda vidogovidogo. Sasa inapokuja kwenye suala la kulinda viwanda, Tanzania nzima inaingia kwenye mkondo huo wakati Zanzibar tunategemea zaidi *importation*. Pia maisha ya Wazanzibari kama hakuna viwanda maana yake hakuna ajira.

Mheshimiwa Spika, alitokea mtafiti mmoja hapa akasema Wazanzibari 33% wanategemea fedha za kugaiwa, 21% fedha wanazozipata hazitoshelezi mahitaji yao. Maana yake 54% hao wote ni tegemezi. Sasa hii maana yake ujue kwamba uchumi wa Zanzibar uko chini sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoleta kodi ambazo tunakinga viwanda vyetu halafu na kule Zanzibar kunaathirika, hii ni kuwaua Wazanzibari. Hili ni jambo ambalo Wazanzibari kwa kweli hawalipendi na tungetamani ulitafakari. Kwa mfano Zanzibar hatuna kiwanda cha biskuti, lakini nafikiri mwaka jana au juzi ulileta kodi ya *35 percent import duty* kwa ajili ya kulinda viwanda vya biskuti, sasa Zanzibar hatuna. Maana yake nini? Sisi sasa tuje tuchukue huku na zile *logistic* za kusafirisha mpaka ukafika kule ni sawa unge-*import* au ingekuwa zaidi. Kwa hiyo, tunaomba zile kodi ambazo mnaziingiza kwa ajili ya kulinda viwanda, kwa vile Zanzibar hakuna, basi kule Zanzibar zisifanye kazi. Tuendelee na kodi zetu zile zile za 25% *import duty* na *VAT* kule ni *15 percent*

twende kazini. Kwa sababu sisi hatuna na tunategemea kuomba, maisha yetu ni magumu, kwa nini sasa mnatuingizia namna ya kulinda viwanda?

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la viwanda vya Zanzibar vinavyoanzishwa, kwa kweli vinakutana na kadhia kubwa sana. Kadhia hizi tunaanzisha viwanda, siyo kwamba hawa watu hawaanzishi, tunaanzisha kule viwanda lakini tatizo ni mfumo wa kodi unakuja kusababisha viwanda vinakufa. Sasa Zanzibar tunaendelea kuwa ombaomba kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili kwa kweli Wazanzibari wanachukia na wanaona kwamba hili suala la kodi bado haliwatendei haki. Mfano mzuri, pale tulikuwa na Kiwanda cha *Aluminum* kimekufa, sasa hivi tunacho Kiwanda cha Nguo cha Basra kinaelekea kufa, tunacho kiwanda cha sukari, sasa hivi sukari yake hainunuliki tena. Kinachotokea sasa ni wafanyabiashara wenye uwezo wanaambiwa nunua tani 5,000 huku tutakupa kibali cha 100,000 huku. Kwa maana hiyo, wafanyabiashara wa kati wanakosa fursa. Sasa hili jambo siyo sahihi, kwa nini iwe hivyo? Tunapokwenda kwenye kuvilinda viwanda, vilindwe katika mfumo ambao wananchi hawatoathirika. Sasa jambo kama hili siyo zuri.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mmoja, tulikuwa na Kiwanda muhimu sana kikubwa mno cha maziwa cha *Azam UHT*. Hiki kiwanda sasa hivi kimefungwa. Kilikuwa kinaajiri wafanyakazi wa kudumu 240, lakini kimefungwa. Pia, maziwa hayo yalikuwa yananywewa Tanzania nzima lakini kimefungwa saizi na kimekufa kwa sababu ya ku-*charge*-iwa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda kinachofanya kazi Iringa, kinachofanya kazi Dodoma kina *charge*-iwa kodi za *supply* lakini siyo kodi za *production*. Sasa ile Azam ikileta pale maziwa yale ambayo watachanganya na *ingredients* nyingine zinakuwa zina *charge*-iwa kodi ambayo huku tukiangalia kwa mfano uzalishaji wa viwanda vingine vinapata *exemption*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tunapoleta malighafi za *crude oil* zinakuwa *exempted* na ata *charge*-iwa kodi wakati anauza. Sasa, kwa nini sasa kiwanda kinaajiri watu 240 na wengine *indirect* ni zaidi ya watu 500. Maana yake unaweza ukachukua zaidi ya watu 800 wanapata faida ya ajira ya kiwanda hiki, kiwanda kimefungwa. Kwa hiyo, jambo hili Waziri wa Fedha aje atuambie kwanza kwa nini kile kiwanda kimefungwa? Alieleze Bunge hapa kwamba wale wamekosa mtaji au ni hili ninalolisema? Kama ni hili ninalolisema wakakae na mwekezaji waangalie njia sahihi ya kukirudisha kiwanda kile ili Wazanzibari wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Vilevile, yeye pamoja na wasaidizi wake wote. Pia, tuwapongeze kwa sababu ya kuratibu uandaaji wa Sheria mpya ya Manunuzi ambayo tunasubiri sana utekelezaji wake japo bado hatujaziona kanuni ili Sheria hii sasa ianze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo langu la kwanza katika kuchangia ni Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi *(FIU)*. Nilisimama hapa mwaka 2023 kuzungumza na kulikuwa na miamala shuku ya shilingi trilioni 280. Jambo hili lilipingwa na Mawaziri, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu; Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe na Waziri wa Mipango Mheshimiwa Profesa Mkumbo, wakasema ni takwimu za kupika kwa ajili ya kuichafua Serikali.

Mheshimiwa Spika, walisema maneno mengi juu ya hilo lakini ninachotaka tu kusema leo ni kwamba, Taarifa ya Kamati inasema; "Tanzania ilitakiwa kuwekwa chini ya uangalizi wa kikosi kazi cha kusimamia mwenendo wa udhibiti wa utakatishaji wa

fedha haramu *(Financial Action Task Force – FATF)*. Jambo hili lingekuwa na madhara hasi kwa Taifa, hatua hii inatokana na kasoro zilizobainishwa na kikosi kazi hicho kwamba Tanzania ni eneo oevu la kutakatisha fedha.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, sasa leo Waziri wa Fedha aniambie kilichoifikisha nchi yetu. Nchi yetu ilikuwa inapigiwa mfano *katika Financial Action Task Force* kwa kufanya vizuri sana katika kukinga haya mambo. Leo tumefikaje mpaka nchi yetu imekuwa eneo oevu la utakatishaji wa fedha haramu? Ametufikishaje hapo? Baada ya nchi yetu kutangazwa kuwa kwenye hatihati ya kuwa chini ya uangalizi wa *FATF* yeye kama Waziri amechukua hatua gani kwa ajili ya kuhakikisha nchi yetu isiingie huko?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nchi yetu ikiingia huko tutakuwa hatuaminiki tena na Tanzania itakuwa ni eneo shuku la ufadhili wa silaha za maangamizi, Tanzania itakuwa ni eneo linalodhaniwa kwamba lina ugaidi unaotamalaki. Sasa leo Waziri atuambie ametufikishaje hapo? Kwa sababu tahadhari tulizozitoa pale mwanzo kwamba hii ilikuwa inatokana na usimamizi dhaifu, tuliona mapema kwamba hii inatokana na usimamizi dhaifu wa usimamizi wa Sera za Fedha. Ukiwa na usimamizi dhaifu wa Sera za Fedha utafikisha tu pale. sasa kama Waziri wa Fedha ametufikisha hapo, leo anasema nini juu ya hili jambo?

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato. Wenzangu hapa wamezungumzia…

**SPIKA:** Mheshimiwa subiri kidogo. Hebu msaidizi chukua hiyo *IPAD*. Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nadhani umekumbuka kunilindia muda wangu.

Jambo la pili, kuhusu uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya CAG. Taarifa ya TAKUKURU inasema kuwa katika mwaka wa 2021/2022 TAKUKURU ilifungua majalada 375 kati yake 156 yalikosa ushahidi wa kufikishwa Mahakamani, 73 yalichukuliwa hatua, 28 yako kwenye hatua ya Mkurugenzi wa

Mashtaka na 41 yalitolewa hukumu na Mahakama, TAKUKURU ikashinda mashtaka 40 na kushindwa shitaka moja.

Mheshimiwa Spika, hapa tunataka tuelezwe vizuri kwa sababu Waziri wa Fedha ndiyo mratibu mkuu wa utekelezaji wa mapendekezo ya *CAG*. Hoja za *CAG* zinakuwa zimepitia nyaraka nyingi sana na ushahidi mwingi sana, inawezekanaje tufike Mahakamani tushindwe kwa majalada 156 ambayo sawa na 42% yakose ushahidi? Mimi ninaamini yawezekana hapa katikati kuna hujuma zinazofanyika za kupoteza ushahidi kwa maksudi na kutaka kuona kwamba taarifa ya *CAG* haina uhalisia inapokuwa inatolewa, sasa ni lazima hapa tuelezwe kwa sababu tunajua.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwa niin hadi leo hao watuhumiwa wa mashauri hayo 28 ambayo yako kwa Mkurugenzi wa Mashtaka anakaa nayo kufanya nini? *CAG* alishasema ni ufisadi, ni rushwa, TAKUKURU imesema ni ufisadi na rushwa, yeye Mkurugenzi wa Mashtaka mpaka leo hii anashikilia mashauri 28 kwa ajili ya kazi gani? Pia tuambiwe hayo mashauri 28 ni ya akina nani, kwa sababu vinginevyo tutakuwa tunakaa hapa tunazungumza mafisadi, tunazungumza wezi, tunazungumza wala rushwa halafu mwisho wa siku wanaenda kubebwa kwa mbereko ya *DPP* wasipelekwe mahakamani, tunataka hiyo ripoti ya mashauri 28 yawekwe kwenye Bunge lako hapa Tukufu watu wasitafute kivuli cha kwenda kujificha kwa *DPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni hili suala la malimbikizo ya kodi ambalo nataka niseme tu kwa kifupi kwa sababu changamoto ya muda, Waziri tulimshauri muda mrefu malimbikizo haya ya kodi kwa ajili ya *TRAB* na *TRAT* na hadi sasa yamefikia trilioni 10.48.

Mheshimiwa Spika, huwezi kukusanya kodi katika mazingira ya namna hiyo, kama unakusanya trilioni 26 kwa mwaka, halafu una malimbikizo ya kodi yaliyoshikiliwa kwenye mamlaka za rufani za kodi trilioni 10.8 hakuna kodi itakusanywa kwenye nchi hiyo! Hapo moja kwa moja kuna njama zinazosukwa tu za kuiba mapato ya Serikali, watu wanakula njama, kuweka kesi mahakamani halafu mimi nipate likizo ya kulipa kodi. Sasa Waziri

haya tulishamshauri muda mrefu, sababu za kuchelewa mashauri haya ni zilezile hazifanyiwi kazi sasa tufanye nini na Waziri wa Fedha? Tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya changamoto ya muda nizungumzie hili suala la wenzangu ambalo wamezungumza la vyanzo vya mapato ya kodi, kwamba tusipolinda viwanda vyetu vya ndani hatuwezi kukusanya kodi. Kama hatuwezi kukusanya kodi, Serikali imeamua kuagiza tani 410 za sukari kutoka nje, wakati katika mwaka wa fedha tulionao wa 2024/2025 tunahitaji *gap sugar* ni tani 120,000 tu, sasa unaagiza tani 410,000 kwa ajili ya kuzipeleka wapi? Tani 410 Serikali inaagiza kutoka nje kwa ajili ya kuzipeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria yetu inasema tunaagiza sukari kutoka nje ni ile *gap sugar* tu, ukiagiza zaidi ya hapo maana yake umeamua uue viwanda vyote hapa nchini, maana yake umeamua wakulima wote wa miwa nchi hii wakose soko, maana yake umeamua kwamba hawa wafanyabiashara ambao tumewapa dhamana ya kuweka viwanda vya sukari hapa nchini wafunge viwanda vyote saba, lakini bado wadaiwe madeni makubwa ya mikopo waliyoichukua kwa sababu hawawezi ku-*survive* tena katika ushindani wa namna hiyo! Tuna taarifa kwamba hata *VAT* wameondolewa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wa viwanda vya ndani sukari wanauza na *VAT,* wale wanaoagiza kwa taarifa zilizopo ni kwamba wameondolewa *VAT,* lakini mbaya zaidi, hapa tulishaamua kwa Marekebisho ya Sheria ya Sukari ya mwaka 2020 waagizaji wa sukari wawe wenye viwanda tu, lakini mpaka sasa hivi Serikali imetoa kibali cha kuruhusu watu wafanyabiashara binafsi kuagiza sukari kutoka nje *contrary* na sheria zetu, haya yameruhusiwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni mifumo ya *TEHAMA*. Kama ni maziko ya nchi yetu kuingia kwenye mgogoro mkubwa mifumo ya *TEHAMA* isiposimamiwa vizuri tunaingia kwenye matatizo makubwa. Sasa hivi *CAG* kama walivyosema Kamati ya Bajeti kwamba amekagua asilimia 11 tu, na mimi nataka

nizungumzie tu jambo moja la ukaguzi wa mbolea ya ruzuku ambayo ni mfumo wa *TFRA*, mfumo wa mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi katika mfumo wa *Subsidy Management System* unaotumia *TRFA* yaani mfumo wa mbolea ya ruzuku, ulibaini kuwa mtoa huduma wa *TEHAMA* wa nje amepewa haki ya kuendelea kuingia kwenye *server* na hifadhi *data* za taasisi kinyume na matakwa. Hii inaashiria hatari ya usalama wa *data,* aidha Maafisa wa TEHAMA wa *TFRA* hawana uwezo wa kupakua *data* kutokana na vikwazo vilivyopo, uingiaji huu wa mtoa huduma wa TEHAMA *(vender)* unaleta hatari kubwa ya usalama wa Taifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nusu dakika tu nihitimishe.

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nusu dakika nihitimishe tu kwa kusema kwamba *vender* huyu ambaye ni mtu binafsi ametujengea mfumo wa TEHAMA bado *server* anayo yeye, bado kanzi *data* anaimiliki yeye, halafu Serikali inaruhusu zaidi ya shilingi bilioni 150 kwenda kwenye mfumo unaotumiwa na mtu binafsi, hizo ni hujuma katika Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mheshimiwa Juma Hamad Omar, ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia, awali ya yote niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya ya kukuza uchumi wa Taifa letu. Kipekee kabisa niwapongeze

waliopewa dhamana katika Wizara hii ya fedha kwa namna ambayo wanatekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kipengele cha 3.6 amezungumzia changamoto za utekelezaji wa mpango na bajeti na mikakati ya kukabiliana nazo, miongoni mwa changamoto alizozitaja alizungumzia mwamko mdogo wa wananchi kudai na kutoa risiti za kielektroniki za *EFD*. Vilevile amezungumzia baadhi ya walipakodi kuficha taarifa za miamala ya biashara na kuendelea kuwepo kwa biashara za magendo hususani mpakani mwa mwambao wa bahari.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu hapa leo muda huu kuna kipengele katika *Quran* kinasema hivi; *"Balil insaanu alaanafsihi baswira, walau alqama adhira"*. Kwamba kila mtu katika nafsi yake ni mwenye kushuhudia, walau kama atakiri vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Waziri unaweza ukawa unajua ni kwa nini wananchi wana mwamko mdogo wa kodi, lakini ninahakika unaweza ukajua ni kwa nini miamala inafichwa na taarifa za wafanyabiashara. Nina hakika Serikali inajua kukosekana kwa *stock* sahihi ya mizigo inayoingizwa kwenye mifumo ya *TRA* ni moja kwa moja itampelekea mfanyabiashara asikubali kuuza mauzo yake kwa kutumia risiti kwa sababu nilichoki-*declare* wakati naingiza mzigo nitakisemaje wakati sija-*declare* mizigo sahihi? Tamko nililolitoa wakati naingiza mizigo lilikuwa ni *false declaration,* ilikuwa *under invoice declaration,* ulikuwa hukutoa tamko sahihi leo unakuja kuniambia nitumie *EFD* kwa sababu kumbukumbu zangu zitatunzwa, zinanisaidia nini kutunzwa *EFD* wakati huku ni kutoa tamko sahihi?

Mheshimiwa Spika, sasa siamini kwamba hawajui *TRA* kwamba kuna *under invoice,* kwamba kuna *false declaration,* kwamba kuna *under declaration* wanajua. Mtu anaingiza *tonner* anasema nimeingiza wino mwingineo, mtu anaingiza *carton* 10,000 huku anasema nimeingiza *carton* 1,000. Haya mnayajua mbona hayajasemwa hapa? Ni akina nani wanafanya *under invoice* hamuwajui? Ni akina nani wanafanya *under declaration*

hamuwajui? Ni akina nani wanafanya *false declaration,* hamuwajui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *black market* haiwezi kuisha Tanzania. *Black market* haiwezi kuisha Kariakoo ni lazima tuwe wakweli wa nafsi zetu, tunaliua Taifa hili, tunaliua Taifa hili kwa kuendekeza undugu, kwa kuendekeza urafiki, kwa kuendekeza watu wanaoumiza Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Tax base* haiwezi ku-*grow* katika Taifa hili haiwezi ku-*grow* iwapo tunawajua, tunawajua watu wanaofanya *consolidation* katika Taifa hili, namna gani ambavyo wanawaumiza wafanyabiashara wa Kariakoo, mnajua. Ninaipongeza Serikali kwa kujaribu kutaka kuitatua changamoto ile ya Kariakoo lakini nyuma yake wako akina nani mnajua! akina nani waligomea mgomo ule, mnajua! Kwa hiyo, inafika wakati najiuliza kama Taifa uwongo huu ni kwa maslahi ya nani? Kudanganyana huku ni kwa maslahi ya nani? Nani aendelee kuumia na nani aendelee kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku Tanzania ni ya kwetu wote, Tanzania ni ya kwetu wote, leo nina muweka mtu *under the bracket*, lakini *next time* nitakuja kumtamka hapa ambaye anafanya *consolidation* katika Taifa hili na anawaumiza Watanzania wengi wakati yeye akijiongezea faida isiyojulikana, na nina uhakika *TRA* mnamjua, na nina uhakika *TRA* mnashirikiana naye mnajua. Yeye anafanya *consolidation,* analipa kwa *control number* ya kwake mwenyewe, kama yeye anafanya *clearing and forwarding* kwa nini asitoe *control number,* yule anayefanya *clearance* ya mizigo yake alipe mwenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika *black market* haiwezi kuendelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ulenge kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kumpa taarifa *Engineer* kwamba yeye amtaje mimi nitamlinda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge kuna taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa taarifa hiyo, lakini nimeshaweka *line of demarcation* kwamba sitamtaja leo lakini *next time* nitamtaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini ninachotaka kusema, ni kwamba ukusanyaji wa kodi kwa kutumia *EFD* hauwezi kufanikiwa kamwe katika Taifa hili, kamwe hauwezi kufanikiwa! Tuje na njia mbadala za kuzuia *false declaration,* njia za kuzuia *under invoice,* njia za kuzuia yote ambayo *TRA* mnashirikiana na watu wengine kwa manufaa ya matumbo yenu na siyo kwa manufaa ya Mama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niiache hiyo *topic* naomba tuende kwenye suala zima la Ofisi ya *TOST*. Sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Usuluhishi na Malalamiko ya Taarifa za Kodi *(TOST)*.

Mheshimiwa Spika, hii ni taasisi ya umma na utendaji wake wa kushughulikia malalamiko ya kodi katika Taifa hili mimi nailinganisha sawa na TAKUKURU na taasisi nyingine ambazo lengo lake ni kumsaidia mwananchi wa kawaida aweze kufanya mambo yake na huduma mbalimbali kwa ufanisi, sheria hii haitoi mamlaka kamili ya kuifanya *TOST* iweze kufanya majukumu yake kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kipengele cha 28(d) cha *Tax Administration Act* kinasema kuwa: "*tax ombudsman shall not review tax decision or objection decision*". Sasa ukiangalia maana halisi ya ofisi hii ni kulalamikia malalamiko ya kodi. Kama *TOST* haiwezi ku-*review decision or* ku-*object decision* iko hapa kwa ajili ya nini? Inaonekana tunafanyiana kizungumkuti tu, sheria hii au

taasisi hii ilianzishwa tangu mwaka 2019 kama sikosei lakini mpaka kuja kufanyakazi kwake imekuja kufanya kazi kuanzia mwaka 2023 *if I am not mistaken*. Kwa maana hiyo, naiona Serikali kama inataka kudanganya toto, isimame kwenye uhalisia, kweli tukusanye mapato na kila mtu alipe kile ambacho kinamstahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda kupitia sheria zetu za kodi hii ni miongoni mwa sheria ambayo mimi naona inapaswa kurekebishwa ili ofisi hii ya *TOST* iwe na mamlaka kamili. Iwe na mamlaka kamili kama ilivyo TAKUKURU ili iweze kujisimamia na kufanya mambo yake kwa usahihi na kwa maslahi mapana ya Watanzania wote, lakini huku unampa mamlaka huku umemfunga kwa mujibu wa Kifungu cha 28(d) haionyeshi dhamira ya kweli ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ninaloomba kuishauri Wizara hii ni wakae pamoja na *TASAC*. *TASAC* iko kwenye Kamati yangu na hili nitakwenda nalo kuhakikisha kwamba hawa *consolidators* wanafanyiwa tathmini, wanafanyiwa *review* na iweze kuwapunguza ambao hawafanyi kazi kwa mujibu wa sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia, natambua juhudi ya Serikali na sekta binafsi katika kupambania na kuwasaidia wajasiriamali wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaongelee wanawake wajasiliamali wa Mkoa wa Dar es Salaam. Wanawake wa Dar es Salaam hawahitaji matrekta, hawahitaji pembejeo, hawahitaji

mbegu, wanahitaji pesa. Dar es Salaam ndiyo Mkoa ambao umebeba sura ya nchi ya Tanzania na Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo lango la biashara. Asilimia 80 ya Wanawake wa Dar es Salaam ni wajasiliamali wadogo, wakubwa na wa kati, 20% tu ndiyo wanawake ambao wameajiriwa. Katika hii 80%, 15% ni wanawake ambao wanajiweza kwenye biashara zao kiasi kwamba wana-*muscles* za kuweza kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha, hawa 65% ni wajasiliamali wadogo ambao wanategemea mitaji kutoka kwenye taasisi binafsi, kutoka kwenye mabenki yetu na kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri, nimefurahishwa sana na kuona kwamba ameunda timu ambayo imehusisha Wizara, TAMISEMI, Mamlaka ya Masoko, Baraza la Uwezeshaji Kiuchumi na Mamlaka ya Bima lakini timu hii imeweza kufanya mafunzo kwenye Mikoa michache sana. Nilikuwa naomba timu hii ingeweza kukaa na Halmashauri zetu wakaongeza nguvu ili Mikoa yote 26 ya Tanzania ikapata mafunzo haya kwa haraka, kwa sababu sina uhakika kama kweli itaweza kumaliza kwa muda mfupi sana wakati mikopo imeshaanza kutolewa, wanawake wanaendelea kupata mikopo na mafunzo hawajapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia wanawake wanaoathirika na mikopo ya kausha damu, Dar es Salaam ndio mkoa unaoongoza. Tanzania ina benki takribani 44 lakini katika benki hizi tumeona angalau benki sita ndio zimeweza kujipambanua kuwa na bidhaa nzuri kwa ajili ya kuwasaidia wanawake. Tumeona kuna benki ya *CRDB,* kuna *NMB,* kuna *NBC,* kuna *AZANIA,* kuna *EQUITY* na *EXIM*. Sasa tunaziomba na benki nyingine ziangalie namna ya kusaidia wanawake na vijana wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna vijana wengi sana hapa Tanzania wamemaliza vyuo na hawajapata ajira na tunaona kabisa ajira zikitangazwa uhitaji ni mkubwa kuliko nafasi zilizopo. Sasa tunaziomba benki zije na *product* ambazo zitasaidia vijana na wanawake lakini pia na benki hizi zimekuwa zikitoa mikopo

midogo midogo kwa wanawake wa chini kabisa ambao wanaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wanawake wako kwenye vikundi vya huduma ndogo za kifedha. Hawa wana mitaji yao ambayo inawasaidia wao kukopeshana wao kama wao; jambo ambalo ni zuri kwao maana linawaepusha na mikopo ya kausha damu lakini wanawake hawa tuwatoe sasa hapa kati nao wapande juu. Kwa nini sasa benki zisiangalie namna ya kuweza kuwasaidia hawa wanawake wa vikundi vya huduma ndogo za kifedha wakaweza kuanzisha kampuni? Kuwe na mikopo ya aina hiyo maana hawa ni wateja wao na wote hawa wanaweka fedha zao benki; *transaction* na ukubwa wao wanauona pale.

Mheshimiwa Spika, kuna vikundi ambavyo vina hela mpaka shilingi milioni 700 au 800 huko benki. Wanashindwaje kuwasaidia kuwakopesha wakafungua viwanda? Tuna wawekezaji wakubwa pale Dar es Salaam na tuna kampuni kubwa pale Dar es Salaam. Wakina mama wakifungua viwanda wanaweza ku-*supply material* mbalimbali na bidhaa lakini pia wakapewa *tender* za usafi kwenye kampuni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Benki ya *CRDB* ina *product* yake nzuri sana ya IMBEJU. Wakina mama kabla hawajapewa ile mikopo wanapewa kwanza elimu. Watakapojiridhisha kwamba wameshakuwa wako vizuri ndiyo wanawapa zile pesa. Kwa hiyo, tunaziomba na benki nyingine ziwasaidie hawa kina mama wasiangalie tu kutengeneza fedha. Wawape elimu kwanza wakishajiridhisha ndiyo wawape zile fedha; wanawaingiza kwenye matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta mtu anakopeshwa fedha hajapewa elimu, hana elimu ya fedha, hajui kutunza mtaji na mwingine anakopa hana hata elimu kwamba kwa nini anakopa. Kuna mtu anakopa kwa sababu ametamani tu kufanya biashara ambayo hata biashara yenyewe hajawahi kuifanya na haijui. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakuomba kupitia hii timu yako tuwasaidie kina mama hawa wa Tanzania. Pia, nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba mmetenga shilingi bilioni

48 kwa ajili ya mikopo kwa wajasiriamali lakini tunaomba fedha hizi utoaji wake uwe wa haki, wa uwazi na uguse makundi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafurahi kuona kwamba unawagusa sana wakina mama lakini tunaomba na vijana wetu. Maana wale watoto ndiyo watoto wetu. Wakina mama tunaumia tunapoona kijana amemaliza chuo upo nae tu nyumbani hana kitu cha kufanya. Tunaomba fedha hizi wakopeshwe wakina mama na vijana lakini wakina mama wakopeshwe wote wasiangaliwe tu hawa wadogo wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta fedha nyingi sana zinagawanywa kidogo kidogo kwenye vikundi kiasi kwamba hatuoni matokeo. Zikopeshwe kwenye vikundi vidogo vidogo lakini na wa kati ili wainuliwe waje kuwa juu na hata wa juu nao wakopeshwe ili wafungue kampuni na viwanda watengeneze ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali iangalie namna ya kuboresha riba kwenye benki zetu hususan kwenye hii mikopo inayowasaidia wajasiriamali. Kuna watu wanatamani kukopa lakini wanashindwa kwa ajili ya hizi riba. Vikundi vya kina mama vinatamani mikopo lakini vinashindwa kutokana na riba kubwa zinazokuwa *charged* na benki. Kwa hiyo, tunaziomba hizi benki ziangalie sana namna ya kuweza kuwawezesha wajasiriamali wa Taifa hili. Italeta maana sana kama Serikali itatengeneza walipakodi wapya kuliko walipakodi walewale kila siku na hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona hapa Mheshimiwa Waziri amesema kuna changamoto katika matumizi ya *EFD*. Mimi nilidhani kwamba changamoto kubwa ni wajasiriamali hawa wadogo watengewe maeneo mahususi ya kufanya biashara zao, wapewe mitaji na wasimamiwe. Hawa wakishakuwa na biashara zao zimesimama vizuri watatumia tu hizo mashinde za *EFD*. Watalipa kodi na tutaongeza ukubwa wa walipa kodi kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Hamad Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ajiandae.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Namshukuru kwa sababu kwa kweli mama anatupendelea. Maendeleo anayoyafanya nadhani ni ya kupigiwa mfano. Nasema hivyo kwa sababu hakuna Mbunge hata mmoja hapa ambaye hakuna alama ya mama yetu huko alikotoka kwa maana ya miradi ya maendeleo; nasema nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nataka nichukue nafasi hii nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Kuna Mheshimiwa mmoja alisema wanatosha mara mbili; mimi nasema wanatosha mpaka watakapokuwa wazee kabisa; nasema hivi kwa sababu ya *experience* ndogo tu. Mwenzenu nilipata bahati ya kuwa Naibu Waziri wa Fedha katika kipindi cha Hayati Rais wa Awamu ya Pili Mzee wetu *al marhum* Ali Hassan Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya kazi chini ya Waziri Msuya, Waziri Marehemu Stephen Kibona na baadaye marehemu Waziri Profesa Kighoma Malima. Nataka niwaambie, kama kuna watu *very conservative* katika dunia hii au katika Wizara, popote, iwe Tanzania au duniani kote na wafanya kazi wake, ni Waziri wa Fedha na Hazina; nasema hivi kwa nini? Kwa sababu huyu ndiye tuliyempa jukumu la kutunza kapu letu na hilo kapu lina mahitaji mengi hasa katika nchi masikini kama hizi. Kwa hiyo, utoaji wake inakuwa anaangalia mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishieni kwamba Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri wake wamekuwa *so accommodative*. Wale wajumbe wenzangu wa bajeti watanambia na hivi karibuni nitasema tunapokaribia

kumaliza. Nina hakika Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu atakuja na mapendekezo mazuri ya kodi ambayo yatawasaidia sana wapiga kura wetu na hiyo ndiyo desturi yake. Kwa hiyo, nasema nampongeza sana na *right from the beginning* nasema naiunga mkono hoja hii 100 kwa 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kidogo tu habari ya wastaafu na nazungumzia hili Fungu 22 ambalo linashughulika na malipo ya wastaafu na mambo mengine. Wastaafu hawa ambao wanalipwa na Hazina kupitia fungu hili kwa kweli ni lazima tuwaonee huruma. *Formula* inayotumika katika kulipa wastaafu ni kwamba mstaafu analipwa *on the basis* ya mshahara wake wa mwisho. Wale wafanyakazi waliofanya kazi katika kipindi cha Mzee Mwinyi au kabla, mishahara yao ilikuwa midogo sana kinyume na sasa. Mimi nakumbuka ni mmoja kati yao, siyo vizuri kujitolea mfano mwenyewe lakini *monthly pension* mwanzo nilipata shilingi 13,400; nakumbuka mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilistaafu mwaka 1995 nikawa napata *monthly pension* 13,400. Mpaka leo hii pamoja na kwamba Idara ya *Pension* inaiongeza hii lakini mpaka leo hii kila mwezi nachukua shilingi 140,000 hicho ndiyo ninachokwenda nacho nyumbani kwangu. Sasa *what is 140,000 shillings* sasa hivi? Ni kidogo hata kima cha chini cha mshahara. Hawa watu walifanya kazi katika *spirit of perfection and dedication;* walifanya kazi katika uaminifu mkubwa na kazi ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo unamuona mstaafu anatoka Makunduchi huko anakuja makao makuu anakuja kupata; mimi napata pesa nyingi kuliko wao kwa sababu nilistaafu nikiwa Waziri. Anakuja kupata pengine kiinua mgongo cha shilingi 50,000. Akipita sokoni tu harudi tena na kitu. Sasa nasema lazima tuwaonee huruma na nashauri, *we do respect, the life expectancy* ya Mtanzania ni baina ya 65 na 75. Sasa hivi mimi hapa nilipo niko miaka 69, *by* tarehe 5 Aprili… *yes! By* tarehe 5 Aprili mwaka unaokuja nafika 70. Kwa hiyo nishapita katika kile kima cha *life expectancy* ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani Waziri Mkuu huko nyuma uliwahi kufanyika utaratibu mmoja kwamba watu hawa wapeni *pension* yao ya miaka 10. Sijui kama tumefahamiana hapo? Kusanyeni *pension* zao za miaka 10 halafu muwape kama mkupuo muondokane nao katika *Register* hii itawasaidia kuwaondosha kwenye *register* lakini angalau watapata cha kufutia machozi waweze kufa salama. Hayo ni mapendekezo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; tunakwenda kwenye *cashless economy* na kila nchi sasa hivi inaelekea huko na mimi naunga mkono sana kwamba matumizi ya pesa mbichi nafikiri siyo vizuri. Mheshimiwa Kandege na ndugu yangu Mheshimiwa Sanga wameeleza vizuri sana faida ya *cashless economy*. Ninachotaka kusema ni kwamba hivi, tunakwenda kwenye *cashless economy* kwa kutumia simu. Mtu kwenye simu yake atakuwa analipa malipo yote pale.

Mheshimiwa Spika, simu hii ni jambo la kusikitisha kwamba wenye simu *smartphones* ni kama 42% kama sikosei. Ni kusema wale wenye *access to the internet we are talking of 42% of the population while 58%* hawana *access to the internet*. Kwa hiyo, nashauri kitu kimoja, hizi simu Mheshimiwa Waziri katika *financial bill* yako itakayokuja huko mbele, hizi *smartphones* jaribu kuziondolea ondolea kodi ili ziwe *affordable*. Kila mtu katika *population* awe na *access to the internet* lakini hata wewe jitihada yako nakupongeza kwa kuondoa tozo. Kuna wakati simu hizi zilikuwa kuna tozo lakini uliondoa nafikiri kama sikosei katika Bajeti ya Julai 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kufurahisha kwamba baada ya kuondoa ile tozo, *the volume of money transfer* miamala ile ya fedha inaonekana kwa maana ya *volume of money transferred* ukilinganisha na *withdrawer; volume of money transferred* ni kubwa sana. Hii inaonesha kwamba tunakwenda pazuri kwa maana ya kulipeleka Taifa hili kutumia au kwenda kwenye *Cashless Economy* lakini nataka ni *pose challenge* hapa. *By tradition* kazi za benki yoyote ni mbili, ni kuweka amana za wateja na kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania ina *policy* ya kuwakopesha hawa wanaitwa *Commercial Banks* na *other financial institutions* kwa kutumia *discount rate on landing. Rate* ya Benki Kuu *prevailing rate* ya kukopesha kwa kutumia hiyo *discount rate on landing* ni 6% lakini *to the contrary,* sasa hapa ndiyo penye tatizo. *To the contrary commercial banks* wanakopesha wateja wao kwa riba siyo chini ya 10%. Sijui kama mnanielewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama wewe unaipata kwa *discount* unayopewa na Benki Kuu, wewe unakwenda kukopesha kwa zaidi ya 10%. Huko ni kuua na ndiyo maana tunakwenda leo, ukienda ukiacha hizi *commercial banks* ukienda kwenye hizi *micro financial institutions* kama *VICOBA,* hao ndiyo tunakwenda kwenye kausha damu. Hatufanyi vyema, nadhani Mheshimiwa Waziri hili ungelisimamia kuhakikisha kwamba ikiwa Benki Kuu inatoa *discount rate on landing* hizi *commercial banks* nazo zisaidie kutoa. Lazima zipate faida ni sawa lakini angalau basi isizidi *a certain amount of 10%* lakini *more than 10%* tunauana jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kwamba hata ukichanganua mikopo iliyotolewa kisekta utakuta kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo kiko chini kabisa. *Personal Loans* hizi Kisekta kwa mfano sekta ya *Building and Construction* imepata 29.9%. Sekta ya *Agriculture* imepata 1.6%, iko chini sana. Nadhani ni vizuri tunapotoa mikopo hii kwa zile *banks* ziangalie sekta zenyewe. Nadhani ningeshauri kwamba kilimo kwa sababu ndiyo Sekta ambayo ime-*employ* watu zaidi ya 30% ya *population* nadhani ingepewa asilimia kubwa. Tukifanya hivyo nadhani tutakuwa tumeusaidia sana uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nadhani naomba kuwasilisha *but once again* nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na naomba tumpitishe bila ya kupingwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayofanya. Pamoja na pongezi hizo ninanomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunaiomba Serikali ihakikishe inashughulikia suala la upungufu wa watumishi katika Ofisi ya *CAG,* lakini pia kuboresha maslahi yao kutokana na umuhimu wake kwa Taifa letu. Upo upotevu mkubwa wa fedha za Umma nchini na taasisi pekee tunayotegemea itusaidie kubaini ili tuweze kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma na kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ni Ofisi ya *CAG.*

Mheshimiwa Spika, pili, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia Duniani, yamesababisha kujikuta nchi zote duniani zinalazimika kutumia teknolojia ya hali ya juu ikiwemo mifumo ya kiteknolojia katika uendeshaji wa taasisi zetu zote na hata halmashauri zetu. Hii imepelekea wezi na wabadhirifu wa fedha za umma kutumia sayansi na teknolojia ya juu kama mifumo ya kompyuta katika kuiba. Hivyo basi hatuna namna ya kukwepa kutumia watumishi wenye ujuzi mkubwa wa kisayansi kama mifumo ya kompyuta, *hackers* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuwa na watumishi wachache katika Ofisi ya *CAG* yenye utaalamu wa hali ya juu ya *hackers* na kompyuta sayansi. Tunaomba sana watumishi hao watengenezewe mazingira mazuri ya kimaslahi ili kuendelea kutumikia katika Ofisi ya *CAG.*

Mheshimiwa Spika, *TRA* tunawapongeza kwa kazi wanayofanya ya kukusanya mapato au kodi nchini. Hata hivyo bado tunahitaji kuongeza juhudi za kuwapa mafunzo watumishi wake na kuhakikisha wanachagua watumishi ambao ni waadilifu kwa kazi hiyo kwa sababu baadhi yao kwa nyakati na mahali tofauti wamekuwa wakitengeneza mazingira ya kuwasumbua wananchi hasa wafanyabiashara kwa kuwatengenezea au kukadiria kodi kubwa ili kutengeneza mazingira ya rushwa. *TRA*

wajihadhari sana na dhambi hii iliyoandikwa kwenye Biblia, Luka 3:12-13[12], "Watoza ushuru nao wakaja kubatizwa, wakamwuliza, mwalimu, tufanye nini sisi?" [13], "Akawaambia, msitoze kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa."

Mheshimiwa Spika, tunaomba *TRA* wasitumike vibaya kutorejesha fedha za watu zilizochukuliwa kwenye maduka ya kubadilisha fedha za kigeni. Mimi na *declare interest,* nilikuwa ni mmoja wa wenye maduka haya, sijarudishiwa fedha zangu kwa kisingizio kuwa *TRA* hatuja *reconcile* nao kitu ambacho tulishakubaliana, kilichobaki wananizungusha tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana katika nchi hii katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wizara nzima ya fedha. Pamoja na nia njema ya Serikali kulipa wakandarasi, lakini ucheleweshaji makubwa ya malipo maana fedha za wakandarasi wengi zipo katika madeni ya Serikali na Serikali hawajawalipa na hawa wakandarasi wa ndani wana madeni ya mikopo kwenye benki na wanatakiwa walipe kwa riba. Je, nao watalipwa na riba?

Mheshimiwa Spika, hii inawafanya wakandarasi wengi kukosa kazi nyingine kwa sababu hawana tena vigezo kama *compliance certificate* kutoka *NSSF/WCF* na kadhalika. Hawapati *tax clearance* ya *TRA* kwa maana malimbikizo ni mengi na makubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni malipo ya *city service levy*. Kampuni nyingi zina mashine moja ya *EFD,* lakini wakandarasi wengi wamefungiwa hizi mashine na kushindwa kudai wateja. Pia, wakandarasi wengi fedha zao zinatolewa bila ridhaa yao.

Mheshimiwa Spika, je, kuna sheria inayomlazimisha mkandarasi kulipa madeni yake kwa muda maalum? Je, Serikali

imewekewa muda wa kumlipa mkandarasi kwa muda maalum? Basi niombe mtoe tamko la jumla kwa hiki kinachoendelea kwamba mtoa huduma na Serikali wapewe muda wa malipo na sio Serikali iseme mitandao inasumbua. Tuwaweke vizuri wakandarasi wa ndani waangaliwe ili kazi nzuri iendelee.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Katibu Mkuu Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Makatibu Wakuu Jenifa Omolo, Amina K. Shaban na Elijah Mwandumbya, wataalamu wa Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na wadau wa maendeleo wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika Sekta ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu umuhimu wa kuwa na timu mmoja ya ukaguzi wa kikodi kwa wafanyabiashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara hapa nchini wakiwemo wale wa kutoka Soko Kuu la Kariakoo kuhusu uwepo wa timu nyingi za ukaguzi pale mizigo yao inaposhikiliwa na mamlaka mbalimbali za kikodi. Jambo hili limekuwa linasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara pindi mizigo yao inaposhikiliwa na *TRA* kwa makosa ya kikodi.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wamesema kwamba imezoeleka kuona mfanyabiashara mmoja akikaguliwa na maofisa wa *TRA* zaidi ya mmoja kutoka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limelalamikiwa kuwa huwa ni chanzo cha kujenga mazingira ya rushwa. Ninaishauri Serikali iliangalie na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa maandalizi ya hotuba nzuri ya bajeti na kazi nzuri mnayofanya. Nina jambo moja kuhusu Benki ya Wananchi ya Mufindi *(MUCOBA)* ambayo imekuwa kwa miaka mingi mkombozi kwa wananchi wa Mufindi na Iringa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Benki ya *MUCOBA* ni Benki ya kwanza ya wananchi na benki nyingine zimekuja baadaye kwa kujifunza kutoka *MUCOBA* na *PBZ* walikuja kuweka mtaji baada ya mazungumzo ya muda marefu. Jambo hili ukiacha uchumi ni mfano mwema wa Muungano na faida zake.

Mheshimiwa Spika, Benki ya *MUCOBA* imekuwa mkombozi kwa sababu inawaondoa wananchi kwenye mikopo maarufu kama kausha damu. Sasa badala ya kuilea benki, *TRA*/Serikali mmekuja mmechukua shilingi milioni 680 matokeo yake *PBZ* wameamua kuondoa mtaji wao. Benki inajikuta inaanza kukosa sifa za *BOT* baadaye Benki itafungwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nashagaa sana benki hii kwa mtaji gani idaiwe shilingi milioni 680? Je, hakuna namna rafiki ya kulishughulikia jambo hili?

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Serikali mtafakari jambo hili, *this is a community bank* jamani. Mimi sio muumini wa kufoka Bungeni, *so* siwezi kuanza kufoka ndio maana nawaomba sana, tazameni jambo hili kwa utulivu.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, suala la mikopo midogo midogo kwa wananchi wa kawaida vijijini bado ni changamoto. Wizara iweke utaratibu wa kuweza kukopesha wananchi kupitia benki zao vijijini. Wananchi wanahitaji shilingi 100,000 mpaka shilingi 500,000 ili kuweza kujikimu na kutatua matatizo yao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo Wizara ipeleke fedha kwenye benki ya *TADB* ili wakulima wetu wapate mikopo. Mikopo ya *TADB* imekuwa ya wakulima wakubwa au wale wanaojulikana na hiyo taasisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho Wizara inunue matrekta na kupeleka moja kwa moja kwenye halmashauri angalau matatu kila kijiji badala ya kushindwa kuwakopesha fedha taslimu. Kazi kubwa ya mkulima ni kulima na kilimo kwa jembe la mkono ni shida kubwa. Serikali ipeleke mikopo na matrekta vijijini.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi *(FIU);* taarifa ya mwaka 2023/2024 ilionesha kuwa hadi kufikia Aprili taarifa ya miamala shuku iliyokuwa imepokelewa na kitengo ni shilingi trilioni 280 ambapo Mawaziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Fedha), Mheshimiwa Hussein Bashe (Kilimo) na Mheshimiwa *Professor* Kitila Mkumbo (Mipango) walipinga hapa Bungeni taarifa hizo na kusema hiyo ni miamala ya kawaida ya wauza vitenge, miamala ya simu, mbolea na kadhalika na wengine tuliohoji suala hili tukaambiwa tunatunga takwimu za uongo ili kuichafua Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, tulirushiwa kila aina ya ubaya baada ya kueleza kuwa kutokana na usimamizi dhaifu wa sera za fedha na bajeti, utakasishaji wa fedha haramu umeongezeka, utoroshaji wa fedha nje ya nchi kupitia mifumo ya kielektroniki na mipakani imeongezeka, pamoja na tuhuma za rushwa, wizi na ufisadi zinazoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri hao walisahau kuwa kazi ya Kitengo cha *FIU* sio kupokea taarifa za miamala ya biashara za kawaida bali ni kupokea taarifa ya miamala shuku *(suspicious transaction)* kutoka kwa watoa taarifa na kuzichakata na kuandaa taarifa fiche kwa ajili ya kupeleka kwenye mamlaka za uchunguzi kwa hatua zaidi za kisheria.

Mheshimiwa Spika, leo Mawaziri hawa watuficha wapi sura zao? Walitaka tuwasikilize wao badala ya taarifa za wataalamu wa kitengo baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti katika ukurasa wa 11 inakiri na nanukuu; "Tanzania ilitakiwa kuwekwa chini ya uangalizi wa kikosi kazi cha kusimamia mwenendo wa udhibiti utakasishaji fedha haramu *(Financial Action Task Force-FATF),* jambo hili lingekuwa na madhara hasi kwa Taifa. Hatua hii inatokana na kasoro zilizobainishwa na kikosi kazi hicho kwamba Tanzania ni eneo oevu la kutakasisha fedha," mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto katika Kitengo cha *FIU;* Waziri wa Fedha ameshindwa kutoa taarifa ya miamala shuku na taarifa fiche katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama inavyoripotiwa kila mwaka. Hii ina maana kuwa kuna mambo ambayo sio ya kawaida ambayo yanafichwa kwa nguvu kubwa na Waziri kwa sababu anazozijua yeye.

Mheshimiwa Spika, Kitengo chenye majukumu makubwa kutengewa fedha kidogo kiasi cha kushindwa kutekeleza majukumu yake. Mwaka 2023/2024 kitengo kilitengewa shilingi bilioni 4.32 tu, lakini katika bajeti ya mwaka huu 2024/2025 imekuwa shilingi bilioni 3.77 licha ya majukumu yao kuongezeka. Bajeti imepungua lakini pia fedha hazitolewi zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza mipango mikakati 24% tu (5/21) kati ya mipango mikakati iliyotolewa na kikosi kazi cha *FATF* na hivyo nchi kuwa kwenye hatari ya kuwa chini ya uangalizi wa chombo hicho. Athari za nchi yetu kuwekwa kwenye uangalizi wa *FATF* ni pamoja na nchi yetu kutokuaminika Kimataifa, kutokopesheka, kuwekwa kwenye hatari ya kufadhili ugaidi na kufadhili silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo; Waziri wa Fedha atoe taarifa kamili ya hali ya utakasishaji wa fedha haramu nchini, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi. Pia, Serikali kwa dharura itekeleze mipango mikakati 21 iliyotolewa na *FATF*.

Mheshimiwa Spika, pia Waziri wa Fedha alieleze Bunge hatua alizochukua baada ya nchi kutuhumiwa kuwa eneo oevu la utakasishaji wa fedha haramu na kufanyike marekebisho ya sheria na kuziwezesha taasisi za ukaguzi na uchunguzi kusomana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya mapato ya kodi, ni lazima kila uchao kutafuta njia za kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Serikali, lakini hivi sasa kampeni nyingi zinafanyika kuua vyanzo vya kodi. Kwa mfano uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi zaidi ya kiwango kinachohitajika nchini itaua viwanda na ajira nchini ambavyo vilikuwa ni chanzo cha mapato ya halmashauri na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, mambo yanayoua viwanda vya ndani mfano uagizaji wa sukari nje ya nchi; Serikali imetoa vibali vya kuagiza sukari nje ya nchi tani 410,000 wakati nakisi ya sukari *(gap sugar)* mwaka 2023/2024 ni tani 120,000 tu kwa ajili ya mwezi Machi hadi Juni, 2024. Hii ni ziada ya tani 290,000, hii ziada ya sukari itapelekwa wapi? Serikali iliongozwa na nini kuruhusu vibali hivi kutolewa? Hii ni kinyume cha Sheria ya Sukari na Kanuni zake inayotaka sukari inayoagizwa kutoka nje ya nchi iwe ni ile ya nakisi *(gap sugar)* tu na si vinginevyo na kiasi hicho kiwe kimethibitishwa na Kamati ya Ushauri wa Kiufundi *(TAC)* ya Bodi ya Sukari Tanzania baada ya kupitia mahitaji na uzalishaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa kuwa sukari inayoagizwa kutoka nje imesamehewa *VAT* 18% wakati sukari inayozalishwa na viwanda vya ndani inatozwa *VAT* 18%. Sukari hii inauzwa kwenye soko moja hivyo viwanda vya ndani haviwezi kushindana na badala yake vitafungwa na nchi kupata hasara kubwa. Pia, msamaha wa *VAT* unaharibu utaratibu wa ulipaji wa kodi na kuvifanya viwanda vya ndani kulipa kodi zaidi. Inafikirisha sana kuona bidhaa za nje zinasamehewa kodi huku bidhaa za ndani zikitozwa kodi bila msamaha.

Mheshimiwa Spika, pia kuna taarifa za uhakika kuwa vibali vya kuagiza sukari vimetolewa kwa watu ambao hawana viwanda vya sukari kinyume na Sheria na Kanuni za Sukari. Waziri

wa Kilimo alipata wapi mamlaka ya kuruhusu wafanyabiashara binafsi kupewa vibali vya kuagiza sukari?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo anapanga kufanya marekebisho ya Sheria ya Sukari Na. 6 ya mwaka 2001 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuwezesha *NFRA* kununua sukari na kuhifadhi kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa wakati tayari ameshatoa vibali kwa wafanyabishara binafsi kuingiza sukari nchini kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Serikali ya kudhibiti uagizaji holela wa sukari kwa kipindi cha miaka saba iliyopita umepelekea uzalishaji wa viwanda vya ndani kuongezeka, viwanda vipya vya sukari kujengwa na nakisi ya sukari *(gap sugar)* kupungua kutoka nakisi ya sukari kutoka tani 144,000 mwaka 2017 hadi tani 30,000 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, madhara yatakayopatikana kufuatia maamuzi hayo ni kama ifuatavyo: -

(i) Serikali itapelekea viwanda vyote saba vya sukari kufungwa kutokana na soko la ndani kutekwa na sukari kutoka nje ya nchi, ajira kupotea, mapato ya Serikali na wakulima wadogo kukosa soko la miwa;

(ii) Nchi kugeuzwa kuwa jalala la sukari *fake* na iliyokwisha muda wa matumizi na kuleta madhara makubwa ya kiafya kwa wananchi. Kutokana na mifumo hafifu ya udhibiti na kwa kuwa nchi yetu ina eneo refu la mpaka wa nchi kavu na majini sukari nyingi itaingia nchini bila kuthibitishwa ubora wake; na

(iii) Ugumu wa kupata mikopo katika taasisi za fedha, maamuzi haya yanaifanya nchi yetu kuwa na sera zisizotabirika za soko la sukari na hivyo kufanya iwe vigumu kupata mikopo ya ndani na nje ya nchi yenye masharti nafuu kwa uzalishaji wa sukari na uwekezaji. Kitendo cha kuruhusu sukari isiyo nakisi itaua viwanda ambavyo hivi sasa vina mikopo mikubwa ya ujenzi na upanuzi wa viwanda na mashamba.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha atuambie nini kilichopelekea yeye na Waziri wa Kilimo kufikia uamuzi huo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifumo ya usimamizi wa fedha za umma; ripoti ya *CAG* ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA ya mwaka wa fedha 2022/2023 inaonesha mapungufu makubwa ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji mapato na matumizi ya Serikali. Hata hivyo *CAG* ameweza kufanya ukaguzi 11% tu kati ya mifumo ya TEHAMA 460 iliyoko kwenye kanzidata ya Serikali Mtandao *(eGA)*.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu iko kwenye hatari kubwa kuwa na mifumo ya ukusanyaji mapato na matumizi ya Serikali ambayo haikaguliwi. Katika ukaguzi uliofanywa na *CAG* ulibaini kuwa, nanukuu; "Ukaguzi katika mfumo wa *Subsidy Management Systems* unaotumiwa na *TFRA* (Mfumo wa Mbolea ya Ruzuku) ulibaini kuwa mtoa huduma za TEHAMA wa nje amepewa haki za kuendelea kuingia kwenye *server* na hifadhi ya *data* za taasisi kinyume na matakwa. Hii inaashiria hatari ya usalama wa *data.* Aidha, maafisa wa TEHAMA wa *TFRA* hawana uwezo wa kupakua *data* kutokana na vikwazo vilivyopo, uingiaji huu wa mtoa huduma wa TEHAMA wa nje *(vendor)* unaleta hatari kubwa ya usalama wa *data.*"

Mheshimiwa Spika, muundaji wa mfumo au wafanyakazi wake wanaweza kuchezea takwimu vyovyote wanavyotaka na hata kuandaa madai hewa na mbolea hewa. Jambo hili limeruhusiwaje na Serikali hadi mali za Umma kugeuzwa kuwa mali binafsi? Waziri wa Fedha unakubali vipi kupeleka fedha za umma zaidi ya shilingi bilioni 150 kwenye mfumo ambao *server* na hifadhi *data* ziko kwenye umiliki wa mtu binafsi? Hii ni hujuma kubwa kwa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, nashauri tufanye mapitio ya haraka kuhusu usalama wa mifumo yetu ya TEHAMA na kuchukua hatua stahili kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malimbikizo ya kodi katika Mahakama za Rufani *(TRAB, TRAT* na *CAT);* kwa muda mrefu

tumelalamikia malimbikizo ya kodi kushikiliwa kwa muda mrefu katika mapingamizi ya kodi katika Mahakama za Rufani za Kodi, Bodi ya Rufani za Kodi *(TRAB)* na Baraza la Rufaa ya Mapato ya Kodi *(TRAT)* na Mahakama ya Rufaa *(CAT)*. Jedwali linaloonesha mtiririko wa malimbikizo ya kodi.

| **Mwaka wa fedha** | **Kiasi (Bilioni)** | **Ongezeko (bilioni)** | **Ongezeko katika asilimia** |
|---|---|---|---|
| 2022/2023 | 10, 048 | 5,650 | 117% |
| 2021/2022 | 4, 836 | (2, 702) | |
| 2020/2021 | 7,542 | 3,667 | |
| 2019/2020 | 3,875 | 1,744 | |
| 2018/2019 | 2,131 | | |

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuitaka Serikali mara kwa mara kuchukua hatua, lakini malimbikizo ya kodi yanayoshikiliwa katika mapingamizi ya Mahakama za Rufani za Kodi yanazidi kuongezeka kila mwaka kama jedwali linavyoonesha. Sababu zinazosababisha kuchelewa kwa maamuzi ya mashauri ya rufaa ni pamoja na kutofanya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi kwa mikoa isiyo na wajumbe na kutoteua kwa haraka Wajumbe, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti na uhaba wa bajeti za Mahakama za Rufani za Kodi, Mahakama ya Rufaa *(CAT),* Baraza la Rufaa ya Mapato ya Kodi *(TRAT)* na Bodi ya Rufaa ya Mapato ya Kodi *(TRAB)*.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha ambaye ndiye mwenye jukumu hili ameshindwa kufanya utekelezaji kila anapoagizwa na Bunge ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 malimbikizo ya kodi yalifikia shilingi trilioni 10.48 ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 5.65 sawa na ongezeko la 117%.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni pamoja na malimbikizo ya kodi kwa makampuni ya madini (Makinikia) yenye thamani ya shilingi trilioni 360 ambazo ziliondolewa kwenye vitabu vya Serikali bila kibali cha Bunge. Kwa nini Waziri wa Fedha alijichukulia mamlaka hayo?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri inaonesha kuwa hadi Aprili, 2024 kuna jumla ya mashauri 452 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.9 yamesikilizwa na kuamuliwa katika Mamlaka za *TRAB* na *TRAT.* Waziri atueleze ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)?* Aidha, hotuba ya Waziri inakinzana na Ripoti ya *CAG* ambapo kufikia Juni, 2023 malimbikizo ya kodi yalikuwa yamefikia shilingi trilioni 10.48, nini sababu za mkanganyiko huo?

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu mfululizo sababu zinazoelezwa za mashauri hayo ni kukosekana kwa Wajumbe wa Bodi za Rufani na bajeti ndogo inayotengewa mamlaka hizo. Kwa nini Waziri wa Fedha anafanya hujuma kubwa kiasi hicho katika Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya *CAG;* taarifa ya TAKUKURU inasema kuwa kufanyia kazi ripoti iliyopita ya *CAG* ya mwaka 2021/2022, TAKUKURU ilifungua majalada ya uchunguzi 375. Kati yake 156 yalikosa ushahidi wa kufikishwa Mahakamani, 73 yalichukuliwa hatua, 28 yako hatua ya Mkurugenzi wa Mashtaka na 41 yalitolewa hukumu Mahakamani wakishinda 40 na kushindwa katika shauri moja.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma inamtaka *CAG* wakati wa ukaguzi akibaini jambo lenye viashiria vya rushwa atoe taarifa kwa TAKUKURU. *CAG* hadi kuibua hoja ya ukaguzi huwa amepitia nyaraka na vielelezo vingi muhimu na majibishano ya ana kwa ana na wakaguliwa hivyo haiwezekani eti 42% ya hoja zake zikose ushahidi Mahakamani. Hapa huwa kuna njama za makusudi zinazofanywa kupoteza ushahidi kwa makusudi ili kutoa unafuu kwa wahalifu na kuifanya

Ofisi ya *CAG* ionekane inaandika taarifa za uongo. Leo *CAG* aulizwe kama kweli hana ushahidi wa mashauri 156.

Mheshimiwa Spika, mashauri 28 tangu yapelekwe na TAKUKURU kwa *DPP* mwaka jana hadi sasa amekaa nayo hataki kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa maana yake Ofisi ya *DPP* inatumika kama mbeleko na kichaka cha kuficha watuhumiwa wa rushwa na ufisadi. Kesi zinazotokana na ripoti ya *CAG* zenye ushahidi wa kutosha inawezekanaje zikae muda mrefu zikichunguzwa? Hayo mashauri 28 yanawahusu kina nani ambao *DPP* hataki wapelekwe Mahakamani? *CAG* amefanya kazi yake vizuri ya kizalendo kwa Taifa lake halafu wahalifu wanakwenda kulindwa na mamlaka zingine za Serikali. Kushindwa kupelekwa vielelezo kwa wakati Mahakamani kunapelekea kesi kuchukua muda mrefu bila sababu za msingi na hata kufutwa au kushindwa kwa kukosa ushahidi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imekuwa haitangazi hadharani majina ya watuhumiwa wa rushwa na ufisadi na imegeuza kuwa jambo la siri hali inayorudisha nyuma mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi nchini, lakini upande wa Zanzibar, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar *(ZAECA)* imekuwa ikiwatangaza kwa majina, vyeo na hasara waliyoisababisha watuhumiwa wote wa rushwa na ufisadi wanaopelekwa Mahakamani bila kujali nafasi zao ndani ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, nionavyo mimi baada ya *CAG* kuwasilisha ripoti yake kwa Umma kuna njama nyingi sana zinafanyika katika mamlaka mbalimbali za Serikali kuwalinda watuhumiwa wa rushwa na ufisadi waliotajwa kwenye ripoti hiyo na ripoti hiyo kutelekezwa na kuonekana kama haina mwenyewe. Ilitegemewa Waziri wa Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha kuwa hoja na kesi zinazotokana na Ripoti ya *CAG* zinasimamiwa kikamilifu. Nashauri yafuatayo:-

(i) Kufanya mapitio upya ya sheria ili kuondoa uwezekano wa watuhumiwa wa ripoti ya *CAG* kuokolewa na mamlaka zingine za Serikali; na

(ii) Kiundwe chombo kingine cha kufuatilia utekekezaji wa ripoti ya *CAG* kwani inakuwa vigumu sana kwa Waziri wa Fedha kufuatilia utekelezaji wa ripoti hiyo hasa pale inapotokea yeye ndio kinara wa tuhuma mbalimbali za rushwa na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Jambo la pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha wakati huu. Nianze kwa kuunga mkono hoja; naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha. Mimi nitachangia hoja tatu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza nitakayochangia ni hoja ya Mfumo wa Ruzuku ya Mbolea. Kwanza, Mheshimiwa Mpina ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba Mfumo wa Ruzuku wa Mbolea *server* na mfumo wote uko mikononi mwa *vendor*. Nataka kulitaarifu Bunge lako Tukufu, Wizara ya Kilimo imemwandikia rasmi *CAG* kumwambia kwamba taarifa hiyo siyo sahihi. Mfumo wote, *server* yote na *access code* ziko *TFRA* chini ya Wizara ya Kilimo na ziko *under e-GA. This has to go on record. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; kwamba mfumo una vihatarishi vya kupoteza fedha za umma. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu, fedha zote zilizotolewa na Serikali kwa kutumia mfumo tunaotumia wa kusajili wakulima na kutoa ruzuku ya mbolea haujapoteza shilingi 100 ya Umma ya nchi hii; na kwenye ripoti ya *CAG* hakuna mahali ambapo *CAG* kasema kuna upotevu wa fedha. Hii iende *on record. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo nataka nichangie na hii nataka niiongee polepole na namuomba Mwenyezi Mungu anipe uwezo huo. Suala la sukari Taifa hili, viwanda sita/saba vya nchi hii viliweka Taifa la Watanzania milioni 61 kwenye mikono yao. Kama Waziri wa Kilimo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu sitaruhusu hilo kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni suala la sukari; sukari ni chakula cha mtu masikini. Sote humu tukienda pale *canteen* unaulizwa, "Unataka na sukari?" Unasema, "Hapana, niwekee asali." Tuna *luxury* ya ku-*choose*. Mwezi Januari na Februari nchi hii sukari ilifika shilingi 10,000. Makampuni haya na viwanda hivi tunavyoviita tuvilinde vilipewa vibali vya kuingiza sukari; havikuingiza sukari. Mnataka niwe Waziri boya wa kukaa hapa kusubiri hili? *I will never allow this* na ninasema hili *clearly*. Nitakuwa *counted for this. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nchi hii ilikuwa ina *sugar gap* ya tani 60,000; tulimpa Kagera *Sugar,* Mtibwa, Bagamoyo na *TPC;* hakuna aliyeingiza hata kilo moja. Mlitaka nikae naangalia?

Mheshimiwa Spika, tulitumia nini? Tumeenda kubadili kanuni za *National Food Reserve Agency* kuruhusu *NFRA* kuwa na *mandate* ya kuingiza sukari. Mimi niseme ndani ya Bunge lako Tukufu Serikali ya Chama cha Mapinduzi itawalinda wakulima, viwanda na walaji; ndiyo jukumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe elimu ndogo, *gap sugar* huwa tunaitoa kwa ajili ya *window* ya mwezi Machi, Aprili na Mei, miezi mitatu. Kutokana na mvua za *El Nino*, baada ya *TMA* kutoa utabiri wa hali ya hewa, tuliyapatia makampuni na viwanda, walete tani 50,000, mpaka mwezi Februari, walikuwa hawajaleta hata kilo moja ya sukari na walipoingiza walifungia kwenye ma-*godown* yao, tulienda kufungua ma-*godown* na polisi. Niingie *on record* na nitatoa takwimu kwanini tumetoa vibali kupitia *AFNRA* vya tani 400,000, *numbers don't lie*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hivi, Serikali iliweka sheria hapa ya kumlinda mlaji na kumlinda mzalishaji, tumewalinda, hatujawahi

ku-*violate* hata siku moja. Mwaka jana tulivyowapa vibali vya kuingiza na mpango mkakati ukiongozwa na *TSPA*, *Tanzania Sugars Producers Association*, ambaye Mwenyekiti wa taasisi hii ni *owner* wa Mtibwa na *Kagera Sugar*.

Mheshimiwa Spika, tulivyowapa kibali cha kuingiza sukari, tumekaa Disemba, hakuna kilo moja iliyoingia, Januari, hakuna kilo moja iliyoingia, mwishoni mwa Januari wameingiza tani 250 wakati wakifahamu *sugar* na *buffer stock* ya mwaka wa nyuma wa uzalishaji hawakuingiza hata kila moja. Kwa hiyo, Taifa lilikuwa halina sukari.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, tumewapa bei elekezi ya kuuza sukari kwa mujibu wa utaratibu ambapo viwandani *X-ware house price* walitakiwa kuuza kati ya shilingi 2,300 na 2,500. Waliwauzia *distributors* kwa shilingi 2,800 mpaka 3,000 na sukari waliyoingiza bandarini tuliyowapa *VAT exemption*, hata wao tumewapa *VAT exemption*, wameingiza bandarini wanaenda kuiuza mfuko wa kilo 50 x-Dar es Salaam shilingi 150,000 mpaka shilingi 160,000, mlaji wa Nzega ale kwa shilingi ngapi? Na mimi nipo Waziri ninaangalia, siwezi kuruhusu, kamwe sitaruhusu. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zipo taarifa za wazi kwamba Waziri hata hao aliosema kwamba aliwapa kibali cha kuagiza sukari, hakutangaza *tender* yoyote na haijulikani aliwapataje, lakini nyaraka zote zipo; na kwa kuwa kuagiza sukari zaidi ya *gap sugar* ni makosa kisheria; na kwa kuwa pia kuwaruhusu watu ambao hawaruhusiwi kwa mujibu wa sheria tuliyonayo sasa hivi ya sukari ni makosa ya kisheria. Endapo nyaraka hizo zote zikiwekwa mezani kwako Waziri atachukua nafasi gani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina umetoa taarifa kuhusu *gap*. Mimi ndiyo nilikuwa namsikiliza, nadhani ndiyo alikuwa anaenda huko kuelezea kwanini ameagiza hicho kiasi kikubwa kuliko kile ambacho kilikuwa kimeelezwa kabla. Sasa wewe mwenzetu umempa taarifa kabla hajachangia. Kwa hiyo, ngoja achangie ndiyo uulize hilo swali lako, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza naomba niongee pole pole tena, narudia, katika mazingira ya kawaida, *gap sugar*, kwanza uagizaji wa sukari ya *gap sugar* huwa hauna tenda, hamna tenda. *Gap sugar* huwa tunaruhusu ili ku-*cover* kipindi cha miezi mitatu ambayo viwanda vinakuwa vimefungwa ambao ni Mwezi wa Tatu…*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ngoja, ukiacha haya aliyosema sasa hivi, wewe ungeenda na ule mtiririko wako ili Bunge likuelewe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nilikuwa naelekea huko.

**SPIKA:** Maana ukianza kumjibu yeye tunakatisha huku kichwani namna tulivyokuwa tunafuatilia uchangiaji wako.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, sawa, najaribu kutaka kuonyesha tunaruhusu uagizaji wa sukari kwa ajili ya kipindi ambacho hatuzalishi, kwa kawaida ni mwezi wa tatu, wa nne na wa Tano na hivi ninavyoongea sasa hivi, viwanda havijaanza uzalishaji. Sasa, *projected gap sugar* mwanzo wa msimu wa uzalishaji mwaka jana mwezi wa tatu, tuli-*project* kwamba tutakuwa na *gap sugar* tani 140,000 na 150,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya *TMA* na hali ya mvua, uzalishaji ukashindikana katika nchi yetu kuanzia Oktoba, Novemba, Disemba, Januari, Februari na Machi ambayo ni hali ya kawaida ya uzalishaji. Lakini leo tunavyoongea, *April* hakuna uzalishaji, Mei hakuna uzalishaji kwa hiyo Taifa letu halina uzalishaji wa sukari kwa miezi nane. Wastani wa matumizi ya sukari katika nchi yetu, kwa siku Tanzania tunakula tani 1,500, kwa mwezi

tunatumia tani 45,000, *simple mathematics*, 45,000 mara nane ni zaidi ya tani 350,000 karibu 360,000. Sasa, kwanini tumeidhinisha ziada ya kufika tani 410,000? Kawaida tutakapofika mwezi wa tatu mwakani, *always* ni lazima tunaposimamisha uzalishaji tuwe na *buffer* ya miezi miwili, hivi ndivyo hesabu zinavyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini kimeendelea? Watanzania mfahamu na Bunge hili lifahamu. Mwaka 2022/2023 tulikuwa na *gap* ya tani 60,000 wakati *retail price* ya sukari ilikuwa wastani wa shilingi 2,600. Walipoacha kuagiza bei ya sukari ikapanda mpaka 3,000, tulipowapa kibali tena kuagiza kwa ajili ya mwaka huu ambao tuna matatizo, wakaacha kuleta sukari Januari na Februari, bei ya sukari ikafika shilingi 8,000 mpaka shilingi 10,000.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati? Nataka nitoe mfano mdogo wa Kagera, kiwanda cha *Kagera Sugar* kiko Kagera, pale Bukoba Wilaya ya Misenyi, nini kinatokea? Mlaji aliyeko Misenyi anakula sukari *almost the same* na mlaji aliyeko Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, mfumo wao wote wa *distribution* ni *cartel system,* msambazaji mmoja tu yuko Mwanza anahudumia mikoa 11. Hatuwezi kuruhusu *ecosystem* ya namna hii, ni lazima Serikali ifanye *intervention* na sisi tumefanya *intervention* na wao nimewaambia njooni mezani tuongee, tukubaliane, tuheshimu Taifa hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri kengele ya pili imeshagonga, nitakuongezea dakika mbili lakini inabidi nimpe nafasi Mheshimiwa Mpina kwa sababu nilimuambia atauliza baada ya wewe kumaliza maelezo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mpina sasa uliza swali lako.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, uagizaji wa *gap sugar* huwa unakuwa *established* na ile timu ya kiufundi ya bodi ya sukari ambayo inafanya na inawajulisha na wadau. Sasa Waziri anasema kwamba ametoa kibali cha tani 410,000 kama *gap sugar*.

Mheshimiwa Spika, nataka kifupi tu, kwamba hicho kibali cha timu ya kiufundi cha Bodi ya Sukari iliyo-*establish* namba mpaka ikapata nchi hii inaweza ikaagiza *gap sugar* ya tani 410,000, hapa athibitishe hilo na aliletee Bunge lako huo ushahidi na mimi nitaleta ushahidi kwamba…

**SPIKA:** Ngoja mpaka nijiridhishe. Mheshimiwa Mpina nisaidie, vibali vya hicho kiasi cha sukari vinavyotolewa, sukari ile inaletwa kwa wakati mmoja? Yaani kwa mfano sasa hivi nchini hiyo sukari yote tumeshaipata ama huwa vinatolewa kwa sura gani?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi kwa taarifa zilizopo katika hiyo tani 410,000 zimeshaingia tani 220,000…

**SPIKA:** Ngoja, na huu ni mwezi wa ngapi?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, huu ni mwezi wa sita.

**SPIKA:** Wa Sita, kwa hiyo, tumebakiza miezi mingapi kufikia kwenye ile *gap*?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, zimebakia tani 190,000 katika zile tani 410,000.

**SPIKA:** Sawa, umeshaeleweka hoja yako kwa Waziri…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kidogo.

**SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, *gap sugar* ambayo imekuwa *established* na hiyo timu ya ushauri wa Bodi ya Sukari ni tani 120,000 tu siyo 410,000 na nchi yetu haijawahi kuwa na *importation* ya namna hiyo hata kama uzalishaji huo anaousema yeye…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hapa jamani kanuni zetu zilivyo, kwa hivyo, Mheshimiwa Mpina ili nikuelewe vizuri, Mheshimiwa Waziri anachokisema wewe hapa kikanuni unamwambia Waziri anadanganya?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, anadanganya na yuko nje ya sheria. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu; Kanuni ya 70 inazungumza kuhusu kutokusema uongo Bungeni na kwa sababu ya muda sitataka kwenda huko kote lakini inataka wewe unayesema mwingine anasema uongo ndiyo uthibitishe. Ndiyo kanuni zetu zinavyotaka, yaani ukimwambia mtu wewe unasema uongo wewe ndiyo unathibitisha uongo wa yule mtu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpina wewe ulikuwa unasema Waziri alete ushahidi, sasa mimi nitauhitaji ushahidi kutoka kwako wa kuonyesha namna ambavyo Waziri anadanganya.

Waheshimiwa Wabunge ni kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 70, 71, inataka hivyo, ndiyo utaratibu ulivyo. Sasa kwa utaratibu huu Mheshimiwa Mpina ndiyo ataleta ushahidi. Sasa zile dakika mbili nampa Mheshimiwa Waziri amalize. Ushahidi wa Mheshimiwa Mpina utakapokuja tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, dakika mbili.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba nimalizie kwa kusema yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ndani ya Bunge lako hili katika Hotuba ya Wizara ya Kilimo, imesema *clearly* kwamba kama nchi tutaagiza jumla ya tani 410,000 au 420,000, kama sikosei mpaka mwezi Disemba mwaka huu. Mpaka sasa, kwa taarifa tulizonazo kama Wizara ya Kilimo na kama alivyosema Mheshimiwa Mpina, anayetathmini na kuamua, kwamba *technical team* ni ya Bodi ya Sukari ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo ndiyo inayofanya tathmini kutambua mahitaji ya nchi na hali ilivyo kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania na kulihakikishia Bunge lako Tukufu mambo makubwa matatu. Moja; nchi hii haitarudia tena ku-*experience* ilicho-*experience* mwezi Disemba, Januari, Februari. Pili; Serikali ya Chama cha Mapinduzi italinda walaji, wakulima, viwanda na wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu; mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa sukari, tutau-*confront* kuondoa mfumo wa *cartel* na kila mkoa utakuwa na msambazaji na kila kiwanda kitakuwa hakijiamulii bei kinavyotaka, Serikali itasimamia jambo hili bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge sikuisoma Kanuni kwa ajili ya muda, lakini naona kuna *concerns* hivi. Kanuni ya 70(2)(3) na (4);

Fasili ya (2) Mbunge yeyote atakapokuwa akisema Bungeni, hatachukuliwa kuwa anasema uongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa ama lililoandikwa na vyombo vya habari.

Fasili ya (3) Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka kuhusu utaratibu na baada ya kuruhusiwa na Spika kudai kwamba Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.

Fasili ya (4) Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

Sasa nimeona niwasomee watu naona wanaanza kupata picha kama Mheshimiwa Mpina amewekwa kona hivi, hapana, ni kanuni zetu zinataka aliyesema mwingine anasema uongo yeye ndiyo athibitishe kwamba huo ni uongo na yeye anao ukweli anaoujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ambayo na mimi umenipa ili kuchangia katika hoja ambayo iko mezani kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Mwenyezi Mungu ambaye ndiyo ametuwezesha tangu bajeti ya sekta ya kwanza ambayo tulianza nayo, Ofisi ya Rais, mpaka leo kumaliza tukiwa katika hali ya uzima na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ndiye mbeba maono ya Watanzania, ambaye kazi zake zimeonekana kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani naweza kusema miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais, kwa mwendo wa kazi wa maendeleo ya Watanzania na Tanzania kwa jumla basi ni sawa na miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenye macho haambiwi tazama, ukienda kuangalia leo miradi ya maendeleo ambayo ipo ndani ya nchi yetu, ukihesabu miradi ile wingi wake na ukubwa wake basi ni sawa na miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana Kamati ya Bajeti, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wenzangu. Kwa kweli, Kamati hii kwangu ni walimu wangu, nimejifunza mengi na ninaendelea kujifunza lakini wanastahiki kupewa sifa na kupongezwa kwa utendaji wao mkubwa wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna muda maalum wa kailula katika maisha yetu lakini Kamati ya Bajeti haipati hata muda wa kufanya kailula kwa sababu ya kazi ambayo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza niseme michango yenu yote tumeipokea kwa mikono miwili. Nimeona kabisa kila mmoja aliyechangia hapa alikuwa anachangia hoja kwa njia ya kujenga. Hata kama mmoja ama mwingine ulimuona *intention* yake kidogo, lakini alikuwa na nia ya kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwapongeze sana Wabunge kwa michango yenu ambayo mmeitoa na tumeipokea yote kwa jumla. Naomba nimpongeze sana na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye kwangu mimi ni mwalimu wangu, mshauri wangu na mlezi, naweza kusema kama ni kocha huyu tungesema ni Juma Mgunda, ndiyo makocha wa Tanzania na kama ni *striker* tungeseme ni Aziz Ki kama angekuwa ni mchezaji, kwa hiyo, nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Nawaambia tu ndugu zangu wana-Iramba kule kwamba, Mheshimiwa Mwigulu anatosha na chenji inabaki. Hakuna haja ya kuhangaika hangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako, kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, pamoja na timu yake yote ya wataalamu kwa sababu, wanafanya kazi nzuri na bora sana. Pamoja na *Commissioners* wa *TRA* na ma-*Commissioners* wa taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, naomba kuwapongeza sana wana-jimbo la Kojani ambao wao kwa kura zao ndiyo nilifika hapa nilipo leo. Kwa hiyo, naomba kuwapongeza na kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba kujielekeza kwenye hoja chache kwa kuwa, nyingi zilizotoka hapa leo ni ushauri, basi naomba kujielekeza kwenye hoja chache. Hoja ya kwanza ambayo imetolewa na Kamati ya Bajeti pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia, ni uteuzi wa Wajumbe katika Bodi ya Rufani za Kodi, yaani *TRAB*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha tayari imeshateua wajumbe katika mikoa 10. Kati ya ile mikoa 12 iliyosalia, tayari mikoa 10 wameshateuliwa na barua zao zimeshawafikia. Miongoni mwa mikoa hiyo, hapa hongera sana, wa kwanza ni Mbeya, wa pili ni Songwe, Iringa, Njombe, Kigoma, Manyara, Mara, Kilimanjaro, Lindi na Tabora. Taratibu za uteuzi katika mikoa miwili iliyobakia zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hoja nyingine, Serikali imeshauriwa kupunguza gharama za miamala katika Mfumo wa Malipo Madogo na ya Papo kwa Papo, yaani *TIPS*. Mfumo wa *TIPS* unaendelea kuboreshwa, ili kuona kwamba, miamala inakuwa nafuu, yaani gharama yake inakuwa nafuu kwa watumiaji kulingana na maisha ya walio wengi katika nchi yetu. Hivyo, napenda kutoa wito kwa Taasisi zote za Fedha zikiwemo benki na taasisi ndogondogo za kifedha wahakikishe kwamba, wanafuata Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kusema, uwajibikaji. Hapa nina maana suala la ukusanyaji wa kodi lisionekane kwamba, ni la *TRA* wala lisionekane kwamba, ni jukumu la Serikali peke yake. Jukumu la ukusanyaji wa kodi ni jukumu la kila mmoja wetu katika Nchi hii ya Tanzania. Kila mmoja anatakiwa a-*play role* yake, ili kusudi tuwe na ukusanyaji mzuri wa mapato, lakini tuwe na ongezeko zuri la mapato kwa sababu, miradi mingi ambayo tunaijenga kwa fedha zetu, inatokana na ukusanyaji wa fedha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo Watanzania wenzangu natoa wito tuoneshe utayari katika ukusanyaji wa fedha. Tunayo *circle* tumeiweka kwamba, hapa kila mtu achukue nafasi yake. Mwananchi nafasi yake yeye ni nini?

Mheshimiwa Spika, kama ni mfanyabiashara, atoe risiti halisi na halali kwa bidhaa ambayo ameuza. Mwananchi na yeye ni nini wajibu wake? Wajibu wake ni adai risiti, tuwe na utamaduni kabisa wa kudai risiti halali, inayokwenda na bidhaa ambayo amenunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni nini wajibu wa *TRA?* Wajibu wa *TRA* ni kukusanya kodi ile kwa ufanisi, kwa busara na bila mabavu, kama alivyosema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa sina shaka kwamba, Watumishi wetu wa *TRA* wanaendelea kufanya kazi hiyo kwa ufanisi. Kwa sasa hakuna mabavu ambayo yanatumika, ikitokea inawezekana ikawa ni bahati mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni nini wajibu wa Serikali baada ya fedha kuingizwa Mfuko Mkuu? Ni kujenga miradi ya maendeleo ambayo leo tunaiona. Kila kona unapokwenda, Halmashauri zote, Wilaya zote kuna miradi ya maendeleo, kama siyo afya ni maji, kama siyo maji ni umeme na kadhalika. Haya ndiyo tunayoyataka kwa hiyo, tuwe tayari Watanzania leo, kila mmoja kuwa na wajibu wake katika suala la ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni hivi leo, mara nyingine, anaonekana mjanja ni yule anayekwepa-kwepa kodi, tuache utamaduni huu. Mtu yule ambaye tuna hakika kwamba, anakwepa kodi, basi tutoe taarifa na tuhakikishe kwamba na yeye amelipa kodi. Suala la uwajibikaji katika jambo la ukusanyaji wa mapato, tuchukue kwamba, huu ni utamaduni kwa kila mmoja wetu Tanzania. Kama vile ambavyo tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mlivyolibeba suala la Sensa Mwaka 2022 hapa Tanzania, tukawa na mafanikio makubwa sana hadi nchi nyingine zinakuja kutuiga sisi au kujifunza kwetu, basi na suala la ukusanyaji wa kodi naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwe

mstari wa mwanzo katika kuonesha wajibu wetu na kuwa tayari katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hoja zangu hizo ambapo Mheshimiwa Waziri yeye ndiyo atakuja kukamilisha, naomba uniruhusu kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri nakwambia tu kwamba, mwenda hidimani ndiye mkosa kwa hiyo, vile kulaumiwa-laumiwa, kukosolewa-kosolewa ni kwa sababu, wewe unafanya kazi nzuri. Unapokuwa unafanya kazi nzuri ni lazima utakosolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano kwenye mpira, hata juzi alisema, aah! amekosa penati ile Aziz Ki kwa sababu, kaipeleka kushoto, alikuwa aipeleke kulia ile, pembe ya kulia angeshinda goli. Aah! sasa wewe unasema hayo uko juu huko kwenye jukwaa. Au unaweza kwenda *masjid*, au unaweza kwenda kanisani, basi mhubiri anakwambia, usipokuja kanisani jumapili tatu wewe utakosa baraka za Mungu.

Mheshimiwa Spika, Imamu Msikitiktini anaweza kukwambia vivyo hivyo. Hii ni kwa sababu, mwenda hidimani ndiye mkosa. Maana yake ni unaambiwa vile, wewe ndiyo upo pale, wewe si ndiyo upo pale Msikitini au Kanisani, sasa maneno yale walipaswa wakaambiwe walioko nje. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kutokea kukosolewa-kosolewa taratibu-taratibu, wewe mwenda hidimani ndiye mkosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla mtoa hoja hajaja kuhitimisha, wako wageni hapa Bungeni.

Tunao wageni 90 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Ujenzi ambao ni Jumuiya ya Wanavyuo wa Karagwe na Kyerwa wanaosoma Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 60 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, hawa ni walimu na

wananfunzi wa Shule ya *St. Joseph Millenium* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 26 wa Mheshimiwa Aida Khenani ambao ni wanachuo wa Diploma ya Uuguzi na Ukunga wa *St. Bakita* kutoka Wilaya ya Nkasi, Mkoa wa Rukwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni wanafunzi 70 kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* cha Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, aje ahitimishe Hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuhitimisha hoja. Awali ya yote nakushukuru wewe mwenyewe na kukupongeza kwa kuendesha vizuri sana mjadala huu. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo ilianzishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Wajumbe wa Bajeti ambao walishiriki katika kutoa mchango wao, kutoa maoni yao ambayo yameboresha zaidi mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Chande, Naibu Waziri wa Fedha, ambaye anafanya kazi nzuri sana na amefanya majukumu yangu yawe mepesi. Nawapongeza Wataalamu wetu wa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake zote ambao tunafanya kazi kwa pamoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ambaye naye amechangia katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi Mwenyezi Mungu anisaidie nijibu kwa upole na taratibu, kama ambavyo mwenzangu amesema. Hoja zote ambazo zimetolewa ambazo zinalenga kutoa ushauri, tumezipokea na tutazifanyia kazi. Baadhi ya maeneo ambayo yamechangiwa, yatapata fursa wakati tutakaposoma Bajeti Kuu ya Serikali, tarehe 13. Mengine yatajitokeza wakati tutakapokuwa

tunawasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)* ya mwaka huu, yale yote ambayo yanahusiana na masuala ya hatua za kikodi.

Mheshimiwa Spika, mimi nafanya ufafanuzi tu katika baadhi ya masuala. Naanza na yale ambayo yanaweza kuleta taharuki, moja ni hili ambalo Mheshimiwa Mpina ameliongelea kwamba, nchi yetu imewekwa kwenye uangalizi na akauliza kwamba, tumefikaje hapo:-

Mheshimiwa Spika, mimi tofauti yangu na Mheshimiwa Mpina huwa siyo uzito wa hoja. Tofauti yangu huwa ni pale ambapo anaileta hoja kama vile Serikali nzima imelala, lakini anaileta katika kipindi ambacho Serikali ilishafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa, jambo hili linaweza likaleta taharuki na hasahasa anapo-*personalize* kwamba, tumfanyaje Mheshimiwa Waziri huyu. Mimi nilipoteuliwa kuwa Waziri wa Fedha, ziara yangu ya kwanza niliyoifanya kwenye hii *Financial Unit* ya taasisi yetu inayosimamia masuala haya, jambo nililopewa mahususi, lilikuwa ni kwamba, nchi yetu imeingia kwenye uangalizi, hapo ilikuwa ni Mwaka 2021. Nilichofanya niliandika taarifa hiyo kwa Mkuu wa Nchi na akaelekeza kwamba, jambo la aina hiyo tulichukulie hatua haraka sana, ni vitu gani vinavyotakiwa?

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitisha kikao cha Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wanaguswa na jambo hili. Tukawa na bangokitita, Waziri kwa Waziri, maeneo ambayo yameguswa na yanaleta uhatarishi huu. Mwaka 2022 Machi, tulileta mabadiliko ya Sheria ambayo ndiyo hasa mambo ambayo tulikuwa tunatakiwa tufanye kama nchi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo yalishafanyika na Kanuni zake zilisharekebishwa tangu Mwaka 2022. Baadhi ya maeneo ambayo yalitakiwa yafanyiwe kazi, yalikuwa ni 25. Sasa hivi tulishavuka nusu ya yale yaliyotakiwa kufanyiwa kazi yakiwemo marekebisho ya Sheria kwa pande zote, Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania pamoja na Zanzibar. Kote Sheria zilisharekebishwa na kanuni zake zilishatungwa na zilishaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, sasa hivi kikao kilichofanyika cha mwisho cha uangalizi tuko kwenye hatua ya kutoka. Hicho ndicho ninachosema kwamba, mwenzetu analileta kwa utisho katika kipindi ambacho Serikali miaka miwili iliyopita imeshalifanyia kazi na *actually* tuko kwenye kutoka kwenye huo uangalizi. Kwa maana hiyo, nimeona niliseme hili, ili lisije likaleta taharuki ilhali Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo huwa inatoa masuluhisho ya matatizo, ilishatoa suluhisho hilo na tunaenda kwenye uelekeo ambao ni mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hasa yale ambayo alikuwa anayasemea kwamba, tumfanye nini Mheshimiwa Waziri huyu, nadhani atakuwa ameshaona kwamba, hilo tulishalifanyia kazi. Kimsingi kwa kuwa, yeye ni Mheshimiwa Mbunge anaongea tumfanye nini Mheshimiwa Waziri huyu katika kipindi ambacho fedha za miradi ya maendeleo zimekwenda kwenye majimbo kuliko kipindi chochote tangu hata yeye apate Ubunge huu kwa hiyo, anachotakiwa kufanywa Mheshimiwa Waziri huyu ni kupongezwa tu kwamba, amemsaidia vyema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majukumu aliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya fedha hizi zilizoko kwenye Bodi ya Rufani za Kodi pamoja na Baraza la Rufani za Kodi, *TRAT* na *TRAB*.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na vikao na taasisi hizi takribani wiki mbili zilizopita. Mwezi uliopita nimekuwa na kikao na kabla ya hapo tumekuwa na *engagement* ndani ya Wizara. Ni kweli, kumekuwepo na mabishano hayo, lakini kama nilivyosema mwanzo, Serikali imechukua hatua.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua ambayo ni kubwa sana Serikali imechukua ni kuanzisha Ofisi ya Msuluhishi wa Kikodi. Hili ni jambo ambalo lilikuwa linatolewa ushauri na Waheshimiwa

Wabunge miaka na miaka, lakini Mheshimiwa Dtk. Samia Suluhu Hassan alipoapa tu, hili lilikuwa jambo la kwanza alilosema, ofisi hii ianzishwe na sasa imeshaanza. Pia, tumeteua wale wataalamu ambao wajumbe walikuwa wanapungua katika mikoa hii kama Mheshimiwa Naibu Waziri wangu wa Fedha alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barua walishapokea na sasa hivi upungufu uko katika maeneo mawili tu ambayo tunakamilisha taratibu za kiuteuzi. Hili jambo nimelifuatilia kwa ukaribu sana, takribani shilingi trilioni 3.2 ni mashauri ambayo yalishaamuliwa. Ukitajiwa mashauri haya, kuna wakati unaweza ukadhani zote ni fedha zinazokusanyika, lakini mabishano mengine ni *refund*. Kwamba, taasisi inaidai Serikali, kampuni inaidai Serikali kwa hiyo, yenyewe inatakiwa iwe *refunded*, inabishaniwa kwamba, hiyo *refund* siyo halali.

Mheshimiwa Spika, uamuzi ukifanyika kwamba, Serikali imeshinda, hauna unachokikusanya. Sanasana ni kwamba, haumlipi yule ambaye anawadai mumpe *refund*. Kwa hiyo, kuna wakati hesabu zinakuwa kubwa kuliko *actual amount* ambayo unaweza ukaikusanya. Hata juzi nilivyokutana na taasisi hizi mbili pamoja na *TRA*, nilielekeza wafanye *reconciliation* ya hizo *numbers* na tutaona kwenye Kamati yetu ya Bunge, ili hizi *figure* ziweze kueleweka.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, mashauri yaliyopo *TRAB* ni takribani shilingi trilioni 6.5 na shilingi trilioni 3.2 ni yale ambayo yalishaamuliwa, mengine yamekatiwa rufaa ambako kuna rufaa za takribani shilingi trilioni 2.6. Kwenye hizo, nilivyoongea na wenzetu wa Mamlaka ya Mapato, walisema takribani shilingi trilioni saba zilishakusanywa na mengine kama nilivyosema ni masuala ya *refund*. Kwa hiyo, hii ni hoja ya msingi, tumepokea na kwa sababu, iko kwenye taasisi za Serikali na inafanyiwa kazi, tumewaambia wafanye huo uoanishaji wa hizo takwimu na watakapokuwa wamekamilisha, sisi tuta-*share* na Kamati yetu ya Bajeti na itaingia kwenye Kumbukumbu Rasmi kwa kutumia utaratibu wetu wa Kamati ya Bunge inapotoa taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tumepokea hoja ambazo zilizotolewa na Kamati, tumepokea hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Martha Gwau ambayo inahusisha Wizara ya Fedha kuimarisha mifumo, hususan katika usimamizi wa mikopo, tumepokea. Hili ni moja ya ambalo tutalitolea pia, tamko tutakapokuja kwenye Hotuba Kubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni hoja ya msingi na kwa kweli, kwenye jambo hili, si tu wananchi wetu wa kada za vijijini ama wananchi wa kawaida, jambo hili linawakumba hata Watumishi wa Serikali, linawakumba hata watumishi walioko kwenye taasisi za kifedha zenyewe. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni kubwa na tunaamini tutalifanyia kazi, ili kuweza kuhakikisha tunaondoa hayo mapungufu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jonas Mbunda, tumepokea hoja yako ya mifumo ya kikodi. Vilevile tumepokea masuala aliyoyasema Mheshimiwa Charles Kimei na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, masuala aliyosema Mheshimiwa Ali King ya wastaafu kulipwa viwango vidogo tumeyapokea. Hoja hii ni kubwa, itafanyiwa kazi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephat Kandege, ameongelea Serikali kuchangamkia fursa za kukuza uchumi:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea jambo hilo na *potential* ambazo amesema zipo ndani ya *BOT* kununua dhahabu. Kuna hatua ya kikodi ambayo tunaendelea kushauriana, tutakapokuja kwenye hatua za kikodi na lenyewe ni moja ya jambo ambalo litajitokeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Leah Komanya ameongelea Ofisi ya *CAG*; Mheshimiwa Leah Komanya, kupitia mchango wako natoa tu taarifa kwamba, tangu Serikali ya Awamu ya Sita imeingia, Bajeti ya *CAG* imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kwa ongezeko kubwa tu. Ndiyo maana imetoka ile iliyokuwa takribani 97 na sasa ni mia naa. Mwaka juzi

ilikuwa kwenye 80 naa na sasa tumeipandisha. Tutaendelea kuipandisha kwa sababu, Mheshimiwa Rais anaamini kwenye masuala ya utawala bora na masuala ya usimamiaji wa fedha za walipakodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Mdee ameongelea jambo la uteuzi:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalijibu, nilishafanya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Mwenisongole ameongelea habari ya *TRA* kuhusu masuala ya *EFD*:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili tutalileta. Tutashauriana masuala ya *Finance Bill* na wenzetu wa Kamati ya Bajeti, tutakubaliana yale masuala ambayo tunahitaji yafanyiwe marekebisho na ya kwenye Sheria inayofuata tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili, naweka tu kumbukumbu sawa na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, hapa nchini, tunapokuwa tunajadiliana masuala ya kodi, mimi nawashauri sana tuache kujadili watu, tujadili kazi wanazofanya kwa sababu, kodi zinatozwa kwenye shughuli inayofanywa, kwenye faida inayopatikana kwenye shughuli inayofanywa. Haya masuala ya kwamba, huyu maskini, ni mambo *very subjective*, ni mambo ambayo ni magumu sana kusema huyu ndiye aliye maskini hasa, ni mambo magumu sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George alikuwa anasema kuna siku Serikali itatoza hata wafugaji. Hatujaomba Bunge lifanye hivyo, ila ukiniuliza maoni yangu, hata hao wanatakiwa watozwe, na sababu ninayo. Kwa sababu gani? Mimi nimetokea kwenye jamii ya kifugaji, lakini kuna baadhi ya wafugaji ambao utakuta ana ng'ombe 1,000, au 2,000, au 3,000, au 5,000, ama ng'ombe 10,000.

Mheshimiwa Spika, kwa utashi wangu ukiniambia kwamba nikachukue kodi ya Mwalimu wa Shule ya Msingi ili nikajenge josho

la mtu mwenye ng'ombe 10,000 kwa sababu eti mfugaji ni maskini, tutabishana mpaka asubuhi, sikubaliani nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ni mfumo unaosababisha mzigo wa kodi ubebwe na wachache kwa kigezo ambacho siyo halali. Tunataka bwawa la mifugo ya mtu mwenye ng'ombe 10,000 lichimbwe kwa kodi ya Nesi! Kuna mfanyakazi analipwa shilingi 300,000/=, ambayo kwa mwaka ni shilingi 3,600,000/=, anatozwa kodi. Halafu tunataka mtu ambaye akiuza mauzo yake akapata shilingi milioni 50, tumwache kwa sababu yeye ni mkulima, tumwache kwa sababu yeye ni mfugaji! Hii siyo haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutaki kuweka mzigo kwa watu ambao wanafanya shughuli za kimaendeleo utakaowafanya wawe masikini, lakini pia mzigo huo usimlemee mtu mmoja. Kwa mfano, zamani Serikali ilikuwa haitoi ruzuku kwa wakulima. Ilikuwa haitoi ruzuku ya mbolea, haitoi ruzuku kwenye mbegu, na ilikuwa haitoi fedha kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunajenga miradi ya umwagiliaji kwa kodi ambayo tumemtoza Mwalimu wa Shule ya Msingi. Tunajenga miradi ya mbegu kwa ajili ya wakulima kwa kodi ambayo tumemtoza Nesi anayepokea shilingi 300,000/=. Leo hii tunatoa ruzuku ya mbolea kwa zaidi ya shilingi bilioni 150, inaenda kwa mkulima. Fedha hiyo, tumekusanya kwa mfanyakazi hata mwenye kima cha chini ambaye analipwa shilingi 300,000/=.

Mheshimiwa Spika, leo hii utaniambiaje kwamba mtu anayeuza mazao akapata shilingi milioni 100, kwa sababu tu yametokana na sekta inaitwa kilimo, kwamba asitozwe, na kwamba tunasema huyo ni maskini, kwamba anayepata shilingi milioni 100 kwa mwaka, ni maskini kuliko anayepata shilingi 3,600,000? Hizi hesabu za wapi? Mimi *calculator* zote ninazotumia zinakataa kuniambia kwamba anayepokea shilingi 3,600,000 ni tajiri kuliko anayepokea shilingi milioni 200. Hii lazima tuiangalie upya kwa vigezo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitasema ukweli daima hata nisiwe maarufu, nitasema ukweli daima. Eeh, wakibaki wananiunga mkono mke wangu, wapigakura wa Iramba na mashabiki wa Yanga inatosha. Lazima niseme ukweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi sana ambalo Bunge lako Tukufu linatakiwa lijikite, ni kila Mtanzania alipe kodi stahiki. Mtu asibebeshwe mzigo asiouweza. Kila Mtanzania alipe kodi stahiki. Kwa sababu ni wajibu wa kila Mtanzania kuijenga nchi hii. Tutavutana mno kama kila mtu atakuwa anatetea kundi lake, kwamba mimi hili ndiyo kundi langu. Halafu unasema hili liondolewe kwenye kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii angalieni ninyi wenyewe, kwenye nchi ambayo ina zaidi ya miaka 60 tulikuwa na mwanafunzi amefaulu masomo yote, anakosa mkopo. Siyo msaada, anakosa mkopo wa kwenda kupata masomo yake, na ndoto yake inashia vile kwa sababu tu hajapata mkopo. Mheshimiwa Dkt. Samia amesema watoto wote wa Kitanzania wapate masomo yao. Tunawapelekaje? Yule ambaye ameshapata fursa angalau kidogo, tushikaneshikane watoto wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii barabara zimevurugika nchi nzima kwa sababu ya mvua. Tunahitaji tuzirejeshe barabara hizi ili wale wale wanaolima wapitishe mazao yao. Sasa niambieni, tutazirejesha barabara zilizoharibika kwa kutumia fedha ya nani? Yaani fedha ya kurejesha barabara zote zilizoharibika ili mazao ya mkulima yapite kwenye hizo Barabara, tutazitoa wapi fedha za aina hiyo? Ni lazima kila ambaye ana ahuweni ya kuchangia maendeleo ya nchi hii ni lazima achangie, tena achangie bila kubishana, Tuchangie bila kuvutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hii lugha ambayo huwa inatolewa Kodi za *TRA, TRA* wale wamepewa dhamana tu. Hizi fedha wanazokusanya haziendi kwenye familia zao, wanakusanya zinakwenda Benki Kuu. Zikitoka huko, ndiyo hizo hizo zinakwenda kwenye Barabara; ndiyo hizo hizo zinakwenda kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati mwingine ni basi tu kwa sababu ukiwa benchi la mbele hapa inabidi uwe msikilizaji zaidi na kupokea zaidi, huwa tunapokea hivyo hivyo, lakini kiukweli kukuta mtu anasema usikusanye hapa, usikusanye hapa, halafu mwishoni anasema jimboni kwangu fedha hazijafika, *it is a primary contradiction* ambayo kwa kweli tunatakiwa tutoke huko. Wenzetu ambao tunawaita wameendelea, wamehama kuhusu haya mambo ya kujadiliana jadiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaomba Bunge lako Tukufu uliwekee siku nyingi sana kujadiliana kuhusu sheria, ili tutakapokuwa tumepitisha sheria tusijadiliane kuhusu utekelezaji wake. Mimi sitabishana kama mtasema kuanzia leo hii kodi ilipwe na wafanyakazi peke yake. Mimi nitaenda kukusanya hao hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtasema kodi ilipwe na mtu anayepata kipato cha shilingi bilioni moja kwenda juu, mimi na watu wangu wa *TRA* tutaenda kukusanya hiyo hiyo, lakini kama tumetunga sheria kwamba yeyote anayestahili kulipa kodi na mimi nikiwa Waziri wa Fedha, yule ambaye anatajwa kulipwa kodi na sheria, nitasimamia, atalipa hiyo kodi ili tuweze kuwasaidia wale ambao wanatakiwa kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Waheshimiwa Wabunge nchi hii ni yote sote. Kwenye nchi hii hamna pande mbili. Nchi hii yote sisi ni Watanzania. Tunachotakiwa, tuwe na moyo wa uungwana, kwa sababu moyo wa uungwana unaongeza ujasiri, moyo wa uungwana unatia nguvu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninyi wenyewe ni mashihidi, na hii nitaisema tena kwa mtiririko mzuri. Katika kipindi hiki ambacho dunia nzima inapitia, ilikuwa inatosha kwa Rais wetu kuachana na baadhi ya miradi, na hata tusibishane kuhusu haya mambo ya fedha kwamba hapa haijafika, hapa haijafika. Pamoja na misukosuko yote hii ya kiuchumi duniani, hakuna mradi ambao umesimama, yote tunaendelea kutengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa limekamilika. Nakumbuka kila wakati umeme ulikuwa unakatika. Sasa bwawa limekamilika, mmeona hiyo *relief* ambayo tumeipata, masuala ya kukatikakatika umeme na kazi inaendelea zaidi. Mmeona majaribio ya reli yameshaanza, na baada ya miaka mingine miwili itatoka hapa Dodoma, labda itakuwa imeshafika Tabora, itatoka Tabora itakuwa imeshafika Mwanza na Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya aina hii yanapofanyika, tulitakiwa tutumie nguvu pia kumtia moyo Rais wetu kwamba Mheshimiwa Rais umefanya kazi kubwa katikati ya kipindi kigumu duniani. Ndiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuna wakati tunaongelea jambo la dola, kama vile dola imekosekana Tanzania peke yake. Dola siyo fedha ya Tanzania. Dola ni fedha ya kigeni, ni fedha ya nchi nyingine. Tunaipataje dola? Tunaipata dola kwa kuuza bidhaa nje, kwa kupata msaada, na kwa kufanya mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, angalia vitu tunavyouza nje, halafu uangalie kama Taifa miradi tunayoitekeleza hapa nchini. Utapataje hiyo *balance?* Hii ni hesabu ya kila mtu tu. Angalieni miradi tunayotekeleza kama Taifa. Hakuna nchi hapa kwenye *SADC* inatekeleza miradi mikubwa kwa mara moja kama Tanzania, wala hakuna nchi Afrika Mashariki, inatekeleza miradi mikubwa kama Tanzania.

Mheshimiwa Spiak, sasa niambieni tumeuza mazao kwenye dhahabu, tukauza kwenye kilimo, tukauza na baadhi ya wafanyabiasha mmoja mmoja, *and then* hizo ndiyo zilizoleta *inflow* ya dola *and then,* angalieni *materials* zinazoingizwa kwa ajili ya kujenga reli, kujenga Busisi, kujenga vituo vya afya kila Kata. Angalieni vile vitu ambavyo vinatumika kwenye miradi, vilivyotoka nje vyote havijanunuliwa kwa shilingi. Lazima pawe na *imbalance* kwenye hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafanyaje? Tumepitisha mkakati kama nilivyowaambia, linapotokea tatizo, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatafuta suluhisho. Tumepitisha mkakati

kwenye Baraza la Mawaziri na tunaenda kuanza kuutekeleza tarehe moja ambao unaleta suluhisho la kudumu *in long run* kuhusiana na haya masuala ya dola. Eh, dola siyo fedha yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine, tumepitisha sheria ya kuweza kuwapa miradi wakandarasi wazawa. Hii nitatoa rai, nitaweka msisitizo kwenye hotuba kuu. Sasa wakati mwingine miradi mingi tunawapa wageni, halafu hata kama tulikopa fedha, wale wanapeka kule, wanalipa wakandarasi wazawa kwa fedha ya shilingi, halafu baadaye tunasema dola imepotea. Sasa kama ilitoka nje na ikaenda nje, unatarajiaje iwepo?

Mheshimiwa Spika, siyo hiyo tu, pia kila kitu tunataka kufanya manunuzi kwa dola…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika tatu malizia…

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi. Tunataka tufanye manunuzi hayo kwa dola. Tunatengeneza *pressure* ya dola kuwa kubwa kuliko ya shilingi. Haya nitayatolea mwongozo pale nitakaposoma Bajeti Kuu ya Serikali. *Otherwise* tumepokea hoja vizuri kwa Waheshimiwa Wabunge, tutazifanyia kazi zile ambazo ni ushauri.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tupitishieni bajeti hii na tutakapokuja kwenye Bajeti Kuu ya Serikali tutapata fursa ya siku nyingi kupokea ushauri, na pia tutapata fursa nzuri ya kupokea maoni yenu na maelekezo yenu na kujadili yale ambayo ni ya kisheria. Leo hii ni bajeti ya ndani ya Wizara ambayo inahusisha mafungu yalioko ndani ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nikiwa namalizia huku nikimtakia heri ya kuzaliwa mke wangu ambaye amezaliwa tarehe kama leo, nipitishieni tu hii bajeti, ipite ili msiharibu sherehe yangu ambayo ipo na nilikuwa nadhani baada ya kazi kubwa ya mwaka mzima, leo hii ndiyo napata shamra shamra. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liliridhie kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 18.17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu nane ya kibajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kifungu1001 – *Administration and Human Resources Management*…….....................………Sh.13, 517,950,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri. Hapa ninayo majina ya Wabunge ambao wanahitaji ufafanuzi kwa mujibu wa Kanuni zetu. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kweli nashindwa hata kuongea kwa kuona Waziri wetu wa fedha anavyocheza na maisha ya Watanzania. Niliongea hapa mapema kuhusu utaratibu wa *TRA* kuamua

kuwatoza wakulima wadogo wadogo kupitia vyama vya msingi kuwalazimisha kutumia mashine za *EFD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi mashine ziko kisheria. Anayetumia mashine ya *EFD* lazima awe na leseni, lazima awe na *TIN Number.* Wakulima wale wadogo wadogo ambao Serikali hii ya CCM imewataka waungane; huyu mwenye gunia tano, mwenye gunia saba, na mwenye gunia kumi waungane kwa pamoja ili wapeleke mazao yao mnadani, leo wewe unawachukulia wale kama wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, Mheshimiwa Waziri analipotosha Bunge kusema kwamba ni sheria. Sheria gani? Bunge lipi lililopitisha? Labda Bunge la mwaka 2019 kwenda nyuma ambalo mimi sikuwa Mbunge, lakini mimi vikao vyote vya Bunge nimehudhuria, hakuna tulichopitisha kumtoza mkulima. Tulichosema, atozwe mfanyabiashara anayezalisha zaidi ya shilingi milioni kumi. Sasa yule sio mfanyabiashara. Ndiyo hapo Waziri anaposhindwa kunielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule ni mkulima na ndiyo maana hana leseni ya biashara, hana *Tin-Number.* Sasa leo unapolazimisha na kusema kwamba Mbunge anataka wakulima wasitozwe kodi, siyo kweli na sijui ni kwa nini Mheshimiwa Waziri anashindwa kunielewa. Wale ni wakulima wadogo ambao hawana msaada na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amewahurumia amewapa ruzuku ya mbegu, ruzuku ya mbolea kuwasaidia. Sasa wewe unataka kuwaongezea. Shida ya Waziri wetu, hapendi kuona mkulima anafaidika na mazao yake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaposema mtu akiuza kwa shilingi milioni 100, hakuna mkulima mmoja mmoja anayefanya hivyo. Mimi nazungumzia vile vyama vya msingi vile vya chini kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoomba, Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina, kwa nini *TRA*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, subiri kidogo ili tuwe tunaelewana vizuri.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI,** Mheshimiwa sifa za mkulima kujiunga kwenye Chama cha Msingi.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima wawe maeneo ya jirani, wanakaa pamoja.

**MWENYEKITI:** Ehe, nyingine.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awe mkulima…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, vyama vya msingi vinaundwa na wakulima wa aina gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya msingi ama *AMCOS* ni muunganiko wa wakulima wadogo ambao wanaanzia idadi ya wakulima 20. Wanapokutana pamoja wanasajili chama cha msingi. Vyama hivi vya msingi vikiwa kwa idadi maalum kama vyama 20, 25, 30 mpaka 100, vinaungana vinatengeneza kitu tunaita *union,* chama kikuu cha ushirika.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa nimemwingiza hapa Waziri wa Kilimo kwa sababu wakati wa bajeti yake, hili jambo tulisema litakuja chini ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu *TRA* wako chini yake.

Sasa nataka nielewe ili jambo hili liende vizuri. Haya, sasa Mheshimiwa Waziri hawa 20, 25 wanaojiunga, lile takwa la wao kuwa na *EFD* ni kama chama kiwe na *EFD* au yule mkulima mdogo mmoja mmoja awe na *EFD?* Lile takwa la kuwa na *EFD* ni yule mkulima mmoja mmoja kwenye *AMCOS* au ni ile *AMCOS* ndiyo iwe na *EFD? (Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeuliza swali zuri sana kwa ajili ya kutoa *guidance* ndani ya Bunge na tulikubaliana mimi na Waziri wa Fedha kwamba kama itatokea hii hoja, nitaitolea maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, takwa la kisheria linalokitaka chama cha ushirika kuwa na mashine ya *EFD* ni chama chochote cha ushirika kinachofanya biashara. Tuna vyama vya ushirika; unakuta ni chama cha ushirika, nitoe mfano kwa jina. Mfano, Chama cha Ushirika cha *KACU* ama Chama cha Ushirika cha *KDCU* ambacho kina *wing* ya kufanya biashara, kwa hiyo, kwenye ile *component* ya kufanya biashara kitatakiwa kutimiza matakwa ya kibiashara kwa maana kuwa na *business license*, kwa maana ya kuwa na *TIN* na *ku-adhere* kwenye ule utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo chama cha msingi kinachofanya kazi ya *aggregation,* kukusanya tu mazao ya wakulima, ambacho hakifanyi shughuli yoyote ya *trade*, hiki chama cha ushirika hakitakiwi kuwa na *business license* wala hakitakiwi kuwa…

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge ngojeni. Kwa hiyo, hivi vyama vya msingi kimoja kimoja, kwa sababu vile vinafanya kazi ya kukusanya, mkusanyiko wake kule juu ndio kitakuja Chama cha Ushirika. Maana yake hoja ya Mheshimiwa Mbunge hazungumzii Chama cha Ushirika ambayo ngazi ile tayari kuna biashara, anazungumzia hii ngazi ya chini ambayo sasa hawa ni wale wakulima ambao wako 20 kwenye kundi hili. *(Makofi)*

Kwa maelezo uliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ni kwamba, huyu anayedaiwa leseni ya biashara, atakayetakiwa kutumia *TIN* na atakayetakiwa kutumia *EFD machine* ni kile cha juu pale ambavyo ni vidogo vidogo vimejiunga pamoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, kwanza sheria ya ushirika ipo wazi na ndio inayo-*guide* namna ya kuunda vyama vya msingi na chama kikuu. Kwenye Taifa letu hili tuna

aina mbili za vyama vikuu vya ushirika. Vipo vyama vikuu vya ushirika ambavyo vinafanya kazi mbili. Wana kiwanda cha kuchakata pamba, lakini wakati huo huo wanakusanya mazao ya wakulima. Kwa hiyo, kwenye *component* ya *trading* ya ku-*run* kiwanda wana-*fall* kwenye eneo lile. Anachokiongelea Mheshimiwa Mbunge kama nimemwelewa vizuri ni kwamba, hoja yake inazungumzia wakulima wadogo ambao wameunganika katika chama cha msingi kutozwa kodi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa, hili la kutozwa kodi labda tutampa nafasi, lakini hoja yake tangu asubuhi ni ya kudaiwa kutumia *EFD* ambayo kimsingi ndio kodi yenyewe. Yeye anasema huyu mdogo ukimdai ile *EFD machine,* kwa maelezo uliyotoa mwenyewe huyu sio mfanyabiashara, yeye si wanakusanya pamoja kama nimeelewa vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo *right*.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu kama akipeleka mazao sokoni, nafikiri huwa analipa ushuru. Kama akipeleka mwenyewe sokoni analipa ushuru. Kama akileta huku kwenye chama, ndio wanafuata sasa kale kautaratibu kadogo huko juu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakulima wadogo wakipeleka kwenye *AMCOS* mazao yao yakiuziwa pale, wanalipa ushuru ambao upo kwenye halmashauri zao. Sasa *EFD… (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa wanalipa ushuru, sasa nataka nielewe, pale pale hawa *AMCOS* moja ilipopeleka, hii moja ndio inayotakiwa kuwa na *EFD?*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Hapana. Mheshimiwa George hoja yako ipo wapi? *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe anajua ukweli ila anaogopa kunyoosha tu

maelezo, lakini kiuhalisia, nazungumzia wakulima wale wadogo wadogo ambao wamekusanya mazao yao. *Transaction* yao wanafanya *once a year* wanapeleka mnadani. Akishachukua zile fedha anakwenda kulipia ada watoto, kununua mbolea, sio kwenye biashara.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Mbunge ngoja tunyooshe vizuri, twende kwenye hoja tunyooke nayo, tukianza huku kwenye matumizi ya baada ya kulipa ushuru anatumia nini, kuna mwingine anaweza kwenda kuongeza mke wa pili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mbunge wewe hoja yako ni kwenye *AMCOS* ile ndogo kudaiwa kutumia *EFD?* Tuachane na haya mengineyo ili nielewe hoja yako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anasema, huyu siye anayedaiwa kutumiwa *EFD*.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachotokea huyu ndiye anayeambiwa atumie *EFD* na wanalazimishwa kununua Mashine ya *EFD*.

**MWENYEKITI:** Sasa hapo nadhani hoja tumeielewa. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo umeelewa hoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha pia umeelewa hoja?

Utaratibu wetu ama sheria yetu haimtaki yule *AMCOS* wa chini kudaiwa kutumia *EFD*. Hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, *either* kule kwake ama wakulima ambao yeye amekutana nao wamemwambia sisi *AMCOS* ndogo hivi kwa nini tunadaiwa *EFD?*

Sasa, hili ni jambo ambalo zaidi ni la utekelezaji kuliko kuwa ni hoja ambayo Bunge linatakiwa pengine lifanye maamuzi kwa sababu kama huo ndio msimamo, maana yake huko kuna

makosa ambayo yamefanyika ambayo yanaweza kurekebika kwa utendaji wa kawaida tu.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Mbozi tu, ni nchi nzima hii kampeni inaendelea. Wamekwenda kwa wakulima wa tumbaku na ufuta kila mahali, vyama vya msingi vya ushirika wanatakiwa watumie *EFD*.

**MWENYEKITI:** Haya wale wenye Vyama vya *AMCOS* huko Mbunge mwingine ukiacha Mheshimiwa George. Mwingine ambaye *AMCOS* yake huko wamedaiwa kutumia *EFD* ni wapi? Hakuna. *(Makofi)*

Sawa, hawajafuatilia? Nani? Haya ngoja, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa uzoefu nataka Bunge lijue mimi nimekuwa *Manager* wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala kwa miaka tisa, nikiwa kama *Manager* Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Sheria ya Ushirika au *TRA* inaitaka chama cha msingi chenye mapato yake zaidi ya milioni 50 kiwe kinalipa kodi. Hiyo ni sheria inataka hivyo, kwa maana gani? Vyama vya msingi wakati mwingine vinafanya biashara, vina magari, vinaagiza bidhaa na vinauza bidhaa mbalimbali. Kutokana na mapato hayo yakifikisha milioni 50 wanatakiwa lazima walipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawalipi kodi kutokana na mazao ya mkulima anayekusanya kwenye maghala. Pia kwa kipindi hiki kifupi, nimepata hayo malalamiko, ni kweli yapo. *TRA* wameandika barua kwa Maafisa Ushirika (Mrajisi wa Mkoa) wakiwaelekeza kwamba, vyama vinatakiwa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria. Sasa, kwa kuwa tafsiri ya vyama vyetu hawa maafisa wanashindwa kutafsiri sheria ile inavyozungumza na wao wanasukuma kama ilivyo, wanalazimisha vyama vilipe kodi, lakini wanapaswa kulipa kodi kama mapato yake yanazidi shilingi milioni 50, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, kwa hiyo masharti ni mawili. Moja, *AMCOS* iwe inafanya biashara. Pili, kiasi kiwe kimezidi hicho alichotaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa George kwako ipo tofauti?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui *AMCOS* zinazofanya biashara, kwangu zinakusanya mazao zinapeleka mnadani. Sasa kama zinafanya biashara, mimi mwenyewe binafsi ni Mwanachama wa *AMCOS* wa chama cha msingi kwenye kijiji changu.

**MWENYEKITI:** Kule kule mnadani sawa, sasa nataka nielewe. *AMCOS* imekusanya mazao, ikapeleka mnadani inapata kiasi gani *AMCOS* hii ambayo labda tuchukue mfano mmojawapo ambao wewe umo?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tena kwa masikitizo siyo kwamba ukipeleka mnadani unalipwa leo, unasubiri tena miezi mitatu, minne.

**MWENYEKITI:** Ni sawa, lakini unapata kiasi gani?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inategemeana na msimu wa mavuno ukoje, inaweza ikawa milioni 40 au 50.

**MWENYEKITI:** Sasa, zikishafika milioni 50 jibu ndio lile pale lazima na wewe ulipe kodi. Kwa nini? Umefanya biashara. *(Makofi)*

Sasa, nadhani Waheshimiwa Wabunge hoja ya msingi imeeleweka na asubuhi kwa sababu hoja hii pamoja na mambo mengine, nilisema Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Kamati yetu ya Bajeti itazame kama kuna mahali ambako kisheria tumefanya makosa, lakini kwa maelezo waliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge hawa wawili na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na kwa sehemu ufafanuzi alioutoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akihitimisha hoja hapa, nadhani tumeelewana kama yapo

makosa ni makosa ya kiutendaji kwa maana ya kwamba, wamedaiwa wale wasiostahili. *(Makofi)*

Kama ni makosa ya kiutendaji ni marekebisho ambayo kwa kweli Mheshimiwa Waziri anaweza kwenda kukaa na taasisi zake huko na kuwaelekeza ule utaratibu unavyopaswa kuwa. Kwa maelezo haya sina hakika sana.

Mheshimiwa Cherehani unataka kusema jambo?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Mbunge pale kwamba, wakulima wa pamba au tumbaku wanalima mkulima mmoja mmoja kupitia *AMCOS* yao. Wanaanza kulima mwezi Oktoba, ikifika mwezi Machi au Aprili, wanaanza kupeleka pamba au mazao yao kwenye *AMCOS* yao ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanapofika kule kila mkulima ana namba yake, mbolea na pembejeo nyingine alizotumia. Siku ile ya mnada ya kuuza, kila mkulima anauza anakatwa deni lake. Fedha zinazolipwa na Kampuni inayonunua kwenye *AMCOS* zile fedha, unaweza ukakuta *AMCOS* ina milioni 200, lakini siyo za *AMCOS* ni za mkulima yule mmoja mmoja mdogo mwenye 200,000 au 300,000 au 800,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *AMCOS* inakuja kwenye zile fedha inapokusanya kuna hela 3% zinaenda halmashauri kama ushuru ambao inalipwa halmashauri. Kwa hiyo, mkulima anaondoka na 500,000 yake, chama cha msingi kinabakiwa na ushuru wake sasa ambao unakuta kimebaki na shilingi 8,000,000.

**MWENYEKITI:** Sawa anayedaiwa hapo ili awe na *EFD* ni yupi?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anayedaiwa kuwa na mashine, mimi sasa ningekuwa nashauri alitakiwa ni Chama Kikuu cha Ushirika ambacho kinafanya aidha biashara…

**MWENYEKITI:** Huku chini kwenye *AMCOS* umeshasema zinaweza kuwa milioni 200 halafu watu wakawa wanagawana 200,000 kila mmoja. Kwa mfano wamegwana shilingi 3,000,000 kila mmoja?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mwenye shilingi 3,000,000 au 2,000,000 ni yule ambaye kidogo ni mkulima mkubwa ambaye fedha hizi na yeye ndiyo anaondoka nazo kwa ajili ya shughuli zake au maboresho ya kilimo.

**MWENYEKITI:** Sasa hata Mheshimiwa Waziri ametoa mfano hapa, hata mwalimu na yeye akilipwa si anaenda na shughuli zake?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo lakini nikuombe, suala hili kwa sababu Waziri wa Fedha na Kilimo wapo, tungepata semina. Wakapata semina kupitia Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Wakurugenzi wa Bodi za Mazao…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Nani anayestahili semina?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa, wapewe semina.

**MWENYEKITI:** Sawa, wakulima. Haya ngoja tumalize hoja yetu hapa, ukitupeleka tena kwenye semina huko tunatoka nje ya mada, utakuwa wa mwisho kuzungumza.

Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mawili ambayo bado hayajaeleweka. Mheshimiwa Mpakate alikuwa akisema kwenye Chama cha Msingi *AMCOS*.

Kama *AMCOS* inafanya biashara inayofikia milioni 50 ndio inayopaswa kulipiwa kodi, lakini siyo fedha za mazao zile zinazokusanywa na wakulima. Kama wakulima wanakusanya mazao yao yafike 200,000 hawatakiwi kutumia hiyo *EFD machine* kwa sababu tayari yale mazao yalishalipiwa ushuru kwenye *AMCOS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo ukiwaambia tena wawe na *EFD machine* unakuwa una…

**MWENYEKITI:** Ngoja hapo hapo. Huo ushuru inayokusanya *AMCOS* ni ushuru wa *AMCOS* au ni ushuru wa Serikali?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wake mpaka Serikalini unaenda.

**MWENYEKITI:** Mpaka Serikalini?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mpaka Serikalini.

**MWENYEKITI:** Ile *AMCOS* inavyobaki na hizo fedha ilizozikusanya. Tuseme zinabaki milioni 20, hiyo *AMCOS* inapaswa kulipa kodi ama hapana?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana hailipiwi kodi. Inayolipiwa kodi kama wamenunua gari, wamejenga ghala, labda wanafanya biashara ya kukamua mafuta. Kwa hiyo, biashara ile ikizidi milioni 50 wanatakiwa walipe kodi.

**MWENYEKITI:** Sasa hapo kuna tofauti gani na maelezo yale niliyoyatoa ya kuhitimisha jambo hili? Kuna tofauti?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na maana kwamba, siyo wakiuza mazao kama hawafanyi biashara wakiuza mazao yasipofika milioni 50 walipe kodi. Siyo sawa. Kama *AMCOS* haifanyi biashara kukusanya mazao tu peke yake…

**MWENYEKITI:** Sasa haya ndio mambo ambayo mtakubaliana nami nimesema yaende Kamati ya Bajeti ili wapate nafasi ya kuyajadili kwa upana. Ni muhimu kwa sababu ukisema huyu ambaye anapata milioni 20 hata kama amepata hatakiwi kulipa kodi. Muuza mitumba ana mtaji wa 20,000. Jamani nadhani tuiache Kamati ya Bajeti ikafanye kazi, itatuletea ushauri hapa ndani namna bora ya kukusanya hizi kodi na namna bora kwa kweli…

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Sijui ni wapi amesimama?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani mimi siyo Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, lakini naomba siku hiyo ikikutana na mimi niruhusiwe kuhudhuria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hizi hoja zote zilizopelekwa kule Kamati ya Bajeti, tutakapoanza hiyo kazi kesho Wenyeviti wa Kamati zetu za Kudumu za Bunge wote wanakuwa ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti.

Sasa, Mheshimiwa Mbunge namna unavyoisema kama vile Kamati ya Bajeti wanaweza kuwa hakuna mtu hata mmoja ambaye anajua jambo hili. Kwa maana ya kuhudhuria Mbunge unaruhusiwa kuhudhuria, lakini siyo kama mjumbe. Ni tofauti na Wenyeviti watakavyokuwa wanahudhuria na utakavyohudhuria usinanii, kule unaruhusiwa kusema lakini huruhusiwi kupiga kura, kama itafikia kwenye kupiga kura. Kwa hiyo, lazima niliweke vizuri maana asije akachukua *show* ya siku nzima. Sasa Kamati hatafanya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti nadhani umesikiliza hapa Hoja za Wajumbe. Kama kuna mahali popote ambapo tunatakiwa tufanye marekebisho basi kamati yetu kwa sababu Serikali pia itakuwepo huko mtashauriana vizuri, ili Bunge lifikie kwenye maamuzi ambayo kwa kweli tusaidiane kwa sababu hizi huduma zinazopelekwa huko zinatusaidia sisi sote, wakati huo huo

pia mkulima lazima na yeye apate faida, ili aendelee kulima na wengine tuendelee kupata chakula. Kwa hivyo, vyote lazima viende kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, haya mwingine aliyetaka ufafanuzi hapa ni Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia, nilisema kwamba, taarifa ya mwaka jana ilionesha kwamba kuna miamala shuku ya trilioni 280. Nikatarajia kwamba, kwenye taarifa hii Waziri wa Fedha ataeleza kwa kina hizo trilioni 280 baada ya uchambuzi zilitengenezwa taarifa fiche ngapi zenye thamani ya shilingi ngapi na hatua gani ambayo imechukuliwa na Serikali hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia la pili, Waziri ameeleza hapa…

**MWENYEKITI:** Ni kwenye miamala shuku hiyo hiyo au ni hoja nyingine?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Hapo hapo kwenye miamala shuku.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha ameeleza hapa kwamba mipango mikakati iliyowekwa na Timu ya *FIU* ilikuwa ni 21. Iliyoshughulikiwa mpaka sasa hivi ni mipango mikakati mitano (5) tu. Kwa hiyo, ndio maana nikasema tupo kwenye *risk* kubwa sana ya kuingia kule kwenye uangalizi. Hapa Mheshimiwa Waziri aliposimama yeye alisema kwamba zilikuwa 25 na amezifanyia kazi zote. Sasa kama Mheshimiwa Waziri alisema hayo kwa bahati mbaya, labda asahihishe kauli yake na atueleze nini sababu ya Serikali kutolitilia jambo hili maanani, kwa sababu ufaulishaji huu wa miamala shuku au utakatishaji wa fedha kwenye nchi hii na nilisema kwamba, kama kuna utoroshaji mkubwa hivi wa fedha, kama kuna…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina unajua unatumia maneno makubwa makubwa, mazito mazito. Hapo umeingia, kwanza umeanza na miamala shuku, umefuata utoroshaji wa fedha, sasa hivi utakatishaji wa fedha. Jielekeze kwenye moja ili tunyooke nalo. Unazungumzia kipi?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yameambatana hivyo hivyo kwa sababu ni jambo moja, hayatenganishiki. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, nasema hivyo kwa sababu pamoja na kwamba mimi siyo mtaalam, lakini humu ndani tuliwahi kuelezwa na Mheshimiwa Dkt. Kimei Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakumbuka. Alieleza kwa kirefu kabisa miamala shuku maana yake ni nini. Sasa, tukichanganya miamala shuku na kila kitu humo ndani naona kama vile hoja yetu inaweza ikawa kidogo shida kuijadili kwenye ngazi hii ya Mshahara wa Waziri.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nisaidie kidogo Bunge lako. Ni kwamba *FIU* inapokea taarifa shuku, ikishazipokea inazifanyia mchakato…

**MWENYEKITI:** Taarifa shuku au miamala shuku? Au vyote vinamaanisha sawa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya miamala shuku. *FIU* wanapokea taarifa ya miamala shuku ambayo ni *suspicious transactions.* Ikishazipokea, inazichakata kwa *level* yake, ikishamaliza kuzichakata ina-*establish* taarifa fiche. Hiyo tarifa fiche inapelekwa sasa kwenye mamlaka za uchunguzi labda *DCI, PCCB* au *DPP* kwa ajili ya hatua nyingine za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu sasa…

**MWENYEKITI:** Sawa umeshaeleweka unataka ufafanuzi gani kutoka kwa Mheshimiwa Waziri?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ninaoutaka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, sisi kama Taifa tulishawekwa, tupo kwenye hatihati ya kuwekwa kwenye uangalizi wa *FATF*. Tulishakuwa kwenye uangalizi wa *FATF* nimesema madhara yake, lakini sioni mikakati ya Serikali iliyowekwa kutoka pale kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Haya ngoja. Mheshimiwa Waziri, Mbunge anataka ufafanuzi wa mikakati ya Serikali kwenye kushughulikia mambo haya.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweke kumbukumbu sawa, pale niliposema 25 ni mpango kazi unaishia mwaka 2020 – 2025 lakini vigezo vilivyowekwa vilikuwa 21 na ambavyo vimeshafanyiwa kazi Mheshimiwa Mbunge amesema vitano, siyo vitano ni 12. Kwa hiyo ndiyo maana nilisema tukiwa pale kwamba tumeshavuka hata hiyo nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango kazi ambao tumeuweka ulianzia kufanya marekebisho ya kimuundo ya kitaasisi ambapo ndiyo tumesema tumefanya marekebisho hapa hapa kwenye Bunge lako Tukufu na kanuni tulishazifanyia maandalizi na zilishakamilika kwa pande zote za Muungano. Hata maoni mengine Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanatoa ilikuwa ni pamoja na kuifanya taasisi yetu hii isimame kwa kujitegemea. Hili jambo tumeshajadiliana ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yalikuwa yanahusisha kuwa na watumishi wa kudumu; jambo hilo linaendelea kufanyiwa kazi. Tumeshakaa ngazi ya Serikali; watapata watumishi kwa sababu walikuwa na uhaba pia wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ilikuwa ni hatua kuchukuliwa zinazohusisha masuala haya yanayohusisha masuala ya mihimili mingine ya kisheria. Kama unavyojua, haya masuala ya Mhimili mwingine ambao ni Mahakama hayaamrishwi na Waziri, kwa hiyo hayo tunaendelea ku-*improve* kama nchi. Ninadhani unaziona taarifa ambazo nchi yetu inapiga hatua

kuhusu uchukuaji wa hatua, iwe kwenye masuala ya kudhibiti masuala ya *money laundering* au masuala ya kigaidi pamoja na hayo mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge lako Tukufu, kwa hiyo, Serikali imechukua hatua na vipengele nimevitaja kwenye huo mtiririko. Vimeshabaki hivi vilivyosalia ambavyo na vyenyewe tunaendelea navyo lakini tumeshavuka nusu kwenye hivyo na kwenye kikao cha mwisho, *indication* tumeshapiga hatua tofauti na tulikotoka kule mwanzo ambako tulikuwa na hali mbaya na hiyo ni *some years*, *2020/2021*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu Wabunge wenzangu waniunge mkono tulijadili hili jambo kwa sababu ya hoja mbili.

**MWENYEKITI:** Haya, toa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja mbili zile; moja, Kamati inasema ...

**MWENYEKITI:** Toa hoja; umeshaeleza mwanzo Mheshimiwa. Toa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaeleza.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninaomba mniunge mkono, Bunge zima li-*support* ili tujadili tumalize.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja haijaungwa mkono; wamesimama watu watatu. *(Makofi)*

Jina lingine la Mbunge anayetaka ufafanuzi ni Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba ufafanuzi kuhusiana na mashauri ya kikodi ambayo yamezungumzwa na Kamati yako ya Bunge na kuna vyombo vitatu vinavyohusiana na mashauri haya: kuna Mahakama ya Rufaa, kwa mantiki ya mfumo wa Kimahakama, kuna Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi na kuna Bodi ya Rufaa ya Mapato ya Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi kwa sababu hili ni jambo ambalo Bunge lilishalizungumzia toka mwaka 2022 na kwa takwimu za kifedha imeongezeka kutoka shilingi trilioni tano mpaka shilingi trilioni 10. Kamati yako imezungumza na Kamati ya Bajeti ni miongoni mwa Kamati ambazo zinafanya kazi wakati *Sessions* za Bunge zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Kamati ya Bajeti asubuhi hii imetuambia kwenye eneo la wajumbe wa mikoani, mikoa 12 ilikuwa haijateuliwa wajumbe. Waziri kupitia Naibu Waziri na yeye mwenyewe anatuambia mikoa 10 wameshaiteua na Waziri ameenda mbele zaidi kusema kwamba na barua wameshapewa. Sasa ninapata mkanganyiko kwamba, kile ambacho Kamati ya Bajeti ambayo inakutana mpaka kipindi hiki cha Bunge imeliambia Bunge hili *as against* kinachosemwa na Waziri na mwenzake, kipi kina ukweli? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo linahusiana na hoja hii hii, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo Kamati ya Bajeti imemrejea inasema; "Sababu ya ucheleweshwaji wa maamuzi wa mashauri ya rufaa ni pamoja na kutokufanywa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi wa Mikoa isiyo na Wajumbe, ..." hilo la kwanza; "Kutoteua kwa haraka Wajumbe, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti na uhaba wa bajeti wa Mahakama za Rufaa za Kodi." Sasa haya ni maeneo ambayo yamechangia kwa kiwango kikubwa kwa fedha kuongezeka kwa 100% na mambo haya kutokufanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Sawa, sekunde 30 hoja yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni moja tu kwa Mheshimiwa Waziri. Je, haya maelezo ambayo Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ndiyo rejea yetu, ndiyo rejea yetu kwa sababu taarifa zake zimekuwa *verified* kwamba, haya maeneo manne ambayo watu hawajateuliwa ndiyo kikwazo. Je, kwa kauli yako wewe, mmeyakamilisha kwa 100% ili hii hoja ya Bunge ambayo imekuwa kiporo kwa miaka zaidi ya miwili iende ikatafutiwe ufumbuzi kwa 100%? Usiponijibu kwa ufanisi nitatoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akitoa ufafanuzi amesema mikoa iliyokuwa imesalia ile 12 mmeshateua 10, kwa hiyo bado miwili. Sawa.

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Mbunge anasema Taarifa ya *CAG*; sasa mimi ninataka nipate ufafanuzi kutoka kwake halafu ninyi ndiyo mtoe ufafanuzi.

Mheshimiwa Halima, *CAG* taarifa yake inayosema hivyo ni ya lini?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekii, taarifa iliyotoka Mwezi Machi 2024 ambayo ndiyo jicho la Bunge ikitekelezwa ndiyo anaenda kufanya *verification*.

**MWENYEKITI:** Mwezi Machi. Kwa hiyo mwaka ule wa *cycle* nyingine, sawa. Kama ndivyo na taarifa hii ya uteuzi imetoka leo, labda uteuzi umefanywa leo.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa Halima kwamba *CAG* aliandika vile na ni kweli walichoandika Kamati ya Bajeti ni kitu sahihi. Isipokuwa labda niombe radhi, utaratibu wa Kiserikali nao hauwi hivyo, kwamba sikuwaandikia barua lakini nimefanya uteuzi tarehe 21 Mei, mwezi jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu taarifa huwa zinaletwa kwako ukiagiza ninakuletea tu na majina yote yako hapa ninayo lakini nimeteua mwezi jana.

Kwa hiyo, ni kweli *CAG* alishandika na ni kweli taarifa ya Kamati ilikuwa inaendelea na sijawajulisha kwa barua kwamba nimeshateua lakini nilishateua na majina yote hayo ninayo na barua walishapokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, ninafikiri Mheshimiwa Halima pamoja na mambo mengine, bado Bunge linayo nafasi ya kupata hizi taarifa kutoka kwa *CAG*. Kwa sababu utekelezaji wa yale anayokuwa ameyasema, Serikali ikishafanya inampelekea taarifa *CAG* halafu inarejea tena kwetu Bungeni kutuambia kwamba wamefikia wapi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninafikiri kwenye kwenye hoja hii, Mheshimiwa Waziri hapa amesema ameshafanya na uzuri kwa kufanya kwake ninamini hukupata nafasi ya kutujulisha sisi kama Bunge, lakini *CAG* utakuwa umeshamjulisha kwa kujibu hoja zake na hayo majibu kwa sababu yatakuja kwenye zile Kamati zetu za *PAC* na *LAAC*, tutapata taarifa za uhakika zaidi huko kwa sababu yeye atajiridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima, ninadhani umejiridhika na haya.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yeah*!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda niliokuwa nimeongeza wa nusu saa bado dakika chache kwisha, kwa hivyo tunasoma mafungu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..……. Sh. 13,517,950,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*............Sh. 1,983,679,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…........................Sh. 101,170,858,000
Kifungu 1004 – *Legal services unit* ……....................Sh. 2,209,992,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*.....................................................Sh. 1,833,276,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…..........................Sh. 1,437,340,000
Kifungu 1007 – *MCC Tanzania* ………………………Sh. 2,076,065,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*…...Sh.2,498,504,000
Kifungu 1011 – *Monitoring and Evaluation Unit*........Sh.2,500,000,000
Kifungu 3001 – *Internal Auditor General*………..............................Sh. 0
Kifungu 5001 – *Government Asset Management Division*………………..……..…..Sh. 9,857,404,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*……………....……..……..Sh.10,536,383,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 01 – Deni la Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration*….…………....sh. 13,131,838,005,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 06 – Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

Kifungu 2001 – *Quality Assurance*……….......…....Sh. 1,567,750,000
Kifungu 2002 – *Technical Audit*……........................Sh. 2,188,530,000
Kifungu 2003 – *Local Government Authorities Audit*...............................Sh.1,627,140,000

Kifungu 2004 – *Ministries, Independent Departments and Audit*……….....…………………Sh. 2,165,330,000
Kifungu 2005 – *Risk Management Systems and Controls*......................................Sh. 817,548,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Business Support Division*…….....….Sh. 2,714,784,000
Kifungu 1002 – *Internal Audit Unit* ………....................….Sh. 188,310,000
Kifungu 1003 – *Finance and Accounts Unit*…………....Sh. 372,700,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit* ……..........................….Sh. 60,860,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……...Sh. 206,540,000
Kifungu 2001 – *Technical Department*……...............….Sh. 663,570,000
Kifungu 2002 – *Zanzibar Office*……..............................…….Sh. 201,550,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*……...................…….Sh. 1,863,941,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……...…….Sh. 72,830,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*…….........................…….Sh. 14,450,000
Kifungu 1004 – *Monitoring and Analysis Unit*………….Sh. 324,180,000
Kifungu 1005 – *Compliance Unit* …...........................……….Sh. 268,520,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*………Sh. 41,870,000
Kifungu 1007 – *Legal and International Coordination Unit*……...........................……..................Sh. 874,666,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……..............................….Sh. 169,740,000
Kifungu 1009 – *Planning Unit*……….........…….....…....Sh. 138,040,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 21 – Hazina**

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Fungu la 21 kuna *addendum*, kwa hiyo sasa litasoma ni shilingi trilioni 1,635,427,521,000.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatujapata taarifa kutoka kwenye Kamati kama kulikuwa na changamoto yoyote ya haya mabadiliko ya fedha. Mheshimiwa Waziri, mabadiliko haya yalishapita kwenye Kamati? Hii *addendum* ilipita kwenye Kamati ya Bajeti?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haujasikika. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu tusomee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu**

**MWENYEKITI:** Ngoja ngoja ngoja, Hazina bado hatujawahoji Wabunge.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 21 – Hazina**

Kifungu 1002 –*Finance and Accounts Unit*…………Sh. 2,128,526,000
Kifungu 1003 – *Finance and Accounts – Debts Services*………………………………………….Sh. 700,000,000
Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPP)*………………………………………….Sh. 2,238,826,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*…….Sh. 701,571,730,150

Kifungu 2002 – *Policy Analysis Division* ..................Sh. 837,354,480,580
Kifungu 4001 – *External Finance Division* ...............Sh. 68,724,846,500
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unit*……….......................……Sh. 9,120,247,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*............................................Sh. 6,639,660,500
Kifungu 6001 – *Debt Market Management*……......Sh. 6,949,204,000
Kifungu 8001 – *National Planning Division*....................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………………….…Sh. 2,629,932,850,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001 – *Consolidated Fund Services*……….Sh. 1,053,302,874
Kifungu 3002 – *Expenditure Management*…………Sh. 3,390,797,000
Kifungu 3003 – *Financial Management*……..…..Sh. 38,007,955,156
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*…...............................….….Sh. 12,193,532,970
Kifungu 3005 – *Sub Treasury Arusha*…..........................….Sh. 363,920,000
Kifungu 3006 – *Sub Treasury Coast* ……......................….Sh. 185,350,000
Kifungu 3008 – *Sub Treasury Iringa*…….........................….Sh. 193,445,000
Kifungu 3009 – *Sub Treasury Kagera*…......................….Sh. 211,365,000
Kifungu 3010 – *Sub Treasury Kigoma*……....................….Sh. 234,180,000
Kifungu 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro*.....................….Sh. 194,020,000
Kifungu 3012 – *Sub Treasury Lindi*……..........................….Sh. 224,690,000
Kifungu 3013 – *Sub Treasury Mara*……..........................….Sh. 194,530,000
Kifungu 3014 – *Sub Treasury Mbeya*……......................….Sh. 184,940,000
Kifungu 3015 – *Sub Treasury Morogoro*……....................Sh. 246,880,000
Kifungu 3016– *Sub Treasury Mtwara*…........................….Sh. 185,412,500
Kifungu 3017 – *Sub Treasury Mwanza*.......................….Sh. 184,770,000

Kifungu 3018 – *Sub Treasury Rukwa*……….....................….Sh. 184,900,000
Kifungu 3019 – *Sub Treasury Ruvuma*…….....................….Sh. 263,000,000
Kifungu 3020– *Sub Treasury Shinyanga*………..............….Sh. 184,070,000
Kifungu 3021 – *Sub Treasury Singida*…........................….Sh. 185,210,000
Kifungu 3022 – *Sub Treasury Tabora*……........................….Sh. 180,570,000
Kifungu 3023 – *Sub Treasury Tanga*…….........................Sh. 207,415,000
Kifungu 3024 – *Sub Treasury Manyara*……......................Sh. 234,560,000
Kifungu 3025 – *Sub Treasury Njombe*……........................….Sh. 238,230,000
Kifungu 3026 – *Sub Treasury Geita*……..........................….Sh. 184,910,000
Kifungu 3027– *Sub Treasury Katavi*……..........................….Sh. 185,050,000
Kifungu 3028 – *Sub Treasury Simiyu*……..........................….Sh. 212,510,000
Kifungu 3029 – *Sub Treasury Songwe*……........................….Sh. 182,520,000
Kifungu3030 –*Sub Treasury Dar es Salaam*……...........Sh. 349,120,000
Kifungu 4001 – *Local Government Finances*…..…….Sh.1,044,370,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*…………..........Sh. 1,276,933,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*………………..Sh. 16,069,458,390
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……......Sh. 1,617,607,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*…….........................….Sh. 510,327,450
Kifungu 1004 – *Ministerial Audit Division*……...........Sh. 12,154,558,000
Kifungu 1005 – *Local Government Authorities Division*……………....……….…....Sh. 23,504,816,080
Kifungu 1006 – *Performance Audits Division*…..........Sh. 6,839,898,530
Kifungu 1007 – *National Account Division*……............Sh.8,139,367,000
Kifungu 1008 – *Technical Support Service Unit*…….Sh. 8,554,328,600
Kifungu 1009 – *Public Authorities Audit Division*…....Sh. 7,320,955,000
Kifungu 1010 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*……………………….........….Sh. 2,276,961,400
Kifungu 1011 – *Procurement Management Unit*…....Sh. 851,405,000
Kifungu 1012 – *Information and Communication Technology Unit*................................Sh. 4,313,640,000
Kifungu 1013 – *Forensic Audit Unit*............................Sh. 4,910,770,550
Kifungu 1014 – *Quality Assurance Unit*......................Sh.1,372,065,000

Kifungu 1015 – *Government Communication Unit*.....Sh. 621,651,000
Kifungu 1016 – *Risk Management and Compliance Unit*…………………………………............Sh. 211,520,000
Kifungu 1017– *Legal Services Unit* ...............................Sh. 759,563,000
Kifungu 1018 – *Parliamentary Coordination Unit*.....Sh. 1,231,940,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE – MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....................................Sh. 1,500,000,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*.............................Sh. 31,613,072,000
Kifungu 1011 – *Monitoring and Evaluation*..................Sh. 500,000,000
Kifungu 5001 – *Government Asset Management Division*..............................................Sh. 1,975,090,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*……………………….Sh. 3,276,590,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 06 – Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

Kifungu 2001 – *Quality Assurance*………...…………Sh. 236,611,000
Kifungu 2002 – *Technical Audit*……………………….Sh. 557,100,000
Kifungu 2003 – *Local Government Authorities Audit*…………...............…………Sh. 123,950,000
Kifungu 2004 – *Ministries, Independent Departments and Audit*…….............………………Sh. 138,690,000
Kifungu 2005 – *Risk Management Systems and Controls*……………..............…………Sh. 173,100,000
*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Business Support Division*……………Sh. 1,598,249,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu halijatengewa fedha.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti Kamati ya Bajeti, *FIU* haina fedha? Ama zinatoka sehemu nyingine?

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haijatengewa.

**MWENYEKITI:** Itafanyaje kazi?

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu ambao Wizara ya Fedha inautumia lakini hii taasisi mara nyingi inapata fedha kutoka nje ambazo inapitia kwenye Mafungu mengine ya Wizara ya Fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa muundo ambao tuko nao kuna *component* ya fedha ambazo hazipiti moja kwa moja kwenye taasisi yetu, kwenye *FIU* na Mafungu hayo ni yale ambayo yanahusisha ufanyaji wa kazi ambao unahusisha taasisi nyingine za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifanya hivyo na haya ni mafungu ambayo yamehamishiwa kwenye Mafungu mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, hebu hili mkalitazame. Sina hakika kama nimeelewa vizuri kwa sababu wasipokuwa na fedha huku kwenye matumizi ya kawaida wametengewa fedha. Kwa hiyo, wametengewa fedha na tumepitisha hapa sasa hivi, shilingi 3,768,237,000 huku kwenye maendeleo ndiyo hawana pesa.

Haya, Mwenyekiti mtalitazama hilo lakini pia Waziri na wewe ukatazame. Kwa sababu bila fedha kitengo hiki jamani si itakuwa mtihani?

Haya, Katibu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 21 – Hazina**

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MESANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 21 - Hazina pia kuna *addendum*. Kwa hiyo sasa litasomeka shilingi 495,063,000,000.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 21 – Hazina**

Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unity (PPU)*....................................................Sh. 1,123,538,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*......Sh. 412,821,473,073
Kifungu 2002 - *Policy Analysis Division*.....................Sh. 73,749,089,927
Kifungu 4001 – *External Finance Division*......................Sh. 707,800,000
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unity*........Sh. 5,853,453,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*..................................................Sh. 328,626,000
Kifungu 6001 – *Debt Management Division*...............Sh. 479,020,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001 – *Consolidated Fund Services*…..…….Sh. 403,600,000
Kifungu 3003 – *Financial Management*……….……Sh. 3,549,408,000
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*…….........……………………Sh. 2,334,547,000
Kifungu 4001 – *Local Government Finances*……..….Sh. 681,610,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*……………...……Sh. 323,220,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*……..……….Sh. 7,678,100,000
Kifungu 1010 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*……………………........……….Sh. 3,789,900,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Hapa Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa hoja, taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge Zima.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshima Wabunge hoja imeungwa mkono na baada ya kuungwa mkono sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Waziri wa Fedha kuhusu Wizara ya Fedha inayohusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na ninyi kuafiki, sasa niseme rasmi kwamba Bunge limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote chini ya Wizara hii na tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa yale yote ambayo mmeyaahidi katika bajeti yenu lakini pia yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyachangia kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi hapa na pale. Basi tunaamini hayo yote pia mmeyachukua kama Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha ulivyosema hapa. Tunaamini mtayatumia hayo katika kwendelea kuifanya nchi yetu iwe bora zaidi katika nyanja zote. Tunawatakia kila la heri.

Pamoja na pongezi hizo na kuwatakia heri, natumia fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Bajeti, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii mnafanya kazi nzuri sana. Tunawashukuru sana kwa kuendelea kuisimamia Wizara hii lakini pia Wizara hii ina majukumu mengi sana na sote tunaitegemea. Kwa hivyo, tunawashukuru na ninyi tunawategemea sana kuisimamia vizuri Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambao siyo Wajumbe wa Kamati hii ahsanteni sana kwa ushiriki wenu. Wengine mmepata nafasi ya kuchangia, wengine mmepata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, pengine hata kwenye kiti chake; kila mmoja kwa mchango alioutoa tunawashukuru sana kwa sababu itaisaidia Serikali yetu kuendelea kutafuta fedha nyingi zaidi lakini pia kuweza kupeleka huko ambako tunataka ziende kwa ajili ya matumizi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kuna jambo nilisema kwenye Kamati ya Matumizi, kwenye Taarifa yetu ya Kamati lakini pia Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri; Fungu 013 limetengewa fedha za matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo hakuna. Kamati ya Bajeti ikalitazame hili nalo katika hizi siku kama kuna sababu ya kuweka basi hizo fedha ziwekwe hapa. Kama watajiridhisha kwamba hakuna sababu za kuweka fedha za maendeleo, hasa kwa kuzingatia yale ambayo Mheshimiwa Waziri umesema hapa kwamba mnayafanyia kazi mengine mmeshayafanyia kazi, bado yale mambo tisa ninafikiri kwa hesabu.

Sina hakika sana kama hayo yote hakuna hata moja linaloangukia kwenye maendeleo. Kwa hiyo, mtashauriana na Kamati ya Bajeti kuhusu fedha zinazohitajika hapo za maendeleo kwa ajili ya hiki kitengo ambacho ni muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine nilikuwa nimemwelekeza Mheshimiwa Mpina kwa mujibu wa Kanuni ya 70 kwamba yeye athibitishe yale aliyosema Waziri amesema uongo, Kanuni ya 70 (6) inataka apewe muda na mimi ninampa mpaka tarehe 14 Juni 2024.

Jambo lingine Mheshimiwa Waziri nimeletewa ujumbe hapa kwamba kuna sehemu ambapo mifumo ya malipo imefungwa kwa muda sasa na kwa sababu tunaelekea mwisho wa mwaka wa fedha. Kwa hiyo, angalieni yale maeneo ambayo hii mifumo imefungwa sasa zile fedha zitashindwa kutumika halafu tutakuwa tumeshaenda kwenye mwaka mwingine halafu zinaanza zile

changamoto ambazo huwa tunazizungumza kila wakati hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mlitazame hilo maeneo yale ambayo mifumo imefungwa, basi mjaribu kufuatilia ili ifunguliwe wakurugenzi waweze kufanya kazi kwa maana ya kwamba kutumia zile fedha kabla mwaka haujaisha na hasa katika miradi ile ambayo ilishaanza kabla na pengine kuna wakandarasi wanadai huko wameshafanya kazi basi mtoe hiyo nafasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge la mwisho, ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete *(JKCI)* wapo Viwanja vya Bunge nyuma ya Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kutoa huduma ya upimaji wa magonjwa ya moyo kama *pressure*, *echo*, sukari na *ECG* kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao tunafuata ule ushauri ambao huwa unatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Afya alisisitiza sana hapa, tukapime huku ndiyo tujue ule ushauri unatufaa ama hapana.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu. Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.24 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 5 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*